**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA KUMI NA NANE**

**Kikao cha Nne - Tarehe 31 Januari, 2020**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

*Spika (Mhe.Job Y. Ndugai) Alikalia Kiti*

**D U A**

*Spika (Mhe.Job Y. Ndugai) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Naomba tukae.

Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na Mkutano wetu wa Kumi na Nane, Kikao cha leo ni Kikao cha Nne. Katibu!

**NDG. LAWRENCE MAKIGI - KATIBU MEZANI:**

**HATI ZA KUWASILISHA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa mezani na:-

**MHE. MIRAJI J. MTATURU (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MIUNDOMBINU):**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu kuhusu shughuli za Kamati kwa mwaka 2019.

**SPIKA:** Ahsante sana, Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira, Wenyeviti mnaowasilisha muwe mnakuwa karibu ili tuokoe muda na anayefuata awe karibu pia. Karibu sana Mwenyekiti kwa niaba ya!

**MHE. JULIUS K. LAIZER (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA VIWANDA, BIASHARA NA MAZINGIRA):**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira kuhusu Shughuli za Kanati kwa mwaka 2019.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Mbunge wa Monduli Mheshimiwa Kalanga.

Katibu!

**NDG.LAWRENCE MAKIGI - KATIBU MEZANI:**

**MASWALI NA MAJIBU**

**SPIKA:** Tunaanza na Ofisi ya Mhehsimiwa Waziri Mkuu, swali la kwanza litauliza na Mheshimiwa Richard Mganga Ndassa, *Senator,* Mbunge wa Sumve

Na. 37

**Ujenzi wa Kiwanda cha Pamba-Kwimba**

**MHE. RICHARD M. NDASSA** aliuliza:-

Kupitia Mifuko ya Jamii tayari tathmini ya kukijenga Kiwanda cha kuchambua pamba *Nyambiti Ginnery* kilichopo Kwimba umeshafanyika, kilichobaki ni uamuzi wa Serikali kuliongezea thamani zao la pamba.

Je, ni lini Kiwanda hicho kitaanza kujengwa?

**SPIKA:** Ahsante majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Wziri Ofisi ya Waziri Mkuu Mheshimiwa Anthony Mavunde tafadhali.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, VIJANA NA AJIRA (MHE. ANTHONY P. MAVUNDE)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri napenda kujibu swali la Mheshimiwa Richard Mganga Ndasa Mbunge wa Sumve kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Jumuiya ya Mifuko ya Hifadhi ya Jamii Nchini inayoundwa na Mifuko ya NSSF, PSSSF, NHIF, WCF na ZSSF imekamilisha mapitio mapya ya upembuzi yakinifu ya ufufuaji wa vinu vya kuchambulia pamba vya Ngasamo, Nyambiti na Kasamwa vilivyoko Mkoani Simiyu, Mwanza na Geita baada ya takwimu za uzalishaji wa kilimo cha pamba kuongezeka hususan katika Mikoa ya Kanda ya Ziwa.

Mheshimiwa Spika, kwa sasa Mifuko inakamilisha taratibu muhimu zinazohusiana na Miongozo ya Uwekezaji kwa kushirikiana na Vyama vya Ushirika vya Mwanza, Simiyu na Geita ili kuwezesha uwekezaji wenye ufanisi na tija taratibu zitakapokamilika.

Mheshimiwa Spika, Utaratibu maalum wa namna ya kuwezesha ufufuaji wa viwanda hivyo unatarajiwa kukamilika ndani ya mwezi Februari, 2020.

**SPIKA:** Mhehsimiwa Ndassa.

**MHE. RICHARD M. NDASSA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana, naomba uniruhuru niipongeze sana Serikali kwa hatua ambayo sasa imefikia kwa sababu kilio kikubwa kwa wakulima wapamba ni kwamba pamba hiyo inatakiwa iongezewe thamani.

Sasa swali langu nimesema kwamba upembuzi tayari umeshakamilisha na viongozi wakuu wa mifuko hii wako Mwanza nasikia, sasa ni lini sasa baada ya hiyo Februari kwa sababu majibu haya yanaweza kusema kwamba ni Februari kumbe ni mwezi mwingine, ni lini sasa hasa ujenzi wa vinu hivi vitatu kwa maana ya hii *Nyambiti Ginnery, Ngasamo Ginnery* pamoja *Kasamwa Ginnery.*

Lini vitaanza kujengwa ili zao la pamba lipate thamani zaidi? Nakushuru.

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri tafadhali, ni lini.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, KAZI, VIJANA NA AJIRA (MHE. ANTHONY P. MAVUNDE):** Mheshimiwa Spika, niruhusu kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Mbunge kwa namna ambavyo anawapigania wakulima wa pamba wa Kanda ya Ziwa na amekuwa mstari wa mbele kuhakikisha kwamba zao hili linaongezwa thamani. Kama Mheshimiwa Mbunge alivyosema leo wakurugenzi wote wa uwekezaji wa mifuko hii wako Mwanza na kesho kuna kikao cha Wakurugenzi Wakuu ambao kupitia kikao hicho tutapata *way forward* ya lini taratibu hizi zitaanza kwa sababu kesho wanakutaka kwa ajili ya mambo ya kitaalam, hivyo nimuombe Mheshimiwa Ndasa awe mvumilivu tusubiri taarifa ya Wakurugenzi Wakuu kesho ili tujue *way forward* ni nini. Nashukuru.

**SPIKA:** Ahsante sana, tunaendelea wengine hamtoki kwenye pamba, Ofisi ya Rais TAMISEMI Mheshimiwa Sixtus Raphael Mapunda Mbinga Mjini Mariam ndiyo kwa niaba haya endelea.

Na. 38

**Kuboresha Huduma za Afya – Hospitali ya Mbinga**

**MHE. MARIAM N. KISANGI (K.n.y. MHE. SIXTUS R. MAPUNDA)** aliuliza:-

Tangu mwaka 2016, Serikali iliahidi kuboresha huduma za afya katika Hospitali ya Wilaya ya Mbinga ikiwa ni pamoja na kujenga wodi ya watoto, chumba cha upasuaji na gari la wagonjwa:-

Je, ni lini Serikali itatekeleza ahadi hizo.

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mheshimiwa Mwita Mwikwabe Waitara tafadhali.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, nakushukuru, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais-TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Sixtus Raphael Mapunda, Mbunge wa Mbinga Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kuboresha miundombinu ya Hospitali ya Halmashauri ya Mji Mbinga ambapo kupitia mapato yake ya ndani Halmashauri ya Mji Mbinga imefanya ukarabati wa jengo la 'Grade A' kwa gharama ya Shilingi milioni 45 na kununua jokofu la kuhifadhia maiti lenye thamani ya Shilingi milioni 29.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2017/2018 Serikali imetoa kiasi cha Shilingi milioni 500 kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Afya Kalembo ili kupunguza msongamano wa wagonjwa katika Hospitali ya Halmashauri ya Mji Mbinga, ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mariam Kisangi nilikuona.

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana Naibu Waziri kwa majibu mazuri, kwa kuwa Wilaya ya Mbinga ni Walaya ambao iko pembezoni sana na wananchi wake wnachangamoto nyingi sana pamoja na majibu mazuri bado kuna tatizo kubwa la kuwa gari la wagonjwa katika hospitali hiyo.

Je, Serikali ina mkakati saa wa kuhakikisha wanawapelekea gari la wagonjwa katika hospitali ya Wilaya ya Mbinga?

Mheshimiwa Spika, swali la pili kwa kuwa matatizo ya hospitali haya yanaendana kabisa na hali ya hospitali Zakiemu Mbagala.

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuongezea hospitali ya Zakiem Mbagala ambayo imezidiwa wagonjwa ni wengi lakini majengo ni machache na wahudumu ni wachache, nakushukuru.

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo kwa kifupi Mheshimwia Naibu Waziri TAMISEMI tafadhali.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA):** Mheshimiwa Spika, kwanza nampongeza Mheshimiwa Mbunge kwa kusimamia Mkoa wa Dar es Salama, pia ni Tanzania kwa ujumla wake hususan jambo la afya ya akinamama na watoto na wazee.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba unapokua unajenga kuboresha huduma za afya ni muhimu kuwa na gari la wagonjwa ili inapokea dharura iwe ni rahisi kumuwaisha katika huduma nyingine ya ziara ya pale alipokuwa, lakini naomba nimuahidi Mheshimiwa Mbunge kwamba kadri kwa uwezo wa Serikali uwezo ukipatikana basi eneo hilo la Mheshimiwa Raphaeri Mapunda litapata gari la wagonjwa kama ambavyo Mheshimiwa Mbunge ameulizia hapa.

Mheshimiwa Spika, naomba niseme tu kwamba mpango wa Serikali ni kuboresha huduma zaafya na kupeleka hufuma karibu na wananchi, tumepokea hoja Mheshimiwa Mbunge bahati nzuri tunaenda kwenye mwaka wa bajeti 2020/2021 basi tuangalie uwezekano wa kupatikana ili tuweze kupeleka fedha katika eneo hili kuboresha huduma ya pale Mbagala pia Mkoa wa Dar es Salam kwa ujumla wake. Na natambua kwamba wnanchi wangu wa Jimbo la Ukonga pia wanaweza wakapata huduma pale Mbagala Zakiemu, ahsante sana.

**SPIKA:** Ahsante nilikuwa mnadhimu wa upinzani Bungeni uliza swali lako.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi niulize swali la nyongeza, wnanchi wa Jimbo la Bunda Mjini na Wilaya ya Bunda kwa ujumla walikubaliana kwamba hospitali ya Manyamanyama iwe hospitali ya Wilaya. Lakini kuna baadhi ya mambo ambayo hospitali hiyo haina pamoja jokofu la kuhifazia maiti. Wananchi wa Jimbo la Bunda Mjini wanapata tabu kupeleka maiti Nyamswa Jimbo la Bunda.

Sasa ningependa kujua ni lini Serikali itapeleka jokofu katika hospitali ya Manyamanyama?

**SPIKA:** Ahsante sana swlai kutoka Mkoa wa Mara hilo, kuna baadhi ya Wabunge wa Mkoa wa Mara siwaoni oni hapa na sina taarifa zao kwa mfano Mheshimiwa Heche simuoni kabisa hapa sijui yuko wapi, Mheshimiwa Naibu jibu swali hilo la Manyamanyama.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA):** Mheshimiwa Spika, ni kweli maneno yako yako ya utangulizi yanafaa sana ndiyo

maana tufanye mabadiliko makubwa katika eneo hili ikiwa na Wabunge wanaopatikana wakatl wote Bungeni kusemea watu wao kama Mheshimiwa Ester Bulaya.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba kwanza Bunge imepata Kituo cha Afya ni suala la kuishukuru Serikali ya Awamu ya Tano ya Dkt. John Pombe Magufuli tumepata hospitali pale inajenga katika eneo hili lengo ni kupunguza msongamano wa wagonjwa katika hospitali hii. Mheshimiwa sema Mheshimiwa hoja yako imepokelewa tuangalie uwezo wa Serikali tupeleke jokofu katika eneo hili ili maiti ikipatikana pale basi iweze kuhifadhimiwa eneo la karibu na kupunguza gharama zausafirishaji wa ndugu wa marehemu, ahsante sana.

**SPIKA:** Ahsante sana kwa majibu hayo, nichukue nafasi hii pia kutambua uwepo wa Mheshimiwa Mbunge wa Arusha Mjini Mheshimiwa Lema baada ya kummisi kwa muda mrefu sana bwana tulikumisi karibu sana Mheshimiwa Lema, karibu sana, tunaendelea na Mheshimiwa Godfrey William Mgimwa Mbunge wa Kalenga tafadhali uliza swali lako kwa niaba yake nakuruhusu Mheshimiwa.

Na. 39

**Tatizo la Ukosefu wa Nyumba Za Walimu–Kalenga**

**MHE. PAULINE P. GEKUL (K.n.y. MHE. GODFREY W. MGIMWA)** aliuliza:-

Tatizo la ukosefu wa nyumba za Walimu kwenye maeneo mengi ya Jimbo la Kalenga kumesababisha Walimu kuhama na hivyo kudhoofisha ukuaji wa elimu kwa ujumla: -

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuisaidia Halmashauri ya Iringa Vijijini ili kuhakikisha inajenga nyumba za kutosha kwa Walimu?

(b) Mapato ya ndani ya Halmashauri hii hayatoshi kujenga nyumba za Walimu. Je, nini mkakati wa Serikali juu ya tatizo hili?

**SPIKA:** Ahsante majibu ya swali hilo bado tuko TAMISEMI.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ahsante, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais-TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Godfrey William Mgimwa, Mbunge wa Kalenga lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2019/2020, Serikali tayari imetoa Shilingi milioni 50 kwa ajili ya ukamilishaji wa ujenzi wa nyumba 2 za walimu katika Halmashauri ya Wilaya ya Iringa. Serikali inaendelea kutafuta fedha kupitia vyanzo mbalimbali kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya shule zikiwemo nyumba za walimu.

(b) Mheshimiwa Spika, Mkakati wa Serikali ni kuziwezesha halmashauri kuandaa maandiko ya miradi ya Kimkakati itakayoongeza mapato ya halmashauri ili kukidhi mahitaji yaliyopo ikiwemo ujenzi wa nyumba za walimu. Aidha, Halmashauri zimeelekezwa kubuni vyanzo vipya vya mapato na kuimarisha makusanyo ya mapato ya ndani na usimamizi wa vyanzo vilivyopo ahsante.

**SPIKA:** Mheshimiwa Gekul.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru naomba niulize maswali mawili ya nyongeza, swali la kwanza Mheshimiwa Naibu Waziri, ukweli ni kwamba halmashauri nyingi hasa za Mijini wamesha *exhaust* karibia vyanzo vyote vya mapato. Sasa nilifikiri kwamba Serikali ingetusaidia kuweka mpango wa haraka kwa ajili ya nyumba za walimu.

Ni lini Serikali itaweka kwenye bajeti kuu fedha za ujenzi wa nyumba za walimu?

Mheshimiwa Spika, swali la pili nishukuru kwanza Serikali ilitupatia fedha milioni 152 kwa ajili ya kukamilisha bweni la Sekondari ya Nakwa katika Halmashauri ya Mji wa Babati lakini ujenzi umefika katika upauzi bado *finishing,* niombe serikali itupatie fedha kwa sababu tatizo la vyanzo vya mapato kuwa vichache kati Halmashauri ya Kalenga ina fafana pia Halmashauri ya Mji wa Babati.

Ni lini Serikali itatupatia fedha kwa ajili ya *finishing* ya bweni la Sekondari ya Nakwa?

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo mawili Mheshimiwa naibu tafadhali Mheshimiwa Mwikwabe Mwita Waitara.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA):** Mheshimiwa Spika, ni kweli tungependa kuona nyumba za walimu katika maeneo ya jirani ili walimu wetu wasiweze kupata shida wnapotoa huduma na kuhudia vijana wetu katika maeneo mbalimbali na hasa Vijijini. Vilevile tungependa pia kuwa na mabweni ya kutosha kwa watoto wa kike ili kuwapunguzia majanga ya kupata mimba na wakati mwingine mazingira magumu kuplekea kufanya vibaya katika mitihani yao.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba tuko kwenye bajeti ya mwaka huu tumetenga fedha ya kukamilisha nyumba zaidi ya 364 katika maeneo mbalimbali, pia kumalizia mabweni na kumbi mbalimbali. Ningependa niseme tu kwa mfano fedha hizi ambazo zinazungumzwa hapa ambazo tungeweza mkopo ambayo wenzetu humu ndani wametuhujumu kwa kufanya hizi fedha zisiweze kuchelewa zingeweza kunufaisha vijana, watanzania wazalendo wenzetu zaidi ya milioni sita, tungeweza kujenga matundu ya vyoo kwenye mashule ya Sekondari, 1000, tungejenga matundu ya vyoo 2000 katika maeneo mbalimbali, kutengeneza kumbi za mikutano, mabwalo na hosteli mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, naomba tu niseme katika jambo hili ni jambo la mkakati la pamoja Serikali, Waheshimiwa Wabunge na wadau mbalimbali tushirikiane tunapoona kutafuta vyanzo mbalimbali vya mapato wenzetu wanapokula kitumbua wasitie mchanga ili fesha ije katika eneo hili na watanzania wapate huduma kama ambavyo imetupasa kufanya, ahsante.

**SPIKA:** Haya majibu ya uhakika kweli kweli, nashangaa kuna swali la nyongeza kweli hapa, haya Mheshimiwa Justin Monko na Mheshimiwa Tendega atafuata Grace.

**MHE. JUSTIN J. MONKO:** Mheshimiwa Spika, kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza, kwa kuwa Serikali imetueleza kwamba ina mikakati mbalimbali ya kuongeza nyumba za walimu na tatizo hili lililopo katika Jimbo la Kalenga linafafana sana na Jimbo la Singida Kaskazini.

Je, Serikali haioni umuhimu sasa katika bajeti hii ya mwaka 2020/2021 kuanza kutenga fedha kwa ajili kutoa posho maalum kwa walimu ili waweze kukodisha nyumba na waishi katika maeneo ambayo yanastahili, ahsante sana.

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri TAMISEMI tafadhali.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA):** Mheshimiwa Spika, ni mapenzi ya Serikali hii ya Awamu ya Tano kwamba tuwe na uwezo wa kuwawezesha walimu wetu wafanye kazi katika mazingira raisi sana na lipokee ushauri wake na kwa sababu yeye ni Mheshimiwa Mbunge na mchakato huo bahati nzuri unaanzia kwenye ngazi ya halmashauri.

Kwa hiyo, ningeomba Waheshimiwa katika halmashauri zetu pale mchakato unaondelea sasa tunatengeneza bajeti tuangalie uwezekano wa kupunguza adha hii kwa walimu wetu; na sisi kama Serikali ngazi ya TAMISEMI tutalipokea na kuanza kulifanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, lakini nitoe wito kwa watanzania tunaoishi katika maeneo ambayo tunatoka hata Waheshimiwa Wabunge na wadau mbalimbali wa elimu hata tukijenga zile nyumba za kawaida na kuweza kuwapangisha walimu kwa bei nafuu walimu wataishi karibu maeno ya shule wataweza kutoa huduma mbalimbali. Tushirikiane pamoja kuweza kupunguza changamoto ya walimu, walimu wafundishe katika maeneo salama, rafiki pia na kodi ambayo ni *affordable* ili waweze kufanya kazi katika urahisi wake, ahsante sana.

**SPIKA:** Ahsante nilishakutaja Mheshimiwa Grace Tendega uliza swali lako.

**MHE. GRACE V. TENDEGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kuniona pamoja na ukosefu wa nyumba za walimu katika Jimbo la Kalenga ni mwaka wa nne sasa walimu hawa hawajapandishwa madaraja na wamekuwa wakipata adha kubwa sana katika masuala hayo ya nyumba.

Ni lini sasa Serikali itawapandisha madaraja walimu hawa ili waweze kuongeza *morale* katika utendaji kazi wao? *(Makofi)*

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo muhimu la linalohusu walimu, Mheshimiwa Naibu Waziri tafadhali.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA):** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba tuna malalamiko mbalimbali mengi ya walimu katika maeneo mbalimbali ya nchi wakionesha kukerwa na kutopandishwa madaraja. Niwaombe pia katika jambo hili pia kwa sababu ya mchakato wa kupandisha madaraja unaanzia kule ngazi ya halmashauri zetu ambako kila Mbunge pale yupo, mchakato unaanzia pale ngazi ile inaenda kwa Afisa Utumishi inakuja kwa Mkurugenzi mpaka maeneo mengine. Tupeane taarifa tumeshatoa maelekezo tumekutana walimu wote na mawakilishi wao kwa maana Maafisa Elimu wa Wilaya na Mikoa na Wakurugenzi na Makatibu Tawala, juzi walikuwa hapa Dodoma, tukaagiza kwamba tupate taarifa.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu unakuta, mwalimu yupo kwenye halmashauri yako Mheshimiwa Mbunge, lakini mwenzake yeye kapanda mara ya kwanza, mara ya mwisho 2013 mpaka leo hajapanda, lakini kuna wengine wamekuwa wakipandishwa. Kwa hiyo, tukipata taarifa mahusui katika maeneo haya tutazifanyiakazi haraka sana. Walimu wanalalamika na wanakwazwa, tungependa tuwaondolee adha, yale mambo ambayo yapo ndani ya uwezo tuyaondoe ili tuondoe kero kwa walimu wetu waendelee kufundisha kwa moyo. Ahsante sana.

**SPIKA:** Ahsante sana. Wakati Mheshimiwa Naibu Waziri anajibu kuhusiana na swali hili ambalo linagusa masuala ya elimu, majibu yake mazuri yaliyohusisha ushauri aliotupatia hapa kuhusu namna ambavyo Waheshimiwa Wabunge wakati mwingine mwenendo wetu unakuwa haueleweki. Kwa mfano, Mbunge mwenzetu labda atakaporudi anaweza akatufafanulia wenzake, Mheshimiwa Zitto Kabwe kuandika barua *World Bank* kwamba nchi yetu ikose fursa ya

mkopo ambayo lengo lake ni elimu kwa sababu ya tofauti za kimtazamo wa kisera ambalo ni jambo la kawaida; mtu unaweza ukawa na utofauti wa sera au mtazamo kati ya wewe Mbunge au upande wa Serikali na kadhalika, lakini kufikia mahali pa ku-*block* Tanzania isipate fursa Fulani, nadhani ni kwenda mbali mno.

Nasema hivyo kwa sababu watoto watakaokosa fursa hiyo ni watoto wa Tanzania, ni Walimu wa Tanzania na ni miundombinu ya elimu ya Tanzania. Sijui katika hilo kama Mbunge sijui unafaidika nini? Kwa sababu kama ni tofauti za kisera, haya ni mambo ya kujadili tu na ndiyo maana sisi ni Wabunge hapa. Kwa kweli limetugusa na kutukera wengi ambao bado hatujaelewa vizuri hili jambo linakujakujaje hili, *how is it possible?*

Kwa hiyo ningependa kutoa ushauri wa jumla tu kwamba, ni vyema kutumia fursa yetu kama Wawakilishi wa wananchi tukaelimishana, tukaelezana na kadhalika kuliko kuwakosesha Watanzania fursa, wakati baadhi yetu hapa watoto wetu wako *Feza boys,* wako *Marian Girls* halafu una-*block* msaada kwa watoto walio wengi wa wapiga kura wetu, jambo ambalo nadhani halifai kabisa.

Tunaendelea na Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Mheshimiwa Mgeni Jadi Kadika, uliza swali lako sasa.

Na. 40

**Athari za Utandawazi kwa Vijana**

**MHE. MGENI JADI KADIKA** aliuliza:-

Utandawazi umechangia sana vijana kupoteza maadili:-

Je, Serikali haioni sasa ni wakati muafaka kwa vijana wetu kuwekewa umri maalum wa kutumia mitandao ili kupunguza mmomonyoko wa maadili?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Habari, Mheshimiwa Juliana Shonza, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mgeni Jadi Kadika, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli utandawazi umechangia sana katika kuleta mmomonyoko wa maadili kwa kiasi kikubwa kwa jamii zetu hususan vijana kupitia intanenti, mitandao ya kijamii na maudhui ya nje kupitia muziki na filamu. Ndiyo sababu ya Serikali kuja na Sheria ya Makosa ya Mtandao *(Cybercrime)* ya mwaka 2015 na Kanuni za Maudhui ya Mtandao na Maudhui ya Redio na Runinga za mwaka 2018 ambazo zimepigiwa sana kelele ndani ya Bunge hili Tukufu kuwa zinaua uhuru.

Mheshimiwa Spika, wazazi na familia kwa ujumla ndio walezi wa kwanza wenye jukumu la kumlea mtoto kuanzia hatua ya awali na hufuatiwa na Taasisi za elimu ya awali, msingi, sekondari hadi elimu ya juu ambao huwaelimisha kwa maneno na vitendo watoto na vijana hususan utambuzi wa mambo mema na mabaya, yanayofaa na yasiyofaa. Baada ya hatua hizi kupita ndipo wajibu mkubwa wa Serikali unajitokeza.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mgeni, swali la nyongeza.

**MHE. MGENI JADI KADIKA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu yake lakini bado nina maswali mawili ya kumuuliza. Swali la kwanza; kwa kuwa vijana wengi au vijana wetu wadogo wanatumia mitandao kwa kutumia simu au ku-*chart* au kuangalia picha za ngono ambazo kuwa huleta hisia mbalimbali. Watoto hao ndiyo wale wanaobeba ujauzito wakiwa na umri mdogo kati ya darasa la sita mpaka darasa la tatu. Je, Serikali inaonaje suala hili?

Mheshimiwa Spika, swali langu la pili; ziko nhi za wenzetu wanazuia mitandao kurusha picha za chafu. Je, Serikali yetu inashindwa nini baada ya kukemea na kudhibiti ili kuzuia mambo haya yasiendelee na wale watakaofanya hivyo wachukuliwe hatua? *(Makofi)*

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Habari, Mheshimiwa Juliana Shonza, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ambayo yameulizwa na Mheshimiwa Mgeni:-

Mheshimiwa Spika, nikianza na swali lake la kwanza ambalo ametaka kujua kwamba kwa upande wa Serikali tunaonaje masuala haya ya utandawazi. Ni kweli tunatambua kwamba, changamoto imekuwa kubwa sana kwa suala zima la maadili na kwa kiasi kikubwa sana inchangiwa na hii mitandao ya kijamii. Ndiyo maana kwa kujua hilo sasa sisi kama Serikali tulikuja na Sheria mbalimbali na Wabunge wa Bunge hili ndiyo ambao walizipitisha hizo Sheria, lengo ni kuhakikisha kwamba, tunawazuia watoto wetu hususan vijana ambao wako chini ya umri wa miaka 18 kuweza kujihusisha na vitu ambavyo havifai kwa Taifa letu. Kwa hiyo, kama ambavyo nimejibu kwenye jibu langu la msingi kwamba jukumu hili siyo jukumu la Serikali peke yake ni jukumu letu sote.

Mheshimiwa Spika, pia katika swali la pili, ametaka kujua kwamba nchi zingine zimefanikiwa kwa kiasi kikubwa sana kuweza kudhibiti vijana wadogo ambao wako chini ya miaka 18 kuangalia vitu ambavyo havifai kwenye mitandao. Bado jibu langu liko pale pale kwamba ni wajibu wetu sote, upande wa Serikali na naweza nikasema kwamba kwa upande wa Serikali tumefanya kazi kubwa sana na ziko sheria ambazo tayari tumeshazipitisha ndani ya hili Bunge, lakini changamoto zimekuwa kubwa kwamba sheria hizi zinapopita Waheshimiwa Wabunge tumekuwa na ile tabia ya kuwa na mgawanyiko.

Mheshimiwa Spika, unakuta sheria tumepitisha kwa mfano, Sheria ya *Cybercrime,* lakini sasa unakuta wengine wanaanza kulalamika kwamba ile sheria inaminya uhuru na inakandamiza, kitu ambacho kinakuwa siyo cha kweli. Kwa hiyo nitoe wito ndani ya hili Bunge kwamba sheria kama hizi zinapopita katika Bunge ni vyema sisi kama viongozi tukawa wa kwanza kuzisimamia, lakini vilevile kwa yale maeneo ambayo sisi tunatoka, tuhamasishe jamii kuona kwamba namna gani ambapo suala zima la malezi siyo suala la Serikali peke yake ni suala la Serikali lakini pamoja na jamii kwa ujumla. Ahsante.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Juliana Shonza kwa majibu hayo. Sasa tunakwenda katika swali namba 41, bado tupo Wizara hii hii ya Habari. Swali linaulizwa na Mheshimiwa Maulid Said Mtulia, Mbunge wa Kinondoni, Mheshimiwa Mtulia, tafadhali.

Na. 41

**Mpango wa Kuimarisha Sekta ya Michezo**

**MHE. MAULID S. MTULIA** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuimarisha Sekta ya Michezo kwa kuandaa Wakufunzi wa Michezo, kujenga viwanja vya kisasa na kuhakikisha upatikanaji wa vifaa vya michezo?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Habari na Michezo, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Maulid Said Mtulia, Mbunge wa Kinondoni, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha Sekta ya Michezo, Serikali imeendelea kutoa mafunzo ya aina mbalimbali yanayohusu taaluma tofauti za Michezo. Kupitia Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, elimu ya michezo hutolewa katika ngazi ya Shahada kupitia idara ya maalum ya *Physical Education and Sports Science*. Aidha, kupitia Chuo cha Maendeleo ya Michezo Malya, Mkoani Mwanza, Serikali inaendelea kutoa mafunzo ya utawala katika Michezo pamoja na ukufunzi katika michezo mbalimbali katika ngazi ya Stashahada, *Diploma in Sport Admistration and Coaching* ambayo hutolewa kwa muda wa miaka miwili.

Mheshimiwa Spika, suala la ujenzi wa miundombinu siyo la Wizara peke yake, letu sote ikiwemo sekta binafsi na halmashauri zote nchini.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mtulia, swali la nyongeza.

**MHE. MAULID S. MTULIA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa ya kuuliza maswali madogo mawili ya nongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri lakini nina maswali yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza, hivi sasa kuna mwamko mkubwa sana Nchini Tanzania kwa wazazi kutaka watoto wao washiriki kwenye michezo hasa ikichagizwa na mafanikio aliyoyapata kijana wetu Mbwana Samatta kucheza katika ligi ya Uingereza na mimi sasa hivi timu yangu ni *Aston Villa,* lakini kuna tatizo kubwa la vifaa vya michezo kwa wananchi wetu ili kuweza kushiriki vizuri michezo.

Je, Serikali ina mkakati gani kuhakikisha vifaa vya michezo yote Tanzania vinapatikana kwa urahisi ili wazazi wachochee mchakato huu wa kuwa na wana michezo wengi Nchini Tanzania?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; Wizara imesema suala la ujenzi wa viwanja ni la wadau na halmashauri na Halmashauri ya Kinondoni imeitikia wito huo kwa kuja na ujenzi wa uwanja wa mpira wa miguu pale Mwenge na vilevile kuna mchakato wa kujenga kituo cha malezi ya watoto ili tupate wachezaji bora kabisa. Serikali inatoa kauli gani kusaidia juhudi hizi ili wanaoonesha nia ya kuleta mabadiliko ya soka wapate kusaidiwa?

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo mawili, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Michezo tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, kwanza nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo la Kinondoni kwa sababu amekuwa ni mdau mkubwa sana wa masuala ya michezo, lakini nadhani hiyo inatokana na kwamba Jimbo lake ni Jimbo ambalo lina wanamichezo wengi pamoja na wasanii wengi. Kwa hiyo naamini kwamba Mheshimiwa Mbunge anafanya kazi nzuri sana na wananchi wake wanajivunia hilo.

Mheshimiwa Spoika, nikija sasa kwenye maswali yake mawili ya nyongeza; swali lake la kwanza amezungumza kwamba ipo changamoto ya vifaa vya michezo; na mimi nikiri kwamba ni kweli kumekuwepo na changamoto ya vifaa vya michezo, lakini kama Serikali hatujakaa kimya na tunayo Sera yetu ya Michezo ya Mwaka 1995 ambayo inazungumza kwamba suala zima la ujenzi wa viwanja pamoja na miundoimbinu yote ya michezo ni suala la Serikali lakini vilevile kwa kushirikiana na wadau.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kwa upande wetu sisi kama Serikali sasa hivi kwa kushirikiana na Wizara ya Viwanda na Biashara tumekuwa tukihamasisha sana wafanyabiashara mbalimbali waendelee kuagiza vifaa vya michezo kutoka nje. Kama hiyo haitoshi kama Wizara vilevile kwa kupitia Sera yetu ya Awamu ya Tano ambayo ni Sera ya Viwanda tumekuwa pia tukihamasisha sana wawekezaji wa ndani pamoja na wawekezaji wa nje kuanzisha viwanda vya vifaa vya michezo kwa sababu tunatambua pamoja na kwamba vifaa vinakuwa ni adimu lakini pia changamoto kubwa imekuwa ni masuala ya kodi. Kwa hiyo hakuna namna nyingine ambayo tunaweza tukafanya kuondokana na tatizo hili, ni lazima sisi kama nchi tuhakikishe kwamba tuna viwanda ambavyo vinahusiana na uchakataji wa hivi vifaa vya michezo. Kwa hiyo, mikakati ipo na sisi kama Wizara tunaisimamia hiyo mikakati na tunamwahidi Mheshimiwa Mbunge kwamba, tatizo hili kwa kadri miaka inavyozidi kwenda tunaendelea kulifanyia utatuzi.

Mheshimiwa Spika, katika swali lake la pili amezungumza namna gani ambavyo Halmashauri ya Kinondoni imeonesha jitihad. Nikiri kwamba ni kweli Halmashauri ya Kiondoni imekuwa ni mfano katika kuweka miundombinu ya michezo na natambua kwamba pia Halmashauri hiyo sasa hivi inamiliki timu ya *KCMC*, kwa hiyo ni namna gani ambavyo wanaonesha kwamba wana jitihada kubwa ya kukuza sekta hii ya michezo. Kwa hiyo, niseme sisi kama Wizara kwa kupitia *TFF* tumekuwa tukiunga mkono jitihada kama hizi za wadau kwa kuwapatia vifaa mbalimbali pamoja na nyasi na vifaa vingine na hayo tayari yameshafanyika kwenye baadhi ya maeneo. Kwa hiyo, nimwombe Mheshimiwa Mbunge kwa kushirikiana pia na Halmashauri ya Kionondoni wapeleke maombi *TFF* ili waone ni namna gani ambavyo wataweza kusaidia hivyo vifaa ili huo uwanja uweze kukamilika na nimwahidi Mheshimiwa Mbunge kwamba, sisi kama Wizara tutakuwa pamoja naye kuhakikisha kwamba uwanja huo unakamilika, lakini vilevile support ya Serikali kupitia *TFF* iweze kuonekana. Ahsante sana.

**SPIKA:** Ahsante sana. Nilikuona Mheshimiwa Cecilia Paresso lakini wewe siyo Mwanamichezo bwana. Haya uliza swali lako labda mpenzi wa michezo.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali dogo la nyongeza. Ni kweli siyo Mwanamichezo, lakini nawakilisha wanamichezo. Watanzania wote leo tunamshangilia na kumfurahia Samatta kwa kusajiliwa na hiyo timu ya Uingereza. *(Kicheko)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, wanataka kujua tu ni timu gani hiyo. Inaitwaje hiyo? *(Kicheko)*

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Spika, *Aston Villa*. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, amesajiliwa kwa sababu ya jitihada zake mwenyewe, sasa inatuambia Watanzania kwamba tunaweza kuwa na Samatta wengi kwa kadri inayowezekana kama Serikali ikiwezekeza vya kutosha kwenye michezo. Sasa kwa nini Serikali isianzishe *Sports Arena* kwenye Majiji Makuu kama ambavyo wanafanya Nchi ya Rwanda ili kuwatoa Samatta wengi?

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Harrison Mwakyembe, Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, majibu tafadhali.

**WAZIRI WA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:** Mheshimiwa Spika, nianze kwanza kwa kumpongeza Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kujibu maswali vizuri sana ya michezo. Naomba nijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Paresso kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, sasa hivi kutokana na juhudi za Serikali pamoja na wananchi wenyewe, tuna wachezaji 22 wanacheza nje ya nchi yetu, wanacheza Kimataifa siyo Samatta peke yake na hii inatokana na uelewa tulioupata Watanzania kwamba vipaji hivi havipatikani ukubwani unaanzia huku chini ndiyo maana Serikali inaingia gharama kila mwaka kuendesha mashindano ya UMITASHUMTA na UMISETA kwa shule za Msingi na shule za Sekondari.

Mheshimiwa Spika, nimalizie tu kwa kusema, sasa hivi wito wetu wa kushiriki kila mtu kujenga viwanja, miundombinu siyo tu Kinondoni imeitikia hata vilabu binafsi kama Simba *Sports Club* wamejenga viwanja viwili Dar es salaam vya nyasi bandia pamoja na nyasi za kawaida, viwanja vizuri nimeenda kuvitembelea. Siyo hivyo tu, Mkoa wa Arusha unaongozwa unastahili pongezi, Halmashauri ya Jiji la Arusha sasa hivi imejenga Ngarenaro kiwanja changamani kizuri ambacho kina *Netball, Basketball* pia *Soccer* lakini vilevile katika Kata nafikiri ya Sinoni kuna Mtanzania ambaye anaishi Marekani anajenga kiwanja kizuri sana kimefikia asilimia 90. Nitoe wito kwa vijana wetu pia wanaoishi Ulaya, nje ya nchi waige huo mfano, wasishinde tu kwenye mitandao ya kijamii. Ahsante sana.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri kwa majibu mazuri sana ya kutia moyo. Umesahau tu kwamba kule Ruangwa kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu pamejengwa kiwanja kizuri sana kwa ajili ya michezo pia. Pia ni kweli kwamba Simba wanajenga kiwanja cha kisasa kabisa, sasa sijui wale wengine wanasubiri nini, kuiga inaruhusiwa jamani. *(Kicheko)*

**SPIKA:** Wizara ya Katiba na Sheria, Mheshimiwa Sophia Hebron Mwakagenda, uliza swali lako tafadhali.

Na. 42

**Mahakama Kuingiliwa na Siasa**

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA** aliuliza:-

Kwa mujibu wa *GN. No.* 222 na 223 ya mwaka 1972 pamoja na marekebisho yake ya mwaka 2002, Wazee wa Mabaraza ya Mahakama wanateuliwa na vikao vya Chama cha Mapinduzi (CCM) na Kamati za Maadili za Mahakimu zipo chini ya Uenyekiti wa Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya:-

Je, ni lini Mahakama itaacha kuingiliwa na siasa?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Katiba na Sheria, Dkt. Augustino Mahiga, tafadhali.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, Mahakama ya Tanzania ni moja ya mihimili mitatu ya dola ambayo kwa mujibu wa Ibara ya 4 na 107(B) ya Katiba, Mahakama ni Mhimili huru na hauingiliwi na chombo chochote katika utekelezaji wa majukumu yake ya utoaji haki.

Mheshimiwa Spika, katika utekelezaji wa majukumu yake, Mahakama imekuwa ikiwatumia Wazee wa Baraza katika ngazi ya Mahakama za Mwanzo na Mahakama Kuu ambao hupatikana kwa mujibu wa Kanuni za Wazee wa Baraza katika Mahakama za Mwanzo *G.N. No*. 222/223 za Mwaka 1972, ambao huteuliwa kulingana na sifa za umri na uzoefu walionao katika masuala mbalimbali hasa ya kijamii katika eneo husika.

Aidha, Wazee wa Baraza huwa na jukumu moja la kuishauri Mahakama na ushauri wao hauifungi Mahakama katika kutoa uamuzi inaouona unafaa. Hata hivyo, Wizara yangu imeanza mchakato wa kuboresha sekta ndogo ya mfumo wa haki, jinsia nchini ambao pamoja na mambo mengine inapitia Sheria za Kamati zote ambazo zimetungwa miaka mingi iliyopita ili ziendane na wakati.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Kamati za Maadili za Mikoa na Wilaya, Sheria ya Usimamizi wa Mahakama ya Mwaka 2011, imebainisha majukumu ya Kamati hizi kwa mujibu wa vifungu vya 50 na 51. Lengo la Kamati hii ni kushughulikia malalamiko ya ukiukwaji wa maadili ya utendaji wa Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo na Mahakimu Wakazi katika kutimiza shabaha na kulingana na kusawazishana *(checks and balances)* katika utendaji wa Mihimili ya dola. Kamati hizi haziingilii uhuru wa Mahakama ambayo inatekeleza majukumu yake ya utoaji haki ambao unatajwa kwa mujibu wa Ibara ya 107 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, ninapenda kulifahamisha Bunge lako Tukufu kuwa, nchi yetu itaendelea kuheshimu misingi ya mgao wa madaraka baina ya mihimili ya Dola na kamwe Mahakama haiwezi na haiingiliwi na chombo kingine cha Dola katika utekelezaji wa majukumu yake.

**SPIKA:** Kwa majibu haya, mana yake Mheshimiwa Sophia swali lako ni la kizushi. Swali la nyongeza Mheshimiwa Sophia Mwakagenda. *(Kicheko)*

**MHE. SOPHIA H. WAKAGENDA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa kuwa Mheshimiwa Waziri amekubali na kukiri kwamba toka mwaka 1972 wazee wa CCM wamekuwa kwenye Baraza za Mahakama: Je, ni lini Serikali italeta sheria tuweze kubadilisha wazee hawa watoke kwa wananchi na siyo kwenye vyama? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili. Kwa kuwa Mheshimiwa Waziri amekiri kwamba wazee hawa wanatoka kwenye Chama cha Mapinduzi, haoni wanakwamisha juhudi za Mahakimu kwa kutoa haki kwa mahabusu wanaotoka Upinzani? *(Makofi)*

**SPIKA:** Najaribu kuangalia, ni wapi Mheshimiwa Waziri amekiri? Mheshimiwa Waziri, majibu tafadhali.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, kwanza lazima tutoe heshima kwa wazee wetu kwa busara zao. Kama wanatoka Chama hiki au chama kile, lakini wazee wetu ni wazalendo, wazee wetu ni walezi, wazee wetu ni kioo cha jamii, tuwape heshima wanayostahili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema, tuko katika mchakato wa kubadilisha mfumo mzima wa Mahakama na hasa katika makosa ya jinai. Sheria hii ilipitishwa mwaka 1972 na ndiyo maana tumeona umuhimu huo na mchakato huo unaendelea na pale utakapokamilika tutawajulisheni. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, samahani, nakurudisha hapa. Katika swali la msingi anasema kwamba umekiri wazee wa CCM ndio wazee wa Baraza. Ni kweli umefanya hivyo? Maana kwenye jibu lako mimi sijaona hilo. Ndiyo swali lake hasa! Unaweza kuchukua dakika moja kulijibu.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kufafanua hilo. Sijakiri hivyo, lakini nilichosema katika maelezo yangu ni kwamba wazee wazee wetu tulionao katika jamii zetu, tuwape heshima na tutambue busara zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pili, nimesema kwamba kama sheria hii ilipitishwa mwaka 1972, Mahakama iko katika mchakato wa kutazama umuhimu wa kurekebisha taratibu hizo za Kimahakama na hasa kwa matumizi na uchaguzi wa wazee ambao watakuwa wanasaidia Mahakama zetu za mwanzo na za juu. Nadhani hiyo ndio ufafanuzi nilioutoa. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri kwa kuliweka vizuri hilo, maana yake Mheshimiwa Sophia alikuwa analipeleka tofauti kabisa.

Tunaendelea na Mheshimiwa Omari Mohamed Kigua Mbunge wa Kilindi uliza swali lako.

Na. 43

**Ukarabati wa Mahakama za Mwanzo Katika Jimbo la Kilindi**

**MHE. OMARI M. KIGUA** aliuliza:-

Serikali imekuwa na utaratibu wa kutenga fedha kwa ajili ya ukarabati wa Mahakama za Mwanzo:-

Je, ni lini Serikali itafanya ukarabati wa Mahakama za Kata za Kimbe, Kwekivu na Kata ya Mswaki ambazo zimechakaa sana?

**SPIKA:** Bado tuko Wizara ya Katiba na Sheria, Mheshimiwa Dkt. Mahiga, majibu tafadhali.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Omari Mohamed Kigua, Mbunge wa Kilindi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, miongoni mwa changamoto zinazoikabili Mahakama ya Tanzania ni uhaba na uchakavu wa miundombinu. Kwa sasa, kuna jumla ya Mahakama za mwanzo 960 katika mikoa yote nchini. Idadi kubwa ya majengo ya Mahakama hizi ni chakavu na ni finyu kuweza kutoa huduma kwa mahitaji ya sasa hususan kukidhi ongezeko la mashauri. Hivyo, majengo mengi yanayohitaji kujengwa upya, ngazi ya Mahakama ya Mwanzo ni muhimu sana kwa kuwa inabeba takriban asilimia 70 ya mashauri yote yanayopelekwa Mahakamani.

Mheshimiwa Spika, katika kukabiliana na changamoto hii, Mahakama imejiwekea mpango wake wa ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya Mahakama kwa awamu.

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Kilindi ina Mahakama za Mwanzo tatu zinazofanya kazi ambazo ni Songe, Mswaki na Kwediboma. Majengo ya Mahakama zote hizi ni ya zamani kiasi cha kuhitajika kujengwa upya, siyo kukarabatiwa. Aidha, Mahakama tatu za Kimbe, Kwekivu na Mswaki alizouliza Mheshimiwa Mbunge, majengo yake hayafanyi kazi kabisa, yamefungwa kutokana na uchakavu.

Mheshimiwa Spika, wananchi waliokuwa wanapata huduma katika Mahakama za Mwanzo za Kwekivu na Kimbe wanalazimika kufuata huduma Mahakama ya Mwanzo Songe ambako ni mbali. Mahakama ya Mwanzo Mswaki inatumia jengo la Kijiji kwa shughuli za Mahakama. Kutokana na hali hiyo, Mpango wa Serikali ni kujenga upya kabisa Mahakama hizi na siyo kufanya ukarabati.

Mheshimiwa Spika, pamoja na ukweli kwamba Mahakama zote zilizotajwa na Mheshimiwa Mbunge ni chakavu sana, lakini bado mahitaji ya Mahakama kwa nchi nzima ni makubwa na hivyo, tutaendelea na kazi ya ujenzi na ukarabati wa Mahakama za Mwanzo na Mahakama za ngazi nyingine kwa awamu kulingana na upatikanaji wa fedha.

Mheshimiwa Spika, kupitia Mpango huo, napenda kumthibitishia Mheshimiwa Mbunge kuwa Mahakama ya Mwanzo Kwekivu na Kimbe zitajengwa katika mwaka wa fedha 2020/2021.

Mheshimiwa Spika, mwisho, ninawashukuru Waheshimiwa Wabunge kwa kuendelea kushirikiana na Serikali na Mahakama na kuona umuhimu wa kuidhinisha fedha zinazohitajika kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa Mahakama zetu nchini. Ninaomba tuendelee kuona umuhimu wa mhimili huu katika utoaji wa haki nchini. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge wa Kilindi, swali la nyongeza.

**MHE. OMARI M. KIGUA:** Mheshimiwa Spika, binafsi namshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa majibu yenye ufasaha wa hali ya juu sana. Ni majibu ambayo yanatoa matumaini makubwa siyo kwa Wilaya ya Kilindi tu, lakini maeneo mengine ya Tanzania kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, pamoja na shukurani hizo, nina swali moja la nyongeza. Mheshimiwa Waziri amekiri kwamba Mahakama hizi ni chakavu na Mahakana zinazofanya kazi ni tatu tu.

Je, Mheshimiwa Waziri yuko tayari sasa kuanzisha hata Mahakama za Mwanzo *I Mean* kuanzisha hata ofisi ndogo ili huduma hii ipatikane kwa muda mfupi wakati tukisubiria ujenzi wa Mahakama hizi za Mwanzo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo kuhusu Mahakama za Mwanzo, Waziri wa Katiba na Sheria, Mheshimiwa Dkt. Mahiga, tafadhali.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nataka nitoa shukurani za pekee kwako. Jana ulikwenda kufungua Mahakama ya Wilaya ya Kondoa na ulifuatana na Jaji Mkuu. Katika hotuba yako ulidhihirisha kwamba ni jitihada za Serikali kujenga Mahakama, kuboresha Mahakama na kujenga Mahakama za karne ya 21 ambazo zina TEHAMA na vifaa vya kisasa vya kielektroniki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nataka kuwahakikishia Waheshimiwa Wajumbe kwamba kwanza kuna huu mpango mahususi wa Mahakama ya Tanzania ya kujenga Mahakama katika ngazi zote mwaka huu na mwaka ujao. Nataka kuwahakikishia kwamba kitendo cha sisi kuamua

kupeleka mashauri kutoka Mahakama hizo chakavu na kwenye maeneo ya awali na ya muda, utaendelea kuboreshwa.

Mheshimiwa Spika, nataka kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba hiyo haitasimamisha hata kidogo usikilizaji wa mashauri katika Mahakama hizo na jitihada za uboreshaji na ujenzi tutazikamilisha katika mwaka huu wa fedha na kuendelea katika mwaka ujao wa 2021. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nami niwataarifuni tu kwamba ni kweli jana nilikuwa Kondoa kwa niaba yenu kuzindua Mahakama ya Wilaya ya Kondoa. Naipongeza sana Wizara hii na Mahakama kwa ujumla. Mahakama zinazojengwa hivi sasa ni za kisasa na ni za kiwango cha juu sana cha ujenzi. Kabisa!

Tunawapongeza sana Mheshimiwa Waziri, mwendelee hivyo, lakini pia kwa niaba ya Wana-Kongwa tunashukuru kwamba kuanzia mwezi wa Tano huu Mahakama ya Kibaigwa pale itaanza kujengwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Fratei Massay Mbunge wa Mbulu, ulitaka kuuliza swali la nyongeza.

**MHE. FLATEI G. MASSAY:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Mbulu Vijijini, Mji wa Haydom hauna Mahakama na kutoka Haydom mpaka Mahakama ya Wilaya ni kilomita 86 na tunayo ahadi ya kujengewa Mahakama ya Mwanzo pale. Kutokana na Mbulu tumeshawapa eneo:-

Je, Mheshimiwa Waziri yuko tayari sasa kutenga bajeti ya kujengewa Mahakama ya Mwanzo katika Mji mdogo wa Haydom? *(Makofi)*

**SPIKA:** Majibu Waziri wa Katiba na Sheria, Mheshimiwa Dkt. Augustine Mahiga kuhusu Mji wa Haydom.

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Spika, nasema Wilaya ya Mbulu ina mahitaji mengi ya huduma, mojawapo ni Mahakama. Kwa mpango nilionyesha hapa, nitafanya ushauriano na Mahakama Kuu na Msajili wa Mahakama tuone kwamba pale Haydom tutachukua hatua gani. Ila kama iko kwenye mpango; na nadhani iko kwenye mpango, nitathibitisha, tutajitahidi kutekeleza hilo.

Mheshimiwa Spika, nataka pia nichukue nafasi kusema, kuna Mbunge alisema juzi kwamba kuna mahabusu ambao wanachukuliwa na bodaboda kutoka Magereza kwenda Mahakamani katika Gereza la Ulanga. Nimezungumza na *DPP* ambaye alikuwa kule Ulanga hivi karibuni, anasema hakuna haja ya kutumia pikipiki wala gari kupeleja mahabusu katika Mahakama ya Ulanga kwa sababu watu wanaweza kutembea siyo zaidi ya mita 500 kutoka kwenye Gereza lile mpaka kwenye Mahakama.

Mheshimiwa Spika, kama Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani alivyosema, taarifa ile ilikuwa imetiwa chumvi. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Wizara ya Maji, Mheshimiwa Susanne Peter Maselle, uliza swali lako sasa.

Na. 44

**Uhaba wa Maji – Misungwi**

**MHE. SUSANNE P. MASELLE** aliuliza:-

Bado kuna shida kubwa ya upatikanaji wa maji kwa wananchi wetu haa maeneo ya vijijini:-

Je, Serikali inatoa kauli gani kuhusukupunguza au kumaliza tatizo hilo kwa wananchi wa maeneo mbalimbali ya Misungwi?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo. Nakutambua Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, Mheshimiwa Jumaa Hamidu Aweso, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Susanne Peter Maselle, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika kukabiliana na changamoto ya maji kwa wananchi wa maeneo mbalimbali ya Misungwi, Serikali imekamilisha ujenzi wa mradi wa maji wa thamani ya shilingi bilioni 12.85 kutoka katika chanzo cha maji cha Nyahiti ambapo wakazi wapato 64,280 wanatarajia kunufaika katika mradi huo hadi kufikia mwaka 2040.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mradi huo, Serikali inatekeleza mradi mkubwa kutoka bomba kuu la usafirishaji maji la *KASHWASA* utakaohudumia vijiji 14 vya Wilaya ya Misungwi kupitia miradi mitano. Mradi wa kwanza ni kufikisha huduma ya maji Mabale – Mbarika, mradi wa pili ni kufikisha huduma ya maji Igenge, mradi wa tatu ni kufikisha huduma ya maji Mbarika – Ngaya, Mradi wa nne ni kufikisha huduma ya maji Ngaya – Matale na mradi wa tano ni kufikisha huduma ya maji Matale – Misasi. Miradi hii ikikamilka itahudumia jumla ya watu 45,788.

Mheshimiwa Spika, aidha, Serikali imeanza kutekeleza miradi katika vijiji vitano vya Kata ya Shilalo kupitia Programu ya Malipo kwa Matokeo, inayofadhiliwa na Benki ya Dunia. Miradi hiyo ikikamilika itahudumia watu wapatao 15,500. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Susanne nimekuona, uliza swali la nyongeza.

**MHE. SUSANNE P. MASELLE:** Mheshimiwa Spika, nina maswali mawili ya nyongeza. Mheshimiwa Waziri amesema kwamba mradi wa kutoka Nyahiti umekamilika, siyo kweli, nilikuwa huko juzi. Mradi huo hautoi maji na Mkandarasi hayuko *site* na hili lilikuwa ni agizo la Mheshimiwa Rais kwamba miradi kama hii yote ikamilike na ifanye kazi. Sasa atuambie, Wizara imekaidi agizo la Mheshimiwa Rais? Je, ni lini wananchi wa Misungwi watapata maji ya uhakika ? Ukizingatia wako karibu kabisa na Ziwa?

Mheshimiwa Spika, swali la pili. Mwishoni mwa mwaka 2019 Serikali iliweka miundmbinu katika Kata ya Shibula na Bugogwa katika Jimbo la Ilemela, lakini maji hayatoki na yakitoka yanakuwa yanatoka kwa kusuasua na pia yanatoka machafu sana…

**SPIKA:** Mheshimiwa Susanne unahutubia badala ya kuuliza swali.

**MHE. SUSANNE P. MASELLE:** Mheshimiwa Spika, najenga hoja.

**SPIKA:** Aaah, uliza swali.

**MHE. SUSANNE P. MASELE:** Mheshimiwa Spika, ni lini sasa wananchi wa maeneo hayo watapata maji ya uhakika ili waweze kufaidi miradi hiyo? Ahsante.

**SPIKA:** Ahsante sana umeeleweka. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi na hasa baada ya kuwa umeshapata mambo haya kutoka kwa Mheshimiwa Mbunge mwenyewe wa Misungwi.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji, kwanza napenda kumfahamisha ndani ya wiki mbili nilikuwa katika Jimbo la Misungwi, nilikuwa na Mheshimiwa Mbunge na tumefanya kazi kubwa. Changamoto iliyokuwepo pale ilikuwa ni Mkurugenzi wetu wa Maji. Tumemwondoa na mradi huu mkubwa utasimamiwa na Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira MWAWASA katika kuongeza utendaji. Mradi umekamilika kwa zaidi ya shilingi bilioni 12 katika kuhakikisha wananchi wa Misungwi wanapata huduma ya maji.

Mheshimiwa Spika, katika eneo la Ilemela pamoja na Nyamagana yake tuna mradi zaidi ya bilioni 38 tunatekeleza katika kuhakikisha wananchi wa Nyamagana pamoja na Ilemela wanapata huduma ya maji na nilikuwepo na Waheshimiwa Wabunge na wanafanya kubwa na nzuri na tumemwagiza Mkandarasi, kabla ya mwezi wa Tatu mradi uwe umekamilika na tutakwenda kuuzindua katika wiki ya maji. Kama tulivyosema, wiki ya maji haitokuwa wiki ya mapambio, wiki ya maji itakuwa ni kazi ya kuzindua miradi mbalimbali ya maji ikiwemo na Nyamagana. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa, karibu robo ya Bunge limesimama. Sasa sijui itakuwaje! Basi naona nichukue nyuma kabisa kule kwa Mheshimiwa Stanslaus Mabula, uliza swali lako, nirudishe swali Kanda ya Ziwa.

**MHE. STANSLAUS S. MABULA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwanza, naipongeza sana Serikali kwa miradi mikubwa ya maji ambayo inatekelezwa kwenye Mkoa wa Mwanza likiwemo Jimbo la Nyamagana na hakika ikikamilika miradi hii itakuwa suluhisho kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali langu dogo la nyongeza kwa Mheshimiwa Waziri, tunao mradi kwenye Kata ya Lwanima wa ujenzi wa tenki la karibia lita 450,000. Ni takribani miaka mitatu sasa na changamoto ni malipo ya *certificate* ya mwisho hayajalipwa mpaka leo. Ni nini kauli ya Serikali kwa watu wa Lwanima ambao mradi huu na tenki hili lenye matoleo zaidi ya 17 katika kila Mtaa? Ni lini fedha hizi zitatoka ili wakazi wa Lwanima waweze kupata maji ya uhakika na salama?

**SPIKA:** Ahsante sana. Majibu kwa kifupi, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, Mheshimiwa Aweso, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji kwanza nipende kumpongeza na nithaminishe kazi kubwa anayoifanya Mheshimiwa Mbunge katika Jimbo lake la Nyamagana, lakini kikubwa maji ni uhai. Ninachotaka kumhakikishia, sisi kama Viongozi wa Wizara hatutakuwa kikwazo kwa Wakandarasi ambao wamefanya kazi yao thabiti kabisa na yenye weledi kuhakikisha kwamba tunawalipa kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, nataka nimhakikishie, katika mfuko huu tutalipa ili mradi ule ukamilike na wananchi wake waweze kupata huduma hii muhimu ya maji. *(Makofi)*

**SPIKA:** Nilikuona Mheshimiwa Dkt. Mary Nagu, swali fupi la nyongeza.

**MHE. DKT. MARY M. NAGU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Wilaya ya Hanang ni moja yenye Wilaya yenye taabu sana ya maji, lakini naishukuru Serikali kwa kazi ambayo tayari imefanyika, lakini bado taabu iko pale pale.

Mheshimiwa Spika, Wakala wa Visima alikuja kule na mashine ndogo akashindwa kuchimba visima. Je, Mheshimiwa Waziri anasemaje? Wakala huyu atarudi lini ili achimbe vile visima ambavyo tulikuwa tunajua watavichimba? Ahsante tena. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Majibu Mheshimiwa Naibu Waziri, Wakala anarudi lini kule Hanang?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kiufupi tu nimwambie mama yangu kwamba, tutawatuma haraka ili kuhakikisha wanakwenda kuchimba visima hivi ili wananchi waweze kupata huduma ya maji, hususan Gehandu.

**SPIKA:** Ahsante. Tunaendelea na swali linalofuata la maji pia, linaulizwa na Mheshimiwa Felster Bura.

Na. 45

**Mahitaji Makubwa ya Maji Safi na Salama – Dodoma**

**MHE. FELISTER A. BURA** aliuliza:-

Kutokana na Serikali kuhamia Dodoma, mahitaji ya maji safi na salama yamekuwa makubwa na kwa sasa mgao wa maji kwa wakazi wa Dodoma umeshaanza:-

Je, Serikali ina mpango gani mahsusi wa kuhakikisha wakazi wa Dodoma wanapata maji safi na salama?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo muhimu sana kwa wananchi wa Mkoa wa Dodoma kuhusiana na shida ya maji, Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Felister Aloyce Bura, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, chanzo kikubwa cha uzalishaji maji kwa matumizi ya wakazi wa Jiji la Dodoma ni visima virefu vilivyochimbwa katika Bonde la Makutopora eneo la Mzakwe. Kuna jumla ya visima vya uzalishaji maji 24 na visima vitano vya kuchunguza mwenendo wa maji ardhini *(observation boreholes)* vimechimbwa katika bonde hilo. Uwezo wa visima vilivyopo Mzakwe kwa sasa pamoja na uwezo wa usafirishaji wa maji ni mita za ujazo 61,500 kwa siku.

Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha huduma ya maji inakuwa ya uhakika, Serikali kupitia Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Jijini Dodoma, imeongeza chanzo kingine cha

maji eneo la Ihumwa chenye uwezo wa kuzalisha maji mita za ujazo 2,773 kwa siku. Chanzo hiki kina visima nane na kinahudumia Mji wa Serikali uliopo Mtumba pamoja na Kijiji cha Ihumwa.

Mheshimiwa Spika, ili kuendelea kuboresha huduma ya maji, kwa mpango wa muda mfupi Serikali inaendelea na utafiti wa maji chini ya ardhi na uchimbaji wa visima virefu katika Mitaa ya Ntyuka, Michese na Nala na uendeshaji wa visima nane katika Mji wa Chamwino. Mpango wa muda wa kati wa ujenzi wa Bwawa la Maji la Farkwa litakalotumika kama chanzo cha nyongeza cha majisafi katika Jiji la Dodoma.

**SPIKA:** Mheshimiwa Bura, swali la nyongeza.

**MHE. FELISTER A. BURA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza. Pamoja na shughuli nyingi za maendeleo zinazofanywa na Serikali ya Awamu ya Tano, naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza, wawekezaji wengi wameamua kuja Dodoma na Serikali yenyewe inakuja Dodoma na vyuo vikuu vingi vinajengwa Dodoma, hasa maeneo ya Nala; na kwa kuwa, maeneo ya pembezoni kama vile Bahi, Wilaya ya Chamwino na maeneo mengine yanahitaji maji kwa ajili ya wawekezaji, je, Serikali iko tayari kuhakikisha kwamba, hao wawekezaji na wananchi wanaozunguka maeneo hayo hawakosi maji kwa ajili ya matumizi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili; kwa kuwa, maji ya Ziwa Victoria yameshaletwa mpaka Nzega na kuna taarifa hayo maji yanakuja mpaka Igunga. Je, Serikali haioni kwamba, suluhu ya kudumu kwa ajili ya mahitaji ya Dodoma ni kuleta maji ya Ziwa Victoria ambayo yatasaidia pia Mkoa wa Singida na Dodoma? *(Makofi)*

**SPIKA:** Nilitulia kidogo kusudi Mheshimiwa Naibu Waziri ulipate hilo; maji ya Ziwa Victoria yafike Dodoma, swali muhimu. Naomba majibu Mheshimiwa. *(Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, naomba nimpongeze mama yangu Mheshimiwa Felister Bura amekuwa mpiganaji mkubwa sana, hususan kwa changamoto ya maji katika Mkoa wa Dodoma.

Mheshimiwa Spika, kikubwa ambacho nataka niwahakikishie wakazi wa Dodoma kupitia uongozi mahiri wa kiongozi wetu wa Wizara ya Maji, Profesa Makame Mbarawa, tumekwishaliona hilo. Moja kuwaagiza *DUWASA* katika kuhakikisha kwenye makusanyo yao ya ndani asilimia 30 wahakikishe wanachimba visima virefu maeneo ya pembezoni ili wananchi wa Dodoma waweze kupata huduma ya maji.

Pili, mpaka sasa tumekwishalipa fidia katika Bwawa la Farkwa kwa wananchi wale ili tuweze kujenga Bwawa la Farkwa. Katika kuhakikisha tunaondoa kabisa tatizo la maji katika Mkoa huu wa Dodoma tumeshaanza kuanzisha timu ya kufanya *study* ya namna gani ya kuanzisha *standard gauge* kubwa katika miradi yetu ya maji. Moja ni katika kuhakikisha tunaandaa *standard gauge* ya kuyatoa maji Ziwa Victoria hadi kuyaleta hapa Dodoma. Subira yavuta heri. Heri itapatikana katika kuhakikisha kwamba, Mradi wa Ziwa Victoria unafikisha maji hapa Dodoma. Ahsante sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Esther Matiko.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Wananchi wa Mji wa Tarime wameendelea kupata adha kubwa ya maji safi na salama na hasa upatikanaji wake. Kupitia Bunge hili nimeshauliza maswali mengi sana na kuchangia na Serikali ikaahidi kwamba, itatoa suluhisho la muda mfupi la kuchimba visima 23 kandokando ya Mji wa Tarime kuweza kuboresha Mradi wa Gamasara na Bwawa la Nyanduruma, lakini zaidi kwenye bajeti iliyopita

waliahidi Mradi wa Ziwa Victoria ambao unatokana na mkopo kutoka India kwamba, unaenda kuanza ambao ni suluhisho la muda mrefu.

Sasa napenda kupata majibu kutoka kwa Naibu Waziri, ni lini sasa hii miradi yote inaenda kutengemaa ili wananchi wa Mji wa Tarime waweze kupata maji safi na salama?

**SPIKA:** Maji Tarime, Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, dada yangu Esther Matiko kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, tulikuwa tuna Mradi pale wa Gamasara ulikuwa ukifanya kazi kwa kusuasua, nilifika na tumechukua hatua kubwa ya kushughulikiana na yule mkandarasi. Wiki hii tunafunga pampu ili kuhakikisha wananchi wale wanapata huduma hii ya maji, lakini tunatambua kabisa Mkoa wa Mara ni maeneo yenye changamoto.

Mheshimiwa Spika, tumepata fedha takribani kwa mikoa 17 mmojawapo ukiwa Mkoa wa Mara na tumekwishatuma fedha zaidi ya Sh.8,345,000,000. Katika jimbo lake mpaka sasa tumekwishatuma pesa zaidi ya Sh.1,345,000,000, hizo fedha ni kwa ajili ya utekelezaji. Kwa hiyo, hizo fedha ziende zikatumike katika kuhakikisha zinachimba visima katika maeneo yenye changamoto ili wananchi wake waweze kupata huduma ya maji.

Mheshimiwa Spika, pia katika kuhakikisha tunatatua kabisa tatizo la maji Rorya pamoja na Tarime ni moja ya maeneo ambayo tumeyaweka katika miji 28 kupitia fedha za India. Tunasubiri kibali kutoka *Exim Bank* ili tuweze kutangaza tenda kwa ajili ya kuwapata wakandarasi na Mradi ule mkubwa wa kuyatoa maji Ziwa Victoria ili wananchi wa Tarime waweze kupata huduma ya maji. Ahsante sana.

**SPIKA:** Waheshimiwa nawaona jinsi ambavyo masuala ya maji yanawagusa. Mheshimiwa Naibu Waziri hebu *scan* tu kidogo uangalie uone jinsi ambavyo shida ya maji bado kubwa pamoja na juhudi mnayoifanya; kwa kweli, muda hautoshi Waheshimiwa nawaomba mkubali tu kwamba, tuendelee, nawaona, lakini sasa muda.

Twende Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano. Swali la Mheshimiwa Dadi Chikota, Mbunge wa Nanyamba, uliza swali lako Mheshimiwa Chikota, tafadhali.

Na. 48

**Barabara ya Mtwara – Newala – Masasi**

**MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA** aliuliza:-

Ujenzi wa Barabara ya Mtwara – Newala – Masasi (kilometa 210) umeanza kwa kiwango cha lami kutoka Mtwara hadi Mnivata (kilometa 50).

Je, Serikali ina mpango gani kwa kilometa 160 zilizobaki?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Mheshimiwa Elias Kwandikwa, tafadhali.

**WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Abdallah Dadi Chikota, Mbunge wa Nanyamba, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa barabara yote ya Mtwara – Nanyamba – Tandahimba – Newala – Masasi, kilometa 210, pamoja na Daraja la Mwiti ulikamilika mwaka 2015. Mpango wa Serikali ni kujenga barabara yote kwa kiwango cha lami kwa awamu. Awamu ya kwanza inahusisha sehemu ya Mtwara – Mnivata, kilomita 50, ambayo utekelezaji wake hadi kufikia Desemba, 2019 ulikuwa asilimia 76. Jumla ya shilingi bilioni 3.4 zimetengwa katika mwaka wa fedha 2019/2020 kwa ajili ya kuendelea na ujenzi.

Mheshimiwa Spika, ujenzi kwa kiwango cha lami kwa kilometa 160 zilizobaki pamoja na Daraja la Mwiti utaanza katika mwaka wa fedha 2020/2021.

**SPIKA:** Mheshimiwa Chikota.

**MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza, kama alivyosema kwenye jibu lake la msingi kuna kiasi cha fedha kimetengwa katika bajeti ya 2019/2020; na kwa kuwa, barabara iliyojengwa kwa sasa imeishia Mnivata na kutoka Mnivata hadi Nanyamba ni kilometa 20; na kwa kuwa, kuna mkandarasi yuko pale.

Je, ni kwa nini sasa, bila kuathiri taratibu za manunuzi, kipande hicho asingepewa mkandarasi ili ajenge kwa kiwango cha lami hadi Nanyamba Mjini?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, Barabara ya Mtwara – Nanyamba – Masasi kuna barabara pacha tunaita Barabara ya Ulinzi ambayo inakwenda mpaka Mahurunga, Kitaya, Mnongodi na Michenjele. Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga barabara hii kwa kiwango cha lami, ukizingatia sasa hivi kuna changamoto ya kiulinzi kati ya Tanzania na Msumbiji?

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Mheshimiwa Kwandikwa, tafadhali.

**WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA):** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Chikota, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza uniruhusu nimshukuru sana na kumpongeza Mheshimiwa Chikota kwa ushirikiano. Kwa kweli, mara zote nimefanya ziara mara nyingi sana kukagua barabara hii Mtwara – Mnivata, lakini muda wote Mheshimiwa Chikota alikuwepo na tumefanya kazi kwa pamoja. Kwa hiyo, Mheshimiwa Chikota namshukuru sana.

Mheshimiwa Spika, niseme tu kama ambavyo nimetoa jibu langu la msingi kwamba, harakati za ujenzi kwa maana ya shughuli za manunuzi zinaendelea ili kujenga kilometa 160 ambazo zimebakia. Kwa hiyo, Mheshimiwa Chikota anafikiria kwamba, ili twende haraka ni kumruhusu mkandarasi aendelee kwa vile tulivyotenga fedha kidogo, lakini nimwombe Mheshimiwa Chikota avute subira na sisi mpango wetu ni kuhakikisha kwamba, tunafanya ujenzi wa haraka, ili wananchi wake kwenye Vijiji vya Malanje, Mnivata, Nanyamba, Mtimbwilimbwi, Mbambakofi, Mtopwa na majirani wa Tandahimba, Newala na kule Lulindi na Masasi waweze kupata huduma hii nzuri ya barabara.

Kwa hiyo, avute subira kwa sababu ziko taratibu za manunuzi zinafuatwa, sasa mkandarasi huyu kama ataomba na atakuwa na sifa basi anaweza akapewa, ili aanze kukamilisha upande ambao ameutaja.

Mheshimiwa Spika, kuhusu barabara pacha, hii barabara ya ulinzi kilometa 310; nimeitembelea baadhi ya maeneo katika sehemu hii ili kuona kwamba, tunafanya maboresho makubwa katika maeneo ambayo ni korofi, maeneo ambayo yanahitaji madaraja na makalavati. Kwa hiyo, cha kwanza ni kuhakikisha kwamba, tunaifanyia maboresho makubwa barabara hii kuhakikisha inapitika, kwa sababu ni muhimu sana katika shughuli za uchumi, lakini na za ulinzi.

Mheshimiwa Spika, sasa tutakwenda kwa kufuata vipaumbele. Tukimaliza barabara hii ambayo nimeitaja tutakwenda kuitazama sasa Barabara ya Ulinzi, ili iweze kuwasaidia wananchi wanaoishi maeneo haya. Ahsante sana.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge kwa sababu ya muda tuendelee na maswali ya Wizara ya Kilimo. Mheshimiwa Joel Mwaka Makanyaga, Mbunge wa Chilonwa, naomba uulize swali lako sasa.

Na. 46

**Mabwawa ya Umwagiliaji Yaliyopungua Kina Jimbo la Chilonwa**

**MHE. JOEL M. MAKANYAGA** aliuliza:-

Je, Serikali inatoa kauli gani juu ya mabwawa ya zamani yanayotumika katika kilimo cha umwagiliaji ambayo yamepungua kina na kushindwa kuwasaidia wananchi hususan Mabwawa ya Kijiji cha Buigiri, Kijiji cha Chalinze na Kijiji cha Izava?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, Mheshimiwa Omary Mgumba, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO (MHE. OMARY T. MGUMBA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Joel Mwaka Makanyaga, Mbunge wa Jimbo la Chilonwa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Bwawa la Buigiri ambalo lipo katika Kata ya Buigiri lilijengwa mwaka 1960 likiwa na uwezo wa kumwagilia hekta 40 na kunyweshea mifugo. Bwawa hilo limekuwa likijaa mchanga na tope kutokana na mafuriko na hivyo kupungua kwa kina cha maji. Pamoja na Serikali kukarabati bwawa hilo katika kipindi cha mwaka 2005 na mwaka 2009 kwa kuongeza kina kwa mita moja bado bwawa hilo liliendelea kujaa mchanga na tope kutokana na shughuli za kibinadamu zinazofanyika juu ya bwawa na kusababisha mchanga na tope kujaa bwawani. Tathmini iliyofanyika mwaka 2012 ilionesha kuwa bwawa hilo linahitaji ukarabati wa sehemu ya kutoroshea maji na kunyanyua tuta ili kuongeza kina kwa gharama ya Shilingi milioni 475.

Mheshimiwa Spika, bwawa la pili Bwawa la Ikowa lililopo katika Kijiji cha Chalinze na Ikowa lilijengwa mwaka 1959 kwa ajili ya kupata maji ya mifugo na kumwagilia jumla ya hekta 96 kati ya hekta 220 katika Skimu ya Chalinze. Kutokana na mabadiliko ya tabianchi na shughuli za kibinadamu katika maeneo hayo, bwawa hilo limekuwa likijaa mchanga na tope kila msimu wa mvua na hivyo kusababisha athari katika tuta na kupungua kwa kina cha maji katika bwawa hilo. Tathmini iliyofanyika mwaka 2012 ilibaini kuwa zinahitajika shilingi bilioni 1.2 kwa ajili

ya ukarabati wa bwawa na kunyanyua tuta ili kuongeza kina cha bwawa na hivyo kuwezesha kumwagilia hekta 220 katika Skimu ya Chalinze.

Mheshimiwa Spika, bwawa la tatu ni Bwawa la Izava lilijengwa miaka ya 1972/1973 kwa ajili ya mifugo na kilimo cha umwagiliaji. Pamoja na changamoto ya kujaa mchanga na matope bwawa hilo limeendelea kutoa huduma kwa wananchi hadi mwaka 2015 ambapo kupitia Mradi wa *TASAF* ililikarabati pamoja na kushirikiana na wananchi kupitia utaratibu wa kufanya kazi za kujitolea na kutumia kiasi cha Sh.7,418,000 kuwalipa wananchi hao. Mwaka 2017/2018, wakati wa mvua za msimu, kingo za bwawa hilo zilibomoka na hivyo kushindwa kutunza maji kwa ajili ya kilimo.

Mheshimiwa Spika, Serikali itatuma timu ya wataalam kwa ajili ya kufanya usanifu wa kina ili kubaini mahitaji halisi ya ujenzi wa mabwawa hayo kwa wakati huu. Aidha, Serikali inashauri wananchi wanaoishi kwenye maeneo ya vyanzo vya maji na na upande wa juu wa bwawa kuacha kufanya shughuli za kibinadamu ili kuboresha mazingira yao na kutatua changamoto za kujaa mchanga na tope ziweze kupata ufumbuzi wa kudumu.

**SPIKA:** Ahsante sana. Majibu yalikuwa marefu kweli. Mheshimiwa Mbunge Makanyaga, uliza swali lako.

**MHE. JOEL M. MAKANYAGA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Pia nashukuru sana kwa majibu mazuri ya Serikali yaliyotolewa hivi punde, lakini pamoja na majibu hayo mazuri naomba niwe na maswali mawili madogo ya nyongeza. Swali la kwanza, Mheshimiwa Waziri amesema Serikali itapeleka wataalam kwa ajili ya kuyachunguza mabwawa hayo waone nini cha kufanya. Je, ni lini Serikali itapeleka wataalam hawa ili wakafanye kazi hiyo ikizingatiwa kwamba, mabwawa haya ni muhimu sana katika kukuza uchumi wa mwananchi mmoja mmoja na uchumi wa Taifa kwa jumla?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, baada ya bwawa la Izava kubomoka mwaka 2017/2018, inaonekana baada ya maji kupita kwa misimu miwili ule mchanga na tope lote lililokuwa limejaa pale chini limeondoka. Je, Serikali haioni pengine hii inaweza kuwa ni muarobaini kwa maana ya dawa ya kuyasafisha mabwawa yetu yaliyojaa tope wakafanya hivyo kwa mabwawa yote ambayo yana matatizo ya tope hapa nchini? Ahsante sana.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Mbunge. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu kwa kifupi, tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO (MHE. OMARY T. MGUMBA):** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Joel Mwaka, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, swali lake la kwanza kwa umuhimu wa kilimo na umuhimu wa wananchi wa Chilonwa, Serikali kwamba, inachukua nafasi hii kuwaelekeza wataalam wa umwagiliaji Kanda ya Dodoma, hususan wa Halmashauri ya Chamwino waende kuanzia kesho kufanya tathmini na kuangalia uharibifu wa mabwawa hayo, ili kuishauri Serikali na kuanza haraka sana kuyaboresha mabwawa hayo ili kuimarisha kilimo cha uhakika katika wilaya hiyo.

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili anasema kwamba, bwawa hili la Izava lilipobomoka maji kwa miaka hii mitatu yamesafisha tope lote. Nimwombe tu Mheshimiwa Mbunge awe na subira, kwa sababu tunapeleka wataalam hivi karibuni kuanzia kesho. Acha waende watathmini halafu watuletee majibu sahihi ya kitaalam, baada ya hapo Serikali itaona ni njia gani nzuri ya kufanya, kwa sababu hii njia ni kutokana na ajali ya mafuriko hatuwezi kusema ikawa ndio njia mbadala sasa ya kusafisha mabwawa yetu yote nchini.

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, kuhusiana na masuala ya mabwawa maji yanayopita kati ya Gairo na Kibaigwa, eneo linaitwa Silwa ni mengi mno na eneo kati ya Kibaigwa na Mtanana kwa kila anayepita kwa gari nafikiri anajionea mwenyewe jinsi ambavyo maji ni mengi sana yanayohitaji mabwawa makubwa katika maeneo hayo.

Kwa hiyo, ningeomba Wizara ya Kilimo muangalie jambo hilo na mlipe nafasi ya kujengwa kwa mabwawa mapya katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Ahmed Ali Salum, Mbunge wa Solwa, bado tuko Wizara ya Kilimo, kwa niaba yake, nakuruhusu Mheshimiwa Lucy.

Na. 47

**Kukamilisha Ujenzi wa Bwawa la Ushololo na Misengwa Katika Kata za Usule na Misengwa**

**MHE. LUCY T. MAYENGA (K.n.y. MHE. AHMED A. SALUM)** aliuliza:-

Bwawa la Ishololo katika Kata ya Usule na Misengwa katika Kata ya Musengwa ni mabwawa ambayo ujenzi wake haujakamilika kwa muda mrefu sasa; na kwa kuwa, tumeshaomba maombi maalum ili tupate fedha za kukamilisha miradi hii miwili:-

Je, Serikali inatoa tamko gani katika kukamilisha miradi hii?

**SPIKA:** Ahsante. Majibu ya maswali hayo, likiwemo Bwawa la Ishololo na Usule.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO (MHE. OMARY T. MGUMBA)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ahmed Ally Salum, Mbunge wa Jimbo la Solwa, lenye sehemu kuu mbili kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Skimu ya Masengwa yenye eneo la ukubwa wa hekta 325 ilijengwa chini ya mradi shirikishi wa kuendeleza kilimo cha umwagiliaji mwaka 2004 kwa ujenzi wa banio na mfereji. Hata hivyo, skimu hiyo inakabiliwa na changamoto ya ukosefu wa maji ya umwagiliaji hususan kipindi cha kiangazi.

Mheshimiwa Spika, kutokana na changamoto hiyo, katika mwaka 2007/2008, Ofisi ya Umwagiliaji Kanda ya Mwanza ilifanya upembuzi wa awali na kupata sehemu ya kujengea bwawa. Katika mwaka wa fedha 2020/2021 Serikali imetenga fedha kwa ajili ya kupitia upya upembuzi wa awali na kufanya upembuzi wa kina wa Mradi wa Umwagiliaji wa Masengwa utakaohusisha ujenzi wa bwawa ili kupata gharama halisi ya ujenzi kwa sasa. Serikali itaendelea kutafuta fedha kutoka vyanzo mbalimbali kwa ajili ya ujenzi wa bwawa mapema iwezekanavyo katika mradi wa umwagiliaji Masengwa baada ya kazi ya upembuzi yakinifu kukamilika.

Mheshimiwa Spika, Mradi wa ujenzi wa Bwawa wa Ishololo uliopo katika Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga Vijijini ni mojawapo ya miradi iliyokuwa ikitekelezwa kupitia Mradi wa Uwekezaji katika Kilimo katika Wilaya yaani *DASIP*. Miradi hiyo ilikuwa inagharamiwa kwa pamoja na Serikali ya Tanzania na Benki ya Maendeleo ya Afrika kuanzia mwaka 2006/2007 hadi mwaka 2013/2014 ambapo jumla ya shilingi Tshs. 572,552,001.79 zilitumika kwa ajili ya ujenzi wa Tuta la Bwawa ambao ulifikia asilimia 26.

Mheshimiwa Spika, kutokana na mradi huo kutokamilika kwa wakati, Wizara katika mwaka 2016 ilipitia upya mpango kabambe wa kuendeleza kilimo cha umwagiliaji ambapo

mradi huo ni mojawapo ya miradi kabambe itakayotekelezwa katika Awamu ya Kwanza. Aidha, Serikali itatuma timu ya wataalam kufanya tathmini ya mahitaji na gharama za kuendeleza mradi huo kwa sasa ili kuanza ujenzi wa mradi huo ikiwemo ujenzi wa bwawa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Lucy Mayenga.

**MHE. LUCY T. MAYENGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwanza kabisa ninaomba niipongeze sana Serikali kwa hatua yake ya kuamua sasa kutuma timu ya Wataalamu kufanya tathmini ili kuweza kuendeleza Bwawa hili lakini nilikuwa naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa hawa Wakandarasi katika nchi nzima wako Wakandarasi ambao wamekuwa wakijenga Mabwawa na wengine wamekuwa wakitudhalilisha na kutusababishia matatizo na kusababisha pesa nyingi za Wananchi na pia vilevile pesa kutoka kwa Wafadhili kuonekana kwamba ni nchi ambayo ni kama vile kuidhalilisha nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wamekuwa wanajenga vitu ambavyo haviko katika viwango na wengine wamekuwa wakishindwa kumaliza,

Je, Serikali iko tayari sasa kufanya tathmini nyingine upya ili hawa Wakandarasi ambao baadhi yao wakiharibu Mkoa mmoja anaenda kwenye Mkoa mwingine waweze kuchukuliwa hatua ikiwemo kushindwa kabisa kupewa kazi na ikiwezekana kutokupewa kazi kabisa katika nchi ya Tanzania ili kuendeleza heshima tuliyonayo kama nchi na kuweza kulinda pesa za wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili, Mheshimiwa Waziri nilikuwa naomba kabla ya tathmini je Mheshimiwa Waziri yuko tayari kuambatana na mimi kuweza kujionea kwa macho yake athari zilizoko pale katika eneo lile ambalo limesababisha kwa kiwango kikubwa wakinamama wanapata shida walikuwa wanalima lakini sasa hivi hawalimi maji walikuwa wanapata eneo la karibu lakini sasa imekuwa wanapata eneo la mbali, ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Lucy, nakushukuru sana, ahsante. Mheshimiwa Omary Mgumba Naibu Waziri majibu kwa kifupi sana kwa sababu ya muda tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO (MHE. OMARY T. MGUMBA)** Mheshimiwa Spika, kwanza naomba unipe nafasi nimpongeze Mheshimiwa Lucy kwa jinsi anavyowapigania Wakulima wote wa Mkoa wa Shinyanga na akishirikiana na Mbunge wa Jimbo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali lake la kwanza, kwanza Serikali tuko tayari na tulishaanza kufanya tathmini ya kina na ndiyo maana tuwaarifu Waheshimiwa Wabunge wanaona Miradi mingi ya Umwagiliaji imechelewa kupelekewa fedha kwa sababu Serikali tumejipa jukumu la kupitia Miradi yote ili kubaini ubadhirifu na jinsi ya kutathmini thamani ya fedha ya Miradi hiyo kabla hatujaanza kupangia fedha nyingine kwa ajili ya kuendelea.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, zoezi hilo la kudumu na tutaendelea na Miradi yote Tanzania kabla hatujaanza kuipatia fedha nyingine. Swali lake la pili, niko tayari kuambatana na yeye baada ya Bunge hili nitaanzia Mkoa wa Shinyanga kwenda kutembelea Mradi huo ili kubaini changamoto hizo tuweze kutafutia ufumbuzi.

**SPIKA:** Kabla hamjaambatana mtaomba Kibali cha Spika eheh? *(Kicheko/Makofi)*

Tunakwenda Wizara ya Madini Mheshimiwa Hussein Nassor Amar Mbunge wa Nyang'hwale, Mheshimiwa Amar tafadhali.

Na. 49

**Kurasimisha Maeneo ya Wachimbaji Wadogo Nyang'hwale**

**MHE. HUSSEIN N. AMAR** aliuliza:-

Katika Jimbo la Nyang'hwale kuna maeneo mengi sana ya Wachimbaji wadogo wa madini ya Dhahabu kama vile Isakeli, Isonda, Lyulu, Nyamalapa, Lubando, Shibalanga na Kasubuya ambayo Wachimbaji hao wanafanya kazi na Dhahabu inapatikana bila utaratibu wowote?

(a) Je, ni lini Serikali itayarasimisha maeneo hayo na kuyagawa kwa Wachimbaji ili watambulike Kisheria na iwe rahisi kwa Serikali kukusanya kodi?

(b) Je, ni lini Serikali itatimiza ahadi yake iliyoitoa mbele ya Waziri Mkuu ya kulitoa eneo la Bululu kwa Wachimbaji wadogo?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri Madini, Mheshimiwa Stanslaus Nyongo karibu tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Madini napenda kujibu swali la Mheshimiwa Hussein Nassor Amar Mbunge wa Nyang'wale lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Madini imedhamiria kuwaendeleza wachimbaji wadogo nchi nzima kwa kuwapatia maeneo ya uchimbaji ili waweze kuchangia uchumi kwa kulipa kodi, kujiajiri na kuongeza kipato cha Taifa.

Mheshimiwa Spika, Kampuni ya Nyanzaga *Mining Co. Ltd* iliyokuwa ikimiliki leseni ya utafiti Na. PL 9662 ya mwaka 2014 iliachia eneo lake lenye ukubwa wa eka 70 katika eneo la Bululu wilayani Nyang'hwale. Aidha, eneo hilo limegawiwa kwa vikundi 22 vya uchimbaji wa madini ya dhahabu ambapo Tume ya Madini ilitoa leseni hizo tarehe 30 mwezi wa kumi na mbili mwaka 2019.

Mheshimiwa Spika, Eneo la Lubando lilikuwa na leseni ya uchimbaji wa kati wa Kampuni ya Busolwa *Mining Co. Ltd*. Hata hivyo, leseni hiyo ilifutwa na Serikali na kupewa wachimbaji wadogo. Aidha, eneo la Lyulu bado lina maombi ya leseni ya uchimbaji wa kati wa Kampuni ya Busolwa *Mining Co. Ltd*.

Mheshimiwa Spika, Wizara kwa kushirikiana na Tume ya Madini inaendelea na juhudi zake za kutafuta maeneo mengine kwa ajili ya wachimbaji wadogo ambapo Tume ya Madini imewataka wamiliki wote wa leseni kubwa za utafiti kutimiza matakwa ya sheria vinginevyo maeneo yao yatafutwa kwa mujibu wa Sheria ya Madini ya Mwaka 2010 na kupewa wachimbaji wadogo. Mwisho, Naomba kutoa wito kwa wamiliki wa leseni za utafiti wote nchini uchimbaji na wafanyabiashara wote wa madini kuendelea kuzingatia sheria za madini ikiwa ni pamoja na kuuza madini kwenye masoko yaliyofunguliwa nchini kote.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge wa Nyang'hwale swali fupi la nyongeza.

**MHE. HUSSEIN N. AMAR:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwanza nianze kumpongeza Mheshimiwa Rais wetu Dkt. John Pombe Magufuli pamoja na Waziri na Naibu Waziri na Watendaji wote wa Wizara kwa kutoa leseni 22 kwa wachimbaji wadogo wa Wilaya ya Nyang'hwale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali kwa kuwa Wachimbaji wengi bado wako maeneo mbalimbali katika Wilaya ya Nyang'hwale kama vile Isekeli, Isonda, Lyulu, Nyamalapa, Ifungandi, Shibalanga pamoja na Kasubuya, Je, Wizara imejipanga vipi kuwapa tena maeneo hayo wale Wachimbaji wadogo.

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kwa kuwa Serikali imeshatoa leseni kwa Wachimbaji wadogo eneo la Bululu hivi karibuni uzalishaji wa dhahabu nyingi zitaanza kutoka lakini kuna jengo ambalo liko tayari kwa ajili ya ununuzi wa dhahabu. Je Serikali iko tayari sasa kukamilisha vibali vyote ili kufungua Jengo hilo la ununuzi wa dhahabu Wilaya ya Nyang'hwale? *(Makofi)*

**SPIKA:** Majibu kwa kifupi Mheshimiwa Naibu Waziri tafadhali, Mheshimiwa Nyongo.

**NAIBU WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa katika majibu ya swali la msingi sisi kama Wizara ya Madini kwa kupitia Tume ya Madini tunaendelea kuhakikisha kwamba yale maeneo yote tunayoyaona kwamba yana madini ambayo wachimbaji wadogo wanaweza wakachimba basi sisi hatuhusiki kabisa kuwapa wachimbaji wadogo na kuchimba na hata katika majibu yangu ya msingi nimetoa wito kwa wale Wamiliki wote wanaomiliki maeneo makubwa ya utafiti na hawayaendelezi yale maeneo na utafiti hauendelei.

Mheshimiwa Spika, sisi kama Serikali tuko tayari kuyafuta maeneo hayo, kufuta leseni hizo za utafiti na kuwapa wachimbaji wadogo ili waweze kuchimba, waweze kulipa Kodi na wao wenyewe waweze kujikimu katika maisha yao. Vilevile niendelee kumshukuru sana Mbunge kwa jinsi anavyofatilia na jinsi anavyokuwa karibu na wachimbaji wadogo katika Jimbo lake kwa sababu tunatambua Jimbo lake lina wachimbaji wadogo wengi sana.

Mheshimiwa Spika, nimuhakikishie katika swali lake la pili ameuliza utayari wa sisi Wizara na Tume ya Madini kuanzisha soko kwa ajili ya kuuza madini katika Jengo ambalo liko tayari nimueleze tu Mheshimiwa Mbunge sisi tuko tayari na sasa hivi nawaagiza Tume ya Madini waende katika Jengo hilo wakague kupitia Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama wa eneo hilo au wa Wilaya ya Nyang'hwale walione kama linatimiza vigezo mara moja soko hilo lifunguliwe na madini yaanze kuuzwa katika soko hilo. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante, tunaenda Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia swali la Mheshimiwa Susan Lyimo Waziri Kivuli Elimu. *(Makofi)*

Na. 50

**Marejesho ya Mikopo ya Elimu ya Juu**

**MHE. SUSAN A. LYIMO** aliuliza:-

Utaratibu wa marejesho ya Mikopo ya Elimu ya Juu umeendelea kukumbwa na changamoto kubwa hasa baada ya ongezeko la asilimia 6 kama *retention fee* na hivyo kusababisha wanufaika wa mikopo kushindwa kumaliza kurejesha mikopo hiyo?

Je, kwa nini Serikali isilete Muswada wa mabadiliko ya Sheria husika utakaokuwa na masharti rahisi kwa wanufaika ili waweze kumaliza kulipa mikopo kwa wakati?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri Elimu, Sayansi na Teknolojia. Mheshimiwa William Tate Ole Nasha tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu:-

Mheshimwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia napenda kujibu swali la Mheshimiwa Susan Anselm Lyimo Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu hutoza asilimia 6 kwenye salio la deni yaani *outstanding loan balance* la mnufaika kwa mkopo kama tozo ya kutunza thamani yaani *value retention fee*. Lengo la tozo hii ni kulinda thamani ya fedha wanazokopeshwa wanufaika wa mikopo ili kuwa na mfuko endelevu utakaoendelea kutoa mikopo kwa wahitaji wengine bila kulazimika kuongeza fedha zaidi kutokana na upotevu wa thamani ya fedha.

Mheshimiwa Spika, kumbukumbu zinaonyesha kuwa wanufaika wanaoanza kurejesha mkopo kwa wakati humaliza kati ya miaka 4 hadi 10 kulingana na kiwango cha mshahara. Hata hivyo, Serikali inaendelea kuboresha mazingira ya urejeshaji wa mikopo kwa wanufaika ili kuwawezesha kurejesha na kumaliza madeni yao kwa wakati.

**SPIKA:** Ahsante kwa majibu mafupi mazuri. Mheshimiwa Susan.

**MHE. SUSAN A. LYIMO**: Mheshimiwa Spika, nakushukuru na niseme tu kwamba majibu ya Waziri hayajaniridhisha hata kidogo kwa sababu swali langu lilihoji matatizo makubwa yaliyopo lakini na kama tuna haja ya kuleta Sheria ndani Bunge lakini bado hajajibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nina maswali mawili ya nyongeza, ukiangalia hata jibu lake ni kweli kwamba bado kuna tatizo kubwa ndiyo sababu wanasema wanaendelea kuboresha, lakini baada ya nyongeza ya asilimia 15 takwimu zinaonyesha toka mwaka 1994 wakati Bodi ya Mikopo imeanzishwa au Sheria hii imeanzishwa kati ya Wanufaika takribani 500,000 ni wanufaika 11,000 tu wameweza kurejesha Mikopo mpaka mwaka jana kwa maana ya kwamba ni asilimia 2.3 tu na hapo bado Sheria ilikuwa haijaongezwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa swali langu, Waziri au Serikali haioni kwamba nyongeza hii kubwa ya makato yatapelekea sasa Wanafunzi badala ya kulipa ndani ya miaka 4 au 10 ambayo anasema Mheshimiwa Naibu Waziri sasa hivi itaenda mpaka miaka 30 kiasi kwamba wanafunzi hawa wanufaika watakuwa ama wameshafariki au wamestaafu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kwa kuwa Serikali za Wanafunzi zimekuwa ndiyo daraja kati ya Serikali na Serikali Kuu kwa maana ya Wizara pamoja na wanafunzi wenyewe na kwa muda mrefu na mimi kama Mshauri wa Wanafunzi nilivyokuwa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam Viongozi hawa wa Wanafunzi wamekuwa wakipata madhara makubwa sana ikiwa ni pamoja na kufukuzwa wakati wanadai madai ya Wanafunzi kwa sababu wote tunajua kwamba Wanafunzi wa Elimu ya Juu wanahitaji Mikopo. *(Makofi)*

**SPIKA:** Tatizo unahutubia sasa Mheshimiwa Susan.

**MHE. SUSAN A. LYIMO:** Mheshimiwa Spika, nilitaka nimalizie.

**SPIKA:** Eeh malizia kwa kuuliza swali.

**MHE. SUSAN A. LYIMO:** Mheshimiwa Spika, wanahitaji mikopo kwa ajili ya kusoma lakini Wanafunzi hao wanakaa zaidi mwezi mmoja bila kupata Mikopo hii, wanapodai wanafukuzwa wakati matatizo makubwa ni kwa Wizara yenyewe pamoja na Vyuo kutopeleka majina.

**SPIKA:** Basi sasa inatosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa ...

**MHE. SUSAN A. LYIMO:** Mheshimiwa Spika, sasa nilitaka kujua…

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu na Profesa alitaka aongezee anasema matatizo ni wewe mwenyewe Wizara. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Waziri majibu tafadhali.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, kuhusu kwamba inachukua muda mrefu sana kwa Wanafunzi hao wanaodaiwa Mikopo kurejesha Mikopo uzoefu wetu Wizarani unaonyesha kwamba tatizo halipo kwa sababu ya *value retention fee* ipo kwa sababu ya watu kutotaka kurejesha Mkopo.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2015 tulipoingia Madarakani urejeshwaji ulikuwa ni shilingi bilioni 23 kwa mwaka lakini baada ya kuweka jitihada napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba mwaka huu tunategemea urejeshwaji utakuwa shilingi bilioni 200 kwa mwaka, mwaka jana ilikuwa bilioni 183.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, shida haipo katika fedha ile, tozo ya kulinda thamani ipo katika watu wenyewe kuhamasika kurejesha Mkopo. Kwa hiyo, kwa sababu tumeweka jitihada kubwa katika urejeshwaji wa Mkopo tumeanza kuona kwamba warejeshwaji wengi wanaanza kurejesha.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo kuhusu kama tuna mpango wa kuleta Marekebisho ya Sheria uzoefu wetu unatuonyesha kwamba Sheria ya sasa na hasa kama ilivyorekebishwa na Bunge hili mwaka 2016 bado inakidhi mahitaji ya utoaji wa Mikopo nchini, lakini pia kama Mheshimiwa Mbunge anaona kwamba kuna haja ya kuleta Marekebisho ya Sheria hiyo ndiyo kazi ya Bunge. Lakini angalau sisi kama Serikali tunaridhika na Sheria ya sasa haijatupa shida yoyote tunachoendelea kusema tu ni kwamba wale waliokopeshwa warejeshe Mikopo kwa sababu usiporejesha kwa wakati ndiyo deni lile linaongezeka na inakuwa ni vigumu kulipa.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na swali lake la pili la kuhusu Serikali za Wanafunzi, nafurahi sana kwamba nimesikia swali hili kutoka kwake kwa sababu ni kweli kwamba Mheshimiwa Susan Lyimo kwa muda mrefu alikuwa ni anafanya kazi kwenye Ofisi ya Mshauri wa Wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, kipindi kile ambacho migomo ilikuwa ni mingi sana. Lakini tunachosema ni kwamba kilichotokea hivi karibuni katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ilikuwa ni kuturudisha nyuma, tulishaondoka kule hatupo tena kwenye enzi ya kuanza kuvutana na Wanafunzi kuhusiana na Mikopo.

Mheshimiwa Spika, Mikopo siku hizi, fedha za Mikopo zinatolewa na Serikali angalau miezi miwili kabla ya Vyuo kufunguliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kinachotokea hili ninaweza nikawahakikishia kwa sababu niko Wizarani kwa zaidi ya miaka miwili, na tena Mheshimiwa Rais mwenyewe anafuatilia kila, tatizo sasa hivi siyo fedha hazitoki Serikalini inakuwa ni changamoto ya michakato ya ndani ya Vyuo

na hata kilichotokea kwenye Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ilikuwa ni sehemu ndogo sana ya wanafunzi ambao bado taarifa zao zilikuwa hazijakamilika. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, hatutakaa tukubali wanafunzi ambao sisi ndiyo tunawapa Mikopo kama Serikali kuitishia Serikali kwamba msipotoa fedha katika masaa sabini na mbili wataandamana. Sio tu kwamba inapingana na Sheria na taratibu za kuendesha Vyuo Vikuu lakini hata katika maadili ya kawaida ya Kitanzania mtoto hawezi kumpa mzazi *ultimatum* kwamba Baba usipoleta karo nakuja nyumbani na utaniona, kwa hiyo, tunaendelea kuwachukua hatua kwa mujibu wa Sheria zilizopo. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana, nimemuona Mheshimiwa Waziri wa Elimu Profesa Ndalichako majibu ya nyongeza tafadhali.

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi niongezee majibu mazuri ambayo Mheshimiwa Naibu Waziri ameyasema, kwanza nimshukuru Mheshimiwa Susan Lyimo Waziri mwenzangu wa Elimu yeye akiwa ni Waziri Kivuli na swali lake kuhusiana na Serikali za Wanafunzi.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii kuwahakikishia Bunge lako Tukufu kwamba Serikali inatambua na kuthamini mchango wa Serikali za Wanafunzi na inatambua kwamba Serikali za Wanafunzi ni daraja muhimu kati ya Wanafunzi na Uongozi wa Chuo lakini pia kati ya Wanafunzi na Serikali kwa ujumla pale ambapo kunakuwa na changamoto za Wanafunzi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ningeomba tu hizi Serikali za Wanafunzi ambazo tunazitambua na kuthamini michango yao watumie njia ambazo ni taratibu zinazotambulika katika kuwasilisha changamoto zao.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na suala la kuchelewesha ulipaji wa fedha kwa ajili ya Wanafunzi, nirudie kusema jambo ambalo Mheshimiwa Naibu wangu amelisema Serikali imekuwa ikitoa fedha miezi miwili kabla ya Chuo kufunguliwa.

Mheshimiwa Spika, kinachotokea na kilichotokea mwaka huu kwa baadhi ya Wanafunzi wapo Wanafunzi ambao anasaini fedha yake ya kutumia ile *boom* ya chakula na malazi lakini anakuwa hasaini kwenye sehemu ya ada za Chuo kwa sababu ile hela haiendi kwake.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kilichofanyika Vyuo vimeangalia kuna Wanafunzi ambao walikuwa wamefika mwaka wa tatu lakini alikuwa hajasaini fedha ya malipo ya Chuo kwa mwaka wa pili na kwa mwaka wa kwanza na kinachotokea asiposaini zile hela Bodi ya Mikopo inazirejesha kwa hiyo, Wanafunzi walikuwa ni wanufaika wa Bodi ya Mikopo lakini walikuwa wanaonekana wanadaiwa kwa sababu hawakuwa wamesaini.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba nichukue nafasi hii kuwasihi Wanafunzi kuhakikisha wanakamilisha taratibu zote ambazo zimewekwa ili waweze kupata fedha zao kwa wakati kwa sababu fedha za Mikopo zipo na Serikali hii inakuwa inazitoa kwa wakati. *(Makofi)*

**SPIKA:** Kwa sababu ya muda. Waheshimiwa Wabunge tuishie hapo na lile swali lililobaki tutalipangia wakati mwingine.

**MHE. DKT. GODWIN O. MOLLEL:** Mheshimiwa Spika, Mwongozo wa Spika.

**SPIKA:** Baadaye kidogo tu, nimalizie matangazo.

Tuna wageni marafiki wa Mheshimiwa Naibu Spika *(friends of Tulia)* kutoka Dar es Salaam wakiongozwa na Christine Kisasa. Naomba msimame hapo mlipo. Ahsanteni sana na karibu sana na Naibu yupo pale, karibu sana kutoka Dar es Salaam, karibu sana.

Pia tuna wageni kule *gallery* wa kutoka Kongwa, ni ndugu zetu wa Kongwa Yetu Kwanza ni 44 wanaongozwa na Irine Kimenya. Naomba wale wa Kongwa Yetu Kwanza msimame. Karibu sana, karibu Wana-Kongwa hapa mjengoni, wengi wenu ni mara ya kwanza kufika. Basi karibuni sana. Mnaweza kukaa. Irine yupo wapi? Ahsante sana. Ahsante Irine. Huyu ni Msukuma mmoja amelowea kule Kongwa, karibu sana Irine. *(Kicheko/Makofi)*

Wengine ni wageni wa Waheshimiwa Wabunge, kwanza ni wageni 27 wa Mheshimiwa Freeman Mbowe, Kiongozi wa Upinzani Bungeni ambao ni Wenyeviti wa Mikoa yote Tanzania Bara na Visiwani wa CHADEMA wakiongozwa na Mwenyekiti Mkoa wa Manyara ambaye pia ni Mwenyekiti wa Umoja wa Wenyeviti wa Mikoa, Dkt. Magoma Magoma. Wale Wenyeviti wa CHADEMA.

Mbona wapo wengi kuliko idadi ya mikoa? Inakuaje tena? Inatakiwa tuwaone 26. Karibuni sana hapa Bungeni. Kama mnavyoona, hawa wanaopiga makofi ndio wa kwenu hawa. Halafu ili kulijua Bunge lilivyo, sasa ngoja muwasikie CCM nao kama wapo. CCM kama mpo! *(Makofi/Kicheko)*

Ahsante sana. Ahsanteni sana Wenyeviti, mnaweza kukaa. Basi hii ndio shughuli yenyewe ilivyo hapa. *(Makofi/Kicheko)*

Wageni 16 wa Mheshimiwa George Simbachawene, Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi ambao ni majirani zake kutoka Jijini Dar es Salaam, wakiongozwa na shemeji yetu, mke wa Mheshimiwa Simbachawene, Mariana Simbachawene. Oooh, karibu sana, sana, sana. Mheshimiwa Simbachawene yupo hapa, anachapa kazi vizuri kabisa. Mnaweza kukaa. Ahsante. *(Makofi/Kicheko)*

Shemeji yetu tunaomba asimame. Eeeh, shemeji hawajakuona bado! Usimame. Eeeh, sawa sawa! Hapo sawa kabisa! Hapo sawa eeh! *(Kicheko)*

Sawa sawa. *(Makofi/Kicheko)*

Wageni watatu wa Mheshimiwa Japhet Hasunga, Waziri wa Kilimo ambao ni wahitimu wa Shule ya Sekondari Iyula kutoka Morogoro, Ndugu Mwende Asheri, Ndugu Mwele Malecela na Ndugu Salome Jacob. Karibu sana popote pale mlipo, karibu sana. *(Makofi)*

Wageni wawili wa Mheshimiwa Subira Mgalu, Naibu Waziri wa Nishati wanatoka Chama cha Walimu Tanzania, ni Ndugu Susan Shesha na Ndugu Zahabu Christopher. Karibuni sana. Wako pale. *(Makofi)*

Wageni 86 wa Mheshimiwa Stanslaus Nyongo, Naibu Waziri wa Madini ambao ni wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma wanaotokea Wilaya ya Maswa wakiongozwa na Ndugu Joseph Ngeleja. Karibu sana Mletu Ngeleja. *(Makofi)*

Wageni 66 wa Mheshimiwa Antony Mavunde, Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu - vijana ambao ni wanafunzi kutoka Shule ya Sekondari Jamhuri ya hapa Dodoma. Vijana wa Jamhuri, karibu sana. Wanapendeza kweli kweli! Shule hii ni shule yenye Kidato cha Kwanza mpaka Kidato cha Sita iko karibu kabisa na uwanja wa Jamhuri pale. *(Makofi)*

Wageni 100 wa Mheshimiwa Shabani Shekilindi, ambao ni wanafunzi na walimu kutoka Shule ya Sekondari St. Marry's Mazinde Juu iliyopo Lushoto Mkoani Tanga. Wameingia kweli! Nadhani hawa bado hawajapa nafasi, wataingia baadaye kidogo.

Wageni watano wa Mheshimiwa Angelina Malembeka ambao ni Makada wa Chama cha Mapinduzi kutoka Ilala Jijini Dar es Salaam na Manyoni Mkoani Singida wakiongozwa na Katibu wa Wazazi Wilaya ya Manyoni, Ndugu Ally Omari. Wana-CCM wale, karibu sana. Wanawapumulia CHADEMA kwa karibu kabisa pale. *(Makofi/Kicheko)*

Mgeni wa Mheshimiwa Halima Mdee, kutoka Jijini Dar es Salaam ambaye ni Naibu Mwanasheria Mkuu wa CHADEMA, Ndugu Peter Kibatala. Hayupo! Yuko wapi? Ameingia mitini. *(Makofi/Kicheko)*

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuaa utaratibu)*

**SPIKA:** Mtera! *(Makofi/Kicheko)*

Mgeni wa Mheshimiwa Allan Kiula, ambaye ni Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi wa Kata, kutoka Mkalama Mkoani Singida, ndugu Shada Mapembe. Karibu sana. *(Makofi)*

Wageni wawili wa Mheshimiwa Joel Makanyaga ambao ni vijana walioamua kusaidia Shule ya Wasioona ya Buigiri iliyopo Chamwino Mkoani Dodoma, wakiongozwa na Diwani wa Kata ya Buigiri Mheshimiwa Keneth Yindi. Karibuni sana, karibu sana. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Emmanuel Mwakasaka, Ndugu Amresha Mfungo. Karibu, karibu sana. (Makofi)

Wageni wawili wa Mheshimiwa Amina Makilagi, ambao ni rafiki zake kutoka Mbulu na Karatu Mkoa wa Manyara, Ndugu Faustine Lazaro na Asteria Mussa. Wale pale! (Makofi)

Mgeni wa Mheshimiwa Grace Kiwelu kutoka Jijini Dar es Salaam ambaye ni Makamu Mwenyekiti wa BAVICHA Taifa, Ndugu Moza Mushi. BAVICHA ndiyo kitu gani? Ndiyo nini hiyo?

Wageni wa Mheshimiwa Sophia Mwakagenda ambao ni Wachungaji kutoka Jijini Dar es Salaam ambao ni Wachungaji kutoka Jijini Dar es Salaam, Mchungaji Julius Goliama na Mchungaji Gideon Ligate. Karibu sana. *(Makofi)*

Wageni waliopo Bungeni kwa ajili ya mafunzo ni wageni 200 kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma wakiongozwa na Mkufunzi wao, Dkt. Mnata Renani. *UDOM* karibu sana wasomi wetu, mnafanya vizuri sana na karibu sana. *(Makofi)*

Nimewona wawili.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Spika, hoja ya dharura.

**MHE. DKT. GODWIN O. MOLLEL:** Hoja ya dharura, Dkt. Mollel huku.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mwakagenda.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Msigwa.

**MHE. DKT. GODWIN O. MOLLEL:** Dkt. Mollel.

**SPIKA:** Kwa sababu ya muda wanatosha hao.

**WABUNGE WENGINE**: Mlinga.

**SPIKA:** Mlinga eeh! Wanatosha hao. Kwa kifupi kifupi, kifupi, kifupi. Tuanze na Mchungaji halafu Mheshimiwa Mwakagenda.

**HOJA YA DHARURA**

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Nasimama kwa Kanuni ya 47 kuhusu kuliomba Bunge lako liahirishe ili tujadili hoja dharura.

Mheshimiwa Spika, *World Health Organization* (*WHO)* imeitangazia duania kwamba *coronavirus* ni janga la kidunia; na hivi tunavyozungumza imeshaua wagonjwa zaidi ya 200; na kila siku wagonjwa wanaoripotiwa ni zaidi 2000 huko China; na nchi nyingi duniani zimekuwa zikiwatoa watu wake kutoka nchi ya China kuwarudisha nyumbani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tatizo hili ni kubwa. Ni vizuri kama Bunge tukajadili tukajua Watanzania wangapi wapo China? Wanaosoma wako wangapi? Wanaofanya biashara wako wangapi? Serikali ina mikakati gani ya kuwarudisha hapa Tanzania?

Mheshimiwa Spika, kama vile haitoshi, Serikali imejipanga vipi, namna gani huu ugonjwa ukiingia hapa Tanzania kuna maeneo gani? Nchi nyingine zimeshaandaa maeneo, *incase* ugonjwa ukilipuka maeneo yapo wapi? Hili ni suala muhimu na nyeti. Natambua kwamba Serikali imesema inapima wagonjwa wakipita pale kwenye mipaka yetu, lakini wataalam wanasema ugonjwa huu unadumu kwa siku 14. Inawezekana wakapimwa wakiingia: Je, kuna mahali wanahifadhiwa ili tujue?

Mheshimiwa Spika, naomba suala hili lijadiliwe. Natoa hoja ili Bunge liahirishwe tuijadili.

**SPIKA:** Sasa Mheshimiwa Mchugaji umetoa maswali kadhaa ambayo nadhani unaipa Serikali ijiandae ikuletee majibu, je, wanafunzi ni wangapi ambao wapo China? Mpango gani wa kuwarudhisha?

Je, hii iko hivi, iko hivi, iko hivi. Kwa hiyo, nadhani hilo sasa naielekeza ya Serikali wachukue jambo hilo na wakati muafaka bado tupo hapa, yatatoka maelezo ya kuhusiana na suala lako. Kwa hiyo, nakushuruku sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwakagenda. *(Makofi)*

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi. Uwepo wa Wabunge wanaowakilisha wanawake kwa maana ya Wabunge Viti Maalum katika Bunge, katika Halmashauri zetu pamoja na Vitongoji na Vijiji ni suala ambalo tulisaini na kuridhia kama Taifa kwenye *Maputo Protocol.*

Mheshimiwa Spika, imekuwa kuna mazoea ya Mawaziri wanapojibu maswali ya Viti Maalum, wanasema Mbunge wa Jimbo pia amelizungumzia. Nataka kujua na unipe mwongozo wako, sisi tuliopo humu ndani hadhi yetu haiko sawa kama Wabunge tunapouliza maswali kwa ajili ya wale tunaowawakilisha? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, ninaomba tupate majibu. Hii imekuwa hasa kwa Wabunge wa Upinzani wanapouliza maswali. *(Makofi/Kicheko)*

**SPIKA:** Sasa Mheshimiwa Waziri akisema na Mbunge wa Jimbo ameshanieleza jambo hili, amekosea wapi? Hajakosea chochote. Kama Waziri wa Maji, ameeleza kwamba wiki mbili zilizopita alikuwa na Mheshimiwa Kitwanga kule Misungwi. *Physically* kwenye ziara. Kwa hiyo, hilo lisikuume wala siyo suala la Mbunge wa aina hii au wa aina hii. Tunaendelea Mheshimiwa Mlinga.

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Nilikuwa mwongozo kutokana na swali Na. 43, Mheshimiwa Waziri wakati akijibu alinukuu swali ambalo niliuliza siku chache zilizopita kuhusiana na mahabusu wa Ulanga kupanda bodaboda. Kwanza Bunge hili lina Mheshimiwa mmoja tu wa Ulanga.

Mheshimiwa Spika, Wilaya yetu ya Ulanga ina Mahakama moja Wilaya na Mahakama za Wilaya nne; na…

**SPIKA**: Mahakama za Mwanzo.

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Mheshimiwa Spika, Mahakama za Mwanzo nne. Naomba kuelezea, sasa nitoe hilo neno bodaboda, yeye atasema huwa wanatumia usafiri gani na hawana usafiri?

Mheshimiwa Spika, Mahakama ya Wilaya iko mita 500 kutoka Gereza, Mahakama ya Vigoi ipo kilometa tatu kutoka Gereza Kuu, Mahakama ya Chilombola ipo kilometa 30 kutoka Gereza Kuu, Mahakama ya Lupilo ipo kilometa 40 kutoka Gereza Kuu, Mahakama ya Mwanzo Ilonga ipo kilometa 61 kutoka Gereza Kuu.

Mheshimiwa Spika, naomba mwongozo wako, maana hilo swali niliuliza Wizara ya Mambo ya Ndani na waliliridhia na baada ya kutoka hapo niliongea nao na waliwasiliana na Mkuu wa Gereza. Leo anakuja Waziri wa Katiba na Sheria anasema mimi nilitia chumvi kauli hiyo.

Mheshimiwa Spika, naomba Bunge lako Tukufu ilifanyie kazi hili ili Waziri aje aombe radhi kama mimi nimekosea nitaomba radhi na Bunge linichukulie hatua. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA**: Ahsante, nimesikia. Mheshimiwa Dkt. Mollel.

**MHE. DKT. GODWIN O. MOLLEL:** Mheshimiwa Spika, nasimama...

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, naomba wanaoongea ongea hebu tusikilizane. Mambo mengine haya yanaweza yakashirikisha watu wengine wengi. Mheshimiwa Mollel, tafadhali.

**MHE. DKT. GODWIN O. MOLLEL:** Mheshimiwa Spika, nasimama kwa Kanuni ya 47(1) kuahirisha shughuli za Bunge ili kujadili jambo la dharura.

Mheshimiwa Spika, hapa juzi mwenzetu Mheshimiwa Zitto ameandika barua kwenye Benki ya Dunia na alipoandika barua kwenye Benki ya Dunia alitaka fedha ambazo zingekuja kusaidia elimu Tanzania zizuiliwe. Kwa kiasi cha hizo fedha, utaona kwamba tungeweza kujenga

shule tano kubwa kwa kila wilaya, pia tungeweza kuwaweka bwenini watoto zaidi ya 2,000 wa kike ambao mwisho wa siku hata kiwango cha mimba kwenye Taifa letu kingeshuka sana.

Mheshimiwa Spika, ikimbukwe tumeapa hapa Bungeni kwa kutumia Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Katiba hiyo imetaja dhahiri maadui watatu wa Taifa letu ikiwepo umasikini, ujinga na maradhi. Ukigusa kwenye eneo hili la elimu ina maana umefuta ujinga, umasikini na maradhi.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu amevunja Katiba yetu, sijui unatuelezaje? Ikumbukwe kwamba hii ni tabia ambayo tunatakiwa sasa tuitafute namna kuishughulikia kwenye Taifa letu. Watu hawa walipinga mradi wa Bwawa la Nyerere na wakahamasisha huko duniani kutafuta watu wa kuwaunga mkono.

Mheshimiwa Spika, ieleweke kwa nini ni hatari sana kwa uchumi wetu na usalama wa nchi yetu? Ni hatari kwa sababu ingeshusha bei ya umeme kwenye Taifa letu, tukapata bei ya umeme rahisi kama nchi nyingine na viwanda vinge-*boost* kwenye nchi hii; na iki-*boost* viwanda wakulima wetu wananyanyuka na uchumi wetu unakua na hata umasikini unapungua kwenye Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, sababu mojawapo ya watoto kupata mimba kwenye hili Taifa ni umasikini, ndiyo maana watoto wanapata mimba. Leo ukienda kutengeneza mradi wa kimkakati ambao unaenda kufanya wakulima na thamani ya mazao yetu yapande, halafu *sabotage* inatokea, maana yake ni jambo linalogusa uchumi na maslahi ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, vilevile wameenda wakagusa mpaka ndege zetu na vitu vingine. Hii hali ikiendelea, usalama wa nchi utakuwa hatarini na hata maadui wetu wa kiuchumi watapata fursa ya kutuingilia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ninaomba nitoe hoja na ninaomba Waheshimiwa Wabunge wenzangu waniunge mkono ili tuone sasa kwa sababu hata Marekani wamemjadili Rais wao pale tu alipoonekana haaminiki anapotoka nje ya Mataifa mengine kuhusu maslahi ya Taifa letu. Leo Mbunge mwenzetu anazunguka dunia na kumekuwa na tabia ya wengi kuzunguka ku-*sabotage* Taifa hili kiuchumi na wakati wengine kutuathiri kiusalama.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja na ninaomba Wabunge wenzangu waniunge mkono. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Spika, Kuhusu Utaratibu.

**SPIKA:** Haya. Kabla sijaamua kuhusu utaratibu, Mheshimiwa Salome.

**KUHUSU UTARATIBU**

**MHE. SALOME W. MAKAMBA:** Mheshimiwa Spika, nasimama kwa Kanuni ya 48(4) ambayo inasema: "Jambo lolote halihesabiwa kuwa ni lenye maslahi kwa Umma iwapo utatuzi wake unategemea hatua zaidi kuliko zile za utekelezaji wa kawaida wa sheria peke yake."

Mheshimiwa Spika, jambo alilolileta Mbunge mwenzangu Mheshimiwa Dkt. Mollel, kwanza tu wengine hatuna taarifa ya kinachoendelea, lakini pili, jambo hili lina utaratibu wake mahsusi wa kisheria wa kulishughulikia. Kwa sababu hizo, kulileta ndani ya Mbunge hili kama hoja ya dharura ni kukiuka Kanuni zetu za Bunge.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kama Mheshimiwa Dkt. Mollel anadhani Mheshimiwa Zitto Zuberi Kabwe amekiuka utaratibu wa Kibunge na jambo hili linatakiwa kushughulikiwa, zipo njia za kisheria zinazoweza kulishughulikia jambo hilo. Kwa hiyo, alipeleke kwenye vyombo vya kisheria badala ya kulileta kama hoja ya dharura ndani ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru Mheshimiwa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Mollel kuna ukiukwaji gani unaouona kuhusiana na jambo hili katika taratibu za Kibunge?

**MHE. DKT. GODWIN O. MOLLEL:** Mheshimiwa Spika, moja, sisi tuliapa kwa kutumia Katiba ya Jamhuri wa Muungano wa Tanzania; na tulipoapa kwa kutumia Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tumeapa kuilinda na kuheshimu. Hapa hatuhitaji kuingilia uhuru wa Wabunge kusema, hatuhitaji kuingilia uhuru wa mtu binafsi kutoa mawazo yake, lakini kikubwa hapa tunachoangalia wote, hapa tuliapa kwa ajili ya kulinda namba moja maslahi ya Taifa la Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, wakati unataka kutoa mawazo yako ambayo una uhuru wa kuyatoa, wakati huo tafakari usalama wa Taifa lako, tafakari usalama wa Taifa lako kiuchumi na tafakari Katiba ambayo umeapa kuilinda.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ninavyopima hapa hoja hii ni nzito, maana ni hoja inayohusu usaliti kwa Taifa kwa kadri ilivyotolewa. Mheshimiwa Dkt. Mollel umesahau kusema nembo ya Bunge imetumika kufikisha ujumbe huo huko. Kwa hiyo, kwa maana ya Kanuni gani imevunjwa, basi liko swali hapa kama kuna kuvunjwa au kutokuvunjwa, lakini *is it okey*?

Kwa hiyo naruhusu kidogo watu wawili, watatu, kama mnataka kusema neno lolote kuhusiana na jambo hili, ni hoja tu ameitoa kwamba Wabunge wenzake mchangie. Natoa dakika chache chache nikipata wawili, watatu, nampa afunge hoja yake halafu mtakishauri kiti ni ninyi Wabunge ndiyo mnaoshauri mambo haya. Kwa hiyo ambao wangependa kuzungumza kidogo naomba msimame.

Nachukua kalamu yangu, siyo wale mnasimama baada ya wenzenu kuongea ndiyo unaanza kusimama. Maana mwingine anasikiliza mwenzake akisema naye ndiyo anapata la kusema. Ngoja nitafute karatasi yangu hapa. Basi mnaweza mkakaa idadi niliyoipata inatosha, tuanze na Mheshimiwa wa *CUF*, Mheshimiwa Bobali.

**MHE. HAMIDU H. BOBALI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Kama nimemwelewa Dkt. Mollel amezungumza kwamba Mbunge mwenzetu ameandika barua. Mimi sijapata bahati ya kuona hiyo nakala ya barua, lakini nijuavyo, pamoja na kuwa Mheshimiwa Zitto ni Mbunge, pia ni kiongozi wa chama cha siasa. Kwa hiyo inawezekana kwenye nakala ya barua aidha amesaini kama kiongozi mkuu wa chama ama amesaini kama Mbunge wa Bunge la Jamhuri…

**SPIKA:** Kwa kuwa hujui chochote kuhusu jambo hilo Mheshimiwa Bobali, utatupotezea muda, maana hujui chochote. Kwa hiyo ningekushauri…

Mheshimiwa Lijualikali, dakika tatu, tatu tu, kama hujui kitu ni vizuri…

**MHE. PETER A. LIJUALIKALI:** Mheshimiwa Spika, najua. Hoja anayoileta Dkt Mollel Mheshimiwa Mbunge kusema kwamba *World Bank* imeinyima Serikali fedha kwa sababu ya Mheshimiwa Zitto. Kwanza hapa ilipaswa Serikali ndiyo ituambie kwanza, Serikali i-*admit,* ni kweli

kwamba imenyimwa fedha hizi kwa sababu ya Mheshimiwa Zitto? Ni kweli kwamba fedha tumenyimwa kwa sababu Mheshimiwa Zitto kasema? Serikali sijaona kama ime-*admit anywhere,* sijaona. Sasa hoja hii inatoka wapi kama Serikali haijasema chochote mpaka sasa hivi, haija-*admit!* Huo msingi wa kusema kwamba Mheshimiwa Zitto ndiyo amesababisha halafu hebu tujiulize Mheshimiwa Zitto kaongea vitu kama hivyo labda ni vya uongo, vipi, ambavyo ni vya uongo mpaka wazungu hao wakakubali, mabeberu hao wakakubali? Watu mnasemaga hapa mabeberu wabaya sisi tuna hela, leo hii tena mnasema mnataka hela zao? Leo hii mmekwama eenhe?

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hoja ya msingi ya kwanza hapa, ni kweli kwamba Serikali imekiri Mheshimiwa Zitto ndiyo kasababisha tumenyimwa fedha? Hoja za Zitto ni za uongo? Ni kweli kwamba Rais hajasema fedha yeye hawezi kusomesha watoto ambao wana mimba? Serikali iseme ni kweli kwamba Mheshimiwa Zitto amesababisha haya yote?

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Silinde, ulisimama au?

**MHE. DAVID E. SILINDE:** Mheshimiwa Spika, nilisimama, sema nilikuwa nina hoja moja tu kubwa kwamba, kabla Bunge halijaingia katika mjadala ilikuwa ni vizuri sasa Serikali itoe taarifa rasmi Bungeni kwamba kitendo ambacho, maana yake sisi wote tunasoma kwenye mitandao, tunaona kwenye *instagram*, kwenye *whatsApp*, ndiyo watu wanaandika kwamba hela zimezuiliwa, lakini mimi siamini kwamba Serikali inaweza kufanyia kazi taarifa za mitandao kwa haya yanayotokea. Kwa hiyo kikubwa kwanza tusubiri, Serikali itoe kwa sababu kama kweli maana yake *obvious* lazima kuna hatua ambazo sisi kama Bunge lazima tutakuja kuzichukua. Kwa hiyo, nataka kwamba Bunge lituelekeze huko kwa maana Serikali, halafu baada ya hapo nafikiri tutakuwa kwenye *ground* nzuri ya kulishughulikia.

**SPIKA:** Ahsante sana. Hoja hii ni ya Mbunge na siyo ya Serikali, kwa hiyo, lakini ushauri wako ni ushauri mzuri pia. Tunaendelea katika waliosimama, Mheshimiwa Keissy ulisimama

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Nilimsikia Mheshimiwa Zitto mwenyewe *Live BBC* akihojiwa na Zuhura Yunus kwenye kipindi maalum na *BBC*. Wote mmeiona kwenye kioo kwenye *TV,* Mheshimiwa Zitto anatoa sababu kwamba *World Bank* inyime mkopo Tanzania kwa sababu watabagua wanawake, kwa sababu anataka wasichana waliopewa mimba mashuleni waendelee na masomo, ametamka kabisa *clip* yake ninayo na *BBC* walitangaza, Mheshimiwa Zitto akihojiwa.

Mheshimiwa Spika, kwanza Mheshimiwa Zitto Kabwe ni Muislam na watu wa Kigoma labda Mashehe wake wanakubali kitu kama hicho cha uzinifu. Dini ya Kiislam inakataza kabisa kuzini, kwa hiyo nashangaa Muislam anasimama hapa kabisa anam-*support* Mheshimiwa Zitto Kabwe kusema kweli tunyimwe mkopo kwa ajili watoto wa kike wanaopata mimba na tumeshuhudia wanaopata mimba zaidi ni watoto wa miaka 14 mpaka 16.

Mheshimiwa Spika, nashangaa na akinamama wanasimama hapa, Mheshimiwa Salome ana-*support* kitu kama hicho, wakati wao ndiyo wanapinga mtoto aolewe zaidi ya miaka 18, wanataka tuongeze watoto barabarani na mitaani, mtoto gani anaweza kwenda shuleni na mtoto wake ananyonyesha. Tukubaliane, nani kati yenu hapa alikwenda shuleni na mtoto ananyonyesha, yuko wapi? Leo Mheshimiwa Zitto Kabwe anataka kutuletea masharti ya ajabu ajabu.

Mheshimiwa Spika, hii ni hatari sana, tunaweza kuja kupata mpaka viongozi wa hali ya juu wasenge kwa tabia hii au wasagaji. Masharti ya mkopo ametangaza kabisa, nilimsikia kwa masikio yangu *BBC* anasema, wanyimwe mkopo kwa sababu watabagua, wanakataa watoto wa kike wajawazito kwenda mashuleni. Ndugu zangu, huyu ni mtu hatari, haikubaliki, anataka

kuleta masharti ya ajabu ajabu, ndiyo kiongozi wa kwanza anapiga kelele mtoto wa miaka 14 anaolewa, leo ana atatuletea mtoto wa kike wa miaka 13 au 14…

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Ally Keissy, Mheshimiwa Bulembo.

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Nilimsikia kwa masikio yangu anasema, wakati Rais Trump wa Marekani anasema Marekani kwanza, wewe unaenda kusaliti nchi huko nchi za nje…

**SPIKA:** Mheshimiwa Bulembo.

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Hufai hata kidogo.

**MHE. ALHAJI ABDALLAH M. BULEMBO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwanza niunge hoja ya Dkt. Pale, lakini usaliti mkiwa vitani pale wakati Kagera, Tanzania inapigana na Uganda, akitoka mtu mmoja akapeleka habari zenu, hatakiwi kuvuka kurudi anatakiwa auawe kule kule. Usaliti anachokifanya Mheshimiwa Zitto ni usaliti mkubwa katika nchi yetu. Sasa nafasi ya kuvumilia mimi si Mwanasheria sijui taratibu za Kibunge, mtu anaposaliti nchi anatakiwa kurudi Bungeni humu? Hatakiwi huyu ni msaliti na Serikali mko pale Wanasheria…

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** Mheshimiwa Spika,taarifa.

**SPIKA:** Endelea Mheshimiwa Bulembo dakika ni chache, ni dakika tatu, tatu tu.

**MHE. ALHAJI ABDALLAH M. BULEMBO:** Mheshimiwa Spika, Wanasheria wako humu, hawa wasaliti wanaotoka Tanzania kwenda nje wakasaliti nchi yetu mnapokeaje *passport* zao kurudi nchini? Si warudie Polisi pale ili tujenge heshima katika nchi. Huyu bwana kazoea, anatakiwa apate kiboko kizuri sana.

**SPIKA:** Mheshimiwa Janeth Mbene ulisimama.

**MHE. JANET Z. MBENE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Napongeza hoja aliyoitoa Dkt. Mollel. Nami bila hata kusema kwamba, Serikali imesemaje au nini, ningependa, kwanza kitu ambacho kinanigusa kwanza ni maslahi ya Taifa. Mtu anapotamka jambo lolote lile hasa anapokuwa kiongozi lazima ajiulize hii inasaidia Taifa langu kwa vipi au itaathiri Taifa langu kwa vipi. Kitendo alichofanya mwenzetu Mheshimiwa Zitto ni usaliti, lakini vile vile wazungu wanasema hakufikiria vizuri juu ya hili jambo. Mimi nimemsikia *BBC* kwenye dira ya dunia. Kwa hiyo kitu ambacho nimekiona ni kuwa amekuwa akitumia *fact* lakini anazi-*twist* ili kujenga hoja ambayo ana ajenda nayo yeye na ajenda niliyoiona mimi ni kisiasa zaidi. Kutofautiana mitazamo kuhusiana na wanafunzi wanaopata ujauzito wakiwa shuleni haimpi uhalali yeye wa kwenda kufanya usaliti aliokwenda kuufanya.

Mheshimiwa Spika, vile vile kitu ambacho mimi nilikiona kwa haraka sana na nikaona huu ni upotoshaji mkubwa sana ni kuzungumzia vile vyuo vya kijamii kuwa ni vya CCM. Mimi wakati nchi yetu ina chama kimoja, mama yangu alikuwa mama maendeleo, ni marehemu sasa, vile vyuo vilikuwa ni vyuo vya Serikali, vile ni vyuo vya Serikali siyo vyuo vya CCM na mpaka leo ni vyuo vya Serikali. Sasa yeye kwenda kule kuwaambia eti hivi ni vyuo vya Chama cha Mapinduzi na kwa hali hiyo hela ikitolewa itakuwa hivi na hivi kwa kweli ni upotoshaji na ni uongo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, anapozungumzia kuwa eti huu ni mwaka wa uchaguzi kwa hiyo tusipate misaada au mikopo ya nafuu, tangu lini wakati wa uchaguzi tunaacha

kufanya maendeleo ya nchi yetu? Tangu lini tunaacha kujenga madarasa? Mwezi huu tuko *busy* tunajitahidi kuhakikisha kuwa madarasa yanakamilika ili watoto wasome wa Vyama vya Upinzani na wa Chama Tawala, hatuangalii mtoto anayeingia ni wa chama kipi, lakini wote waingie darasani kusoma. Je, hilo analizungumzia kuwa ni suala la uchaguzi? Kwa hiyo kwa kweli naona amepotosha kwa makusudi kwa ajenda yake binafsi ya kuleta fujo nchi kwetu.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Mary Chatanda, dakika tatu

**MHE. MARY P. CHATANDA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru. Nami niseme kwamba ndugu yangu huyu Zitto ni msaliti, kwanza ametusaliti sisi Wabunge kwa kutumia nembo kinyume kabisa na sharia, kwa sababu nembo hii ipo kisheria. Sisi kama Wabunge hatukumtuma kwenda kuandika hayo aliyoandika kwa kutumia nembo ya Bunge letu. Kwa hiyo, nafikiri kwamba Mheshimiwa Zitto angeweza kutumia nembo inayomhusu yeye mwenyewe binafsi au chama chake, lakini bila kutumia nembo ambayo inatumika na Bunge.

Mheshimiwa Spika, naomba nishukuru kwa kunipa hii nafasi, lakini kwa kweli mwenzetu huyu ametusaliti, ni vizuri akapatiwa adhabu anayostahili.

**SPIKA:** Mheshimiwa Stanslaus Mabula ulisimama, halafu Mheshimiwa Nkamia.

**MHE. STANSLAUS S. MABULA:** Mheshimiwa Spika, ukweli ni kwamba lazima tukubali kinga ni bora kuliko tiba. Sisi kama Wabunge niungane kabisa na Mheshimiwa Mollel moja ya jukumu letu ni kuisaidia nchi.

Mheshimiwa Spika, sasa nilikumbushe Bunge mwaka 2012, 2013 na 2014, Serikali ndipo ilipotafuta fedha kwa ajili ya miradi ya uboreshaji wa majiji na miji, ndipo zilipopatikana fedha za *TSP,* lakini fedha zile hazikutajwa kama zinakuja kuisaidia CCM. CCM sisi tupo tumejiandaa na kushinda ni kawaida yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa hoja anazotumia Mheshimiwa Zitto kama alivyosema pale Mheshimiwa mama Mbene, fedha hizi anadai zinakuja kuisaidia Serikali ya Chama cha Mapinduzi, anasahau miradi yote iliyopatikana kwa mkopo.

Mheshimiwa Spika, leo ukienda Kigoma ni mji ambao umebadilika ndani ya muda mfupi, miaka minne hii unaona mji mzima umejaa barabara za lami, sasa hoja yangu kwa watu wa Kigoma na Mbunge wao, watusaidie na Bunge lako lazima lichukue hatua, tufike sehemu kama Wabunge tuondokane na habari ya ushabiki ambayo haiwezi kutusaidia kama nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, fedha hizi leo kila Mbunge hapa akisimama analia habari ya maboma kwenye Jimbo lake, tumelia hapa toka juzi kwamba tunalalamika vyumba vya madarasa havitoshi watoto wa kidato cha kwanza hawajapokelewa, Serikali imefanya jitihada, imepata wadau, *World Bank* wamekubali kwa jitihada kubwa zinazofanywa na Serikali wako tayari kutoa fedha, leo mtu mmoja tu anakwenda kuanza kupotosha taarifa hizi na upatikanaji wa fedha hizi, Bunge lako kama lina namna ya kuchukua hatua, ni lazima tufanye kazi, iwe kazi ya kuijenga nchi na siyo kubomoa nchi, lazima tutoke huko.

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Nkamia.

**MHE. JUMA S. NKAMIA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuchangia hoja ya Mheshimiwa Mollel. Nafahamu Mheshimiwa Zitto ni Mbunge mwenzetu na hizi fedha pia zingeenda kusaidia wananchi wa Kigoma anakotoka yeye, lakini kwa lugha

nyepesi tu watu wa namna hii wanaitwa *mercenaries,* yuko tayari kufanya lolote kwasababu analipwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimemshangaa Mbunge mwenzangu mmoja pale anasema kwamba Mheshimiwa Zitto pengine amezungumza kama kiongozi wa kisiasa, lakini ametumia nembo ya Bunge siyo ya chama chake na nimeshangaa hata wale waliokuwa wanamhoji nadhani hawakuwa makini sana. Vyuo hivi vya Maendeleo ni vya Serikali na bado ni vya Serikali na Mheshimiwa Zitto anajua na dunia inajua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mwalimu Nyerere aliwahi kusema, nanukuu hakutumia maneno mazuri sana, lakini Mwalimu Nyerere alisema, *mercenaries* wana tabia za kimalayamalaya na alisema tutawasaka watu wenye tabia za kimalaya malaya mpaka tuwamalize. Sasa hili alilofanya mwenzetu huyu *mercenary* ni umalaya malaya wa kisiasa na matokeo yake tukiendekeza watu wa namna hii, tutakwenda pabaya. Nina hakika hata alipokuomba kibali cha kusafiri nje hakusema anakwenda kufanya nini, hizi hela zingesaidia mpaka Kigoma. Wamarekani wale leo, mtu yeyote ambaye anasaliti Taifa lao wanamsaka, hata wakati wa vita vya Iraq, Wamarekani wale hata kama walikuwa wanadanganya ama walikuwa wanasema ukweli walikuwa kitu kimoja *for the interest of the country.*

Mheshimiwa Spika, nikuombe tufike hatua watu wa namna hii wanaoyumbisha nchi wachukuliwe hatua. Ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Mollel ifunge hoja yako kwa sababu ya muda.

**MHE. DKT GODWIN O. MOLLEL:** Mheshimiwa Spika, kwanza niseme kwamba, sijasema fedha zimesimamishwa, lakini kuna mtu ametishia usalama wa Taifa letu. Hata hivyo, ameandika barua kana kwamba Wabunge wote ndiyo msimamo wetu. Kwa hiyo nataka kwanza niwaombe Wabunge wenzangu wazalendo, tuandike barua nyingine kwenda huko huko Wabunge wote kusema huyo hatumjui na wala hatukumtuma kama Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, pia nikuombe sasa kwamba, naomba kwa kufuata taratibu za Bunge, kwa kufuata kanuni za nchi na sheria na nchi, nakuomba hili jambo liende kwenye mfumo ambao utatuletea watu wa aina hiyo ambao wanasaliti Taifa hili, wanatakiwa kufanywa nini? Isiishie tu hapo, kuna waliofanya ambao ni Watanzania wazalendo, Watanzania waliosoma kwa kodi ya Watanzania, Wanasheria wanajiita Mawakili, walishirikiana kukamata ndege zetu katika maeneo mbalimbali, kama itathibitika ni kweli na wakaonekana walishiriki hivyo, nao tuwaweke kwenye *group* hilo ambalo litahusu hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile kuna hizi *NGOs* ambazo ni za haki za binadamu, tuziombe hatutaki kuziingilia ila tuziombe kwamba, wakati wanaongea na watu wenye mlengo fulani ni vizuri wakatoa muda wa kusikiliza pande zote kabla ya kwenda kwenye *conclusion,* kwa sababu inaonekana mara nyingi *conclusion* zinafanyika kwa kusikiliza upande mmoja.

Mheshimiwa Spika, ahsante na naomba hili jambo lichukuliwe hatua. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Ahsanteni Waheshimiwa Wabunge, muda unatosha ili tuweze kuendelea na shughuli nyingine. Nimalizie tu kwa kusema kwamba, kwa kweli kama Spika tunasikitika kwa mambo ya namna hii na Mheshimiwa Spika Mstaafu Mama Makinda ametoka hapa juzi, kama mtakumbuka maneno yake akiwa mtu mzima alituasa na hasa alizungumza zaidi na Wabunge vijana kwamba katika Taifa lolote utaifa ni jambo la kwanza. Kuona fahari katika kwenda nje na kuisaliti nchi yako, ni jambo ambalo si sawa. Mkopo huo unahusiana na

kuja kuboresha elimu, kuboresha elimu, ingekuwa ni jambo fulani lingine sijui nitoe mfano gani sijui, jambo *unique specific* linaloelekea mahali fulani, labda sijui kujenga kitu gani Kongwa, mtu akapinga hata Umoja wa Mataifa, ni sawa lakini hii ni kuboresha elimu nchi nzima na sisi Wabunge tunajua jinsi tulivyo na matatizo makubwa ya elimu.

Sisi Wabunge tunajua jinsi tulivyo na matatizo makubwa ya elimu, nina shule za Sekondari baadhi yake watoto wanakalia vigoda vya miguu mitatu, hawana madawati na sekondari yangu moja nimeitembelea juzi ina vyoo viwili/matundu ya vyoo mawili; moja la wasichana na moja la wavulana shule nzima. Unapomsikia mtu anasema *World Bank* wasitoe fedha Serikali ikapata ili iboreshe elimu nashindwa hata kuelewa ni kwa nini.

Hata uwe mpinzani vipi kuna mahali ambapo kidogo unasita. Ndiyo maana *Trump* hivi sasa yuko kwenye Bunge la juu la *Senate* baada ya kuhukumiwa na lile Bunge la Wananchi wa Marekani, kosa lake nini anashirikiana na nchi ya kigeni katika masuala ambayo yanaathiri *interest* ya nchi yake, Rais wao yupo katika kesi katika Bunge lao. Sasa sisi Mbunge wetu kama ya Trump. *(Makofi)*

Kwa hiyo, inasikitisha lakini sasa niseme tu kwamba katika jambo hili kuna *criminality* kidogo, kuna *element* hasa kwenye kutumia nembo ya Bunge, kuna *element* ya ujinai fulani. Kwa hiyo, tumuombe Mwanasheria Mkuu wa Serikali hilo sisi tulitupe huko zaidi, muangalie mkiona ujinai katika jambo hili basi muweze kuchukua hatua. *(Makofi)*

Sisi kama Wabunge na Bunge tuna *register* kwamba kwa kweli hatujafurahishwa na mwenzetu, abadilike tabia, yako mambo mengi kama nilivyosema asubuhi kama una tofauti za kisera mnapambana katika tofauti za kisera. Lakini tofauti za kisera haziwezi kusababisha usababishe nchi nzima tukose fursa, watoto wa Tanzania wakose fursa kwa sababu wewe hukubaliani na sera fulani au na jambo fulani, tunadhani si sahihi jambo hili.

Kwa hiyo, tunakuachia Mwanasheria Mkuu wa Serikali utaliangalia katika utaratibu huo na Serikali nayo inatoa *passport* iwe inaangalia kwani lazima kuwapa watu wa namna hii? Ndiyo mambo ya kutazama haya. *(Makofi)*

Nashukuru sana, Katibu tuendelee!

**NDG. LAWRENCE MAKIGI – KATIBU MEZANI:**

**HOJA ZA KAMATI**

**SPIKA:** Kabla hatujaendelea Mwanasheria Mkuu amesimama.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Spika, maelekezo yako Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali imeyapokea na tutalifanyia kazi kwa mujibu wa sheria zilizopo. *(Makofi)*

**SPIKA:** Nashukuru sana. Katibu.

**NDG. LAWRENCE MAKIGI – KATIBU MEZANI:**

**HOJA ZA KAMATI**

**TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MIUNDOMBINU KUHUSU SHUGHULI ZA KAMATI KWA MWAKA 2019**

**NA**

**TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA VIWANDA, BIASHARA NA MAZINGIRA KUHUSU SHUGHULI ZA KAMATI KWA MWAKA 2019**

**SPIKA:** Nakuita Mheshimiwa Mwenyekiti ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu anakuja mwenyekiti mwenyewe Mheshimiwa Kakoso karibu sana na uendelee tafadhali.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Spika, ifuatayo ni taarifa ya mwaka ya shughuli za kamati kwa kipindi cha mwezi Februari, 2019 hadi Januari 2020 taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge sehumu ya kwanza, kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu za Bunge, Kanuni ya 117 (15), Toleo la Januari, 2016. Naomba kuwasilisha mbele ya Bunge lako tukufu, Taarifa ya Mwaka ya Utekelezaji wa Shughuli za Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu kwa Mwaka 2019 hadi 2020.

Mheshimiwa Spika, taarifa hii imegawanyika katika maeneo manne yaani, Sehemu ya Kwanza ambayo ni utangulizi wenye maelezo ya jumla; Sehemu ya Pili ina Majukumu yaliyotekelezwa; Sehemu ya Tatu inahusu Ushauri wa Kamati na Sehemu ya Mwisho ambayo ni Hitimisho.

Mheshimiwa Spika, Wajumbe wa Kamati hii ni wameorodheshwa kama inavyoonekana katika sehemu hii ya taarifa. Katika kipindi cha kuanzia mwezi Februari 2019 hadi mwezi Januari, 2020, Kamati ilitekeleza majukumu yake kwa njia ya vikao mbalimbali pamoja na ziara za ukaguzi wa miradi ya maendeleo kama zinavyoonekana kwenye taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipata fursa ya kupitia na kuchambua utekelezaji wa Bajeti ya Wizara hii kwa Mwaka wa fedha 2018/2019; pamoja na Mapendekezo na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020.

Kwa mwaka wa fedha 2019/2020, Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano imeidhinishiwa jumla ya shilingi trilioni 4.9 hili ni ongezeko la takribani shilingi bilioni 692,418,457,819. Ongezeko hili ni la asilimia 17 ukilinganisha na bajeti ya mwaka wa fedha uliopita 2018/2019 ambapo iliidhinishwa bajeti ya Shilingi trilioni 4.2. Mchanganuo wa Mgawanyo wa fedha kwa mwaka wa fedha 2019/2020 katika kila Sekta ni Shilingi 1,330,194,268,268 kwa ajili ya Sekta ya Ujenzi, shilingi tirioni 3,629,130,373,895 Sekta ya Uchukuzi na shilingi bilioni 3,973,197,000 Sekta ya Mawasiliano.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwani mwenendo wa Bajeti inayotengwa kwa ajili ya Sekta ya miundombinu niwakuridhisha na kumekuwepo na ongezeko la fedha zinazotengwa na kuidhinishwa mwaka hadi mwaka jambo linaloashiria kuwa Serikali imeipa sekta ya miundombinu fedha nyingi za kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Uchukuzi Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania-*TPA* taarifa hii imeeleza kuhusu maendeleo ya ujenzi wa bandari nchini ikijumuisha bandari ya Dar es Salaam, Bandari ya Tanga, Bandari ya Mtwara na Bandari za Maziwa Makuu. Pamoja na

jitihada zote zinazofanyika na Serikali katika kuhakikisha mazingira ya bandari nchini yanaboreka, Serikali hainabudi kuendelea kufanya utafiti na kupunguza vikwazo mbalimbali vinavyosababisha wafanyabiashara wa ndani na nje ya nchi kuhama kutumia bandari zetu.

Mheshimiwa Spika, Kampuni ya Huduma za Meli (MSCL) Kamati inaipongeza Serikali kwa kuzingatia ushauri wake kuhusu kuimarisha njia za ukusanyaji mapato ya *MSCL* kwa kufunga mitambo ya kieletroniki kwa ajili ya kukatia tiketi abiria. Baada ya kuanza kukata tiketi za abiria za kieletroni kati ya bandari ya Mwanza Kaskazini na Nansio, Ukerewe mapato yameongezeka ambapo katika mwaka wa fedha 2018/2019, Kampuni imefanikiwa kukusanya kiasi cha Shilingi bilioni 1.6 ikilinganishwa na kiasi cha huko nyuma kiasi cha Shilingi bilioni 1.2.

Mheshimiwa Spika, reli Kamati inatoa pongezi kwa jitihada mbalimbali zinazofanywa na Serikali ili kufufua na kuimarisha shirika la reli na mtandao wake hapa nchini ambapo Serikali katika Mwaka wa Fedha 2019/2020 imetenga kiasi cha shilingi Trilioni 2.9 kwa ajili ya miradi ya maendeleo ya Shirika hilo.

Mheshimiwa Spika**,** Kamati ilipokutana na Serikali mnamo mwezi Oktoba, 2019 ilielezwa kwamba ujenzi wa Reli ya Kati kwa kiwango cha kisasa *(Standard Gauge)* unaendelea ambapo kipande cha Dar es Salaam hadi Morogoro (300Km) ulifika asilimia 66.6. Vilevile, ujenzi wa kipande cha Morogoro Makutupora (422Km) utekelezaji wake ulifika asilimia 18.

Mheshimiwa Spika, hali ya reli ya Tanzania na Zambia TAZARA katika vikao vya Kamati vilivyofanyika Januari, 2020; Kamati ilipokea taarifa ya Utendaji wa TAZARA. Hata hivyo, taarifa hiyo inaonesha bado utendaji wa TAZARA si wakuridhisha kutokana na changamoto mbalimbali zikiwemo kukosa mtaji wa uendeshaji, huduma duni kutokana na uchakavu na uhaba wa injini na mabehewa. Migomo ya mara kwa mara ya wafanyakazi kutokana na kutolipwa mishahara kwa wakati, uchakavu wa njia katika baadhi ya maeneo hivyo kuwekewa vidhibiti mwendo, kuathirika kwa mizania ya mamlaka kutokana na madeni na hivyo kuifanya TAZARA ishindwe kujiendesha vizuri.

Mheshimiwa Spika, kuhusu malipo ya mishahara ya wafanyakazi wa TAZARA, Serikali ya Tanzania imeendelea kulipa mishahara wafanyakazi wa TAZARA upande wa Tanzania ambapo hadi mwezi Desemba, 2019 jumla ya Shilingi Bilioni 118.582 zilikuwa zimeshatolewa na Serikali.

Mheshimiwa Spika, sekta ya Ujenzi wakala wa barabara Tanzania *TANROADS* pamoja na mafanikio mbalimbali Wakala wa Barabara uliyoyapata, Wakala huu unakabiliwa na changamoto zifuatazo:- Fedha za miradi ya Maendeleo kutotolewa kwa wakati. Hali hii ilisababisha baadhi ya miradi kutokamilika kwa wakati kutokana na baadhi ya Makandarasi kusimama kufanya kazi na wengine kutekeleza kazi kwa kasi ndogo; Uharibifu wa miundombinu unaofanywa na watumiaji wa barabara hususan uzidishaji wa uzito, uharibifu na wizi wa alama za barabarani;

Mheshimiwa Spika, kuongezeka kwa gharama za miradi kutokana na kuongezeka kwa riba zitokanazo na ucheleweshaji wa malipo ya kazi za fedha za ndani.

Mheshimiwa Spika, madai ya Makandarasi na Wahandisi Washauri. Aidha, Ucheleweshaji wa utekelezaji wa miradi kutokana na Sheria mpya ya Kodi ya Ongezeko la thamani *(Value Added Tax-VAT),* Upatikanaji wa hati ya msamaha wa kodi unachukua hadi miezi sita baada ya kusainiwa kwa mkataba wa kazi. Hali hii siyo tu inachelewesha utekelezaji wa mikataba lakini pia inaweza kuleta migogoro ya mikataba yenye gharama kubwa za nyongeza kwa Mkakati; Idadi ndogo ya wataalam kulingana majukumu Wakala unahitaji jumla ya wafanyakazi wa nyongeza wa fani mbalimbali wapatao 1,089.

Mheshimiwa Spika, Ujenzi wa Viwanja vya Ndege Miradi mbalimbamli ya ujenzi wa viwanja vya ndege inaendelea katika mikoa mbalimbali, kama vile kigoma, Mpanda, Mtwara, Mwanza, Arusha, Sumbawanga, Shinyanga, Kilimanjaro, Msalato, Tabora na Songwe. Hata hivyo, miradi hii inakabiliwa na changamoto kubwa ya ufinyu wa bajeti na kutokutolewa fedha kwa wakati. Mfano; kiwanja cha ndege cha Songwe, Mwanza na Arusha vinakabiliwa na changamoto ya ufinyu wa bajeti hali inayopelekea kuchelewa kukamilika kwa miradi hii.

Mheshimiwa Spika, kwa Kiwanja cha Ndege cha Dodoma na Songwe, Kamati imekuwa ikihimiza umuhimu wa kuwekwa kwa taa za kuongozea ndege ambazo zitasaidia ndege kutua nyakati za usiku na hata mchana wakati wa ukungu mkubwa. Hali kadhalika, kuwekwa kwa uzio kuzunguka mipaka yote ya Kiwanja ili kuongeza usalama wa kiwanja na kuepuka uvamizi na wananchi wa maeneo jirani.

Mheshimiwa Spika, Wakala wa Majengo Tanzania *(TBA)* Wakala huu unakabiliwa na changamoto ya malimbikizo makubwa ya madeni ya ujenzi, ushauri, pango la nyumba pamoja na mauzo ya nyumba ambayo Wakala unazidai Wizara, Idara pamoja na Taasis za Serikali ambayo ni zaidi ya shilingi bilioni 20. Changamoto zingine ni pamoja na mahitaji makubwa ya nyumba za watumishi wa umma ukilinganisha na kasi ndogo ya ujenzi, riba kubwa kwa ajili taasisi za fedha, kasi ya mabadiliko ya teknolojia katika vifaa, mbinu na ubunifu kwenye sekta hii.

Mheshimiwa spika, Sekta ya Mawasiliano Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania *(TCRA)* Madhumuni ya kuanzishwa kwa Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania-*TCRA* ni kusimamia Makampuni ya Mawasiliano nchini yakiwemo Makampuni yanayotoa huduma za Simu, Utangazaji, Intaneti, Posta na Usafirishaji wa Vifurushi.

Mheshimiwa Spika, kupunguza vitendo viovu kwenye mitandao. Katika kuutekeleza ushauri huu, zoezi la usajili wa laini za simu kwa kutumia alama za vidole lilizinduliwa rasmi nchi nzima kuanzia tarehe 1 Mei, 2019 ambapo wamiliki wote wa laini za simu ambao hawajajisajili kwa njia ya biometria walitangaziwa kujisali upya kwenye maduka ya watoa huduma wao. Ili mmiliki wa simu aweze kusajiliwa imelazimu kuwa na kitambulisho cha Taifa zilizotolewa na *NIDA*.

Mheshimiwa Spika, Kamati imejulishwa kuwa usajili wa laini za simu umeongezeka kutoka laini milioni 22,515,203 mwaka 2011 hadi kufikia milioni 45 tarehe 26 Januari, 2020 idadi ya laini zilizosajiliwa kwa alama za vidole zimefikia milioni 30 sawa na asilimia 66. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Maoni na Ushauri wa Kamati Katika kipindi cha miaka mitatu ya Fedha, yaani Mwaka 2016/2017 hadi 2019/2020, Serikali imeonesha kuzingatia ushauri wa Kamati kwa kuongeza fedha kwa ajili ya kuendeleza na kuimarisha Miundombinu nchini. Mwaka wa fedha 2016/2017 ilitenga shilingi trilioni 4.3, mwaka 2017/2018 shilingi trilioni 4.5, mwaka 2018/2019 shilingi trilioni 4.2 na mwaka 2019/2020 shilingi trilioni 4.9.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuendelea kutoa kipaumbele na kuongeza fedha kwa ajili ya ujenzi, ukarabati na uendelezaji wa Miundombinu nchini. Hata hivyo, pamoja na shabaha nzuri ya Serikali katika masuala ya miundombinu, Kamati inasisitiza fedha kutolewa kwa wakati ili kuharakisha utekelezaji wa miradi ya maendeleo na kuepuka limbikizo la madeni.

Mheshimiwa Spika, Sekta ya Uchukuzi Mamlaka ya Bandari Tanzania; Kwa Kuwa, Mamlaka ya Bandari Tanzania ndiyo Mamlaka iliyokasimiwa jukumu la kusimamia bandari nchini; Mamlaka hii inayo miradi mingi ya ujenzi na ukarabati wa bandari ambapo kwa sasa

Mamlaka ya Bandari ipo katika hatua ya kuboresha kwa kufanya ukarabati wa bandari kama vile bandari ya Dar es Salaam na Mtwara.

Kwa hiyo basi, Kamati inaendelea kusisitiza ushauri inaishauri yafuatayo; Kubakisha angalau asilimia 40 ya makusanyo ya Mamlaka ya Bandari Tanzania ili Mamlaka hii iweze kuendeleza baadhi ya miradi katika bandari zake, kama vile, miradi ya ujenzi wa bandari ya Kalema, Kigoma na Mtwara, ambayo inagharimu takribani shilingi bilioni 20 wakati mapato ya bandari kwa mwaka ni takribani shilingi bilioni 270; *(Makofi)*

(ii) Kuharakisha mchakato wa ununuzi wa *flow meter* mpya kwa ajili ya upimaji wa mafuta yanayoingia Bandari ya Dar es Salaam. Kutokuwepo kwa mtambo wa kupima kiasi cha mafuta *(flow meter)* kunasababisha kutokujua kwa uhakika kiwango cha mafuta kinachoingia bandari ya Dar es Salaam; Kufanyike juhudi za makusudi ili kuweza kuhamisha Gati la Mafuta lililopo kurasini *(KOJ)* na kujenga Gati Namba 13 na 14; Serikali kufanya ukarabati wa bandari zingine muhimu kama vile bandari ya Tanga, Mtwara, Mwanza, Kigoma na bandari ya ziwa Nyasa. Vilevile, bandari zilizo katika vipaumbele vya Serikali kama vile Bandari ya Mbegani-Bagamoyo na Bandari ya Mwambani- Tanga kuanza kutekelezaji wake; Wadau wote wa bandari waunganishwe kwenye mfumo wa kielektroniki unaotumiwa na bandari ili kuweza kuharakisha uondoshwaji wa mizigo bandarini kwani wakati mwingine mizigo inachelewa kutokana na wadau wengine kama Mkemia mkuu, Shirika la Viwango Tanzania-*(TBS),* Wizara ya Nishati na Wizara ya Madini na wengine wengi kutokuwemo kwenye mfumo huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mchakato wa kuwa na eneo Kurasini-Shimo la Udongo ambalo litatumika kuegesha magari yanayoingiza na kutoa mizigo bandarini sasa ufanyike kwa haraka ili eneo hilo lipatikane kwani mojawapo ya kero za wafanyabishara wanaotumia Bandari ya Dar es Salaam ni kutokuwa na maegesho jambo ambalo husababisha usumbufu na gharama zisizotabirika; Serikali kuharakisha ujenzi wa bandari za nchi kavu ili kupunguza gharama kwa wateja kusafiri mpaka Dar se salaam kwa ajili ya kutoa mizigo. Ni muda sasa tangu Serikali imeanza mipango ya kujenga bandari kavu katika maeneo ya Kwala -Pwani, Ihumwa - Dodoma, Katosho-Kigoma na Misungwi –Mwanza; Serikali kuharakisha majadiliano na wabia ili ujenzi wa Bandari ya Bagamoyo uweze kuanza kwani kukamilika kwa bandari hii kutatoa fursa nyingi za kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, Watumishi wa bandari nchini wapewe nafasi ya kwenda kujifunza katika Bandari nyingine zinazofanya vizuri ili kuweza kufahamu …..

**SPIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti samahani kidogo utaendelea baada ya dakika mbili tatu subiri kidogo tubadilishane naomba nimuite Mheshimiwa Chenge

*Hapa Mwenyekiti (Mhe. Andrew J. Chenge) Alikalia kiti*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwenyekiti endelea!

**MHE. MOSHI S. KAKOSO - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Watumishi wa bandari nchini wapewe nafasi ya kwenda kujifunza katika Bandari nyingine zinazofanya vizuri ili kuweza kufahamu wenzao wanachokifanya; na hatimaye kuweza kubaini mbinu za ushindani katika biashara; Bandari Bubu zirasimishwe haraka ili zifanye kazi kulingana na kanuni na taratibu za kisheria na kuongeza wigo wa ukusanyaji kodi na udhibiti wa biashara haramu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ujenzi wa reli nchini Serikali imeonesha nia ya dhati ya kujenga upya Reli ya Kati katika kiwango cha kisasa *(standard gauge);* ambapo mradi umeanza mwezi

April, 2017 na unatekelezwa kwa Awamu Tano. Kwa kuwa, katika uhalisia Tawi la kutoka Tabora-Kigoma-Uvinza- Msongati na Kaliua-Mpanda-Kalema ndilo lenye mizigo mingi inayotoka na kwenda nchi za jirani kama vile DRC Congo, Burundi na Rwanda. Hivyo basi, Kamati inaendelea kusisitiza na kushauri, ujenzi wa reli hii uzingatie kwanza maeneo yenye faida za kichumi na kuweka kipaumbele kwanza kiwekwe katika tawi lenye mizigo mkubwa ambalo ni tawi la Tabora – kigoma -Uvinza- Msongati; Kaliua – Mpanda –Kalema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali izingatie kuwashirikisha wataalam wa ndani (wazawa) katika ujenzi wa reli ya kati ili kuwa na mradi endelevu pale wataalam wa nje watakapoondoka. Serikali iangalie uwezekano wa kupata mkopo wa gharama nafuu ambao utatumika kununua vichwa na mabehewa ya treni ili Shirika la Reli Tanzania- *TRC* liweze kuondokana na changamoto ya upungufu wa vichwa vya treni arobaini na tano (45) pamoja na mabehewa ili *TRC* iweze kufanya kazi zake kwa ufanisi na kuanza kupata faida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Utendaji wa Reli ya Tanzania na Zambia (TAZARA) TAZARA inamilikiwa na nchi mbili (Tanzania na Zambia) kwa asilimia 50:50; kwa muda sasa utendaji wa TAZARA umekuwa si wakuridhisha; Kamati inashauri yafuatayo; Serikali iweke mkakati wa dhati kuinusuru TAZARA ili iweze kujiendesha moja kwa moja. Mkakati uwe ni kufanya mazungumzo na Serikali ya Zambia na kufikia muafaka wa namna bora ya uendeshaji wa reli hii, ikiwa ni pamoja na, kufanya mapitio ya kurekebisha Sheria iliyoianzisha TAZARA, Namba 23 ya Mwaka 1975; Serikali ilipe madeni ya wafanyakazi; pamoja na, kuendelea kusaidia kulipa wafanyakazi wa TAZARA mishahara mpaka hapo itakapokuwa imejiimarisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege (TAA) ndiyo iliyokasimiwa jukumu la kusimamia kuendesha viwanja vya ndege nchini, Kamati imebaini changamoto mbalimbali zinazokabili viwanja vya ndege nchini ikiwemo migogoro ya mipaka, Kamati inaishauri kuhakikisha inapata hati za viwanja vya ndege kwani Kamati imejulishwa kuwa viwanja vya ndege 11 tu vilishapatiwa hati miliki kati ya viwanja 59 vinavyomilikiwa na Mamlaka ya Viwanja vya Ndege. Vilevile, kuhakikisha viwanja vingine vilivyobakia vinapimwa na kupatiwa hati miliki. Kuongeza udhibiti na ulinzi katika viwanja vya ndege vikiwemo vya mikoa hasa vilivyopo mpakani kama vile Mtwara, Kigoma na Kagera kuepuka viwanja hivi kupitisha biashara haramu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imechukuwa hatua kufufua Shirika la Ndege Tanzania kwa kuwekeza kununua ndege mpya. Kwa kuwa ndege hizo zitakuwa kichocheo cha uchumi wa Tanzania katika kuwekeza kupata usafiri wa ndani na nje ya nchi, hivyo itimiza malengo ya kukuza Pato la Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inashauri kuwa na mikakati mikubwa ya Kitaifa ya kuhakikisha kuwa *ATCL* inakuwa na uwezo wa kushindana kutengeneza faida; *ATCL* iangaliwe kama Kampuni ya kibiashara na siyo ya kutoa huduma tu; *ATCL* ijitangaze kwenye vyombo vya Kimataifa ambavyo huonyesha safari zake za ndege dunia nzima. Aidha, Kampuni hii sasa ijipange kuingia katika soko la kujitangaza katika vyombo vya habari, majarida na vipeperushi mbalimbali; na Shirika liendelee la Ndege kufanya utaratibu wa kuongeza safari za ndani na za kikanda ili kuimarisha mtandao wa safari zake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa, Serikali imeonesha dhamira ya dhati kuikwamua Kampuni ya Huduma za Meli *(MSCL)* kwa kulipa malimbikizo ya miezi 28 ya mishahara ya wafanyakazi pamoja na kuanza ukarabati na matengezo ya meli katika Maziwa Makuu; uwekezaji huu ni mkubwa ambao unahitaji mikakati na mipango kabambe kuhakikisha *MSCL* inainuka na kuweza kujiendesha pasizo ruzuku ya Serikali. Hivyo basi, Serikali kujipanga kutengeneza meli zote 14 zilizopo katika Maziwa Makuu ili kuiwezesha Kampuni ya Meli Tanzania

kumudu kujiendesha kibiashara. Aidha, kipaumbele kiwekwe kwa Ziwa Tanganyika ambako kuna uhitaji mkubwa wa usafiri katika Ziwa Tanganyika. Serikali sasa iharakishe ujenzi wa meli mpya na kufanya ukarabati wa meli ya MV. Liemba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kampuni ya Huduma za Meli kupanga mipango ya kujiendesha kisasa kwa kuweka teknolojia ya kufatilia matumizi ya mafuta kwenye meli *(Flow Scanner)* na kuweka mfumo wa kuweza kufuatilia mahali meli ilipo kila wakati *(trucking system)*, kwani hii itasaidia kuziba mianya ya upotevu wa fedha za Kampuni hiyo. Vile vile Kampuni ya Meli Tanzania kufanya kazi kwa ukaribu na Mamlaka ya Bandari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wakala wa Barabara Tanzania *(TANROADS)* ndio umekabidhiwa jukumu la ujenzi wa barabara na ukarabati hapa nchini. Pamoja na jitihada za Serikali zinazofanywa za kujenga barabara bado kumeendelea kuwepo na changamoto mbalimbali ambazo ni viwango vya uzito wa magari kuzidisha viwango vya mizigo unaoharibu barabara na wizi wa alama barabarani. Hivyo basi, Kamati inazidi kushauri yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ifanye mapitio mapya kwa ajili ya kuongeza fedha za dharura kwa ajili ya barabara ikizingatiwa mvua kubwa zinazonyesha nchini ambazo zimefanya uharibifu mkubwa sana. Mfano, gharama za kazi za dharura zimekadiriwa kuwa jumla ya shilingi bilioni 15 ambazo ni zaidi ya bajeti ya dharura iliyopangwa kwa mwaka 2019/2020. Serikali iangalie upya utaratibu wa manunuzi pamoja na upatikanaji wa hati ya misamaha ya kodi ya ongezeko la thamani *(VAT)* na kukarabati baadhi ya barabara za mikoa zilizo katika hali isiyoridhisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Wakala wa Barabara *(TANROADS)* umepewa jukumu la ujenzi wa Viwanja vya Ndege bado kuna changamoto kubwa ya ujenzi na uboreshaji wa viwanja vya ndege. Hivyo basi, Kamati inashauri yafuatayo: Serikali kuhakikisha inatoa fedha iyoidhinishwa kwa wakati na kuendeleza viwanja vya ndege.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Chuo cha Ujenzi Morogoro. Vyuo hivi vimekuwa vikitoa mafunzo ya teknolojia stahiki yanguvukazi katika ukarabati wa matengenezo ya barabara kwa Wasimamizi, Wakaguzi wa Barabara, Wahandisi na Mafundi. Hivyo, vimekuwepo kwa muda mrefu lakini bado havijasajiliwa jambo ambalo halitoi hamasa kwa wengi kujifunza katika vyuo hivi. Kamati inashauri Serikali iviunganishe vyuo hivi na kuvisajili ili viweze kutoa mafunzo yanayostahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Wakala wa Ufundi Tanzania *(TEMESA)* unakabiliwa na changamoto, mabadiliko ya teknolojia, vifaa vya kisasa vinavyoweza kuendana na magari na ukosefu wa mitambo, hivyo, changamoto hizi zinasababisha *TEMESA* kufanya kazi kwa kubahatatisha ambako kunatumia muda mwingi na gharama kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inashauri Serikali kuajiri wataalam waliobobea kwenye fani hii ya ufundi wa magari kuhakikisha kunakuwa na mitambo ya kisasa kuendana na kukua kwa teknolojia husika; Wakala wa Ufundi na Umeme kuharakisha mchakato wa kuchagua karakana za kutengenezea magari ya Serikali kwenye wilaya ili kuondoa usumbufu wa magari ya Serikali kusafiri umbali mrefu kwenda kufanya matengenezo kwani kuna wilaya nyingine ziko mbali na eneo la Makao Makuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Sekta ya Mawasiliano, kuhusu Zoezi la usajili wa laini za simu, ni endelevu na limekuwa changamoto ambapo wananchi wengi wameshindwa kusajili kutokana na kutokupata namba za usajili wa *NIDA* na Kitambulisho cha Taifa. Takribani laini

milioni 15 zimefungiwa kwa kukosa usajili wa *biometric,* jambo ambalo linaweza kusababisha upotevu wa fedha kwa Serikali. Hivyo basi, Kamati inashauri Serikali yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali itenge fedha za kutosha kwa Wizara ya Mambo ya Ndani ili *NIDA* iweze kuwa na mitambo mingi ya kutengenezea vitambulisho. Hili liende sambamba na kuongeza rasilimali watu ambao watasaidia usajili wa kupata vitambulisho vya Taifa hasa kwenye maeneo ya vijijini pembezoni mwa nchi. Utambuzi wa wananchi kwa ajili ya kupata vitambulisho *NIDA* iharakishe hasa viongozi katika ngazi za vijiji ili kuweza kupata uhakiki wa uhalali wa uraia na kurahisisha zoezi la kupata vitambulisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilibaini masuala mbalimbali yanayohitaji kutafutiwa ufumbuzi Mfuko wa Mawasiliano kwa wote uweze kuimarika na kufanya kazi zake vizuri. Kamati inaendelea kusisitiza ushauri wake Serikali kupitia na kuangalia upya taratibu za umilikishwaji wa ardhi hasa maeneo yanayojengwa minara ili kuweka utaratibu wa maeneo yaliyokodiwa na kununuliwa kwa ajili ya ujenzi wa minara kumilikiwa na Serikali za vijiji kuliko ilivyo sasa. Hii itasaidia sana kwani fedha zitakazopatikana kutokana na kukodi ama kununua eneo hilo zitatumika kwa maendeleo ya wananchi walio wengi tofauti na ilivyo sasa ambapo maeneo mengi yaliyojengwa minara yananufaisha watu wachache. Serikali kuhakikisha inaweka mabango yanayoonesha ushiriki wake kwenye minara husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutekelezwa kwa mradi wa wa Misimbo ya Posta kuna manufaa makubwa kwani itawezesha kuwepo kwa utambulisho wa makazi ya watu na makampuni na hatimaye kurahisisha shughuli zote za kijamii na kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shirika la Posta Tanzania linahitaji mtaji ili liweze kujiendesha kibiashara na kukabiliana na ushindani wa soko katika Sekta ya Posta. Pamoja na changamoto ya mtaji, linakabiliwa na madeni ya pensheni kwa wafanyakazi wa iliyokuwa Posta ya Jumuiya ya Afrika Mashariki. Kamati inashauri yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ichukuwe jukumu la kulipa madeni ya pensheni kwa wafanyakazi wa iliyokuwa Posta ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ili kuliondolea Shirika hili mzigo wa kulipa wastani wa shilingi milioni 74 kila mwezi fedha ambazo zingepelekea kwenye uendeshaji wa shirika hilo. Serikali kupitia Wizara ya Fedha na Mipango kuona namna ya kufuta deni lililosalia la shilingi bilioni 15 baada ya kusamehe shilingi bilioni 12 zilizokuwa za riba, tozo na adhabu ambazo Shirika la Posta lilikuwa linalipa kwa Mamlaka ya Mapato Tanzania *(TRA).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Shirika la Mawasiliano Tanzania *(TTCL)* Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha Wizara, Taasisi na Mashirika yake yote yanayodaiwa na *TTCL* yanakuwa mfano kwa kulipa madeni yote yanayodaiwa na *TTCL* kwa kuwa fedha hizo za gharama za simu hutengwa kila mwaka katika bajeti za Wizara, Taasisi na Mashirika yao. Shirika la Mawasiliano Tanzania liweke mkakati madhubuti ya kukusanya madeni na Serikali ikamilishe Kanuni za namna ya kuendesha na kusimamia miundombinu ya kimkakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha taarifa hii mbele ya Bunge lako tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, kwa namna ya pekee napenda kumpongeza na kumshukuru Waziri wa Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Mheshimiwa Eng. Isack Kamwele, akishirikiana na Manaibu Mawaziri Mheshimiwa *Engineer* Atashasta Nditiye na Mheshimiwa Elias Kwandikwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Kamati inawashukuru Makatibu Wakuu wa Wizara hii, Elius Mwakalinga (Sekta ya Ujenzi), Eng. Dkt. Leonard Chamuriho (Sekta ya Uchukuzi), Eng. Dkt. Maria Sasabo (Sekta ya Mawasiliano) pamoja na Naibu Katibu Mkuu Dkt. Jim Yonazi. Kamati pia inawashukuru wakuu wa taasisi, Wakurugenzi na wafanyakazi wote ambao wameipa Kamati ushirikiano mkubwa. Ni kwa ushauri na utaalam uliowezesha Kamati kutekeleza majukumu yake na kuwasilisha taarifa hii leo katika Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile nachukua fursa hii kumshukuru Katibu wa Bunge Ndugu Stephen Kagaigai kwa kuwawezesha Kamati wakati wote ilipokuwa inatekeleza majukumu yake. Aidha, shukrani za kipekee ziende kwa Mkurugenzi wa Idara za Kamati za Bunge Ndugu Michael Chikokoto, Mkurugenzi Msaidizi Ndugu Gerald Magili, Katibu wa Kamati Ndugu Hosiana John. Vilevile, nashukuru wafanyakazi wote wa Ofisi ya Bunge kwa ushirikiano wao ulioiwezesha Kamati yangu kutekeleza majukumu yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kueleza shughuli zilizotekelezwa na Kamati, maoni na ushauri, sasa naomba kutoa hoja kwamba Bunge lipokee, lijadili na kuikubali Taarifa ya Mwaka ya Shughuli za Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu kwa kipindi cha Januari, 2019 hadi Januari, 2020 pamoja na maoni na ushauri uliopo katika taarifa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba izingatiwe kuwa baadhi ya maeneo ambayo hayajasomwa yawe kwenye kumbukumbu ya *Hansard*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja, mimi Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. *(Makofi)*

**TAARIFA YA MWAKA KUHUSU SHUGHULI ZA KAMATI KWA KIPINDI CHA FEBRUARI 2019 HADI JANUARI 2020 - KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

**SEHEMU YA KWANZA**

1.0 **UTANGULIZI**

**Mheshimiwa Spika,** awali ya yote, naomba taarifa hii iingizwe kwenye Hansard kama ilivyo.

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu za Bunge, Kanuni ya 117 (15), Toleo la Januari 2016, naomba kuwasilisha mbele ya Bunge, Taarifa ya Mwaka ya Utekelezaji wa Shughuli za Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu kwa kipindi cha Februari 2019 hadi Januari 2020.

**Mheshimiwa Spika**, taarifa hii imegawanyika katika maeneo manne yaani, Sehemu ya Kwanza ambayo ni utangulizi wenye maelezo ya jumla; Sehemu ya Pili inahusu Majukumu yaliyotekelezwa; Sehemu ya Tatu inahusu Ushauri wa Kamati na Sehemu ya Mwisho ambayo ni Hitimisho.

1.1 **Wajumbe wa Kamati**

**Mheshimiwa Spika,** Wajumbe wa Kamati hii ni wameorodheshwa kama inavyoonekana katika sehemu hii ya taarifa.

1.2 **Shughuli zilizotekelezwa katika Kipindi cha Mwaka 2019/2020**

**Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha kuanzia mwezi Februari 2019 hadi mwezi Januari, 2020 , Kamati ilitekeleza majukumu yake njia ya vikao mbalimbali pamoja na ziara za ukaguzi wa miradi ya maendeleo kama zinavyoonekana kwenye taarifa hii.

**SEHEMU YA PILI**

## 2.0 UCHAMBUZI WA SHUGHULI ZILIZOTEKELEZWA NA KAMATI

### 2.1 Bajeti ya Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipata fursa ya kupitia na kuchambua utekelezaji wa Bajeti ya Wizara hii kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019; pamoja na Mapendekezo na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020.

**Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2019/2020, Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano imeidhinishiwa jumla ya **Shilingi Trilioni 4.9 (4,963,297,839,163),** hili ni ongezeko la takribani **Shilingi bilioni 692,418,457,819.** Ongezeko hili ni la **asilimia 17** ukilinganisha na bajeti ya mwaka wa fedha uliopita 2018/2019 ambapo iliidhinishwa bajeti ya **Shilingi trilioni 4.2 (4,270,879,381,344).**

Mchanganuo wa Mgawanyo wa fedha kwa mwaka wa fedha 2019/2020 katika kila Sekta ni **Shilingi 1,330,194,268,268** kwa ajili ya Sekta ya Ujenzi, **Shilingi 3,629,130,373,895** Sekta ya Uchukuzi na **Shilingi 3,973,197,000** Sekta ya Mawasiliano.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaipongeza Serikali kwani mwenendo wa Bajeti inayotengwa kwa ajili ya Sekta ya miundombinu niwakuridhisha na kumekuwepo na ongezeko la fedha zinazotengwa na kuidhinishwa mwaka hadi mwaka jambo linaloashiria kuwa Serikali imeipa sekta ya miundombinu.

### 2.2 Sekta ya Uchukuzi

#### 2.2.1 Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania-TPA

**Mheshimiwa Spika**, taarifa hii imeeleza kuhusu maendeleo ya ujenzi wa bandari nchini ikijumuisha bandari ya Dar es Salaam, Banadri ya Tanga, Bandari ya Mtwara na Bandari za Maziwa Makuu.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na jitihada zote zinazofanyika na Serikali katika kuhakikisha mazingira ya bandari nchini yanaboreka, Serikali hainabudi kuendelea kufanya utafiti na kupunguza vikwazo mbalimbali vinavyosababisha wafanyabiashara wa ndani na nje ya nchi kuhama kutumia bandari zetu.

#### 2.2.2 Kampuni ya Huduma za Meli (MSCL)

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaipongeza Serikali kwa kuzingatia ushauri wake kuhusu kuimarisha njia za ukusanyaji mapato ya MSCL kwa kufunga mitambo ya kieletroniki kwa ajili ya kukatia tiketi abiria. Baada ya kuanza kukata tiketi za abiria za kieletroni kati ya bandari ya Mwanza Kaskazini na Nansio, Ukerewe mapato yameongezeka ambapo katika mwaka wa fedha 2018/2019, Kampuni imefanikiwa kukusanya kiasi cha **Shilingi bilioni 1.6 (1,600,169,896.00)** ikilinganishwa na kiasi cha **Shilingi bilioni 1.2 (1,222,964,110.00)** zilizokusanywa 2017/18 kabla ya mfumo kuanza, hii ikiwa sawa na ongezeko la asilimia 30.84.

Vilevile, Kamati inaipongeza Serikali kuzingatia ushauri wake kuhusu kulipa malimbikizo ya mishahara ya watumishi ya miezi 28 ambapo zimelipwa jumla ya **Shilingi bilioni 2.1** kwa ajili ya malimbikizo ya mishahara ya watumishi ya miezi 28. Aidha, June, 2019 Serikali ilitoa kiasi cha **Shilingi Bilioni 5.9** kwa ajili ya kuwezesha uendeshaji wa Kampuni kwa kipindi cha mpito cha miezi 27 kinachoanza Aprili 2019 hadi June 2021.

2.2.3 **Reli**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inatoa pongezi kwa jitihada mbalimbali zinazofanywa na Serikali ili kufufua na kuimarisha mtandao wa reli nchini ambapo Serikali katika Mwaka wa Fedha 2019/20 imetenga kiasi cha **shilingi Trilioni 2.9** kwa ajili ya miradi ya maendeleo ya Shirika la Reli.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilipokutana na Serikali mnamo mwezi Oktoba, 2019 ilielezwa kwamba ujenzi wa Reli ya Kati kwa kiwango cha kisasa (Standard Gauge) unaendelea ambapo kipande cha Dar es Salaam hadi Morogoro (300Km) ulifika asilimia 66.63. Vilevile, ujenzi wa kipande cha Morogoro Makutupora (422Km) utekelezaji wake ulifika asilimia 18.58.

**Mheshimiwa Spika**, kipande cha Tanga-Moshi (350Km) ukarabati umekamilika na huduma za usafirishaji wa mizigo ulizinduliwa mwezi Julai, 2019. Aidha, ukarabati wa kipande cha Moshi-Arusha (86Km) umefikia asilimia 40. Kwa upande wa reli ya Mtwara-Songea-Mbamba Bay, Kamati imejulishwa kuwa Shirika la Reli limeingia Mkataba na Mtaalam Mshauri Februari, 2019 kwa ajili ya kuunadi mradi kwa sekta binafsi kazi inayotarajia kukamilika Februari, 2020.

2.2.4 **Mamlaka ya Reli ya Tanzania na Zambia-TAZARA**

**Mheshimiwa Spika,** katika vikao vya Kamati vilivyofanyika Januari, 2020; Kamati ilipokea taarifa ya Utendaji wa TAZARA. Hata hivyo, taarifa hiyo inaonesha bado utendaji wa TAZARA si wakuridhisha kutokana na changamoto mbalimbali zikiwemo kukosa mtaji wa uendeshaji, huduma duni kutokana na uchakavu na uhaba wa injini na mabehewa, migomo ya mara kwa mara ya wafanyakazi kutokana na kutolipwa mishahara kwa wakati, uchakavu wa njia katibaadhi ya maeneo hivyo kuwekewa vidhibiti mwendo, kuathirika kwa mizania ya mamlaka kutokana na madeni na hivyo kuifanya TAZARA ishindwe kukopesheka, hali ya kutoaminiana kati ya viongozi na wafanyakazi wan chi mbili zinazomiliki reli hii na uchakavu wa mfumo wa mawasiliano na ishara.

**Mheshimiwa Spika,** Kuhusu malipo ya mishahara ya wafanyakazi wa TAZARA, Serikali ya Tanzania imeendelea kulipa mishahara wafanyakazi wa TAZARA upande wa Tanzania ambapo hadi mwezi Desemba, 2019 jumla ya **Shilingi Bilioni 118.582** zilikuwa zimeshatolewa na Serikali ya Tanzania kwa ajili ya kulipa mishahara. Aidha, kuhusu madeni ya wastaafu wa upande wa Tanzania hadi mwezi Juni, 2019 jumla ya **Shilingi Bilioni 14.7** zimelipwa.

2.2.5 **Kampuni ya Ndege ya Tanzania-ATCL**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaipongeza Serikali kwa jitihada za dhati na makusudi za kufufua Kampuni hii ya Ndege ya Tanzania kwa kununua ndege mpya nane. Uwekezaji huu mkubwa wa Serikali umesababisha kupanuka kwa mtandao wa kutoa huduma ambapo hivi sasa ATCL inatoa huduma ya usafiri wa anga katika vituo 17, kati ya hivyo vituo 10 ni vya ndani na nchi (Bukoba, Dodoma, Dar es Salaam, Iringa, Kigoma, Kilimanjaro, Tabora, Mbeya, Mwanza na Zanzibar) na vituo 7 ni vya nje ya nchi (Bujumbura, Entebbe, Hahaya, Harare, Johhannesburg, Lusaka na Mumbai).

Vilevile, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuhakikisha ATCL inarudi katika mifumo ya mauzo na usambazaji wa tiketi pamoja na mifumo ya usuluhishi wa tiketi na mauzo kwenye umoja wa mashirika ya ndege duniani (IATA). Aidha, kufuzu kupata cheti cha usalama katika usafiri wa anga jambo linaloongeza iamani kwa wateja.

**Mheshimiwa Spika**, Changamoto zinazoikabili ATCL ni pamoja na uchache wa wataalam hususan marubani na wahandisi, madeni yaliyolimbikizwa miaka ya nyuma yanayofikia **Shilingi bilioni 180** ambapo katika mwaka wa fedha 2019/20 ATCL ilitengewa **Shilingi bilioni 35.865**, na changamoto nyingine ni ukosefu wa taa za kuongozea ndege katika baadhi ya viwanja vya ndege jambo linalosababisha ndege kutua wakati wa mchana tu.

2.3 **Sekta ya Ujenzi**

2.3.1 **Wakala wa Barabara Tanzania- TANROADS**

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na mafanikio mbalimbali Wakala wa Barabara uliyoyapata, Wakala huu unakabiliwa na changamoto zifuatazo: -

a) Fedha za miradi ya Maendeleo kutotolewa kwa wakati. Hali hii ilisababisha baadhi ya miradi kutokamilika kwa wakati kutokana na baadhi ya Makandarasi kusimama kufanya kazi na wengine kutekeleza kazi kwa kasi ndogo;

b) Uharibifu wa miundombinu unaofanywa na watumiaji wa barabara hususan uzidishaji wa uzito, uharibifu na wizi wa alama za barabarani

c) Kuongezeka kwa gharama za miradi kutokana na kuongezeka kwa riba zitokanazo na ucheleweshaji wa malipo ya kazi za fedha za ndani, madai ya ''idle time" kwa Makandarasi na Wahandisi Washauri;

d) Ucheleweshaji wa utekelezaji wa miradi kutokana na Sheria mpya ya Kodi ya Ongezeko la thamani (Value Added Tax-VAT), Upatikanaji wa hati ya msamaha wa kodi unachukua hadi miezi sita baada ya kusainiwa kwa mkataba wa kazi. Hali hii siyo tu inachelewesha utekelezaji wa mikataba lakini pia inaweza kuleta migogoro ya mikataba yenye gharama kubwa za nyongeza. Mkakati;

e) Idadi ndogo ya wataalamu kulingana majukumu Wakala unahitaji jumla ya wafanyakazi wa nyongeza wa fani mbalimbali wapatao 1,089.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na changamoto hizo, pia Kamati imebaini changamoto nyingine kubwa ya ucheleweshwaji wa malipo ya fidia kwa wananchi wanaopisha maeneo ya ujenzi wa barabara kwani wananchi husimamishwa kuendeleza na hata kutumia maeneo hayo ilhali hakuna malipo yoyote waliopewa hivyo kurudisha nyuma maendeleo ya mwananchi.

2.3.2 **Ujenzi wa Viwanja vya Ndege**

**Mheshimiwa Spika,** Miradi mbalimbamli ya ujenzi wa viwanja vya ndege inaendelea katika mikoa mbalimbali, kama vile kigoma, Mpanda, Mtwara, Mwanza, Arusha, Sumbawanga, Shinyanga, Kilimanjaro, Msalato, Tabora na Songwe.

**Mheshimiwa Spika**, Hata hivyo, miradi hii inakabiliwa na changamoto kubwa ya ufinyu wa bajeti na kutokutolewa fedha kwa wakati. Mfano; kiwanja cha ndege cha Songwe, Mwanza na Arusha vinakabiliwa na changamoto ya ufinyu wa bajeti hali inayopelekea kuchelewa kukamilika kwa miradi hii. Kutokutolewa fedha za miradi hii kwa wakati kunaathiri utekelezaji wa

majukumu ya Sekta ya Ujenzi kwani kumekuwa na ongezeko la gharama kutokana na riba, mabadiliko ya bei za vifaa vya ujenzi na mabadiliko viwango vya kubadilisha fedha.

**Mheshimiwa Spika**, kwa Kiwanja cha Ndege cha Dodoma na Songwe, Kamati imekuwa ikihimiza umuhimu wa kuwekwa kwa taa za kuongozea ndege ambazo zitasaidia ndege kutua nyakati za usiku na hata mchana wakati wa ukungu mkubwa. Hali kadhalika, kuwekwa kwa uzio kuzunguka mipaka yote ya Kiwanja ili kuongeza usalama wa kiwanja na kuepuka uvamizi na wananchi wa maeneo jirani kukatiza katika maeneo ya Kiwanja.

2.3.3 **Wakala wa Majengo Tanzania (TBA)**

**Mheshimiwa Spika,** Wakala huu unakabiliwa na changamoto ya malimbikizo makubwa ya madeni ya ujenzi, ushauri, pango la nyumba pamoja na mauzo ya nyumba ambayo Wakala unazidai Wizara, Idara pamoja na Taasis za Serikali ambayo ni zaidi ya **shilingi bilioni 20.**

Changamoto zingine ni pamoja na mahitaji makubwa ya nyumba za watumishi wa umma ukilinganisha na kasi ndogo ya ujenzi, riba kubwa kwenye taasis za fedha, kasi ya mabadiliko ya teknolojia katika vifaa, mbinu na ubunifu kwenye sekta ya ujenzi inaugharimu Wakala fedha nyingi za kuwapatia mafunzo wataalam wake ili waendane na mabadiliko hayo na vifaa vya ujenzi vyenye gharama kubwa katika soko kusababisha kuongeza gharama za ujenzi.

2.4 **Sekta ya Mawasiliano**

2.4.1 **Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA)**

**Mheshimiwa spika,** Madhumuni ya kuanzishwa kwa Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania-TCRA ni kusimamia Makampuni ya Mawasiliano nchini yakiwemo Makampuni yanayotoa huduma za Simu, Utangazaji, Intaneti, Posta na Usafirishaji wa Vifurushi.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imekuwa ikiishauri mara kwa mara kuwa Serikali kupitia Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania idhibiti mawasiliano ya ulaghai na hatimae kupunguza vitendo viovu kwenye mitandao. Katika kuutekeleza ushauri huu, zoezi la usajili wa laini za simu kwa kutumia alama za vidole lilizinduliwa rasmi nchi nzima kuanzia tarehe 1 Mei 2019 ambapo wamiliki wote wa laini za simu ambao hawajajisajili kwa njia ya biometria walitangaziwa kujisali upya kwenye maduka ya watoa huduma wao. Ili mmiliki wa simu aweze kusajiliwa imelazimu kuwa na kitambulisho cha Taifa au namba za kitambulisho cha Taifa (NIN) zilizotolewa na NIDA.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imejulishwa kuwa usajili wa laini za simu umeongezeka kutoka laini 22,515,203 mwaka 2011 hadi kufikia laini 45,312,588 tarehe 26 Januari, 2020. Idadi ya laini zilizosajiliwa kwa alama za vidole ni **30,030,178** sawa na asilimia **66.3** ya laini zote hivyo idadi ya laini ambazo bado hazisajiliwa ni 15,282,410.

**Mheshimiwa Spika**, zoezi hili la usajili wa namba za simu ni endelevu kwani mahitaji ya kuwa na laini ya simu kwa ajili ya mawasiliano yataendelea kuwepo siku hadi siku. Hata hivyo, Kamati imebaini kuwa zoezi hili limekuwa na changamoto kwani wananchi wengi hawakufikia hatua ya usajili kutokana na huduma kupatikana Wilayani ambako ni umbali mrefu toka vijijini, kuchelewa kupata namba za NIDA au vitambulisho vya Taifa na hivyo wengi wao wamesajili laini kwa kuazima vitambulisho jambo ambalo si sahihi kwani bado Serikali haitaweza kupata taarifa halisi za watumiaji wa simu.

2.4.2 **Mradi wa Postikodi na Simbo za Posta**

**Mheshimiwa spika,** mradi wa anuani za makazi ni muhimu kwani ni mradi ambao utarahisisha shughuli zote za kijamii, kiuchumi na kisiasa kuweza kufanyika kwa urahisi na kuokoa muda. Miongoni mwa huduma zitakazorahisishwa na kuwapo kwa mfumo huu ni pamoja na; huduma

za umeme, gesi, maji, mabenki, ulinzi na usalama, huduma za dharura kama zima moto ,magari ya wagonjwa, pamoja na wasambazaji wa vifurushi.

**Mheshimiwa spika**, Kamati hairidhishwi na kasi ya utekelezaji wa mradi huu ukilinganisha na umuhimu wake kwa Taifa. Vile vile fedha zinazotengwa kwa ajili ya kutekeleza mradi huu zimekuwa hazitolewi kwa wakati.

2.4.3 **Shirika la Posta Tanzania –TPC**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuzingatia ushauri wa Kamati ulioiomba Serikali kupitia Wizara ya Fedha na Mipango kuona namna ya kufuta deni la **Shilingi Bilioni 26** ambalo Shrika la Posta lilikuwa likidaiwa na Mamlaka ya ya Mapato Tanzania-TRA.

Kamati imefarijika kupewa taarifa kuwa Serikali kupitia Sheria ya Msamaha (Amnesty) imekubali kufuta deni la Shirika la **Shilingi Bilioni 12** lililokuwa limetokana na tozo, riba, na adhabu. Hata hivyo Kamati bado inaona umuhimu wa kufuta deni lililosalia la takribani **Shilingi bilioni 15** ili kupunguza mzigo wa madeni kwa Shirika.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imebaini kuwa, Shirika hili linakabiliwa na changamoto ya mzigo wa kulipa pensheni wafanyakazi wa iliyokuwa Posta ya Jumuiya ya Afrika Mashariki wastani wa **Shilingi Milioni 74** kila mwezi fedha ambazo zingeweza kuelekezwa kwenye uendeshaji wa Shirika.

**Mheshimiwa Spika**, changamoto nyingine inayolikabili Shirika la Posta ni Shirika kuendelea kuwepo kwenye orodha ya mashirika yaliyotakiwa kurekebishwa na Serikali mwaka 1997. Hatua hii inalifanya Shirika kutoelewa hatima yake na hivyo kuathiri utendaji wake.

2.4.4 **Shirika la Mawasiliano Tanzania – TTCL**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuzingatia ushauri wake ilioutoa kuhusu Serikali kuangalia upya utaratibu ambao umeruhusu baadhi ya Makampuni ya Simu kumiliki mikongo yao sambamba na mkongo wa Taifa. Kamati imejulishwa kuwa Serikali imeufanyia kazi ushauri huu na kuwasimamisha watoa huduma hao.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na juhudi za Serikali inazozifanya ili kuiimarisha TTCL, bado Shirika la Mawasiliano Tanzania limeendelea kukabiliwa na mbalimbali ikiwemo: -

a) Madeni ya zamani ambayo yanatokana na kutumia huduma mbalimbali ambayo mengi yao Shirika linaidai Serikali na Taasis zake ambapo hadi mwezi June, 2019 kiasi cha **Shilingi bilioni 23** zilikuwa zinadaiwa;

b) Kutokukamilika kwa Kanuni ambazo zitatoa maelekezo ya namna ya Shirika kuendesha na kusimamia miundombinu ya kimkakati ya mawasiliano;

c) Shirika kuwa na mtaji mdogo kwa ajili ya uwekezaji na kushindwa kukabiliana na mabadiliko ya teknolojia yanayokwenda sanjari na kasi ya uwekezaji;

d) Sheria ya manunuzi kwa mashirika ya umma ambayo inaleta urasimu unaokinzana na ushindani wa kibiashara; na

e) Uharibifu nanukataji wa miundombinu ya Mkongo unaotokana na shughuli za binadamu, hujuma, na shughuli za maendeleo kama ujenzi na upanuzi wa barabara.

## SEHEMU YA TATU

### 3.0 **MAONI NA USHAURI WA KAMATI**

### 3.1 **Bajeti**

**Mheshimiwa Spika,** Katika kipindi cha miaka mitatu ya Fedha, yaani Mwaka 2016/2017 hadi 2019/2020, Serikali imeonesha kuzingatia ushauri wa Kamati kwa kuongeza fedha kwa ajili ya kuendeleza na kuimarisha Miundombinu nchini. Mwaka wa fedha 2016/2017 ilitenga **shilingi trilioni 4.3**, mwaka 2017/2018 **shilingi trilioni 4.5**, mwaka 2018/2019 **shilingi trilioni 4.2** na mwaka 2019/2020 **shilingi trilioni 4.9.**

Kamati inaipongeza Serikali kwa kuendelea kutoa kipaumbele na kuongeza fedha kwa ajili ya ujenzi, ukarabati na uendelezaji wa Miundombinu nchini. Hata hivyo, pamoja na shabaha nzuri ya Serikali katika masuala ya miundombinu, Kamati inasisitiza fedha kutolewa kwa wakati ili kuharakisha utekelezaji wa miradi ya maendeleo na kuepuka limbikizo la madeni.

### 3.2 **Sekta ya Uchukuzi**

#### 3.2.1 **Mamlaka ya Bandari Tanzania**

**Kwa Kuwa,** Mamlaka ya Bandari Tanzania ndiyo Mamlaka iliyokasimiwa jukumu la kusimamia bandari nchini;

**Na kwa Kuwa**, Mamlaka hii inayo miradi mingi ya ujenzi na ukarabati wa bandari ambapo kwa sasa Mamlaka ya Bandari ipo katika hatua ya kuboresha kwa kufanya ukarabati wa bandari kama vile bandari ya Dar es Salaam na Mtwara;

**Kwa hiyo basi**, Kamati inaendelea kusisitiza ushauri inaishauri yafuatayo; -

a) Kubakisha angalau **asilimia 40** ya makusanyo ya Mamlaka ya Bandari Tanzania ili Mamlaka hii iweze kuendeleza baadhi ya miradi katika bandari zake, kama vile, miradi ya ujenzi wa bandari ya Kalema, Kigoma na Mtwara, ambayo inagharimu takribani **shilingi bilioni 20** wakati mapato ya bandari kwa mwaka ni takribani **shilingi bilioni 270**;

b) Kuharakisha mchakato wa ununuzi wa flow meter mpya kwa ajili ya upimaji wa mafuta yanayoingia Bandari ya Dar es Salaam. Kutokuwepo kwa mtambo wa kupima kiasi cha mafuta (flow meter) kunasababisha kutokujua kwa uhakika kiwango cha mafuta kinachoingia bandari ya Dar es Salaam;

c) Kufanyike juhudi za makusudi ili kuweza kuhamisha Gati la Mafuta lililopo kurasini (KOJ) na kujenga Gati Namba 13 na 14;

d) Serikali kufanya ukarabati wa bandari zingine muhimu kama vile bandari ya Tanga, Mtwara, Mwanza, Kigoma na bandari ya ziwa Nyasa. Vilevile, bandari zilizo katika vipaumbele vya Serikali kama vile Bandari ya Mbegani- Bagamoyo na Bandari ya Mwambani- Tanga kuanza kutekelezwa;

e) Wadau wote wa bandari waunganishwe kwenye mfumo wa kielektroniki unaotumiwa na bandari ili kuweza kuharakisha uondoshwaji wa mizigo bandarini kwani wakati mwingine mizigo inachelewa kutokana na wadau wengine kama Mkemia mkuu, Shirika la Viwango Tanzania-

(TBS), Wizara ya Nishati na Wizara ya Madini na wengine wengi kutokuwemo kwenye mfumo huo;

f) Mchakato wa kuwa na eneo Kurasini-Shimo la Udongo ambalo litatumika kuegesha magari yanayoingiza na kutoa mizigo bandarini sasa ufanyike kwa haraka ili eneo hilo lipatikane kwani mojawapo ya kero za wafanyabishara wanaotumia Bandari ya Dar es Salaam ni kutokuwa na maegesho jambo ambalo husababisha usumbufu na gharama zisizotabirika;

g) Serikali kuharakisha ujenzi wa bandari za nchi kavu ili kupunguza gharama kwa wateja kusafiri mpaka Dar se salaam kwa ajili ya kutoa mizigo. Ni muda sasa tangu Serikali imeanza mipango ya kujenga bandari kavu katika maeneo ya Kwala -Pwani, Ihumwa -Dodoma, Katosho-Kigoma na Misungwi –Mwanza;

h) Serikali kuharakisha majadiliano na wabia ili ujenzi wa Bandari ya Bagamoyo uweze kuanza kwani kukamilika kwa bandari hii kutatoa fursa nyingi za kiuchumi katika ukanda huo. Vile vile, Serikali kulipa fidia kwa wananchi waliobakia ndani ya eneo linalotarajiwa kujengwa bandari hii ili kuepuka migogoro isiyo ya lazima wakati mradi huu utakapoanza

i) Watumishi wa bandari nchini wapewe nafasi ya kwenda kujifunza katika Bandari nyingine zinazofanya vizuri ili kuweza kufahamu wenzao wanachokifanya; na hatimaye kuweza kubaini mbinu za ushindani katika biashara;

j) Bandari Bubu zirasimishwe haraka ili zifanye kazi kulingana na kanuni na taratibu za kisheria na kuongeza wigo wa ukusanyaji kodi na udhibiti wa biashara haramu.

3.2.2 **Ujenzi wa reli nchini**

**Kwa Kuwa**, Serikali imeonesha nia ya dhati ya kujenga upya Reli ya Kati katika kiwango cha kisasa (standard gauge); ambapo mradi umeanza mwezi April, 2017 na unatekelezwa kwa awamu tano;

**Na kwa Kuwa**, katika uhalisia Tawi la kutoka Tabora- Kigoma-Uvinza- Msongati na Kaliua-Mpanda-Kalema ndilo lenye mizigo mingi inayotoka na kwenda nchi za jirani kama vile DR Congo, Burundi na Rwanda;

**Kwa hiyo basi**, Kamati inaendelea kusisitiza ushauri wake kuwa; -

a) Ujenzi wa reli hii uzingatie kwanza maeneo yenye faida za kichumi na kipaumbele cha kwanza kiwekwe katika tawi lenye mzigo mkubwa ambalo ni tawi la Tabora – kigoma -Uvinza- Msongati; Kaliua – Mpanda –Kalema;

b) Serikali izingatie kuwashirikisha wataalam wa ndani (wazawa) katika ujenzi wa reli ya kati ili kuwa na mradi endelevu pale wataalam wa nje watakapoondoka; na

c) Serikali iangalie uwezekano wa kupata mkopo wa gharama nafuu ambao utatumika kununua vichwa na mabehewa ya treni ili Shirika la Reli Tanzania- TRC liweze kuondokana na changamoto ya upungufu wa vichwa vya treni arobaini na tano (45) pamoja na mabehewa ili TRC iweze kufanya kazi zake kwa ufanisi na kuanza kupata faida;

d) Ili kuepusha uvamizi wa maeneo ya reli, ni vema sasa Shirika la Reli Tanzania kuweka alama zinazoonesha mwisho wa eneo la reli ili kuondoa usumbufu kwa wananchi; na

e) Shirika la reli kuanza kujiendesha kisasa kwa kufunga vyombo vya kielektroniki ili kuweza kutunza kumbukumbu zote za kiutendaji, ufatiliaji wa mizigo kwa wateja, uthibiti wa mafuta, udhibiti wa mwendo na usalama. Hii italifanya Shirika hili kuweza kujiendesha kisasa na kupunguza gharama za uendeshaji;

3.2.3 **Utendaji wa Reli ya Tanzania na Zambia (TAZARA)**

**Kwa Kuwa,** TAZARA inamilikiwa na nchi mbili (Tanzania na Zambia) kwa asilimia 50:50;

**Na kwa Kuwa**, kwa muda sasa utendaji wa TAZARA umekuwa si wakuridhisha;

**Kwa hiyo basi,** Kamati inashauri yafuatayo: -

a) Serikali iweke mkakati wa dhati kuinusuru TAZARA ili iweze kujiendesha. Moja ya mkakati uwe ni kufanya mazungumzo na Serikali ya Zambia na kufikia muafaka wa namna bora ya uendeshaji wa reli hii, ikiwa ni pamoja na, kufanya mapitio ya kurekebisha Sheria iliyoianzisha TAZARA, Namba 23 ya Mwaka 1975;

b) Serikali ilipe madeni ya wafanyakazi; pamoja na, kuendelea kusaidia kulipa wafanyakazi wa TAZARA mishahara mpaka hapo itakapowekeza mtaji wa kutosha; na

c) Serikali kujenga kipande cha reli chenye urefu wa kilometa 18 kwenda kwenye mgodi wa Magamba ili kuweza kurahisisha usafishaji wa makaa ya mawe kwani mzigo unaotoka ni mkubwa hivyo unaweza kupatia TAZARA mapato ya kutosha kujiendesha.

3.2.4 **Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania-TAA**

**Kwa Kuwa**, Mamlaka ya Viwanja vya Ndege ndio iliyokasimiwa jukumu la kusimamia na kuendesha viwanja vya ndege nchini;

**Na kwa kuwa**, Kamati imebaini changamoto mbalimbali zinazokabili viwanja vya ndege nchini ikiwemo migogoro ya mipaka;

**Kwa Hiyo Basi,** Kamati inaishauri yafuatayo; -

a) Kuhakikisha inapata hati za Viwanja vya Ndege kwani Kamati imejulishwa kuwa viwanja vya ndege kumi na moja (11) vimeshapatiwa hati miliki kati ya viwanja hamsini na nane (59) vinavyomilikiwa na Mamlaka ya Viwanja vya Ndege. Vile vile, kuhakikisha viwanja vingine vilivyobakia vinapimwa na kupatiwa hati miliki pamoja na uzio ili kujiepusha na uvamizi wa maeneo jambo ambalo huleta migogoro na wananchi na kusababisha Serikali kuingia gharama kubwa kwa ajili ya fidia; na

b) Kuongeza udhibiti na ulinzi katika Viwanja vya Ndege vilivyopo Mikoani hasa vilivyopo mpakani kama vile Mtwara, Kigoma na Kagera ili kuepuka viwanja hivi kupitishwa biashara haramu;

3.2.5 **Kampuni ya Ndege ya Tanzania-ATCL**

**Kwa Kuwa**, Serikali imechukuwa hatua ya kufufua Shirika la ndege la Tanzania kwa kuwekeza kununua ndege mpya;

**Na kwa Kuwa**, ndege hizo zitakuwa kichocheo cha Uchumi wa Tanzania katika kuwawezesha kupata usafiri wa ndani na nje ya nchi, hivyo kutimiza malengo na kukuza Pato la Taifa;

**Kwa hiyo Basi,** Kamati inaishauri yafuatayo:-
a) Kuwa na mikakati mikubwa ya kitaifa ya kuhakikisha kuwa ATCL inakuwa na uwezo wa kushindana na kutengeneza faida;

b) ATCL iangaliwe kama Kampuni ya kibiashara na sio yakutoa huduma;

c)ATCL ijitangaze kwenye vyombo vya Kimataifa ambavyo huonyesha safari za ndege dunia nzima. Aidha, Kampuni hii sasa ijipange kuingia katika soko kwa kujitangaza katika vyombo vya habari, majarida na vipeperushi mbalimbali;

d) Shirika liendelee kufanya utaratibu wa kuongeza safari za ndani na za kikanda ili kuimarisha mtandao wa safari zake;

e) ATCL ichukue hatua madhubuti ili kuimarisha utalii wa ndani ya nchi;

f) Ni vema Shirika likajipanga kumudu ushindani wa kibiashara katika safari za Kimataifa;

g) Kuwa na mkakati wa kuongeza marubani pamoja na maslahi yao ili kuwa katika nafasi nzuri kibiashara;

h) Shirika lisimamie ipasavyo nidhamu ya watumishi wake kwani yamekuwapo malalamiko kutoka kwa wateja kuhusu vitendo vya ukosefu wa nidhamu kwa baadhi ya watumishi. Vilevile, watumishi waajiriwe kwa kuzingatia vigezo vya sifa na uwezo.

3.2.6 **Kampuni ya Huduma za Meli (MSCL)**

**Kwa Kuwa**, Serikali imeonesha dhamira ya dhati ya kuikwamua Kampuni ya Huduma za Meli kwa kulipa malimbikizo ya miezi ishirini na nane (28) ya mishahara ya wafanyakazi pamoja na kuanza ukarabati na matengezo ya meli katika maziwa makuu;

**Na Kwa Kuwa,** uwekezaji huu ni mkubwa ambao unahitaji mikakati na mipango kabambe kuhakikisha MSCL inainuka na kuweza kujiendesha pasizo ruzuku ya Serikali na hata kutoa gawio kwa Serikali;

**Kwa Hiyo Basi,** Kamati inashauri yafuatayo: -

a) Serikali kujipanga kutengeneza Meli zote kumi na nne (14) zilizopo katika Maziwa Makuu ili kuiwezesha Kampuni ya Meli Tanzania kumudu kujiendesha kibiashara; Aidha, kipaumbele kiwekwe kwa Ziwa Tanganyika ambako kuna uhitaji mkubwa ya usafiri katika Ziwa Tanganyika, Serikali sasa iharakishe ujenzi wa meli mpya na kufanya ukarabati wa meli ya MV Liemba;

b) Kampuni ya Huduma za Meli kupanga mipango ya kujiendesha kisasa kwa kuweka teknolojia ya kufatilia matumizi ya mafuta kwenye meli (Flow Scanner) na kuweka mfumo wa kuweza kufatilia mahali meli ilipo kila wakati (trucking system) kwani hii itasaidia kuziba mianya ya upotevu wa fedha za Kampuni; na

c) Kampuni ya Meli Tanzania kufanya kazi kwa ukaribu na Mamlaka ya Bandari Tanzania pamoja na Shirika la Reli kwani kufanya hivyo kutawezesha kuongeza hamasa kwa wafanyabiashara kuweza kusafirisha mizigo toka Dar es salaam mpaka Uganda na hatimaye kupunguza gharama kwa wafanyabiashara na kuongeza pato la Taifa na hata kufikia kuweza kutoa gawio la faida kwa Serikali;

### 3.3 **Sekta ya Ujenzi**

#### 3.3.1 **Wakala wa Barabara Tanzania-TANROADS**

**Kwa Kuwa**, Wakala wa Barabara nchini- TANROADS ndio umekabidhiwa jukumu la ujenzi na ukarabati wa barabara kuu nchini;

**Na kwa Kuwa**, pamoja na jitihada za Serikali kujenga barabara; bado kumeendelea kuwepo na changamoto mbalimbali kama vile barabara kuharibika, matuta yasiyo na viwango, uzito uliozidi wa mizigo unaoharibu barabara na wizi wa alama za barabarani;

**Kwa hiyo Basi,** Kamati inazidi kusisitiza ushauri ufuatayo; -

a) Serikali ifanye mapitio mapya kwa ajili ya kuongeza fedha za dharura kwa ajili ya barabara hasa ukizingatia mvua kubwa zinazoendelea kunyesha nchini ambazo zimesababisha uharibifu mkubwa sana. Mfano; gharama za kazi za dharura zimekadiriwa kuwa jumla ya **shilingi bilioni 15** ambazo ni zaidi ya bajeti ya dharura iliyopangwa kwa mwaka 2019/20 ya **shilingi bilioni 8.297;**

b) Serikali iangalie upya taratibu za manunuzi pamoja na upatikanaji wa hati ya msamaha wa kodi ya ongezeko la thamani (VAT) kwani taratibu hizi zimekuwa ni moja ya sababu za ucheleweshaji wa miradi;

c) Kukarabati baadhi ya barabara za Mikoa zilizo katika hali isiyoridhisha na kutopitika hasa wakati wa mvua na kuathiri shughuli za kiuchumi na kijamii;

d) Kuhakikisha inaunganisha Miji yote Mikuu na Mikoa iliyosalia kama vile Mikoa ya Katavi- Kigoma, Katavi-Tabora, Kigoma-Kagera na Njombe-Makete-Mbeya kwa barabara za lami ili kufungua fursa za maendeleo katika maeneo hayo;

e) Kuendelea na ujenzi wa barabara za lami hasa maeneo yanaochochea Uchumi wa Taifa letu kama vile maeneo yenye vivutio vya utalii, kilimo, viwanda na madini;

f) Wizara ya Ujenzi isimamie Sheria za barabara kwa kutoa elimu kwa wananchi kwa kutumia vyombo vya habari kama runinga, magazeti na redio. Pia kufanya mikutano na kuweka alama zitakazoonesha mwisho wa eneo la barabara;

g) Matuta madogo madogo ya barabarani maarufu kwa jina la rasta na matuta makubwa yasiyo na kiwango yaondolewe kwa kuwa yanasababisha ajali na uharibifu wa magari. Aidha matuta yabaki sehemu zenye umuhimu tu na yawe na kiwango maalumu;

h) Kutungwa kwa Sheria ya kudhibiti uuzaji wa vyuma chakavu ili kunusuru miundombinu yetu iliyogharimu fedha nyingi na kwa usalama wa watumiaji wa barabara zetu; na

i) Kuendelea kununua mizani ya kisasa ambazo zinauwezo wa kupima uzito wa magari huku yakiwa kwenye mwendo (Weight in Motion) na kuzifunga katika maeneo yenye msongamano mkubwa wa kupima magari;

j) Halmashauri zishirikiane na TANROADS na TARURA kutenga maeneo ya kuegesha magari (parking) ili kuzuia magari yanayoegeshwa muda mrefu kandokando mwa barabara na kusababisha uharibifu;

k) Barabara zinazounganisha Mikoa hususan barabara ya Lindi- Morogoro ijengwe ili kurahisisha usafiri na kupunguza umbali kwa wananchi wanaotoka Mikoa ya Lindi, Mtwara; Pia barabara

ya Arusha-Ngorongoro-Serengeti na barabara ya Simiyu-Arusha, barabara ya Kibingo-Kibondo-Kasulu, barabara ya Malagarasi-Uvinza na barabara ya Kazilambwa-Ilunde;

l) Fidia itolewe kwa wananchi ambao wamepisha ujenzi miundombinu mbalimbali nchini hususan barabara;

m) Ujenzi wa barabara uzingatie pia ahadi mbalimbali zilizotolewa na viongozi; na

n) Katika mikataba ya ujenzi wa barabara kuwe na kipengele cha wakandarasi kupanda miti pembeni mwa barabara ili kuboresha mazingira ya barabara na kupendezesha miji;

3.3.2 **Ujenzi wa Viwanja vya Ndege**

**Kwa kuwa**, Wakala wa Barabara Tanzania-TANROADS umepewa jukumu la ujenzi wa Viwanja vya Ndege nchini;

**Na kwa kuwa**, bado kuna changamoto kubwa ya ujenzi na uboreshaji wa viwanja vya ndege;

**Kwa hiyo basi**, Kamati inashauri yafuatayo: -

a) Serikali kuhakikisha inatoa kwa wakati fedha yaliyoidhinishwa kuendeleza viwanja vya ndege nchini hususan Kiwanja cha ndege cha Mwanza, Songwe na Mtwara;

b) Katika ujenzi na ukarabati wa Viwanja vya Ndege, Serikali ijikite zaidi katika kujenga na kuendeleza viwanja vya ndege vya kimkakati ambavyo vitasaidia kukuza pato la taifa kwani Kamati imebainika kuwa kati ya Viwanja vya ndege 59, Viwanja vitano tu (5) tu sawa na 8% ndivyo vinavyochangia mapato ya Serikali;

c) Kuboresha mifumo ya jengo la pili la abiria Katika Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Julius Nyerere Dar es Salaam, ili kuwa na muonekano mzuri na kuleta taswira nzuri ya nchi; na

d) Kuharakisha ulipaji wa fidia kwa wananchi waliopisha ujenzi wa viwanja ndege.

3.3.3 **Wakala wa Majengo Tanzania**

**Kwa Kuwa**, Kumekuwepo na changamoto ya mahitaji makubwa ya nyumba kwa ajili ya watumishi wa umma na ujenzi wa majengo ya Serikali;

**Na kwa Kuwa,** kumekuwepo pia na ushindani mkubwa katika nyanja za ujenzi nchini;

**Kwa Hiyo Basi,** Kamati inalishauri Bunge kuwa;

a) Serikali kuimarisha uwezo wa Wakala wa Majengo Tanzania-TBA ili iweze kuzalisha fedha na kuchangia Pato la Serikali. Ni vyema Wakala huu pamoja na kujenga nyumba za gharama nafuu, kuhakikisha nyumba hizo zinakuwa katika hali ya ubora na viwango vinavyostaili;

b) Wakala wa Majengo nchini kufanya ukarabati wa nyumba zake zilizo maeneo mbalimbali ya nchi kwani nyingi ziko katika hali isiyoridhisha hasa kwenye mifumo ya umeme na maji machafu na hivyo kuhatarisha maisha ya wapangaji;

c) Serikali itenge fedha kwa ajili ya kufanya ukarabati kwenye majengo ya Ikulu ndogo zilizopo kwenye Wilaya mbalimbali nchini kote;

d) Serikali kuajiri wafanyakazi wa kutosha ili kuongeza usimamizi wa miradi mingi na mikubwa inayosimamiwa na Wakala huu; na

e) Serikali na taasisi zake kuhakikisha zinalipa madeni yote yanayodaiwa na Wakala wa Majengo kwani madeni hayo yamekuwa moja ya kikwazo kinachozorotesha maendeleo ya Wakala.

#### 3.3.4 **Chuo cha Ujenzi Morogoro na Chuo cha Mafunzo ya Teknolojia Stahiki ya Nguvu Kazi Mbeya**

**Kwa Kuwa**, vyuo hivi vimekuwa vikitoa mafunzo ya teknolojia stahiki ya nguvukazi katika ukarabati na matengenezo ya barabara kwa wasimamizi, wakaguzi wa barabara, wahandisi na mafundi;

**Na Kwa Kuwa,** vyuo hivi vimekuwepo kwa muda mrefu, lakini bado havijasajiliwa jambo ambalo halitoi hamasa kwa wengi kujifunza katika Vyuo hivi;

**Kwa hiyo basi,** Kamati inashauri yafuatayo: -

a) Serikali iviunganishe vyuo hivi na kuvisajili ili mafunzo yanayotolewa katika vyuo hivi yaweze kutambulika;

b) Serikali ivitengee bajeti ya kutosha vyuo hivi ili viweze kuwa na mvuto kwa watu wengi kujiunga na kupata elimu kwani bado kuna uhitaji mkubwa wa wataalam hasa wa barabara katika Halamashauri nchini ambapo wataalam hao wanategemewa kutoka katika vyuo hivi; na

c) Serikali inunue mitambo angalau mitatu (3) mipya kwa ajili ya kufundisha kwa vitendo kwani taaluma inayotolewa katika Chuo cha Ujenzi Morogoro inahitaji elimu ya vitendo zaidi kuliko nadharia.

#### 3.3.5 **Wakala wa Ufundi na Umeme Tanzania-TEMESA**

**Kwa kuwa,** Wakala wa Ufundi na Umeme Tanzania unakabiliwa na changamoto zikiwemo za ukosefu wa rasilimali watu wenye ueledi wa kwenda samabamba na mabadiliko ya teknolojia, vifaa vya kisasa vinavyoweza kuendana na magari, na ukosefu wa mitambo ya kisasa;

**Na kwa Kuwa**, changamoto hizi zinaisababisha TEMESA kufanya kazi kwa kubahatisha ambako kunatumia muda mwingi na gharama kubwa;

**Kwa hiyo Basi,** Kamati inashauri yafuatayo: -

a) Serikali kuajiri wataalaum waliobobea kwenye fani ya ufundi wa magari na kuhakikisha kunakuwa na mitambo ya kisasa ili kuendana na kukua kwa teknolojia kwani mara nyingi magari ya Serikali yamekuwa yakitengenezwa kwenye karakana binafsi za mitaani jambo ambalo si sahihi;

b) Wakala wa Ufundi na Umeme kuharakisha mchakato wa kuchagua karakana za kutengeneza magari ya Serikali kwenye Wilaya ili kuondoa usumbufu wa magari ya Serikali kusafiri umbali mrefu kwenda kufanya matengenezo kwani kuna Wilaya zingine ziko umbali mrefu kwenda Makao Makuu ya Mkoa;

c) Wakala kuchukuwa hatua za makusudi na kuweka mkakati wa kudumu ili kukusanya madeni yake ambayo kwa kiasi kikubwa inazidai taasisi za Serikal ili Wakala huu uweze kijiendesha kibiashara badala ya kutegemea ruzuku kutoka Serikalini; na

d) Udhibiti wa Mapato katika vivuko, ni vema Serikali ione umuhimu wa kuwa na mashine za kukata tiketi za kieletroniki na kutenga eneo kwa abiria ambao tayari wameshakata tiketi kama inavyofanyika katika kivuko cha Magogoni Dar es Salaam kwani bado watu wengi wanapita na kusafiri kutumia vivuko pasipo kulipa nauli. Haya yafanyike katika vivuko vyote nchini ili kuepusha upotevu wa mapato kwa Serikali;

3.4 **Sekta ya Mawasiliano**

3.4.1. **Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania-TCRA**

**Kwa kuwa**, zoezi la usajili wa laini za simu ni endelevu na limekuwa na changamoto ambapo wananchi wengi wameshindwa kusajili kutokana na kutokupata namba ya usajili wa NIDA au Kitambulisho cha Taifa;

**Na kwa Kuwa**, takribani laini Milioni 15 zimefungiwa kwa kukosa usajili wa biometria, jambo ambalo linaweza kusababisha upotevu wa fedha kwa Serikali;

**Kwa Hiyo Basi,** Kamati inashauri Serikali yafuatayo: -

a) Serikali itenge fedha za kutosha kwa Wizara ya Mambo ya Nchi, ili NIDA iweze kuwa na mitambo mingi ya kutengeneza vitambulisho. Hili liende sambamba na kuongeza rasilimali watu ambao watasaidia usajili wa kupata vitambulisho vya Taifa hasa kwenye maeneo ya vijijini na pembezoni mwa nchi;

b) Utambuzi wa wananchi kwa ajili ya kupata vitambulisho NIDA, ishirikishe viongozi katika ngazi za vijiji ili kuweza kupata uhakika wa uhalali wa uraia na kurahisisha zoezi la kupata vitambulisho;

c) TCRA kwa kushirikiana na NIDA, ziandae utaratibu (application) ambao utamwezesha mwananchi kutambua laini za simu ambazo zimesajiliwa kwa kutumia kitambulisho chake cha Taifa.Utaratibu huu utamwezesha mwananchi kufanya mawasiliano na NIDA pamoja na TCRA ili waweze kubaini umiliki wa simu hizo na kuchukuwa hatua stahiki;

d) Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania iendelee kutoa elimu kwa umma na taarifa kwa wananchi kupitia redio, magazeti, mitandao ya kijamii kuhusu usajili wa laini za simu;

e) TCRA, iendelee kuutunza na kuusimamia Mfumo wa usimamizi na ufuatiliaji wa mawasiliano ya simu (TTMS);

f) Kuendelea kudhibiti mawasiliano ya ulaghai na hatimaye kupunguza vitendo viovu vinavyofanyika kupitia njia ya mtandao na ili kuimarisha usalama wa watu na mali zao; na

g) Kuendelea kukabiliana na changamoto za kukua kwa teknolojia ya habari na mawasiliano na changamoto zake kama vile uhalifu mitandaoni unaojumuisha kashfa kwa watu, usambazaji wa picha zisizostaili hivyo kuharibu maadili, mila na desturi zetu. Aidha, Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania-TCRAiendeleekuisaidiaJeshilaPolisikatikakutekelezasheriaya Cyber Crimena kuwabana wahalifu.

3.4.2. **Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote-UCSAF**

**Kwa Kuwa**, Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF) ulianzishwa kwa lengo la kusambaza mawasiliano hasa katika maeneo ya pembezoni yasiyo na mvuto wa kibiashara;

**Na kwa Kuwa,** Kamati ilibaini masuala mbalimbali yanayohitaji kutafutiwa ufumbuzi ili Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote uweze kuimarika na kufanya kazi zake vizuri;;

**Kwa Hiyo Basi**, Kamati inaendelea kusisitiza ushauri wake kwamba:-

a)Serikali kupitia na kuangalia upya taratibu za umilikishwaji ardhi hasa maeneo yanayojengwa minara ili kuweka utaratibu wa maeneo yaliyokodiwa ama kununuliwa kwa ajili ya ujenzi wa minara kumilikiwa na Serikali za vijiji husika. Hii itasaidia sana kwani fedha zitakazopatikana kutokana na kukodi ama kununua eneo la mnara zitatumika kwa maendeleo ya wananchi waliowengi tofauti na ilivyo sasa ambapo maeneo mengi yaliyojengwa minara yananufaisha watu wachache na baadhi ya Serikali za vijiji kutokuambulia chochote;

b)Serikali kuhakikisha inawekwa mabango yanayoonesha ushiriki wake katika ujenzi wa minara ambayo imetoa ruzuku;

c)Serikali kuweka mpango wa uwiano wa mawasiliano nchi nzima hasa maeneo ya mipakani ambapo mara nyingi watu katika maeneo hayo hupata mawasiliano ya nchi jirani jambo ambalo linawakosesha haki yakupata taarifa za nchi yao;

d)Serikali kuhakikisha inasimamia kuwepo kwa ushirikiano katika mifumo ya miundombinu (Infrastructure Sharing) na kuyaelekeza makampuni ya simu kushirikiana katika ujenzi wa minara na kufunga antenna zao katika mnara mmoja ili kuepuka matumizi ya eneo kubwa la ardhi kwa kuwa mlundikano wa minara katika eneo moja;

e)Halmashauri na Serikali za vijiji zitoe ushirikiano wa kutosha na wa haraka pale ambapo maeneo yanahitajika kwa ajili ya ujenzi wa minara ili kuweza kurahisisha kupata mawasiliano;

f)Mfukowa Mawasiliano kwa Wote utoe elimu kwa wananchi ili wajue umuhimu na uwekezaji unaofanywa na Serikali katika kuleta maendeleo hususan katika ujenzi wa minara ya mawasiliano ili wananchi watoe ushirikiano wa ulinzi ili vifaa vya minara view salama;

g)Serikali kujenga miundombinu ya barabara katika maeneo yaliyojengwa minara ili kurahisisha utoaji wa huduma za minara na wananchi kwaujumla. Vilevile kurahisisha shughuli zingine za maendeleo kama vile utalii, kilimo na hata uwekezaji; na

h)Minara yote iliyojengwa na inayoendelea kujengwa iwe kwenye uwezo wa 3G na 4G tofauti na ilivyo sasa katika viwango vya 2G ambayo inanyima wananchi wengi fursa ya huduma ya data ambayo ingeweza kurahisisha huduma za afya(afya mtandao), elimu mtandao.

3.4.2 **Mradi wa Anuani za Makazi na Misimboya Posta**

**Kwa Kuwa**, kutekelezwa kwa mradi huu kuna manufaa makubwa kwani utawezesha kuwepo kwa utambulisho wa makazi ya watu na makampuni na hatimae kurahisisha shughuli zoteza kijamii, kiuchumi na kisiasa;

**Na kwa Kuwa,** Kamati hairidhishwi na utekelezaji wa mradi huu kwani umekuwa ukisuasua;

**Kwa Hiyo Basi,** Kamati inashauri yafuatayo;-

a) Wizara husika ikiwemo Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi; TAMISEMI na Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano zikae na kuona namna nzuri ya kuhakikisha mradi huu muhimu unatekelezwa haraka na kwa ufanisi ; na

b) Fedha kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huu zitolewe kama zilivyoidhinishwa na kwa wakati ili mradi huu muhimu ukamilike.

3.4.3 **Shirika la Posta Tanzania**

**Kwa Kuwa**, Shirika la Posta linahitaji mtaji ili liweze kujiendesha kibiashara na kukabiliana na ushindani wa soko katika sekta ya posta;

**Na Kwa Kuwa,** pamoja na changamoto ya mtaji pia linakabiliwa na changamoto ya Madeni ya pensheni kwa wafanyakazi wa iliyokuwa Posta ya Jumuiya ya Afrika Mashariki;

**Kwa hiyo basi,** Kamati inashauri yafuatayo: -

(a) Serikali ichukuwe jukumu la kulipa madeni ya pensheni kwa wafanyakazi wa iliyokuwa Posta ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ili kuliondolea Shirika mzigo wa kulipa wastani wa **shilingi milioni 74** kila mwezi, fedha ambazo zingeelekezwa kwenye uendeshaji wa shirika;

(b) Serikali kupitia Wizara ya Fedha na Mipango kuona namna ya kufuta deni lililosalia la **shilingi bilioni 15** baada ya kusamehe **shilingi bilioni 12** zilizokuwa za riba, tozo na adhabu ambazo Shirika la Posta lilikuwa na Mamlaka ya Mapato Tanzania -TRA; na

(c) Serikali iliondoe Shirika la Posta katika orodha ya mashirika yanayosubiri kurekebishwa ili liweze kutumia rasilimali zilizopo kufanya uwekezaji kwa lengo la kujiendesha kwa tija;

3.4.4 **Shirika la Simu Tanzania-(TTCL Corporation)**

**Kwa Kuwa,** Shirikala Mawasiliano Tanzania linaendelea kukabiliwa na changamoto kubwa ya madeni ambayo inaidai Serikali pamoja na vyombo vyake**;**

**Na kwa Kuwa,** madeni haya yanaathiri utendaji kazi wa Shirika;

**Kwa Hiyo Basi,** Kamati inashauri yafuatayo: -

a) Serikali kuhakikisha Wizara, Taasisi na Mashirika yake yote yanayodaiwa na TTCL yanakuwa mfano kwa kulipa madeni yote yanayodaiwa na TTCL kwa kuwa fedha hizo za gharama za simu hutengwa kila mwaka katika bajeti za Wizara/Taasisi na Mashirika yao;

b) Shirika la Mawasiliano Tanzania liweke mikakati madhubuti ya kukusanya madeni;

c) Serikali ikamilishe Kanuni za namna ya kuendesha na kusimamia miundombinu ya kimkakati ya mawasiliano;

d) Serikali kuhakikisha kunakuwa na mpango endelevu wa kuulinda na kuuendeleza Mkongo wa Taifa;

e) Serikali ifikie makubaliano ya jinsi TTCL inavyoweza kufaidika kifedha kutokana na jukumu lake la usimamizi na uendeshaji wa Mkongo wa Taifa; na

f) Serikali iangalie namna itakavyoweza kusaidia TTCL kwa kupunguza urasimu uliopo katika hatua za manunuzi ya umma, ili TTCL iweze kwenda kasi na kuweza kushindana na Makampuni mengine ya mawasiliano.

**SEHEMU YA NNE**

4.0 **HITIMISHO**

**Mheshimiwa spika,** napenda kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha Taarifa ya hii mbele ya Bunge lako Tukufu. Aidha, kwa namna ya pekee napenda kumpongeza na kumshukuru Waziri wa Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Mhe. Eng. Isack Kamwelwe (Mb) akishirikiana na Manaibu Mawaziri Mhe. Eng. Atashasta Nditiye, (Mb) na Mhe. Elias Kwandikwa, (Mb).

Aidha, Kamati inawashukuru Makatibu Wakuu wa Wizara hii Arch. Elius A. Mwakalinga (Sekta ya Ujenzi); Eng. Dkt. Leonard Chamuriho (Sekta ya Uchukuzi), Eng. Dkt. Maria Sasabo (Sekta ya Mawasiliano); pamoja na Naibu Katibu Mkuu Dkt. Jim Yonazi. Kamati pia inawashukuru Wakuu wa Taasisi, Wakurugenzi na wafanyakazi wote ambao wameipa Kamati ushirikiano mkubwa. Ni kwa ushauri na utaalam wao umeiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake na kuwasilisha taarifa hii leo katika Bunge lako tukufu.

**Mheshimiwa Spika**, vile vile nachukua fursa hii kumshukuru Katibu wa Bunge Ndugu Stephen Kagaigai kwa kuiwezesha Kamati wakati wote ilipokuwa inatekeleza majukumu yake. Aidha, shukrani za pekee ziende kwa Mkurugenzi wa Idara za Kamati za Bunge Ndugu. Michael Chikokoto, Mkurugenzi Msaidizi Ndugu. Gerald Magili Katibu wa Kamati Ndugu Hosiana John. Vilevile, nawashukuru wafanyakazi wote wa Ofisi ya Bunge kwa ushirikiano wao ulioiwezesha Kamati yangu kutekeleza majukumu yake ipasavyo.

4.1 **Hoja**

**Mheshimiwa Spika,** baada ya kueleza shughuli zilizotekelezwa na Kamati, Maoni na Ushauri, sasa naomba kutoa Hoja kwamba Bunge lipokee, lijadili na kuikubali Taarifa ya Mwaka ya Shughuli za Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu kwa kipindi cha Januari 2019 hadi Januari 2020 pamoja na Maoni na Ushauri uliopo katika taarifa hii.
**Mheshimiwa Spika,** naomba kutoa hoja.

Moshi Seleman Kakoso, Mb
**MWENYEKITI**
**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MIUNDOMBINU**
31 Januari, 2020

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Hoja imetolewa imeungwa mkono. Tunakushukuru sana Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu Mheshimiwa Kakoso. *(Makofi)*

Ahsante. Namwita sasa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira. Makamu. *(Makofi)*

**MHE. KANALI (MST) MASOUD ALI KHAMIS - MAKAMU MWENYEKITI WA KUDUMU WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA VIWANDA, BIASHARA NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamazi za Kudumu za Bunge za Viwanda Biashara na Mazingira, naomba kuwasilisha Taarifa ya Mwaka ya Shughuli zilizotekelezwa na Kamati ya

Kudumu ya Bunge ya Viwanda Biashara na Mazingira katika kipindi cha kuanzia Februari, 2019 hadi Januari 2020.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 117(15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016; kwa niaba ya Wajumbe wenzangu wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda Biashara na Mazingira, naomba kuwasilisha taarifa inayoelezea shughuli zote zilizotekelezwa na Kamati kwa kipindi cha kuanzia Februari, 2019 hadi Januari, 2020. Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira inatekeleza majukumu yake kwa mujibu wa fasili ya 6(1) ikisomwa pamoja na fasili ya 7(1) ya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Januari, 2016.

Mheshimiwa Mwenyekiti, majukumu yaliyotekelezwa na Kamati katika kipindi cha Februari, 2019 hadi Januari, 2020 kwa kuzingatia kanuni tajwa hapo juu ni pamoja na kupokea taarifa za utekelezaji wa majukumu ya Wizara na taasisi zinazoripoti kwa Kamati; Ukaguzi wa miradi ya maendeleo, kuchambua Taarifa za Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 pamoja na makadirio na mapato na matumizi ya mwaka unaoendelea wa 2019/2020; kuchambua na kushauri juu ya Mikataba ya Kimataifa inayopendekezwa kuridhiwa na Bunge ambayo iko chini ya Wizara zinazoisimamia; Vikao na wadau wa Sekta zinazosimamiwa na Kamati kwa lengo la kusikiliza maoni yao na kushiriki warsha na semina za kujenga uelewa kwa Wajumbe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati wa kupitia na kuchambua Taarifa ya Utekelezaji wa Wizara ya Viwanda na Biashara pamoja na Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira), kwa mwaka wa fedha 2018/2019, Kamati ilitoa mapendekezo kwenye maeneo kadhaa. Kamati imearifiwa kuwa na utekelezaji wa mapendekezo hayo na kujiridhisha kuwa Serikali imejitahidi kuzingatia mapendekezo ya Kamati. Hata hivyo, kuna baadhi ya mapendekezo ambayo Kamati iliyaona hayajatekelezwa kwa ufanisi na kushauri Serikali kuongeza kasi ya utekelezaji wa mapendekezo hayo. Mapendekezo hayo ni kama yanavyoonekana katika Taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Viwanda, Biashara na Mazingira ilifanya ziara za ukaguzi wa ufanisi uliopo katika kutekeleza Miradi ya Maendeleo kama inavyoelekezwa na Kanuni ya 98 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge. Miradi iliyotembelewa na Kamati ni pamoja na Mradi Na. 6260 ambao unahusu kuziongezea uwezo taasisi mbalimbali zilizopo chini ya Wizara ya Viwanda na Biashara; Mradi Na. 5301unaohusu Mabadiliko wa Tabianchi katika Mji wa Bagamoyo; na Mradi Na. 6507unaohusu Ujenzi wa Ofisi ya Baraza la Taifa la Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira na Shughuli za Usimimamizi wa Mazingira katika Ziwa Manyara.

Mheshimiwa Mwneyekiti, maelezo ya utekelezaji wa miradi ni kama inavyoonekana kwenye taarifa ya Kamati kwa sababu ya muda naomba nisiisome.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama inavyoelekezwa na Kanuni 98 (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Kamati ya Viwanda Biashara na Mazingira ilifanya uchambuzi wa Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara inayozisimamia. Kwa mwaka wa fedha 2018/2019 pamoja na kufanya ulinganisho wa utekelezaji wa bajeti ya makadirio mapato na matumizi ya mwaka wa fedha 2019/2020. Uchambuzi huu ulizingatia Fungu 44 na 60 chini ya Wizara ya Viwanda na Biashara na Fungu 31 Ofisi ya Makamu wa Rais Mazingira. Mwenendo wa utekelezaji wa bajeti wa mwaka wa fedha 2018/2019 pamoja na mpango wa bajeti wa mwaka wa fedha 2019/2020 ni kama unavyoonekana katika taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha kuanzia Machi, 2019 hadi Januari, 2020 Wajumbe walipokea, kuchambua na kujadili taarifa mbalimbali za utekelezaji wa wizara na taasisi zilizo chini ya Wizara ya Viwanda na Biashara pamoja na Ofisi ya Makamu wa Rais

(Mazingira) kuhusu masuala ya usimamizi wa mazingira. Baadhi ya taarifa zilizowasilishwa kwenye Kamati ni kama ifuatavyo:-

(a) Taarifa ya Viwanda na Biashara ya kuhusu utekelezaji wa mradi wa matrekta wa *URSUS,* Kibaha. Shirika la Maendeleo ya Taifa *(NDC)* ndiyo shirika mama ambalo kihistoria ndiyo lilianzisha mashirika na makampuni na viwanda vyote vya Serikali hapa nchini. Moja ya lengo la shirika hili ilikuwa ni kuongeza ufanisi katika Sekta ya Kilimo. Hivyo, Serikali iliamua kutekeleza mradi wa kuunganisha matrekta ya *URSUS.* Mradi huo unatekelezwa kwa mujibu wa mkataba uliongiwa na kampuni ya *URSUS* ya Poland na SUMA JKT, mkataba huo ambao ulifanyiwa marekebisho Agosti, 2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa mradi huu mpaka sasa ni kwamba matrekta yaliyoingizwa nchini ni 825 ambapo ilipaswa kuwa tumepokea matrekta 2,400; na mpaka sasa yameuzwa matrekta 586 kati ya yaliyopokelewa. Ujenzi wa kiwanda cha kuunganisha matrekta unaendelea na umefikia asilimia 60 ambapo ujenzi huu tayari umechelewa kwa sababu ulipaswa kukamilika mwezi Juni, 2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkataba wa mauziano ya matrekta kati ya kampuni ya *URSUS* na SUMA JKT una changamoto nyingi hali iliyotokana na uhalisia kwamba kama nchi tumeshalipa asilimia 65 ya fedha kulingana na mkataba, wakati *URSUS* wanaonekana kushindwa kukamilisha upande wao wa mkataba, kwani mpaka sasa walitakiwa wawe wameshaleta matrekta 2,400 lakini wameleta matrekta 825 tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna changamoto nyingine nyingi. Kutokana na changamoto hizo, Kamati inaishauri Serikali kukaa chini na Serikali ya Poland na kufanya mapitio ya mkataba husika kwa manufaa ya pande zote mbili.

(b) Taarifa ya Wizara ya Viwanda na Biashara kuhusu utekelezaji wa mpango wa kuboresha mfumo wa udhibiti wa biashara nchini na maoni ya wadau ya sekta ya viwanda na biashara kuhusu hali ya biashara na mazingira ya kufanya biashara nchini baada ya Serikali kuanza utekelezaji wa mpango huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpango wa kuboresha mfumo wa udhibiti wa biashara nchini *(blue print)* ni andiko maalum liliandaliwa kwa lengo la kuweka misingi endelevu ya kuboresha mazingira ya kufanya biashara hapa nchini. Andiko hili limefafanua changamoto mbalimbali zilizokuwa zikilalamikiwa na kukwamisha biashara nchini pamoja na mapendekezo na ufumbuzi wake. Utekelezaji wa *blue print* umeshaanza na baadhi ya kazi zimeshaanza kutekelezwa.

Aidha, wakati Bunge linapitisha Bajeti ya Serikali ya mwaka 2019/2020 Serikali iliwaaminisha wafanyabiashara, wawekezaji na wananchi kwa ujumla kuwa inaanza kutekeleza kwa nguvu zaidi mpango kazi wa kuboresha mazingira ya biashara ili mazingira ya biashara nchini yawe rafiki zaidi na yenye gharama nafuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tija ya utekelezaji wa mpango huu bado haijaonekana. Kuna changamoto ambazo kamati pamoja na wadau wanaona hazijapatiwa ufumbuzi. Changamoto hizo ni ugumu wa kutekeleza mfumo wa ukusanya kodi kwa njia ya elektroniki, malalamiko juu ya wingi wa mamlaka ya udhibiti, tena hazifanya kazi kwa pamoja. Mfano, kuna baadhi ya ukaguzi zinazofanywa na *OSHA* hufanywa tena pia na *fire*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hatua za kulinda soko la ndani bidhaa zinazozalishwa nchini Serikali iliongeza kodi ya bidhaa toka nje ambazo ni jambo jema sana, lakini athari za tozo hizo inaenda hadi kwenye bidhaa ambazo hazipatikani hapa nchini, hivyo kuleta ugumu

wa uingizaji wa bidhaa hizo na zikipatikana nchini zinakuwa na gharama kubwa. Kwa lengo la kutatua hilo, Kamati inaishauri Serikali kufanya uchambuzi wake wa kubainisha bidhaa ambazo hazizalishwi nchini na kuzitolea vikwazo ili ziweze kuingizwa kwa urahisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto katika kupata vibali vya ajira au kuhuisha vibali hivyo ambavyo vilikuwa na mlolongo wa malalamiko yasiyo ya lazima ambayo yanapelekea kukatisha tamaa wawekezaji nchini. Kamati inaishauri Serikali kutia mkazo katika kusimamia suala la vibali vya ajira ili kuendelea kuvutia uwekezaji mpya na teknolojia mpya kuja kuwekeza hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, madini yatumikayo katika malighafi za viwandani, mfano, madini ya kuzalisha *gypsum*, saruji, chokaa kutozwa mrabaha kama ilivyo madini ya vito jambo hili linapelekea kuongeza gharama za uzalishaji kwa kuwa mwisho wa siku bidhaa inayozalishwa italipiwa tena kodi. Kamati inashauri Serikali kuangalia namna ya kuondoa kodi hii katika madini hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana changamoto hizo ambazo ni baadhi tu inadhihirisha kuwa, bado hatujafanikiwa sana kuboresha mazingira ya kufanyia biashara nchini. Kamati inashauri Serikali kukamilisha mchakato wa kuandaa sheria za uwekezaji, bidhaa ambayo ndio inatazamiwa kwenda sambamba na *blueprint* na kutoa nafasi kwa mabadiliko pindi changamoto zinapotokea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa ya utekelezaji wa bajeti Wizara ya Viwanda na Biashara kwa kipindi cha Julai hadi Desemba, 2019. Katika kipindi cha mwaka 2019/2020, Wizara ya Viwanda na Biashara katika mafungu yote mawili, Fungu 44 na Fungu 60 iliidhinishiwa jumla ya shilingi bilioni 100.3 ambapo shilingi bilioni 48.8 ni za matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 51.5 ni za miradi ya maendeleo. Aidha, Wizara ilipanga kukusanya maduhuli ya jumla ya shilingi milioni 6.3. Hadi kufikia mwezi Desemba, 2019, Wizara ilikuwa imepokea shilingi bilioni 21.7 kwa Mafungu yote mawili kwa ajili ya matumizi ya kawaida ya wizara na Taasisi. Kiasi hiki ni sawa na asilimia 44.42 ya kiasi kilichoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya matumizi ya kawaida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa makusanyo hadi kufikia Desemba 2019 Wizara haijapata makusanyo ya aina yoyote. Kwa upande wa fedha kwa ajili ya miradi ya maendeleo hadi kufikia Desemba 31, 2019, Wizara haikupokea fedha yoyote kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Kamati inaendelea kuishauri Serikali kupeleka kiasi kilichoidhinishwa na Bunge kwa lengo la kuziwezesha Wizara zetu kutekeleza majukumu yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa ya hali ya mazingira nchini ni taarifa inayoandaliwa kwa mujibu wa kifungu cha 175(1) ya Sheria ya Mazingira ambacho kinamwelekeza Mkurugenzi wa Mazingira kuandaa na kuchapisha taarifa ambayo itabainisha hali ya mazingira, changamoto za utekelezaji pamoja na mapendekezo ya hatua za kuchukuliwa ili kukabiliana na changamoto za uharibifu wa mazingira na kuwasilisha Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa ya tatu ya hali ya mazingira ya mwaka 2018, imebainisha changamoto kadhaa kwanza asilimia 61 ya ardhi ipo kwenye hatari ya uharibifu. Pili ukataji holela wa misitu uharibifu wa mifugo, uharibifu wa mifumo ya ekolojia, kuongezeka kwa kusambaa kwa viumbe vimabamizi, udhibiti mbovu wa taka ngumu, utiririshaji wa maji taka ya viwandani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uharibifu wa mazingira nchini kwa kiasi kikubwa umechangia athari mbalimbali ikiwepo uharibifu wa bionuai ya misitu na viumbe wengine. Kupungua kwa mazao kutokana na uharibifu wa ardhi unaoendelea. Kuongezeka kwa migogoro ya ardhi

inahusisha jamii ya wafugaji na wakulima na kuongezeka kwa magonjwa kama vile kipindupindu na homa ya matumbo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa kampeni ya upandaji miti imelegalega na imekosa ufuatiliaji. Kamati inashauri Serikali kabla ya kutekeleza kampeni yoyote ya upandaji miti ifanye utafiti wa kubaini aina ya miti inayostawi katika sehemu husika, kwani ustawi wa miti unategemea hali ya hewa na eneo husika. Vilevile Kamati inashauri kampeni hizi zitoe miti ya matunda kwani itawavutia sana wananchi kuitunza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vibali vya uvunaji misitu vinatolewa na *TFS* na tozo ya shughuli hiyo inaenda huku huko *TFS* wakati marekebisho ya madhara yanayotokana na uvunaji yanafanywa na Wizara yenye dhamana ya mazingira ambapo hawanufaiki na tozo za shughuli hiyo. Kamati inaishauri Serikali kuisimamia *TFS* na kuhakikisha zoezi la utoaji vibali linafanyika kwa kushirikiana na Wizara ya Mazingira kwa lengo la kushauriana juu ya uvunaji endelevu. Vilevile Kamati inaishauri Serikali tozo ya uvunaji wa misitu walau kwa asilimia chache nyingine katika mfuko wenye dhamana ya mazingira ili iweze kufanya shughuli za utunzaji wa mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inashauri Serikali wahakikishe wafanyabiashara wakubwa na wadogo kuwekeza katika uzalishaji wa mkaa mbadala ili kupunguza kasi za ukataji miti kwa ajili ya kuzalisha mkaa, vilevile kupitia mikopo inayotolewa na halmashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa ya utekelezaji wa bajeti na majukumu ya Ofisi ya Makamu Rais, Mazingira pamoja na Baraza la Taifa la Uhifadhi wa Usimamizi wa Mazingira kwa kipindi cha Julai hadi Desemba, 2019. Katika mwaka wa fedha 2019/2020, Ofisi ya Makamu wa Rais Mazingira pamoja na Baraza la Taifa la Uhifadhi ya Usimamizi wa Mazingira waliidhinishiwa bilioni 22.7 kwa ajili ya kutekeleza majukumu yake katika fedha hizo bilioni 18.2 za miradi ya maendeleo na bilioni 4.48 matumizi ya kawaida. Hadi kufikia 31 Desemba, 2019 ambayo ni nusu ya mwaka wa fedha shilingi bilioni 6.78, ambapo bilioni 3.98 zilitolewa kwa ajili ya mishahara na matumizi na kiasi kilichobaki shilingi bilioni 2.5 ndio kilitolewa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upatikanaji wa fedha za matumizi za kawaida ni wa kuridhisha, lakini mwenendo wa upatikanaji fedha za miradi ya maendeleo sio wa kuridhisha ambapo asilimia 15.4 ya fedha za miradi ya maendeleo ndio zilikuwa zimepokelewa ambazo ni fedha za nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa fasili ya 6(b), kifungu cha 53 ukisoma pamoja na fasili ya 7(4)(b) na Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira inatekeleza jukumu la kushughulikia mikataba inayopendekezwa kuridhiwa na Bunge iliyopo chini ya Wizara ya Viwanda, Biashara pamoja na Ofisi ya Makamu wa Rais, Mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa katika kutekeleza jukumu hilo hoja ya Serikali kuhusu Bunge kuridhia Mikataba, Itifaki sita ziliwasilishwa kwenye Kamati na kuchambuliwa na hatimaye kuishauri Serikali juu ya namna bora ya utekelezaji wa mikataba hiyo. Pia kulishawishi Bunge juu ya mkataba husika. Kamati inasisitiza wizara husika kufanya jitihada za kuanza kutekeleza mikataba na itifaki husika ili tuanze kupata manufaa na faida zinazoambatana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni na mapendekezo, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, amedhamiria kuipeleka nchi yetu katika Uchumi wa Kati kupitia ujenzi wa viwanda. Katika kutekeleza hili tunaendelea tumeshuhudia

utekelezaji wa miradi mbalimbali ya kimkakati ambayo moja kwa moja inaenda kuchochea ujenzi wa Sekta ya Viwanda. Miradi hiyo ni kama ile ya Mradi wa Julius Nyerere Hydro Power Plant (JNHPP), *Standard Gauge Railway (SGR)* na ununuzi wa ndege).

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaendelea kupongeza na kuunga mkono juhudi mbalimbali za Serikali ambazo zimelenga kuimarisha Sekta za Viwanda, Biashara na Uwekezaji na hatimaye kuweka mazingira mazuri ya kufanyia Biashara hapa nchini. Takwimu za Mwaka huu zinaonyesha kuwa Tanzania tumepanda kwa nafasi tatu katika orodha ya nchi zenye mazingira mazuri ya kufanyia biashara kutoka namba 144 mpaka 141, hili linadhihirisha kuwa kuna juhudi zinafanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na pongezi hizi, Kamati inaendelea kuishauri Serikali kuyashughulikia ipasavyo masuala yafuatayo:-

(1) Utekelezaji wa miradi Mikubwa ya Kielelezo chini ya Sekta ya Viwanda; na

(2) Utekelezaji wa mradi wa kufufua viwanda vilivyobinafsishwa na vilivyosimama uzalishaji kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwenendo usioridhisha wa upataji fedha kutoka Hazina. Mwenendo usio mzuri wa upatikanaji fedha kutoka Hazina kwa Wizara ya Viwanda na Biashara, jambo linalopelekea kukwama kwa majukumu ya Wizara iliyobeba mwelekeo wa nchi kwa sasa wa kujenga uchumi wa kati kupitia viwanda:-

KWA KUWA Serikali iliwasilisha mbele ya Bunge mpango wa mapato na matumizi uliojipambanua vizuri sana, lakini changamoto ipo katika kutekeleza mpango huo;

NA KWA KUWA, athari ya mwenendo usio mzuri wa upatikanaji fedha imeonekana katika utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo ambapo tumeshuhudia miradi hii ikichukua muda mrefu kukamilika jambo ambalo kwa upande mmoja linaongeza gharama ya miradi hiyo;

HIVYO BASI**,** Kamati inaishauri Serikali kupanga mipango ya matumizi inayoendana na uhalisia wa makusanyo ya nchi. Sambamba na hilo Bajeti inayoidhinishwa na Bunge itolewe kwa wakati ili kuwezesha utekelezaji wa majukumu yaliyokusudiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *VAT refund* kwa wafanyabiashara na wenye viwanda. Wazalishaji wengi wanakumbana na changamoto ya upungufu wa mitaji kutokana na malimbikizo makubwa ya madai ya Kodi ya Ongezeko la Thamani *(VAT refund)* yanayolipwa kwa Mamlaka ya Mapato Tanzania *(TRA)* kwa mujibu wa Sheria ya Fedha ya Mwaka 2014 ambayo ilianza kutumika mwaka 2015:-

KWA KUWA, malipo haya yanatekelezwa kisheria na kwa mujibu wa Sheria hii, fedha hizo zinapaswa kurejeshwa kwa wahusika, lakini mwenendo wa urejeshaji wa fedha hizi si wa kuridhisha, unalalamikiwa na kusababisha kupungua kwa mitaji ya wafanyabiashara wanaolipa kodi hiyo, jambo linalowaweka katika hali ya kulazimika kukopa ili waweze kuendelea na shughuli za uzalishaji;

NA KWA KUWA, Madeni hayo yamekuwa makubwa na ni mzigo kwa Serikali ambapo kwa viwanda vinne (4) tu kama vile Tanga *Pharmaceutical Limited*, *Alliance One, Tobacco*, *ALAF Limited* na Mufindi *Paper Mills Limited* vinadai jumla ya shilingi bilioni 55.5;

HIVYO BASI, Kamati inaishauri Serikali kwa taarifa ambazo zimekwishahakikiwa iangaliwe namna ya kurejesha fedha hizi za *VAT* kwa wahusika tena kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ushuru wa Forodha wa 15% kwa sukari ya Viwandani. Kamati inatambua nia nzuri ya Serikali kuanzisha kodi hii, lakini uchambuzi wa Kamati ulibaini kuwa hatukufanya maandalizi ya kutosha katika kusimamia utekelezaji wake na hili limedhihirika:-

KWA KUWA, ni takriban miaka minne (4) sasa tangu kuanzishwa kwake, lakini mwenendo wa Serikali katika urejeshaji wa fedha hizo sio wa kuridhisha pamoja na kuwa baadhi ya taarifa zimekwisha hakikiwa na kuwasilishwa;

NA KWA KUWA, utekelezaji wa tozo hii umeonekana kuambatana na changamoto ambayo imepelekea kuathiri mitaji ya wafanyabiashara nchini;

NA KWA KUWA, fedha hizo ni sehemu ya mtaji wa kiwanda na ilipaswa kurudishwa ili iendelee kutumika katika kuendeleza shughull za uzalishaji;

NA KWA KUWA Serikali imeanzisha Ushuru wa Stampu ya Kielektroniki *(Electronic Tax Stamp – ETS)* ambao umekwishaanza kutumika kwa baadhi ya viwanda na mfumo huu una uwezo wa kufanya kazi ya kuhakiki iliyokuwa ikikusudiwa na Sheria ya Ushuru wa Forodha wa 15% katika Sukari ya Viwandani;

HIVYO BASI, Kamati inaishauri Serikali kuangalia namna ya kuachana na Mfumo wa Ushuru wa Forodha wa 15% kwa sukari ya viwandani na badala yake tukatumia taarifa za *ETS* kuhakiki matumizi ya Sukari ya Viwandani ambao ndio umeonekana kuwa wa uhakika zaidi. Sambamba na hili Serikali iangalie namna ya kupunguza kodi ya *ETS*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imenadi Azma ya Ujenzi wa Tanzania ya Viwanda na tunashukuru wawekezaji mbalimbali wa ndani na nje ya nchi wamelipokea vizuri azma hiyo na kuamua kuwekeza katika viwanda vya uzalishaji wa bidhaa mbalimbali. Kamati ilipata fursa ya kushuhudia baadhi ya viwanda ambavyo vimewekeza kwa uwezo wa kuzalisha bidhaa zinazotosheleza mahitaji ya soko la ndani na hata kuuza nje ya nchi mfano Viwanda vya Chuma, Marumaru, Mabati na Saruji:-

KWA KUWA, nchi yetu ipo katika kujijenga kiuchumi wa viwanda;

NA KWA KUWA kipindi hiki cha mpito bado hatujafanikiwa kujenga mazingira ambayo yatapunguza gharama za uzalishaji jambo linalopelekea bidhaa zetu za ndani kuwa na bei kubwa na kukumbana na changamoto ya kushindwa kushindana katika soko la ndani na bidhaa zinazotoka nje na duniani kwa ujumla;

HIVYO BASI, Kamati inaishauri Serikali kuona namna ya kuvilinda viwanda vyetu kwa kuweka uwiano wa kodi kwa bidhaa zinazoingia ili kuhakikisha bidhaa za ndani zinaweza kushindana katika soko, hatua hii itasaidia kujiepusha kuwa soko la bidhaa za wenzetu. Suala la kulinda viwanda vya ndani limefanikiwa katika kulinda viwanda vya Sukari, kwa mfano huu inamaanisha tunaweza kuvilinda na viwanda vingine. Pia sambamba na hili, Serikali iongeze nguvu ya kuvisimamia viwanda vya ndani kuhakikisha vinazingatia ubora unaotakiwa sokoni. Vilevile tuongeze kasi ya kutengeneza mazingira ambayo yataenda kupunguza gharama za uzalishaji hususani kodi zinazoambatana na uzalishaji ili kuwezesha kupunguza bei za bidhaa hizo ili kuweka uwiano wa bei.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuhamasisha uwekezaji tumefanikiwa kuwavutia wawekezaji kuja nchini na kuwekeza na wengine wameleta teknolojia mpya ambayo haipo kabisa Tanzania, wawekezaji wengi wamekuwa wakihitaji kuhakikishiwa kwa kuona wameruhusiwa kuja na watu wao ambao wanafahamu biashara zao, lakini changamoto imekuwa katika kupata au kuhuisha ya vibali vya ajira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hitimisho, napenda kukushukuru wewe kwa uongozi wako uliotukuka na kunipa fursa ya kuwasilisha taarifa hii. Pia napenda kuchukua fursa hii pia kumshukuru Mheshimiwa Spika, Naibu Spika pamoja na Wenyeviti wote Bunge kwa kuratibu na kusimamia vema shughuli za Bunge. Aidha, naomba kuchukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu, Mbunge kwa kuaminiwa na Mheshimiwa Rais na kupewa dhamana ya kuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, natumai atafanya kazi kwa ukaribu na Kamati hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya pekee naomba kuwashukuru Wajumbe wote wa Kamati ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira, kwa kutekeleza majukumu yao kwa uadilifu wa hali ya juu. Aidha, nawashukuru na kuwapongeza kwa ushirikiano walioutoa katika kuandaa taarifa hii hadi kukamilika kwake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia nitumie fursa hii kuwashukuru na kuwapongeza Mawaziri, Manaibu Waziri wote wa Wizara ya Viwanda na Biashara pamoja na Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Makatibu Wakuu pamoja na watendaji wote wa Wizara na Taasisi zote zilizopo chini ya Wizara hizo kwa ushirikiano walioutoa kwa Kamati kwa kipindi chote hiki.

Vilevile naomba kumshukuru Katibu Wa Bunge Ndugu Stephen Kagaigai kwa ushirikiano ambao amakuwa akiutoa katika Kamati kuhakikisha tunaendelea kutekeleza majukumu ya Kamati kikamilifu. Pamoja na yeye namshukuru Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge, Ndugu Michael Chikokoto, Makatibu wa Kamati Ndugu Zainab Mkamba na Ndugu Mwajuma Ramadhan pamoja na msaidizi wa Kamati Ndugu Pauline Mavunde, kwa kuratibu vyema Shughuli za Kamati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naliomba Bunge lako Tukufu lipokee na kuijadili taarifa hii na hatimaye kukubali maoni, ushauri na mapendekezo ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira. Naomba pia taarifa yetu yote ya Kamati iiingie katika kumbukumbu za Bunge yaani *hansard.*

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**MHE. JULIUS K. LAIZER:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki

# TAARIFA YA MWAKA YA SHUGHULI ZILIZOTEKELEZWA NA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA VIWANDA, BIASHARA NA MAZINGIRA KWA KIPINDI CHA KUANZIA FEBRUARI, 2019 HADI JANUARI, 2020 - KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

[*Inatolewa Chini ya Kanuni ya 117 (15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016]*

## SEHEMU YA KWANZA

## 1.0 MAELEZO YA JUMLA

### 1.1 Utangulizi

**Mheshimiwa Spika** kwa mujibu wa Kanuni ya 117(15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016 na kwa niaba ya Wajumbe wenzangu wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira naomba kuwasilisha taarifa inayoeleza shughuli zote zilizotekelezwa na Kamati kwa kipindi cha kuanzia Februari, 2019 hadi Januari, 2020.

**Mheshimiwa Spika**, taarifa hii imegawanyika katika sehemu kuu **Nne**, Sehemu ya Kwanza ni Utangulizi, Sehemu ya Pili inaelezea namna Kamati ilivyotekeleza majukumu yake kwa kipindi cha Februari, 2019 hadi Januari, 2020, Sehemu ya Tatu inaelezea Maoni na Mapendekezo ya Kamati na Sehemu ya Nne ni Hitimisho.

### 1.2 Majukumu ya Kamati

Kwa mujibu wa Fasili ya 6 (1) ya Nyongeza ya Nane, ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Kamati ya Viwanda, Biashara na Mazingira ina jukumu la kusimamia shughuli za Sekta za Viwanda, Biashara na Mazingira. Kwa muktadha huo na kwa kuzingatia matakwa ya Fasihi ya 7(1) ya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za kudumu za Bunge, Majukumu yanayotekelezwa na Kamati hii ni haya yafuatayo:-

(i) Kushughulikia Bajeti za Wizara ya Viwanda na Biashara na Ofisi ya Makamu wa Rais-Mazingira;

(ii) Kushughulikia Miswada ya Sheria na Mikataba inayopendekezwa kuridhiwa na Bunge chini ya Wizara ya Viwanda na Biashara na Ofisi ya Makamu wa Rais-Mazingira;

(iii) Kushughulikia Taarifa za utendaji za kila mwaka za Wizara na Taasisi inazozisimamia; na

(iv) Kufuatilia utekelezaji wa majukumu ya Wizara inazozisimamia.

### 1.3 Njia zilizotumika kutekeleza Majukumu ya Kamati

**Mheshimiwa Spika,** katika kutekeleza majukumu yake kwa lengo la kusimamia na kuishauri Serikali Kamati ilitumia njia mbalimbali ikiwa ni pamoja na:-

(i) Kupokea, kuchambua na kujaili taarifa mbalimbali za utendaji za Wizara na taasisi zilizopo chini ya usimamizi wa Kamati; Taarifa hizi zilijumuisha taarifa za kawaida za utekelezaji wa majukumu ya Wizara pamoja na taarifa za utekelezaji wa Bajeti za Wizara inazozisimamia;

(ii) Kupokea, kuchambua, kujadili na kushauri juu ya Mikataba ya Kimataifa iliyopendekezwa kuridhiwa na Bunge ambayo ipo chini ya Wizara inazozisimamia;

(iii) Ziara za ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo, Kamati ilifanya ziara katika miradi mbalimbali kwa lengo la kukagua utekelezaji wa miradi hiyo na kubaini ufanisi uliopo katika kutekeleza wake;

(iv) Kufanya Vikao vya pamoja na wadau wa Sekta ya Viwanda na Biashara kwa lengo la kufahamu namna wanavyoendesha shughuli zao (mafanikio na changamoto zao) kisha kuishauri Serikali kwa nia ya kuboresha; na

(v) Kushiriki warsha na semina mbalimbali zilizoendeshwa na wadau wa Sekta za Viwanda, Biashara na Mazingira wa lengo la kuwajengea wajumbe uelewa juu ya sekta hizo.

## SEHEMU YA PILI

## 2.0 UCHAMBUZI WA MATOKEO YA UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA KAMATI

**Mheshimiwa Spika,** kwa kipindi cha kuanzia Februari, 2019 na Januari, 2020 kulikuwa na jumla ya vikao vya Kamati vinne (4), ambapo Kamati iliendelea kutekeleza majukumu yake ikiwa ni katika kuzisimamia Wizara zake mbili (2) yaani Wizara ya Viwanda na Biashara na Ofisi ya Makamu wa Rais- Mazingira na Taasisi zilizopo chini Wizara hizo.

**Mheshimiwa Spika,** Majukumu yaliyotekelezwa na Kamati ni pamoja na kupokea taarifa za utekelezaji wa majukumu ya Wizara na taasisi zinazoripoti kwa Kamati; Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo; kuchambua taarifa za utekelezaji wa Bajeti za Wizara kwa Mwaka wa Fedha ulioishia (2018/2029) pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka unaoendelea (2019/2020); kuchambua na kushauri juu ya Mikataba ya Kimataifa iliyopendekezwa kuridhiwa na Bunge ambayo ipo chini ya Wizara inazozisimamia; Vikao na wadau wa Sekta zinazosimamiwa na Kamati kwa lengo la kusikiliza maoni yao; na kushiriki warsha na semina za kujenga uelewa kwa Wajumbe.

### 2.1 TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MAPENDEKEZO YA KAMATI

**Mheshimiwa Spika,** wakati wa kupitia na kuchambua taarifa ya utekelezaji wa Wizara ya Viwanda na Biashara pamoja na Ofisi ya Makamu wa Rais-Mazingira, kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019, Kamati ilitoa mapendekezo kwenye maeneo mbalimbali. Kamati imearifiwa juu ya utekelezaji wa mapendekezo hayo na kujiridhisha kuwa, Serikali imejitahidi kuzingatia mapendekezo ya Kamati. Hata hivyo, kuna baadhi ya mapendekezo ambayo Kamati imeona Serikali inahitaji kuongeza kasi ya utekelezaji wake, maeneo hayo ni pamoja na;-

i) Kwa upande wa Wizara ya Viwanda na Biashara, Kamati inaendelea kuishauri Serikali juu ya utekelezaji wa maagizo yafuatayo;-

***a) Kuchukua hatua kwa wawekezaji ambao bado hawajaitikia wito wa Serikali wa Kufufua viwanda walivyobinafsishiwa. Sambamba na hilo Serikali iangalie namna ya kuunda Tume Maalumu itakayofuatilia eneo la viwanda vilivyobinafsishwa kwa lengo la kufuatilia kwa ukaribu na kujua ukweli wa eneo hili****; na*

***b) Kuendelea na juhudi za kuziwesha taasisi zake za utafiti ikiwemo CAMARTEC, SIDO, TIRDO na TEMDO ili ziweze kubuni zana mbalimbali za kilimo ambazo zitasaidia na kumrahisishia mkulima kuendeleza shughuli zake kwa urahisi ukizingatia Kilimo ndio shughuli kuu ya watanzania walio wengi.***

ii) Kwa upande wa Ofisi ya Makamu wa Rais-Mazingira, Kamati inaendelea kuishauri Serikali juu ya utekelezaji wa maagizo yafuatayo;-

***a) Serikali kufanye Tathimini ya Athari kwa Mazingira- EIA katika maeneo ambayo yametengwa kwa ajili ya wachimaji wadogo wa madini kabla ya kuwakabidhi ili kuepusha athari za kimazingira zinazoweza kujitokeza;*** na

***b) Kutoa elimu kwa jamii kukusu athari za kuharibu vyanzo vya maji ya Bonde la Mto Ruaha Mkuu, na kuliingiza bonde hilo katika orodha ya maeneo lindwa kwa kutumia Sheria ya Mazingira ya Mwaka 2004, kwa lengo la kulinda bonde letu lakini pia kutoa uhakika wa maji katika Mradi Mkubwa wa Umeme unaotekelezwa (Stigler's Gorge).***

## 2.2 UKAGUZI WA MIRADI YA MAENDELEO

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ya Viwanda, Biashara na Mazingira ilifanya ziara za ukaguzi wa ufanisi uliopo katika kutekeleza Miradi ya Maendeleo kama inavyoelekezwa na Kanuni ya 98 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge toleo la Januari, 2016. Katika kipindi cha terehe 14 hadi 21 Machi, 2019 Kamati ilitembelea miradi mitatu (3) inayotekelezwa na Wizara ya Viwanda na Biashara pamoja na Ofisi ya Makamu wa Rais-Mazingira. Miradi hiyo ni **Mradi Na. 6260 – *Institutional Support*** ambao unahusu kuzijengea uwezo taasisi mbalimbali zilizopo chini ya Wizara ya Viwanda na Biashara; **Mradi Namba 5301, Fungu 31** unaohusu Mabadiliko wa Tabianchi katika Mji wa Bagamoyo; **Mradi Namba 6507** unaohusu Ujenzi wa Ofisi ya Baraza la Taifa la Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira; na Shughuli za Usimimamizi wa Mazingira katika Ziwa Manyara.

### 2.2.1 Mradi Na. 6260 - Institutional Support

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipata fursa ya kutembelea na kukagua utekelezaji wa **Mradi Na. 6260** - *Institutional Support*, katika Kituo cha Zana za Kilimo na Teknolojia Vijijini - (CAMARTEC), Shirika la Uhandisi na Usanifu wa Mitambo Tanzania (TEMDO) na Shirika la Viwango Tanzania (TBS);

#### a) Kituo cha Zana za Kilimo na Teknolojia Vijijini - (CAMARTEC)

**Mheshimiwa Spika**, Kituo cha Zana za Kilimo na Teknolojia Vijijini - (CAMARTEC) ni moja ya taasisi inayosimamiwa na Wizara ya Viwanda na Biashara. Kituo hiki kinajihusisha na uendeshaji na uhaulishaji wa teknolojia za zana za kilimo, nishati, maji safi na taka, vifaa vya ujenzi na majengo vijijini. Katika Mwaka wa Fedha 2018/2019 CAMARTEC kupitia **Mradi Namba 6260 - *Institution Support*** iliidhinishiwa Shilingi **3,000,000,000.00** kwa ajili ya kutekeleza majukumu yake.

Fedha hizo zililenga kuendeleza utafiti wa teknolojia, kukuza wazalishaji wa ndani wanaojihusisha na zana za kilimo, kuhakiki ubora wa zana za kilimo, kuimarisha miundombinu ya utafiti wa zana za kilimo, kusambaza zana za kilimo kwa wakulima zilizofanyiwa utafiti na kushughulikia masuala yanayohusu tafiti katika kutunza mazingira.

**Mheshimiwa Spika,** wakati wa ziara, Kamati ilikuta hali ya *CAMARTEC* si ya kuridhisha, karakana zake zimejaa mitambo chakavu na teknolojia zinazotumika ni duni, jambo linalopelekea kuzalisha zana duni na za gharama ya juu ukilinganisha na hali halisi ya soko kwa sasa. Aidha, kwa takribani miaka mitatu mfululizo kituo kilikuwa hakijapokea ruzuku kutoka Serikalini na hivyo kimekuwa kikitekeleza majukumu yake katika mazingira magumu.

Pia, kituo kimekuwa kikikabiliana na changamoto mbalimbali kama vile; Upungufu wa watumishi wenye taaluma za uhandisi, watafiti na mafundi sanifu wakati kada hizo ndio uhai wa kituo na majukumu ya kituo hayataweza kutekelezwa pasipokuwa na wataalamu wa kutosha wa kada tajwa hapo juu.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya kutembelea na kukagua utekelezaji wa Shughuli za Kituo cha Zana za Kilimo na Teknolojia Vijijini - (CAMARTEC), Kamati ilikuwa na maoni na ushauri ufuatao**; -**

i) Teknolojia inabadilika kwa kasi sana hivyo basi shughuli za ubunifu, usanifu na utafiti zinahitaji mafunzo ya mara kwa mara ili kuhuisha taaluma hizo. Serikali ihakikishe inaziwezesha taasisi zote zinazojihusisha na utafiti wa teknolojia kupata fursa za mara kwa mara kwenda kujifunza kwa nchi zilizoendelea;

ii) Serikali itoe fedha za bajeti ya maendeleo zilizoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya CARMATEC, kwa lengo la kuiwezesha kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi uliokusudiwa ukizingatia kuwa chanzo kikuu cha mapato cha taasisi hii ni ruzuku kutoka Serikalini;

iii) Kamati inaishauri Wizara kutenga bajeti ya kutosha ambayo itaweza kutosheleza asilimia kubwa ya gharama za uzalishaji jambo litakalowawezesha kuuza bidhaa zao kwa gharama nafuu na kuwanufaisha watu wa hali zote. Ushauri huu umezingatia dhana ya kuanzisha Kituo hicho ambayo iliwalenga Watanzania wa hali ya chini kwa kuzalisha zana za kilimo na teknolojia vijijini, lakini zana zinazotengenezwa na kituo kwa sasa zimekuwa na ghali na walengwa kushindwa kuzimudu; na

iv) Shughuli za kilimo zinahusisha mnyororo wa thamani mpaka bidhaa kumfikia mlaji sokoni, kwa lengo la kuwasaidia wakulima wetu na kulinda ubora wa mazao yao, Kamati inaishauri Serikali kupitia CAMARTEC kujipanga kuzalisha zana/mashine ambazo zitamsaidia mkulima kuanzia hatua ya kuandaa shamba, kulima, kuvuna, kuongeza thamani na mwisho kufika kwa mlaji.

**b) Shirika la Uhandisi na Usanifu wa Mitambo Tanzania (TEMDO)**

**Mheshimiwa Spika,** Shirika la Uhandisi na Usanifu wa Mitambo Tanzania – TEMDO kwa Mwaka wa Fedha ilipangiwa Bajeti kupitia **Mradi namba 6260 - *Institution Support*,** ya Shilingi 4,000,000,000.00 kwa ajili ya kutekeleza majukumu yake.

**Mheshimiwa Spika**, majukumu yaliyopangwa kutekelezwa ni pamoja na kujenga miundombinu ya kiatamizi cha teknolojia na biashara pamoja kuwajengea uwezo wajasiriamali wa kati na wadogo; Kupitia upya sheria iliyoanzisha Shirika; kubuni na kuendeleza chasili cha mtambo wa kukausha mazao ya kilimo, kubuni na kutengeneza chasili cha mtambo mdogo wa kusindika chai; Kubuni na kuendeleza utengenezaji wa mtambo wa kuhifadhi baridi (cold room) ambao utasaidia kuhifadhi bidhaa mbalimbali. Pamoja na hilo shirika Kuendeleza na kuhamasisha utumiaji wa technolojia za utengenezaji na uzalishaji wa bidhaa mbalimbali kama vile marumaru, kwa mfano Vigae kwa kutumia malighafi zinazopatikana nchini.

**Mheshimiwa Spika**, Wakati wa ziara ya Kamati iliyofanyika tarehe 16 Machi, 2019 katika Shirika, Kamati ilikuta kazi mbalimbali zikiendelea ikiwemo ufungaji (installation) wa mashine mpya za kisasa ndani ya karakana hiyo ya Shirika na majaribio ya mashine hizo. Shughuli zote zilizokuwa likiendelea katika eneo la shirika zilitekelezwa kwa kutumia Shilingi 1,582,240,655.00 ambapo shilingi 1,263,435,000.00 ilikuwa ruzuku kutoka Serikalini kwa bajeti ya mwaka wa fedha 2017/2018 ambazo pia zilipelekwa mwishoni mwa mwaka wa fedha, na shilingi 318,805,655.00 makusanyo ya Shirika kwa mwaka 2017/2018.

**Mheshimiwa Spika**, Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2018/2019 mpaka kufikia tarehe 16 Machi, 2019, Shirika halikuwa limepokea kiasi chochote kutoka Serikalini kwa ajili ya kutekeleza shughuli za maendeleo.

**Mheshimiwa Spika**, Shirika linakabiliwa na changamoto mbalimbali ambazo ni upungufu wa fedha za kufanyia utafiti jambo linalopelekea Shirika kushindwa kufanya utafiti kwa uwezo wake wote; ukosefu wa fedha za Matumizi Mengineyo (OC) hali inayopelekea Shirika kushindwa kumudu shughuli zake zilizokuwa zimekusudiwa kutekelezwa; upungufu wa wafanyakazi wenye taaluma ya kada ya uhandisi na usanifu; na uhaba wa rasilimali fedha hivyo kupelekea kushindwa kusambaza mashine na mitambo iliyozalishwa na Shirika kwa kiwango kilichotarajiwa.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya ziara ya Kamati katika Shirika la Uhandisi na Usanifu wa Mitambo Tanzania (TEMDO), ilikuwa na maoni na ushauri ufuatao;-

i) Serikali kuhakikisha fedha iliyoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya Shirika inapelekwa na kwa wakati, ili kuendelea kuboresha na kuliwezesha shirika hilo kutekeleza dhamira ya kuanzishwa kwake;
ii) Kwa kuzingatia mwenendo wa upatikanaji wa fedha kutoka Hazina kwenda kwa taasisi za utafiti sio wa kuridhisha, na kuna baadhi ya miaka zimekuwa hazipelekwi kabisa, jambo linalokwamisha utekelezaji wa majukumu ya taasisi hizo. Kamati inaishauri Serikali kama inaona utaratibu wa kutoa mwaka hadi mwaka ni mgumu ni bora ikajipanga kuzipatia taasisi hizi mitaji ili ziweze kujiendesha bila kusubiri ruzuku;

iii) Kama ilivyo kwa taasisi nyingine zote za utafiti duniani, wafanyakazi wa TEMDO wanatakiwa kupatiwa mafunzo ya mara kwa mara yanayoendana na hali ya mabadiliko ya teknolojia. Hivyo Serikali ijitahidi kuiwezesha TEMDO kwenda kujifunza kwa nchi zilizoendelea kiteknolojia; na

iv) Taasisi itoe elimu na kujitangaza kwa wananchi kuhusu kazi wanazozifanya. Hatua hiyo itaongeza uelewa kwa jamii juu ya shughuli wanazozifanya na hatimaye kukuza soko na mauzo ya shirika.

**c) Mradi wa Kuboresha Miundombinu za Shirika la Viwango Tanzania (TBS);**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipata fursa ya kutembelea Mradi wa kuboresha Miundombinu ya Shirika la Viwango Tanzania (TBS). Mradi huu unatekelezwa chini ya **Mradi Namba 6260 - *Institutional Support*** na unatekelezwa kwa kutumia fedha za ndani za Shirika pamoja na ruzuku kutoka Serikalini.

Katika Mwaka wa Fedha 2018/2019, TBS kupitia mradi huu ilitenga shilingi **2,000,000,000.00** kwa ajili ya kuendeleza ujenzi wa maabara ya kisasa kwa ajili ya Shirika. Mradi huu unahusisha ujenzi wa *Test House* ambayo itakuwa ni jengo la ghorofa nane ambalo ndani yake inatarajiwa kujengwa maabara za kisasa zitakazo endana na mahitaji ya shirika.

**Mheshimiwa Spika,** Wakati wa Ziara ya Kamati mnamo tarehe 20 Machi, 2019, Kamati ilikuta ujenzi ukiendelea na hatua za awali za ujenzi wa jengo hilo zilikuwa zimekamilika, hivyo hatua za umaliziaji (finishing) zilikuwa zikiendelea.

**Mheshimiwa Spika**, utekelezaji wa mradi ulikuwa ulipangwa kutekelezwa ndani ya wiki 69 yaani kuanzia Januari, 2018 hadi Aprili, 2019. Utekelezaji huu ulikuwa nje ya muda kwa kuzingatia hatua ambayo Kamati iliyoikuta wakati wa ziara yake;

**Mheshimiwa Spika**, kuhusu gharama za Mradi, imekadiriwa kutumika shilingi **19,325,304,165.00** na kwa hatua za awali za ujenzi ambazo kamati ilizikuta wakati wa ziara yake, ujenzi ulikuwa umekwishatumia shilingi **6,727,643,213.00.**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati pia ilijulishwa juu ya changamoto wanazokabiliana nazo TBS katika utendaji wao. Baadhi ya changamoto zinazowakabili ni upungufu wa rasilimali watu, mishahara midogo kwa watumishi wa shirika jambo linalopelekea kushuka kwa morali, Upungufu wa vifaa vya maabara kwa ajili ya kufanya vipimo mbalimbali jambo linalopelekea baadhi ya maabara za shirika kutopata cheti cha umahiri, Utayari wa umma kuhusu umuhimu wa viwango katika kulinda afya na usalama wa walaji ni mdogo na uwepo wa bidhaa zisizo na viwango kupitia njia za panya jambo linalopelekea lawama kurudi kwa TBS pale bidhaa hizo zinapokutwa sokoni, kuwa Shirika halitimizi majukumu yake.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya kupokea taarifa ya utekelezaji ya Mradi na kutembelea na kukagua utekelezaji wa mradi huo, uchambuzi wa Kamati ulibaini kuwa gharama iliyokadiriwa katika utekelezaji wa ujenzi wa jengo hilo ni kubwa. Kamati ilihoji juu ya gharama hizo, majibu ya TBS yalikuwa gharama hizo zinatokana na kuwa jengo linalojengwa ni jengo maalumu na linatofauti na majengo mengine.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati haikuridhishwa na majibu yaliyotolewa na TBS, hivyo Kamati iliitaka Wizara ya Viwanda na Biashara kufanya uchunguzi maalumu katika Mradi huo na kuiwasilishwa kwa Kamati ili kubaini uhalisia wa gharama za mradi huo.

**Mheshimiwa Spika,** baada ya Ukaguzi na kupokea taarifa ya Wizara Kamati ilikuwa na maoni yafuatayo juu ya utekelezaji wa Mradi huo;-

i) Kwa kuwa mradi huu unatarajiwa kuiongezea TBS uwezo wa kuhudumia sampuli nyingi na kwa haraka na kuiwezesha kuendana na mahitaji. Kamati inaishauri Serikali kuwaongezea uwezo watumishi wa TBS kwa kuwawezesha kupata mafunzo yatakayowasaidia kuandaa viwango/vipimo vipya ambavyo kwa sasa TBS haina uwezo wa kuvikagua na imekuwa ikiwaelekeza wadau kwenda kupima bidhaa zao nje ya nchi. Mfano ni bidhaa za *electronics* hususani simu na televisheni;

ii) Maboresho ya Maabara za TBS yaende sambamba na kuongeza vifaa vya maabara kwa ajili ya kufanya vipimo mbalimbali ili kuleta tija inayokusudiwa; na

iii) Serikali kwa kushirikiana na Shirika kuongeza kasi ya kutoa elimu kwa umma juu ya umuhimu wa viwango katika kulinda afya na usalama wa walaji. Hatua hii itapunguza matumizi ya bidhaa zisizo na viwango na hatimaye hatua kwa hatua tutapunguza uingizaji wa bidhaa zisizo za viwango kwa njia ya panya kwa kuwa zitakosa soko.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati iliendelea na ufuatiliaji wa Mradi wa Ujenzi wa Jengo la Maabara la TBS ambapo katika vikao vya Kamati vya Mwezi Januari, 2020 ilihoji juu ya hatua iliyofikiwa katika Ukaguzi Maalumu uliombwa ufanyike na kuarifiwa kuwa Ukaguzi ulifanyika na umekamilika. Aidha, kwa mara kadhaa Kamati ilijaribu kuomba taarifa iliyotokana na ukaguzi huo maalumu kuhusu gharama za Mradi wa Jengo la TBS lakini haikufanikiwa kupatiwa taarifa hiyo jambo linalopelekea hali ya sintofahamu kwa kamati kuhusu matokeo ya taarifa ya ukaguzi huo maalumu. Hivyo, Kamati inaendelea kusisitiza Serikali kupitia Wizara ya Viwanda na Biashara kuwasilisha kwenye Kamati taarifa hiyo kwa lengo la kamati kujiridhisha na gharama zilizotumika katika ujenzi wa jengo na kuiwezesha Kamati kulishauri Bunge ikiwa na uelewa wa kutosha juu ya utekelezaji wa mradi huo.

### 2.2.2 Mradi Namba 5301, Fungu 31

**Mheshimiwa Spika,** Kamati pia ilitembelea **Mradi Namba 5301** wa kuhimili Mabadiliko ya Tabianchi kwa eneo la Bagamoyo. Lengo la Kamati kutembelea Mradi huu ni kubaini namna

Mabadiliko ya tabianchi yameathiri mazingira yetu na kwa namna Serikali inakabiliana na athari zake.

**Mheshimiwa Spika**, Ofisi ya Makamu wa Rais-Mazingira inatekeleza Miradi mbalimbali ikiwemo Mradi wa Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi **(Mradi namba 5301)** mradi huu umeanzishwa baada ya kubaini athari za mabadiliko ya tabianchi ambazo zimeendelea kujidhihirisha katika maeneo mbalimbali Duniani. Mfano ongezeko la usawa wa bahari (sea level rise) kwa sentemita **19** katika kipindi cha miaka **50** ambapo kwa Tanzania ongezeko hilo limechangia uharibifu wa mwambao wa Pwani hususani katika maeneo ya Kisiwa Panza Zanzibar, Mto Pangani, Fungu la Nyani Rufuji, na baadhi ya visima vya maji baridi katika maeneo ya Bagamoyo kuharibiwa na maji chumvi.

**Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa Pwani ya Bagamoyo Mabadiliko ya Tabianchi yameathiri visima vya asili ambapo kina cha maji ya bahari kuongezeka na kufikia usawa wa meza ya maji (*water table*) na kupelekea maji hayo ya bahari kuingia katika visima vya asili na kuleta madhara kwa watumiaji wa maji ya visima hivyo.

Kwa kutambua uharibifu huo, mradi umehusisha ujenzi wa visima vikubwa vya maji masafi na ujenzi wa miundombinu ya uvunaji maji ya mvua. Mradi unatekelezwa na Ofisi ya Makamu wa Rais-Mazingira chini ya ufadhili wa *Least Development Countries Fund-LDCF* na umegharimu takriban jumla ya Shilingi **1,171,668,189/=**

**Mheshimiwa Spika,** wakati wa ziara ya Kamati, mradi ulikuwa umekamilika.

**Mheshimiwa Spika,** maoni na Ushauri wa Kamati kuhusu utekelezaji wa **Mradi Namba 5301**, **Fungu 31** unaohusu Mabadiliko ya Tabianchi Wilayani Bagamoyo ni;-

i) Serikali itumie mradi huu kama mfano, na kwa kupitia Wizara ya Maji na Ofisi ya Makamu wa Rais-Mazingira Serikali ijipange kutafuta miradi mingine mingi ya aina hii ili kuwaokoa wananchi kuendelea kutumia maji yasiyo salama; (kwa sasa mradi umetekelezwa katika maeneo machache tu wakati athari mabadiliko ya tabianchi imeharibu visima vingi vya asili na kusababisha upungufu wa maji na madhara ya kiafya kwa wakazi wa eneo lote la Ukanda wa Pwani ya Bagamoyo.)

ii) Kwa maeneo ambayo mradi unatekelezwa, wananchi wapatiwe elimu ya kutosha juu ya mradi huo ikihusianishwa na mabadiliko ya Tabianchi na waelimishwe jinsi ya kutunza mradi hiyo ili uweze kuwa endelevu;

iii) Kwa mradi ya namna hii ambayo inatekelezwa katika halmashauri zetu ni vema tukatumia wahandisi wa halmashauri kwa lengo la kupunguza gharama, kutokana na ukweli kwamba fedha zinazotumika kumlipa mhandisi mshauri ni nyingi na kupelekea kuongezeka kwa gharama za mradi; na

### 2.2.3 **Mradi Namba 6507, Fungu 31**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilitembelea **Mradi Namba 6507** ambao unahusu Ujenzi wa Ofisi ya Baraza la Taifa la Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira – *NEMC*. Mradi wa Ujenzi wa Ofisi za NEMC unahusisha ujenzi wa Jengo kwa ajili ya Maabara na Ofisi za Baraza na ulianzishwa kwa lengo la kupunguza gharama ya Baraza itokanayo na kodi ya pango.

Tangu kuundwa kwa Baraza mwaka 1983 lilikuwa likipanga katika majengo mbalimbali na juhudi za NEMC kupatiwa ofisi za Serikali zilishindikana na mnamo mwaka 2009 Bodi ya NEMC

iliagizwaa kutafuta ofisi za kudumu na ndipo Baraza lilipochukua uamuzi wa kununua kiwanja na kujenga jengo lake katika Mkoa wa Dar es Salaam.

Baada ya kutolewa agizo hilo ndipo Mradi huu ulianzishwa na kupangwa kutekelezwa kupitia ruzuku kutoka Serikalini pamoja na makusanyo ya ndani ya Baraza. Mradi umehusisha ununuzi wa viwanja vinne (vitatu Dar es salaam Mikocheni na kimoja Dodoma) pamoja na ujenzi wa jengo la ghorofa mbili katika viwanja vya Mikocheni- Dar es Salaam. Mradi umegharimu jumla ya shilingi **5,564,364,893.00** ambapo shilingi **1,650,000,000.00** ni ruzuku kutoka Serikalini na shilingi **3,253,464,893.00** ni fedha za ndani za Baraza na **660,900,000.00** ni Msaada kutoka Benki ya Dunia.

Mchanganuo wa fedha za Mradi ni shilingi **660,900,000.00** kwa ajili ya Ujenzi wa jengo, shilingi **4,903,464,893.00** kwa ajili ya viwanja vinne ambapo viwanja vitatu vipo Dar es Salaam Mikocheni na kiwanja kimoja kipo Dodoma.

**Mheshimiwa Spika,** Wakati wa ziara ya Kamati ilikuta mradi umekamilika ambapo Jengo la ghorofa mbili likukuwa limejengwa; Mashine za kisasa kwa ajili ya utafiti zilikuwa zikiendelea kufungwa na Baadhi ya watumishi walikuwa wameanza kuhamia katika jengo jambo lililopunguza msongamano uliokuwepo katika majengo yaliyokuwa yakitumika awali.

**Mheshimiwa Spika,** Changamoto katika utekelezaji wa Mradi huu ilikuwa ni mabadiliko ya mpango wa awali wa ujenzi wa jengo ambalo lililengwa kutumika upande mmoja kwa ajili ya ofisi na upande mwingine kwa ajili ya Biashara. Mabadiliko haya yalipelekea kuchelewesha utekelezaji wa mradi sababu Baraza lililazimika kuanza upya mchakato wa upatikanaji wa mchoro wa jengo jipya;

**Mheshimiwa Spika,** Kamati pia ilifahamishwa changamoto za Baraza katika utekelezaji wa Majukumu yake ambapo moja ya changamoto kubwa ni upungufu wa watumishi ambao ni wataalamu wa masuala ya mazingira jambo linalopelekea kushindwa kutekeleza jukumu la ukaguzi wa masuala ya mazingira kwa ufanisi. Makadirio ya Baraza ili waweze kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi wanahitaji angalau wafanyakazi 2000 na lakini kwa sasa wana wafanyakazi 250.

**Mheshimiwa Spika,** hapo awali Ofisi za Baraza hazikuwa na hadhi inayoendana na ukubwa wa ofisi hii huko Duniani, walikuwa wanatumia nyumba walizozikuta wakati wananunua viwanja na kupelekea baadhi ya ofisi kuwa katika stoo ya nyumba hizo. Hatua hii ilikuwa ikipelekea baadhi ya wawekezaji hususani kutoka nje ya nchi kukosa imani na huduma za Baraza. Jengo limeipa Baraza sehemu ya kufanyia kazi lakini pia imelipa Baraza hadhi inayostahili ni hatua nzuri;

**Mheshimiwa Spika,** kwa kuwa Serikali imeamua kuhamia Dodoma pamoja na Taasisi zake, Kamati inaishauri Serikali kuziwezesha taasisi hizo kifedha ili ziweze kujenga ofisi zake kama ilivyofanya kwa Wizara. Hatua hiyo itaondoa gharama za ukodishaji wa majengo.

**Mheshimiewa Spika**, Kamati inatambua ukubwa wa jukumu la ukaguzi na usimamizi wa mazingira, idadi ya wataalamu 250 wa masuala ya mazingira haitoshi. Kamati inaishauri Serikali kutoa vibali vya ajira ya wataalamu wa mazingira kwa kuwa bila kuwa na watumishi wa kutosha hawataweza kutekeleza majukumu yao ipasavyo na lawama zitaendelea kutolewa kwa Baraza kwamba halitekelezi majukumu yake.

#### 2.2.4 **Shughuli za Usimimamizi wa Mazingira katika Ziwa Manyara**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipata fursa ya kutembelea Hifadhi ya ziwa Manyara kwa lengo la kujionea hali ya mazingira katika eneo la hifadhi ya ziwa Manyara, changamoto na mkakati wa Serikali katika kukabiliana na athari za kimazingira katika eneo hilo la hifadhi.

**Mheshimiwa Spika**, Shughuli za uhifadhi wa Mazingira katika ziwa Manyara zinatekelezwa na TANAPA na zinahusisha shughuli zifuatazo; Kutoa elimu ya mazingira na Sheria ya Usimamizi wa Mazingira katika ngazi ya wilaya na Halmashauri za Mkoa wa Manyara, Kufanya ufuatiliaji wa wachimbaji wadogo na wakubwa ili waweze kuchimba kwa kufuata taratibu na sheria zilizopo, na Kutengeneza mabwawa (makingia maji) kuzunguka eneo la ziwa ili yaweze kupokea maji ya mvua yanayotoka katika maeneo ya miinuko kwa ajili ya kuchuja tope, hivyo mabwawa hayo kusaidia kupunguza uingiaji wa tope katika ziwa Manyara;

**Mheshimiwa Spika,** Shughuli za uhifadhi wa Mazingira katika Ziwa Manyara zinakumbana na changamoto zifuatazo;-

i) Ukosefu wa fedha kwa ajili ya kutekeleza shughuli za uhifadhi na usimamizi wa mazingira katika eneo la hifadhi, jambo linalopelekea athari za uharibifu kuendelea na kupelekea kuhatarisha eneo la hifadhi hususani ziwa Manyara;

ii) Shughuli za kibinadamu (kilimo kisichofuata kanuni za kitaalamu, uwepo wa mifugo mingi) katika maeneo ya karibu na ziwa Manyara zinazopelekea tope jingi kuelekea ziwani na kupunguza kina cha maji;

iii) Mabadiliko ya Tabianchi ambayo hupelekea ukame na kukauka kwa vyanzo vya maji yatiririkayo kwenda ziwani na kupelekea kukauka kwa ziwa;

iv) Shughuli za kibinadamu katika eneo la hifadhi zisizolenga matumizi endelevu ya rasilimali za asili jambo linalopelekea kuharibu mfumo zima wa Ikolojia ya Tarangire na ziwa Manyara na kuviweka katika hatari ya kutoweka; na

v) Mimea vamizi/wageni katika baadhi ya vyanzo vya maji vya ziwa Manyara ambavyo hupelekea maji kushindwa kufika ziwani, hali hiyo pia hupunguza vyanzo na upatikanaji wa maji na hatimaye kuharibu mazingira wanyamapori.

**Mheshimiwa Spika,** Baada ya ziara katika ziwa Manyara Kamati ilikuwa na maoni na ushauri ufuatao;-

i) Serikali itumie matakwa ya Sheria ya Mazingira ya mwaka 2004 kufanya mchakato wa haraka wa kuliingiza ziwa Manyara katika maeneo lindwa kwa lengo la kuliweka katika usimamizi maalumu. Hatua hii ichukuliwe kwa maziwa yote ambayo yapo katika hatari ya namna hii likiwepo zawa Jipe na Chala;

ii) Serikali iangalie namna ya kuwasaidia na kuwasimamia wakulima na wafugaji kufanya shughuli zao mbali na miinuko kwa lengo la kuzuia maporomoko ya udongo na tope katika ziwa Manyara ambayo yanapekekea kupungua kwa kina cha ziwa na kuliondolea uwezo wa kutunza maji kwa muda mrefu; na

iii) Serikali ichukue jitihada za makusudi kuhakikisha wanalinusuru ziwa Manyara na Bioanuai zake kwa kuzingatia kuwa ziwa na Bioanuai hizo ndio kivutio kikubwa kinachovuta utalii katika hifadhi ya Manyara, changamoto zinazopelekea kukauka kwa ziwa kupelekea kupungua kwa shughuli za utalii katika hifadhi ya Manyara.

## 2.3 UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2018/2019

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa Kanuni ya 98 (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016 Kamati za Bunge za Kisekta hufanya uchambuzi wa taarifa za utekelezaji wa Bajeti za Wizara zinazozisimamia kwa mwaka wa fedha unaoishia pamoja na kufanya ulinganisho wa Utekelezaji wa Bajeti na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha unaofuata.

### 2.3.1 Uchambuzi wa Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara ya Viwanda na Biashara kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipokea, kuchambua na kujadili taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara ya Viwanda na Biashara kwa mwaka wa fedha 2018/2019 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020. Kamati ilifanya uchambuzi wa taarifa zilizowasilishwa Wizara na ilizingatia makusanyo ya maduhuli, fedha zilizoidhinishwa kwa mwaka wa fedha husika na upatikanaji wa fedha kutoka Hazina.

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2018/2019, Wizara na taasisi zilizopo chini yake ilipanga kukusanya jumla ya Shilingi **20,006,300,000** kutoka katika makusanyo ya ada za leseni, mauzo ya nyaraka za zabuni na faini ya kukiuka Sheria ya Leseni ya Biashara. Hadi kufikia kufikia Juni, 2019 Wizara ilikuwa imekusanya jumla ya Shilingi **8,990,341,969.04** kiasi ambacho ni sawa na asilimia **44.94** tu ya lengo lililo kusudiwa.

**Mheshimiwa Spika**, Uchambuzi wa Kamati ulibainisha kuwa, makusanyo ya Wizara yalikuwa pungufu kwa asilimia **55.94**. Kamati iliishauri Serikali kupanga bajeti ya makusanyo maduhuli kwa kuzingatia uhalisia wa vyanzo vyake vya mapato ili kuwa na uhakika wa kufikia malengo.

**Mheshimiwa Spika**, Katika Mwaka wa Fedha **2018/2019**, Wizara ya Viwanda na Biashara ilitengewa na kuidhinishiwa jumla ya shilingi **143,334,153,648.00** kati ya fedha hizo Shilingi **100,024,525,000.00** ikiwa kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo na Shilingi **43.309.628,648.00** kwa ajili ya matumizi ya kawaida kwa mafungu yake yote mawili **Fungu 44** Viwanda na **Fungu 60** Biashara.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilielezwa, hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2019, Wizara ilikuwa imepokea jumla ya Shillingi **59,628,585,389.66** kutoka Hazina kwa ajili ya mafungu yote **44** na **60** ambapo Shilingi **13,639,752,487.00** kwa ajili ya miradi ya maendeleo na Shilingi **45,988,832,902.00** kwa ajili ya mishahara na matumizi mengineyo.

**Mheshimiwa Spika**, Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2019, kati ya Shilingi **100,024,525,000.00** fedha kwa ajili ya miradi ya maendeleo ni Shilingi bilioni **13,639,752,487.00** tu ndizo zilikuwa zimepokelewa kwa mafungu yote mawili **44** na **60** kutoka bajeti ya Fedha za Ndani, kiasi hiki ni sawa na asilimia **13.63** ya fedha zote za Miradi ya Maendeleo.

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa uchambuzi wa takwimu Kamati imesikitishwa na utoaji wa fedha kutoka Hazina ambao umekuwa siyo wa kuridhisha. Kamati inaendelea kuishauri Serikali kupeleka fedha zilizoidhinishwa na Bunge kwa wakati ili kuiwezesha Wizara kutekeleza majukumu yake ipasavyo.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya kuchambua utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa mwaka wa fedha unaoishia, kamati hufanya ulinganisho wa makisio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha unaofuata kwa lengo la kupata uhalisia wa kiasi kinachoombwa ukilinganisha na

utekelezaji wa mwaka ulioisha katika kipengele cha ukusanyaji wa maduhuli na kipengele cha maombi ya fedha.

**Mheshimiwa Spika,** Katika mwaka wa fedha 2019/2020 wizara ya viwanda na biashara imepanga kukusanya Shilingi **6,300,000.00** kwa **Fungu 44 na 60** kutokana na uuzaji wa nyaraka za zabuni. Kiasi cha makusanyo kwa mwaka wa fedha 2019/2020 kimepungua kwa kiasi kikubwa ukilinganisha na mpango wa makusanya ya mwaka wa fedha 2018/2019. Maelezo ya wizara yalikuwa ni kwamba chanzo kikubwa cha makusanyo ya wizara kilikuwa uuzaji wa leseni za biashara na faini zitokanazo na leseni za biashara ambavyo kwa sasa vimehamia Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA). Wizara imebakiwa na uuzaji wa nyaraka za zabuni ambazo mapato yake ni madogo. Kamati iliishauri wizara kuweka mikakati mahususi ya kutafuta vyanzo vingine/vipya vya mapato ili waweze kuongeza makusanyo.

**Mheshimiwa Spika,** Katika mwaka wa fedha 2019/2020, wizara ya viwanda na biashara kwa mafungu yote mawili (Fungu **44** na **60**) ilitengewa Shilingi **100,384,738,648.00** ambapo Shilingi **48,884,738,648.00** kwa ajili ya matumizi ya kawaida na Shilingi **51,500,000,000.00** kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Bajeti ya mwaka wa fedha 2019/2020 ni pungufu kwa asilimia **29.9** ya shilingi **143,334,153,648**.00 ya bajeti iliyotekelezwa kwa mwaka wa fedha 2018/2019 na athari kupungua huku imeonekana hasa kwenye fedha za miradi ya maendeleo ambazo zimepungua kwa asilimia **48.51** ya kiasi kilichokuwa kimepangwa katika mwaka 2018/2019.

**Mheshimiwa Spika,** Uchambuzi wa Kamati ulibaini kuwa utengaji wa bajeti ni jambo moja na utekelezaji wa bajeti hiyo ni jambo lingine. Umuhimu upo katika utekelezaji wa bajeti ambao umekuwa ukikwamishwa na mwenendo usioridhisha wa Upatikanaji wa fedha kutoka Hazina. Kamati inaendelea kuisisitiza Serikali kuwa fedha zinachoidhinishwa na Bunge zitolewe tena kwa wakati kwa lengo la kutekeleza majukumu yaliyokusudiwa.

### 2.3.2 Uchambuzi wa Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Ofisi ya makamu wa Rais-Mazingira kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2018/2020

**Mheshimiwa Spika**, Katika kufuatilia utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Rais - Mazingira kwa mwaka wa fedha 2018/2019, Kamati ilijikita katika kuchambua mwenendo wa makusanyo ya maduhuli, upatikaji wa fedha zilizoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya Miradi ya maendeleo pamoja na fedha zilizotengwa ili kutekeleza majukumu mengine ya Ofisi.

**Mheshimiwa Spika**, Ofisi ya Makamu wa Rais-Mazingira hufanya Makusanyo kupitia Baraza la Taifa la Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira - *NEMC.* Katika Mwaka wa Fedha 2018/2019 Baraza lilipanga kukusanya kiasi cha Shilingi **18,877,446,995.00** kutoka katika vyanzo vyake vya ndani. Kamati ilijulishwa kuwa, hadi kufikia tarehe 13 Juni, 2019 Baraza lilikuwa limekusanya Shilingi **10,430,060,727.00** tu sawa na asilimia **44.8** ya makadirio yake. Kamati inaendelea kusisitiza Baraza kupanga lengo la maduhuli kwa umakini mkubwa na kuzingatia uhalisia wa vyanzo vyao vya mapato na uwezo wao wa kukusanya.

**Mheshimiwa Spika**, Katika mwaka wa fedha **2018/2019** Ofisi ya Makamu wa Rais Idara ya Mazingira iliidhinishiwa jumla ya Shilingi **8,118,494,000.00.00** kwa ajili ya kutekeleza majukumu yake. Hadi kufikia tarehe 14 Machi, 2019 Ofisi hii ilikuwa imepokea shilingi **4,167,969,635.79** tu, sawa na asilimia **51.3** ya fedha zote zilizokuwa zimeidhinishwa na Bunge.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati haikuridhishwa na bajeti iliyopokelewa kwa ajili ya masuala ya uhifadhi na usimamizi wa mazingira. Aidha, pamoja na udogo wa bajeti bado fedha imekuwa haitolewi yote jambo ambalo linakwamisha utekelezaji wa majukumu ya uhifadhi wa mazingira.

Kamati iliishauri Serikali kuweka mikakati na msisitizo katika kuwezesha shughuli za usimamizi wa mazingira kwa kupeleka fedha za kutosha zikiwepo fedha za ndani na kuzipeleka kwa wakati.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya kuchambua utekelezaji wa Mpango wa Bajeti ya uhifadhi wa mazingira kwa mwaka wa Fedha 2018/2019, Kamati ilifanya ulinganisho uchambuzi wake juu ya utekelezaji wa bajeti hiyo na Makisio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha unaofuata. Katika mwaka wa fedha 2019/2020 Ofisi ya Makamu wa Rais-Mazingira kupitia Baraza la Taifa la Uhifadhi na Usimamizi Mazingira (***NEMC***) imepanga kukusanya shilingi **18,218,915,442.00.00** kutokana vyanzo vyake vya ndani. Makisio ya mwaka wa fedha **2019/2020** yalikaribiana kabisa na malengo ya Mwaka wa Fedha 2018/2019 ambayo yalitekelezwa kwa asilimia **55.2** tu hivyo kukosa uhalisia.

**Mheshimiwa Spika,** Ofisi ya Makamu wa Rais-Mazingira, Idara ya Mazingira katika mwaka wa fedha **2019/2020** iliomba kuidhinishiwa Shilingi **22,708,713,882.00** kwa ajili ya kutekeleza majukumu yake. Kiasi hiki ni ongezeko la asilimia **179.71** ya bajeti ya mwaka 2018/2019. Ongezeko hili lilikuwa katika upande wa fedha za miradi ya maendeleo ambapo iliongezeka kutoka Shilingi **3,524,540,000.00** Mwaka 2018/2019 mpaka shilingi **18,218,915,442.00** Mwaka wa Fedha 2019/2020.

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa kamati ulibaini kuwa ongezeko hili lilitokana na jitihada za Ofisi ya Makamu wa Rais- Mazingira kuandaa maandiko mengi na mazuri ambayo yaliweza kushawishi wafadhili kutupatia fedha. Kamati ilipongeza jitihada hizo na kuiomba Ofisi hii kuongeza kasi ya kuandaa maandiko mengi zaidi kwani fursa ya kupata fedha ya maendeleo kwa njia ya ufadhili bado ni kubwa.

## 2.4 TAARIFA MBALIMBALI ZA UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA WIZARA YA VIWANDA NA BIASHARA NA TAASISI ZILIZO CHINI YAKE

**Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha kuanzia Machi 2019 hadi Januari, 2020, Wajumbe walipokea, kuchambua na kujadili taarifa mbalimbali za Utekelezaji wa majukumu ya Wizara na Taasisi zilizo chini ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji pamoja na Ofisi ya Makamu wa Rais-Mazingira taarifa hizo ni kama zifuatavyo:-

a) **Kupokea na kujadili taarifa ya Wizara ya Viwanda na Biashara kuhusu Utekelezaji wa Maazimio ya Bunge yanayohusiana na majukumu ya Wizara hii, yaliyotokana na Mapendekezo ya Kamati ya Viwanda, Biashara na Mazingira katika Taarifa yake ya Mwaka iliyowasilishwa katika Mkutano wa Bunge wa Mwezi Februari, 2019**

**Mheshimiwa Spika,** mnamo Mwezi Februari, 2019 Kamati ya Viwanda kama ilivyo kwa Kamati nyingine za Bunge iliwasilisha Bungeni ya Taarifa ya Mwaka ya Shughuli ilizotekeleza kwa kipindi cha Machi, 2018 hadi Januari, 2019, kwa mujibu na kwa kuzingatia matakwa ya Kanuni ya 117 (15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016. Taarifa ya hii ilitoa mapendekezo ambayo yalijadiliwa na hatimaye kupitishwa kuwa Maazimio ya Bunge;

**Mheshimiwa Spika,** Naomba kuliarifu Bunge lako Tukufu na kuwa Kamati ya Viwanda, Biashara na Mazingira ilifuatilia utekelezaji wa Maazimio Tisa (9) ya Bunge yalielekezwa kwa Wizara ya Viwanda na Biashara kwa lengo la kuiwezesha kupata mrejesho wa maazimio yaliyotolewa na kufahamu hatua mbalimbali za utekelezaji wake kwa lengo la kuendelea kufuatilia utekelezaji wake;

**Mheshimiwa Spika,** Katika kuchambua taarifa ya Wizara Kamati ilibaini na kushauri katika maazimio (maeneo) ambayo hawakuridhishwa na maelezo (hatua) ya utekelezaji wake. Maeneo hayo ni pamoja na;-

i) Mwenendo usioridhisha juu ya upatikanaji wa fedha kwa Wizara unatokana Serikali, Kamati ilipewa maelezo kuwa hii inatokana na pesa nyingi kuelekezwa kwenye miradi mikubwa ya kimkakati kama Mradi kufua umeme wa maji wa Stiglers Gorge na mradi wa ujenzi wa Reli wa Standard Gauge.

- Kamati ilisisitiza kwa kuwa Serikali iliwasilisha mpango wa Bajeti yake Bungeni iliyojipambanua kwa kuzingatia mahitaji halisi ya kila sekta na mahali fedha zitakapopatikana. Kamati inaishauri Serikali kutekeleza Bajeti iliyoidhinishwa na Bunge kama ilivyo;

- Kamati inaendelea kusisitiza Serikali (Wizara) kupanga Bajeti inayoakisi makusanyo halisi ya Nchi. Vile vile Wizara ilishauriwa kuwa na utaratibu wa kujipangia miradi michache ya kuitekeleza kwa kipindi husika na utekelezaji wa miradi hiyo uwe na muda maalumu (time frame). Jambo litakalosukuma utekelezaji wake kwa kujua kuwa lazima ikamilike ndani ya muda fulani;

ii) Kusasua kwa utekelezaji wa Mradi wa Chuma cha Liganga na Makaa ya Mawe ya Mchuchuma ambapo Kamati iliishauri Serikali kutafuta mbobezi wa lufanya utafiti kwa niaba ya Serikali badala ya kutumia ripoti ya Mbia tu ambayo ilitiliwa mashaka. Maelezo ya Serikali ni kuwa utafiti ulishafanywa na mbia na ripoti hiyo ndio ilitumika kuingia mkataba wa awali wa utekelezaji wa mradi.

- Kwa kuwa imeripotia kuwa mikataba ya mradi wa Liganga na Mchuchuma inafanyiwa mapitio upya kwa lengo la kuiboresha. Kamati inaendelea kuisisitiza Serikali kutafuta mbobezi (expert) ambae atatumika kufanya upembuzi yakinifu katika miradi hiyo kwa niaba ya Serikali, kwa lengo la kutoa uwazi (transparence) wa hali halisi iliyopo katika miradi hiyo, kwa manufaa ya pande zote mbili yaani muwekezaji na Serikali. Kutumia taarifa ya mbia kufanya maamuzi kunaleta mashaka kwani muwekezaji anaweza kujipendelea;

iii) Utekelezaji wa Mradi wa kufufua kiwanda cha Matairi cha *General Tyre* kuchukua muda mrefu, maelezo ya Serikali ni kuwa inandaa mpango madhubuti na uwekezaji.

- Kamati inaendelea kuishauri Serikali kuandaa mpango madhubuti wa kufufua kiwanda hicho. Pia Kamati imeishauri Serikali kuweka muda maalumu (time frame) ya kutekeleza mpango huo na pindi muda huo utakapoisha kukawa hakuna lililofanyika, Serikali ichukue uamuzi wa kubadilisha matumizi ya eneo hilo la kiwanda;

iv) Bajeti ndogo inayotengwa na kupelekwa kwenye Shirika la Maendeleo la Taifa – NDC haiendani na majukumu makubwa ya Shirika

- Kamati inashauri kwa udogo huo wa Bajeti, ni vema NDC ikajipanga katika kila Mwaka wa Fedha ikaamua kujikita na mradi mmoja ili kuutekeleza kikamilifu; na

- Vile vile, Kamati inaendelea kuisisitiza Serikali kulitengea Shirika la Maendeleo la Taifa – NDC bajeti kulingana na majukumu ya Shirika hilo.

b) **Kupokea na kujadili Taarifa ya Wizara ya Viwanda na Biashara kuhusu Mradi wa Matrekta ya URSUS TAMCO – Kibaha.**

**Mheshimiwa Spika,** Shirika la Maendeleo la Taifa – NDC ndio shirika mama ambalo kihistoria ndio lilianzisa Mashirika, makampuni na viwanda vyote vya Serikali nchini. NDC inamilikiwa na Serikali kwa asilimia miamoja na linatekeleza majukumu yake yaliyowekwa kisheria kwa kuzingatia Sheria ya Makampuni ya Mwaka 1992 pamoja na uamuzi wa Baraza la Mawaziri wa Mwaka 1996 Paper Na. 6/96.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa kuzingatia Sheria tajwa Shirika linatekeleza majukumu yake ya kusimamia na kuendeleza viwanda mama vya kimkakati ambavyo vilianzishwa na Serikali kwa makusudi ya bidhaa zake kuwa malighafi ya viwanda vingine; pale ambapo mwekezaji anataka kuwekeza kwa ubia na Serikali, na kuainisha na kuendeleza maeneo yenye fursa za kiuchumi ambapo sekta binafsi haioneshi nia ya kutaka kuwekeza katika maeneo hayo.

**Mheshimiwa Spika,** kwa lengo la kuongeza ufanisi katika Sekta ya Kilimo ili tuweze kuzalisha mazao ya kutosheleza mahitaji ya nchi ya chakula pamoja na kuvihudumia viwanda vyetu Serikali iliamua kutekeleza kuunganisha Matreka aina ya URSUS. Mradi huu unatekelezwa kwa mujibu Mkataba ulioingiwa kati ya Kamapuni ya URSUS S.A ya Poland na SUMA JKT na mkataba huo unaojulikana kama **"Supply of Tractors, Implements, Spare Parts and releted Services of 22 Octoba, 2015"** ambao ulifanyiwa marekebisho Agosti, 2018.

**Mheshimiwa Spika,** Mkataba huu una maeneo manne ambayo ni kuingiza nchini matrekta 2400 na zana zake kutoka Poland vikiwa katika vipande vikubwa na vingine katika mfumo wa vipuri; ujenzi wa kiwanda cha kuunganisha matrekta; kuanzisha vituo nane (8) vya kuhudumia matrekta katika sehemu mbalimbali nchini na kufundisha wataalamu wa kitanzania nchini Poland;

**Mheshimiwa Spika,** utekelezaji wa mradi huu mpaka sasa ni kwamba yaliingizwa nchini matrekta 825 ambapo ilipaswa kuwa tumepokea matrekta 2400 na mpaka sasa yameuzwa matreka 586 kati ya yaliyopokelewa; ujenzi wa kiwanda cha kuunganisha matrekta unaendelea na umefikia asilimia 60 ambapo ujenzi huu tayari umechelewa sababu ulipaswa kukamilika mwezi Juni, 2018; vituo vya marekebisho hakuna hata kimoja ambapo kwa mujibu wa mkataba vilitakiwa kuwa vimeshaingia kutoka Poland; mafundi na wasimamizi 27 wamekwishapata mafunzo ya kuunganisha tekta za URSUS;

**Mheshimiwa Spika,** Mkataba wa Mauziano wa Matrekta hayo kati ya Kampuni ya URSUS na SUMA JKT una changamoto sana. Hali hiyo inatokana na uhalisia kwamba kama nchi tumekwisha lipa asilimia **65** ya fedha kulingana na mkataba, wakati URSUS wanaonekana kushindwa kukamilisha upande wao wa mkataba kwani mpaka sasa walitakiwa wawe wameshaleta matrekta 2400, lakini wameleta matrekta 825 tu. Vilevile taarifa zilizopo ni kuwa Kampuni ya URSUS imeshindwa kuendelea na uzalishaji matrekta kwa kuwa ipo katika hatua ya kufilisiwa kupitia mahakama. Kamati inaishauri Serikali kuchukua hatua stahiki juu ya Mkataba huo;

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaishauri Serikali kukaa chini na Serikali ya Poland na kufanya mapitio na *re-negotiation* ya mkataba husika kwa manufaa ya pande zote mbili;

**Mheshimiwa Spika,** Matrekta yanayouzwa kupitia mradi huu yamekuwa yakilalamikiwa na wakulima kuwa yanaharibika mara kwa mara. Kamati inaishauri NDC kuhakikisha kabla Trekta halijaenda kwa mkulima linafanyiwa ukaguzi wa kutosha na kufanya marekebisho maeneo ambayo yameonekana yana matatizo; na

**Mheshimiwa Spika,** NDC imekuwa ikikiri changamoto ya Matrekta hayo kwa wakulima na kuwaelekeza mahali pakupata *spare* (vipuri) nzuri ambazo zinazalishwa na washindani wao. Jambo hilo linaua soko la Matrekta ya URSUS sababu linawadhihirishia wakulima kuwa matrekta ya washindani ndio bora kuliko ya URSUS yanayouzwa na NDC;

c) **Kupokea na kujadili Taarifa ya Wizara ya Viwanda na Biashara kuhusu Utendaji wa Shirika la Viwango Tanzania (TBS);**

**Mheshimiwa Spika,** Shirika la Viwango Tanzania *–TBS* inajukumu la kusimamia shughuli za utayarishaji wa viwango na udhibiti wa ubora wa bidhaa zinazozalisha nchini na zile zinazoingia kutoka nje, TBS inatekeleza majukumu hayo kwa mujibu wa Sheria Na. 2 ya Mwaka 2009. Pamoja na majukumu tajwa hapo juu Sheria ya Fedha ya mwaka 2019 ililiongezea Shirika majukumu ya udhibiti wa usalama wa chakula na vipodozi majukumu ambayo yalikuwa yanatekelezwa na iliyokuwa mamlaka ya Chakula na Dawa TFDA.

**Mheshimiwa Spika,** Miongoni mwa madhumuni ya kuanzishwa kwa TBS ni kudhibiti uingizaji wa bidhaa zisizokidhi viwango ndani ya nchi ili kuhakikisha ni bidhaa bora tu lakini bado kuna baadhi ya wafanyabiashara wasio waaminifu ambao bado wanaendelea kutumia njia za panya kuingiza bidhaa zao. Kamati inaishauri Serikali kuiongezea nguvu TBS kwa kuwaongezea watumishi wakaguzi ili kuongeza kasi ukaguzi na kuiokoa jumii juu ya matumizi ya bidhaa zisizo na viwango. Jambo hili liende sambamba na TBS kuongeza kasi ya kutoa elimu kwa jamii juu ya madhara ya kutumia bidhaa zisizo na viwango;

**Mheshimiwa Spika,** Idadi kubwa ya wajasiriamali wadogo wanazalisha bidhaa za chakula, vinywaji baridi na moto, sabuni, maji na vipodozi ambapo jukumu la kuwakagua bidhaa hizo zililikuwa chini ya TFDA na sasa limehamia TBS ambao kwa sasa tu wanalalamikia upungufu wa watumishi hususani wakaguzi. Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha wanaiwezesha TBS kwa kuwapatia rasilimali watu na fedha ili kuhakikisha majukumu mapya ya TBS yanatekelezwa kwa kiwango kilichokusudiwa.

**Mheshimiwa Spika,** katika kudhibiti ubora wa bidhaa zinazotoka nje ya nchi TBS inatumia mfumo wa Ukaguzi wa bidhaa hizo kwa kutumia mfumo wa (PVOc) ambazo bidhaa hizo hukaguliwa kabla ya kuingia nchini, mfumo wa PVOc unalalamikiwa sana kwa kuwa baadhi ya Wakaguzi wanaotumiwa na TBS si waaminifu. Wakaguzi hao wamekuwa wakitoa vyeti vya ubora bila kukagua bidhaa, hivyo kutoa mianya kwa baadhi ya wafanyabiashara wasio waaminifu kuingiza bidhaa zisizokidhi viwango. Kamati inaishauri Serikali kufanyakazi kwa karibu sana na Wakaguzi wa nje ya nchi kuhakikisha kabla ya kutoa vyeti vya ubora wawe wanakagua bidhaa zote.

**Mheshimiwa Spika,** kwa kuzingatia jukumu la TBS la udhibiti ubora, Kamati inaishauri Serikali kupitia TBS kusimamia suala la mifuko mbadala ya mifuko ya plastiki na kuhakikisha inazalishwa kwa ubora na viwango stahiki. Nchi imepiga marufuku matumizi ya mifuko ya Plastiki lakini hatukujiandaa kupata mifuko mbadala inayokidhi viwango, mifuko mbadalsa iliyopo sokoni inapatikana kwa bei kubwa na imekuwa ikichanika na kuleta hasara kwa watumiaji (bidhaa zao kumwagika).

**Mheshimiwa Spika,** Viwanda vingi hapa nchini vinalalamikia kukosa soko la bidhaa zao na moja ya chanzo cha jambo hilo ni ushindani usio wa haki katika soko unaoshababisha na uwepo wa bidhaa duni sokoni zinazouzwa kwa bei ya chini. Mfano bidhaa ya Mabati, Chuma, vigae, ceiling borad na zinginezo. Kamati inaendelea kuisisitiza Serikali kuiongezea TBS rasilimali watu na fedha ili kuongeza kasi ya ukaguzi na kuiwezesha kufikia maeneo mengi zaidi ili kudhibiti uingizaji wa bidhaa duni sokoni.

d) **Kupokea na kujadili Taarifa ya Wizara ya Viwanda na Biashara kuhusu Utendaji wa Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania (TANTRADE)**

**Mheshimiwa Spika,** Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania (TANTRADE) ni taasisi ya Serikali iliyoundwa chini ya Sheria Na. 4 ya Mwaka 2009 kwa dhumuni la kuwezesha ukuaji wa uchumi wa Tanzania kwa kuendeleza na kutangaza biashara ndani na nje ya nchi. TanTrade inatekeleza dhima yake kwa kutafuta masoko ya bidhaa na huduma zinazozalishwa nchini, kushauri maendeleo ya biashara nchini na kusimamia Sekta ya Maonyesho nchini;

**Mheshimiwa Spika,** majukumu mengine ya TanTrade ni pamoja na kufanya utafiti wa biashara na masoko; kutoa ushauri wa biashara na masoko; kujenga uwezo wa sekta ndogo (SMEs) ili ijiendeshe kiushindani; kutangaza bidhaa za ndani katika soko la nje; kutoa ushauri wa sera za biashara na uwezeshaji nchini;

**Mheshimiwa Spika,** nchi yetu imejielekeza katika ujenzi wa Uchumi wa Kati kwa kupitia Viwanda na tunaishukuru sana Sekta binafsi imetoa muitikio mkubwa kwa kuanzisha viwanda mbalimbali na kwa viwanda vilivyokuwa vipo vilipanua uzalishaji wake kuhakikisha wanaendana na kasi ya nchi. Changamoto ya upatikanaji wa Soko la bidhaa zetu inashusha ari ya wawekezaji wetu, Kamati inaishauri TanTrade kutumia fursa wanayoipata ya kushiriki katika mikutano mbalimbali ya biashara Duniani kuitangaza Tanzania na bidhaa zake.

**Mheshimiwa Spika,** bidhaa za Tanzania zinachangamoto ya vifungashio ambavyo kimsingi ndio vinauvyoweza kuongeza ubora na tathmini. Vilevile kuna uhaba wa upatikanaji wa vifungashio nchini. Vifungashio vinavyotengenezwa nchini sio shindani katika soko la Kimataifa, kwa mfano Bidhaa ya Asali inatakiwa kufungashwa katika chupa ya kioo lakini upatikanaji wa chupa hizo ni changamoto, jambo linalopelekea wajasiriamali nchini kutumia chupa za plastiki hivyo kupelekea kushindwa kuuzwa kimataifa. Kamati inaishauri Serikali kutafuta ufumbuzi wa haraka juu ya changamoto ya vifungashio;

**Mheshimiwa Spika,** TanTrade inajukumu la kutafuta masoko ya mazao yanayozalishwa nchini. Hivyo basi Kamati imeishauri mamlaka hiyo kushirikiana kwa ukaribu na Wizara ya kilimo kutoa elimu kwa Wakulima nchini juu ya viwango vya ubora wa mazao vya kimataifa. Hatua hii itasaidia wakulima kuzalisha mazao yatakayoweza kushindana katika masoko ya kimataifa na kuwatoa wakulima katika kilimo cha mazoea;

**Mheshimiwa Spika,** TanTrade ilikuwa inatumia waambata wa biashara waliopo katika ofisi za balozi zetu nje ya nchi kupata taarifa mbalimbali na kuhamasisha watu kuja Tanzania kuwekeza au kufanya biashara. Kwa sasa TanTrade haina waambata hao jambo linalowawia viguma kujitangaza ukizingatia uwezo wa TanTrade wa sasa ambapo haiwezi kuzunguka nchi zote na kutafuta fursa. Kamati inaishauri Serikali kurudisha utaratibu uliokuwepo awali wa kuwa na waambata wa biashara katika balozi zetu, kwa kuanzia tunaweza kuchagua nchi chache za mfano ambapo TanTrade imeona kuna fursa kubwa katika nchi hizo. Sambamba na hilo waambata hawa wawe ni wabobezi wa mambo ya biashara ili kuwawezesha kushiriki kikamilifu katika shughuli zote za fursa (mikutano na makongamano ya kibiashara duniani); na

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaishauri TanTrade kuongeza kasi ya kutafuta masoko ya nje ya bidhaa zetu ili kuongeza uuzaji wa bidhaa nje ya nchi. Jukumu hili liende sambamba na kusoma kwa makini na kufahamu bidhaa zinazohitajika katika soko la kimataifa ambazo zinapatikana nchini, kisha kurudi na kuwaelimisha wazalishaji wa ndani ili kuwaweka katika nafasi ya kushindana sokoni.

e) **Kupokea na kujadili Taarifa ya Wizara ya Viwanda na Biashara kuhusu Utendaji wa Wakala wa Vipimo Tanzania (WMA);**

**Mheshimiwa Spika,** Wakala wa Vipimo Tanzania WMA ni taasisi ya Serikali iliyoanzishwa kwa mujibu wa Sheria ya Wakala wa Serikali Na. 30 ya Mwaka 1997 na inatekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Sheria ya vipimo Sura Na. 340. Wakala ilianzishwa kwa madhumuni ya kutekeleza programu ya kuboresha utumishi wa Umma kwa lengo la kuongeza tija na ufanisi katika utoaji wa huduma kwa umma kupitia matumizi ya vipimo sahihi;

**Mheshimiwa Spika,** majukumu ya Wakala ni pamoja na kuhakikisha vipimo vyote vinavyotumika katika Sekta ya Biashara, Afya, Usalama na Mazingira kwa lengo la kuilinda jamii na madhara yatokanayo na matokeo ya upimaji usiosahihi; kutoa ushauri wa kitaalamu kwa Serikali, mashirika, taasisi na wadau wengine kuhusiana na vipimo; kutoa huduma ya ugezi na leseni za ufundi na uandaaji wa vipimo mbalimbali; kukagua na kuhakiki bidhaa zilizofungashwa toka ndani na nje ya nchi; kusimamia matumizi sahihi ya vipimo kwa njia ya kufanya ukaguzi wa mara kwa mara;

**Mheshimiwa Spika,** Pamoja na majukumu makubwa na muhimu ya Wakala bado inakabiliwa na changamotoa mbalimbali ambazo ni pamoja na upungufu wa rasilimali watu na fedha jambo linaloathiri utekelezaji wa majukumu yake kwa ufanisi; uwezo wa maabara usioendana na ongezeko la uwekezaji na unaoendelea kufanyika nchini hivyo kushindwa kutekeleza majukumu kwa ufanisi;

**Mheshimiwa Spika,** idadi ya Maafisa vipimo haiendani na uhitaji wa huduma ya Wakala wa Vipimo jambo linalowapelekea kuhudumia sehemu ndogo sana ya Nchi (uhitaji ni watumishi 666 lakini kwa sasa wapo 133). Upungufu huo unatokana na uchache wa wahitimu wenye fani ya Vipimo nchini ambapo kwa sasa mafunzo hayo yanatolewa na chuo cha CBE tu na kila mwaka wanahitimu wanafunzi wasiozidi 40. Kamati inaishauri Serikali kuhamasisha na kutoa motisha kwa wasomi wa fani hiyo, kwa lengo la kupata wahitimu wengi watakaoajiriwa na kuongeza ufanisi kwa Wakala wa Vipimo nchini;

**Mheshimiwa Spika,** Wakala wa Vipimo ihakikishe inafuatilia na kujua minada ya mazao yote inayoendeshwa nchini na kushiriki kwenye minada hiyo kwa kipindi chote cha mnada kwa lengo la kuwasaidia wakulima wetu ambao kwa sasa wanaibiwa sana na Makarani wa minada hiyo kwa kuchezesha mizani makusudi ili kutoa hesabu zisizo sahihi;

**Mheshimiwa Spika,** Wakala wa Vipimo iongeze nguvu katika kukagua na kurekebisha mizani yote katika Vituo vya Afya nchini. Ubovu wa mizani hiyo umekuwa umekuwa na athari kwa vipimo vya uzito katika hospitali na hivyo kupelekea wagonjwa kupewa dawa zisizoendana na uzito wao (under or over prescription); na

**Mheshimiwa Spika,** Mita za maji na mita za umeme ni eneo ambalo linalalamikiwa sana, watumiaji wamekuwa wakilalamika kutozwa zaidi ya matumizi yao. Kamati inaishauri Wakala wa Vipimo kuhakikisha wanashirikiana na mamlaka husika kukagua mita hizo kabla hazijafungwa kwa watumiaji.

**Mheshimiwa Spika,** Mita za maji na mita za umeme ni eneo ambalo linalalamikiwa sana, watumiaji wamekuwa wakilalamika kutozwa zaidi ya matumizi yao. Kamati inaishauri Wakala wa Vipimo kuhakikisha wanashirikiana na mamlaka husika kukagua mita hizo kabla hazijafungwa kwa watumiaji.

f) **Kupokea na kujadili Taarifa ya Wizara ya Viwanda na Biashara kuhusu Utendaji wa Chama cha Hakimiliki Tanzania (COSOTA)**

**Mheshimiwa Spika,** Chama cha Hakimiliki Tanzania (COSOTA) kimeundwa chini ya Kifungu cha 46 cha Sheria Na. 7 ya Hakimiliki na Hakishirikishi ya mwaka 1999. Chama hiki kiliundwa kwa madhumuni la kulinda, kusimamia, kutetea na kukuza maslahi ya watunzi na wabunifu katika Nyanja za Sanaa (artistic work) na kazi za maandishi (literary works).

**Mheshimiwa Spika,** majukumu ya COSOTA ni pamoja na kukuza na kulinda maslahi ya watunzi, wachapishaji, watangazaji, wasanii wafasiri kwa kukusanya na kusambaza mirabaha au ujira utokanao na haki zao za kisheria; kutafuta, kusambaza na kutangaza haki za wamiliki; kutoa uthibitisho wa wamiliki pale inapotokea ubishani au ukiukwaji wa haki; na kuchapisha na kusambaza taarifa, majarida, vitabu, vipeperushi au maandiko yanayohusiana na hakimiliki na haki za wasanii;

**Mheshimiwa Spika,** katika utekelezaji wa majukumu ya COSOTA wanakabiliana na changamoto mbalimbali ikiwemo ufinyu wa rasilimali watu na fedha na vitendea kazi kama magari jambo linalokwamisha utekelezaji wa majukumu ya Chama; uelewa mdogo wa jamii juu ya kazi za COSOTA jambo linalopelekea watumiaji wa kazi za sanaa (vyombo vya habari, maktaba, vyuo na sehemu zinazotoa nakala za kazi za maandishi) kukataa kulipa mirahaba na mwisho wa siku COSOTA kushindwa kuwalipa wasanii mirahaba yao; na uzamani wa sheria ya Hakimiliki na hakishirikishi ambayo haiendani na mazingira ya sasa, mfano udogo wa adhabu inayotolewa ukilinganisha na kosa lililofanyika;

**Mheshimiwa Spika,** bila shaka sote tunatambua namna Sekta ya sanaa nchini ilivyotoa ajira kwa vijana wengi, mfano sanaa za muziki, maigizo, ngoma za asili, uandishi, uchoraji n.k, lakini vijana hao wamekuwa wakikumbana na changamoto ya kudhulumiwa hususani katika mikataba wanayoingia kwa ajili ya kusambaza kazi zao. Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha inaipatia COSOTA rasilimali watu na fedha (bajeti ya COSOTA iliyoidhinishwa na Bunge) kwa lengo la kuiwezesha kutekeleza shughuli zake, lakini pia huhakikisha wanawafikia na kuwasimamia wasanii wengi zaidi;

**Mheshimiwa Spika,** COSOTA iongeze kasi ya kujitangaza kwa lengo la kuwaweka wasanii wetu katika nafasi ya kufahamu kiundani kazi na faida za kuwa mwanachama wa COSOTA. Hatua hiyo itaongeza wanachama na kuongeza pato la chama, lakini pia itawasaidia wasanii nchini kupata wasimamizi wa haki zao na watetezi pindi wanapoingia katika migogoro.

**Mheshimiwa Spika,** Kampuni za muziki za nje ya nchi zimekuwa zikiwalaghai wasanii wetu na kuwaingiza katika mikataba ya kinyonyaji ambapo mwisho wa siku msanii anakuwa anafanya kazi isiyomnufaisha. Kamati inaishauri COSOTA kuongeza kasi ya kuwafikia wasanii wetu na kuhakikishwa wanashirikiana kwa kuwapa ushauri stahiki wakati wanapotaka kuingia mikataba na makampuni mbalimbali Duniani; na

**Mheshimiwa Spika,** Kumekuwa na malalamiko juu ya COSOTA kuchelewesha kutoa mirabaha na vilevile kutoa mirabaha kiasi kidogo jambo linalopelekea baadhi ya wasanii kutoona umuhimu wa kuwa wanachama. Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha inaisimamia COSOTA kuhakikisha kila mwanachama anapata stahiki yake tena kwa wakati muafaka.

g) **Kupokea na kujadili Taarifa ya Wizara ya Viwanda na Biashara kuhusu Utekelezaji wa Mpango wa Pili wa Maendeleo ya Taifa (2016/17 – 2020/21) kwa Sekta ya Viwanda na Biashara; Ukuaji wa Sekta ya Viwanda nchini na Mchango wake katika Pato la Taifa ikihusianishwa na Utekelezaji wa lengo namba 9 la Malengo ya Maendeleo endelevu.**

**Mheshimiwa Spika,** Mpango wa Pili wa Taifa wa Maendeleo (2016/17-2020/21) pamoja na Lengo Na. 9 la Malengo ya Maendeleo Endelevu kwa pamoja vimeweka kipaumbele cha kuongeza mchango wa Sekta ya Viwanda katika kuzalisha ajira kwa watanzania, kuongeza mchango katika pato la Taifa, kuongeza idadi ya makampuni yanayouza bidhaa nje ya nchi, kuahamasisha sekta binafsi kushiriki katika ujenzi wa viwanda na kuongeza fursa ya masoko;

**Mheshimiwa Spika,** katika kujipima mafanikio ya utekelezaji wa azma ya ujenzi wa Tanzania ya Viwanda, Kamati inaishauri Serikali kuvitambua Viwanda vikubwa na vidogo vyote vilivyoanzishwa tangu Mpango huu uanze utekelezaji pamoja na mchango wake katika uchumi tangu kuanzishwa mpaka sasa;

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inaishauri Serikali kuangalia tena tafsiri yake ya Dhana ya Viwanda na kisha kulingana na tafsiri hiyo ifanye jitihada ya kuvitambua viwanda vyote nchini pamoja na mchango wake na changamoto zake kwa lengo la kutafuta hatua zinazoweza kuchukuliwa kusaidia ukuaji wa Viwanda hivyo ili kuongeza ukuaji wa uchumi nchini;

**Mheshimiwa Spika,** Mpango unaelekeza Sekta ya Viwanda kuongeza mchango katika kuzalisha ajira kwa watanzania kutoka asilimia 8 mwaka 2015 hadi asilimia 12.5 mwaka 2020. Katika kutekeleza hili Kamati inasisitiza Serikali kuzingatia maslahi ya wafanyakazi na maslahi hayo yatazamwe katika pande mbili ambayo ni kipato cha mfanyakazi na mazingira ya kufanyia kazi;

**Mheshimiwa Spika,** Mpango wa kuongeza fursa za masoko hususani yenye upendeleo wa ushuru wa forodha katika jumuiya za Kikanda pamoja na dhamira ya kuongezeka idadi ya Makampuni yanayouza bidhaa nchi za nje kutoka 247 mwaka 2015 hadi 729 mwaka 2020. Kamati inaishauri Serikali kufanya mapitio ya sheria zinazosimamia sekta ya biashara kwa lengo la kuweka ushindani wa sawa kati ya viwanda vyetu vya ndani na bidhaa zinazotoka nje ya nchi ili kuweza kulinda viwanda vyetu; na

**Mheshimiwa Spika,** Viwanda vingi vilivyobinafsishwa au vilivyo na wabia kutoka nchi nyingine havifanyi kazi kwa ufanisi na vingine vimefungwa. Mfano wa Kiwanda cha MWATEC Tabora na URAFIKI Dar es Salaam. Kamati inaishauri Serikali kufuatilia kwa ukaribu uendeshwaji wa viwanda vyote vya aina hiyo na kutafuta njia ya kuvirudisha katika ufanisi wake uliosimikwa na ikibidi tutafute wawekezaji wengine katika viwanda hivyo.

h) **Kupokea na kujadili Taarifa ya Wizara ya Viwanda na Biashara kuhusu Utekelezaji wa Mpango kuboresha Karakana za SIDO nchini kwa lengo la kuziwezesha kuwahudumia wahitaji wengi zaidi kwa ufanisi uliokusudiwa; na Kutembelea SIDO – Dodoma.**

**Mheshimiwa Spika,** Shirika la kuhudumia Viwanda Vidogo SIDO imeanzishwa kwa lengo la kusimamia uanzishwaji na ukuaji wa Viwanda vidogo vinavyozingatia kuongeza thamani ya rasilimali zilizoko nchini; kuendeleza na kutumia teknolojia rahisi inayopatikana nchini; kutoa kipaumbele miradi ya uzalishaji inayotumia zaidi nguvukazi; kutoa huduma kwa viwanda vidogo nchini; na kuwezesha utekelezaji wa bidhaa za kutosheleza mahitaji ya wananchi hasa vijijini na ziada kuuzwa nje ya nchi. Majukumu haya yanatekelezwa kwa kuzingatia Sheria iliyoanzisha Shirika ambayo ni Sheria ya Bunge Na. 28 ya Mwaka 1973;

**Mheshimiwa Spika,** katika kutekeleza jikumu la kuendeleza na kutumia teknolojia rahisi inayoweza kutumika katika viwanda vidogo SIDO ilianzisha vituo vya kuendeleza teknolojia (Technological Development Centre). Vituo hivi vinatoa huduma ya kufanya marekebisho ya mitambo na mashine inayopatikana SIDO; kubuni, kutengeneza na kuuza mashine, vipuri na vifaa mbalimbali kwa wana viwanda nchini. Kwa sasa tuna jumla ya vituo saba (7) ambavyo vinapatikana katika Mikoa ya Iringa, Mbeya, Lindi, Kigoma, Arusha, Kilimanjaro na Shinyanga.

**Mheshimiwa Spika,** Vituo vya kuendeleza Teknolojia SIDO ni vya muda mrefu (vilijengwa miaka ya 1980) na vimechaakaa jambo linalopelekea hata ufanisi wake kuwa mdogo na kushindwa kutimiza malengo yaliyokusudiwa. Kwa kuwa vituo hivyo vipo saba tu nchini na vyote vina mahitaji makubwa ya kifedha kwa ajili ya ukarabati. Kamati inaishauri Wizara katika kila mwaka wa fedha iweke lengo la kuvikarabati walau kituo kimoja ili kiweze kufanya kazi kwa ufanisi uliokusudiwa.

**Mheshimiwa Spika,** Wajasiriamali wengi hawana elimu juu ya uwepo wa vituo vya mafunzo vya SIDO na faida zake, vituo hivyo vinauwezo wa kuhudumia wajasiriamali wachache sana kwa wakati mmoja. Kwa mfano kituo cha SIDO Dodoma kina uwezo wa kuhudumia wanafunzi 70 tu kwa muhula mmoja, kuna umuhimu wa kupanuliwa kwa kituo hicho, kwa kufanya hivyo kitawezesha kupunguza changamoto ya ajira kwa mkoa wa Dodoma na mikoa ya karibu. Kamati inaishauri Serikali kuviwezesha vituo hivyo kwa kuviongezea majengo, vifaa vitakayoweza kuhudumia wanafunzi wengi zaidi na kuwajengea uwezo wa kujitangaza;

**Mheshimiwa Spika,** Wajasiriamali wanaopata mafunzo kupitia SIDO, kipindi wanapomaliza mafunzo wanahitaji mitaji ya kwenda kuanza uzalishaji na kuingia sokoni. SIDO ilikuwa na mpango mzuri wa kuwakopesha kupitia mfuko wa kuwahudumia wajasiriamali (NEDF) lakini mfuko huo unakabiliwa na changamoto ya ufinyu wa mtaji, wakati maombi ya mikopo ni mengi na upatikanaji wa fedha kutoka Hazina hauridhishi. Kamati inaishauri Serikali kupitia BOT kuwadhamini SIDO kwa mabenki ili waweze kukopesha fedha zitakazotunisha mfuko wa NEDF na kuuwezesha kuhudumia wajasiriamali wengi zaidi;

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inatambua kuna Kodi ya Kuendeleza Ufundi Stadi ambayo inalipwa na waajiri wote kwa lengo la kuendeleza Ufundi Stadi nchini. Kamati inaishauri Serikali walau kiasi cha asilimia kumi (10) kielekezwe katika uendelezaji wa teknolojia katika taasisi zetu za teknolojia. Jambo hilo litatoa moyo kwa walipaji wa tozo hiyo kwa kuona fedha wanazotoa zinaenda kuendeleza taasisi ambazo zitaenda kusaidia sekta mbalimbali ikiwemo Sekta ya Viwanda pia;

**Mheshimiwa Spika,** kwa sasa Nchi ina vituo saba tu vya kuendeleza teknolojia chini ya SIDO, kutokana na umuhimu wa vituo hivyo Kamati inaishauri Serikali kuiwezesha SIDO kuanzisha vituo hivyo katika maeneo mengi zaidi nchini kwa lengo la kuhudumia watu wengi zaidi.

i) **Kupokea na kujadili Taarifa ya Wizara ya Viwanda na Biashara kuhusu Utendaji wa Shirika la Utafiti wa Maendeleo ya Viwandani Tanzania (TIRDO).**

**Mheshimiwa Spika,** Shirika la Utafiti wa Maendeleo ya Viwandani Tanzania (TIRDO) liliundwa kwa mujibu wa Sheria ya Bunge Na. 5 ya mwaka 1979 kwa lengo la kufanya utafiti na kutoa huduma za kitaalamu ili kuendeleza viwanda nchini. Shirika limepewa jukumu la kufanya tafiti zitakazosaidia katika kutathimini na kuibua teknolojia pamoja na malighafi inayopatikana hapa nchini kwa ajili ya kutumika katika uzalishaji viwandani hatimaye kuendeleza ukuaji wa viwanda nchini;

**Mheshimiwa Spika,** Shirika linatekeleza majukumu mbalimbali ikiwa ni pamoja na kufanya tafiti ya teknolojia zinazotoka ndani na nje ya nchi kwa ajili ya matumizi ya viwandani; kuendeleza na kutoa mafunzo yenye kuwawezesha kufanya utafiti wa kisayansi na kiteknolojia unaoendeleza viwanda; kusimamia na kusambaza matokeo ya tafiti zinazofanywa na Shirika; kuanzisha mfumo wa kutunza taarifa za kitaalamu na kusambaza matokeo ya utafiti wa aina yeyote unaofanywa hapa nchini;

**Mheshimiwa Spika,** majukumu mengine ya Shirika ni kutoa ushauri wa kitaalamu kwa Serikali na mashirika yanayohusika na uzalishaji viwandani kwa lengo la kuendeleza viwanda na matumizi ya teknolojia mpya; na kuishauri Serikali na viwanda kuanzisha mfumo wa kudhibiti shughuli za viwandani kuepuka/kupunguza uchafuzi wa mazingira wakati wa uzalishaji kwa kutumia teknolojia zinasofaa;

**Mheshimiwa Spika,** Kamati iliarifiwa kuwa katika mwaka wa fedha 2018/2019 Shirika lilifanikiwa kutekeleza mambo mbalimbali ikiwepo Usimamizi wa uanzishaji wa ujenzi wa viwanda mfano kiwanda cha Bidhaa za Ngozi Moshi, kiwanda cha bidhaa za Pamba za Hospitali Simiyu, kiwanda cha mafuta ya Mawese Kigoma. Shirika lilifanya ukaguzi wa kitaalamu katika viwanda vya Tanganyika Packers Shinyanga na Mbeya, kiwanda cha mafuta Ilulu, viwanda vya Korosho na vinginevyo. Pia Shirika lilitoa huduma za kitaalamu viwandani kama vile ukaguzi wa mazingira ya viwanda, ukaguzi wa matumizi bora ya nishati na huduma nyinginezo. Vilevile Shirika lilifanya tafiti mbalimbali ikiwepo mfumo wa usindikaji wa zao la muhogo, urejeshaji wa taka ngumu za ngozi, teknolojia ya briketi za makaa ya mawe, kuongeza thamani katika mabaki ya mbegu za mafuta kwa ajili ya kupata protini iliyobaki kwa lengo la kutumika kama chakula cha binadamu na mifugo.

**Mheshimiwa Spika,** Pamoja na majukumu haya muhimu bado shirika linakabiliana na changamoto ambazo zinazoathiri utekelezaji wa majukumu yake, miongoni mwa chanagamoto hizo ni pamoja na ufinyu wa bajeti ya Shirika; uchelewaji wa fedha toka hazina hususani fedha za miradi ya maendeleo; deni la kodi ya ardhi ambalo ni kubwa na linaendelea kukua kila mwaka kutokana na hali duni ya fedha ya Shirika; huduma TIRDO huzitambulika Kimataifa (*Accredited Facility/laboratory*) jambo linalosababisha Viwanda vinavyomilikiwa na makampuni ya Kimataifa kukataa kufanyiwa kazi na TIRDO hivyo kuikosesha baadhi ya kazi; Upungufu wa wafanyakazi na wanaendelea kupungua kutokana na udogo wa mishahara; uchakavu wa majengo na vitendea kazi; uvamizi wa sehemu ya viwanja vya Shirika jambo linalopelekea kuwa na kesi mahakamani na shirika halina uwezo wa kuendesha kesi hizo;

**Mheshimiwa Spika,** TIRDO inakabiliwa na deni kubwa la Kodi ya Ardhi, lakini pia upatikanaji wa fedha za maendeleo kwa taasisi hii bado ni mdogo jambo linalopelekea kushindwa kulipa deni hilo. Kamati inaishauri Serikali kuangalia namna ya kulifuta deni hilo ukizingatia TIRDO ni taasisi ya kutoa huduma na pia ni Serikali. Hivyo TIRDO kulipa deni hilo ni sawa na kutoa fedha Serikalini na kuilipa tena Serikali kitu ambacho hakileti tija;

**Mheshimiwa Spika,** TIRDO ni taasisi muhimu sana katika Ujenzi wa Tanzania ambapo pindi itakapowezeshwa kutekeleza majukumu yake kikamilifu hususani jukumu la kufanya ukaguzi na kuwaelimisha wenye viwanda juu ya ubora wa bidhaa. Jambo litakalo rahisisha kazi ya TBS na itapunguza malalamiko yaliyopo sasa juu ya TBS kuhusu utoaji wa Vyeti vya Ubora. Kamati inaishauri Serikali kuiwezesha taasisi hii kwa kuwapatia rasilimali watu na fedha ili iweze kutekeleza majukumu yake ipasavyo;

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaendelea kuishauri Serikali kuzipatia mitaji taasisi zake ili ziweze kujiendeleza zenyewe na kuacha utegemezi wa ruzuku kutoka Serikalini. Jambo hilo linaweza kufanyika katika kila mwaka wa fedha kwa kutenga mtaji wa taasisi chache; na

**Mheshimiwa Spika,** katika kutatua changamoto ya uhaba wa wataalamu wa ndani wanaoweza kuhudumia viwanda vyetu na ambao wanaujuzi na teknolojia zilizopo sokoni. Kamati inaishauri Wizara ya Viwanda na Biashara kushirikiana na Wizara ya Elimu kuandaa mitaala itakayofundishwa katika vyuo vikuu mbalimbali nchini pamoja na vyuo vya ufundi kama vile VETA kwa lengo la kuwaandaa wazawa kuhudumia sekta ya Viwanda kwa ufanisi.

j) **Kupokea na kujadili Taarifa ya Wizara ya Viwanda na Biashara kuhusu Namna Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA) inavyosimamia Mfumo wa Hakimiliki Bunifu (Intellectual Property);**

**Mheshimiwa Spika,** Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA) ilianzishwa kwa mujibu wa Sheria ya Wakala wa Serikali Na. 30 ya Mwaka 1997 kwa lengo la kuweka mazingira rafiki ya kutoa huduma bora za usajili wa Makampuni, Majina ya Biashara, alama za biashara na huduma; kutoa Leseni za Viwanda na Biashara; pamoja na kulinda vumbuzi mbalimbali nchini;

**Mheshimiwa Spika,** Miliki ubunifu (Intellectual Property) ni mali itokanayo kutumia akili kuunda au kutengeneza vitu mbalimbali kama fasihi, kazi za sanaa, michoro na alama kwenye bidhaa na huduma, wakati Mfumo wa Miliki Ubunifu inahusu uwezo wa ubunifu wa binadamu na mfumo wa kisheria wa ulinzi wa bunifu hizo. Miliki ubunifu imegawanyika katika sehemu mbili ambazo ni uzalishaji mali kwenye Viwanda (Industrial Property) na haki miliki (Copyrights) ambazo inahusu kazi za fasihi;

**Mheshimiwa Spika,** Mfumo wa miliki Bunifu una faida mbalimbali ikiwepo kulinda ajira za wabunifu na kuwa na uhakika wa bunifu zao kuwa hazitaibiwa; kutambulika kwa bidhaa inapoingia sokoni hivyo kuleta matumizi sahihi ya alama za biashara na huduma (hakuna uchakachuaji); kutoa nafasi kwa taasisi za utafiti kunufaika na tafiti zao kwa kuuza kwa wazalishaji wafanyabiashara; na kuleta chachu ya kuzalishwa kwa teknolojia mbalimbali nchini kwa kuwa wabunifu wanajua watalindwa na sheria na hatimaye kunufaika na bunifu zao;

**Mheshimiwa Spika,** Sheria zote zinazotumika katika usimamizi wa Miliki Ubunifu ni za muda mrefu jambo linalotoa wasiwasi kama zinaendana na mazingira ya sasa ya biashara. Kamati inaishauri Wizara kuhakikisha sheria hizo zinaboreshwa ili ziweze kuendana na mazingira ya sasa ya kufanyia biashara;

**Mheshimiwa Spika,** Mpango wa Serikali kuweka nembo (branding) Mazao yetu ya kipekee yanayoingia katika soko la Dunia itasaidia nchi kujitangaza. Kamati inaipongeza Serikali kwa mpango huo na inashauri utekelezwe haraka iwezekanavyo kama ilivyofanyika kwa korosho ya Tanzania (TanKorosho);

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaishauri Serikali kupitia taasisi zake kuelimisha wazalishaji wa ndani umuhimu wa viwango na ubora wa bidhaa zao, sambamba na hilo elimu itolewe juu ya umuhimu wa kupenda bidhaa zetu za ndani. Hatua hiyo itasaidia kuwafanya wazalishaji wa ndani kuanza kubrand bidhaa zao kuwa zinatoka Tanzania. Hali ya sasa ni kuwa wazalishaji wengi wanaogopa kusema bidhaa zao zinatoka Tanzania kutokana na imani iliyojengeka kwa jamii zetu kuwa bidhaa za Tanzania hazina ubora kama zile zinazotoka nje. Mafanikio ya haya yatapelekea kuitangaza Tanzania; na

**Mheshimiwa Spika,** Elimu kuhusu Miliki Ubunifu bado haijawafikia watu wengi hususani wajasiriamali, jambo linalowapelekea kuzalisha bidhaa zao na kuziingiza sokoni bila kuzibrandi,

ambapo hupelekea watu wengine kuziiba na kuzibrandi majina yao na kunufaika zaidi kwa kuzifanya ni za kwao. Kamati inaishauri BRELA kuongeza kasi ya kutoa elimu juu ya umuhimu na faida ya kuwa na cheti cha Miliki ubunifu kwa lengo la kulinda haki za wajasiriamali wetu.

k) **Kupokea na kujadili Taarifa ya Wizara ya Viwanda na Biashara Mpango wa Serikali kuhamasisha Uwekezaji katika maeneo ya EPZ na SEZ;**

**Mheshimiwa Spika,** Mamlaka ya EPZ inatekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Sheria ya Bunge (EPZ.Act, 2006) pamoja na marekebisho yake ya mwaka 2008 na 2012. Mamlaka hii imepewa majukumu mahsusi ya kuandaa mipango ya kuhamasisha kikanda na kimataifa ubunifu au uanzishaji, uendelezaji na uendeshaji wa maeneo ya uzalishaji wa viwanda kwa ajili ya mauzo ya nje ya nchi (*Export Processing Zone - EPZ*) na maeneo maalumu ya kiuchumi (*Special Economic Zone - SEZ*);

**Mheshimiwa Spika,** Uhamasishaji wa uwekezaji unaongozwa na hatua kuu tatu ambazo ni Utwaaji wa Maeneo ya SEZ ambapo Mamlaka ya EPZ hutwaa na kumiliki maeneo hayo kwa niaba ya Serikali, maeneo hayo hutwaliwa kwa kuzingatia vigezo mbalimbali ikiwepo vile vya kimkakati, kiuchumi, kijamii na kiusalama; hatua ya pili ni Uendelezaji wa Maeneo ya SEZs ambapo baada ya kutwaa maeneo Mamlaka ya EPZ huendeleza maeneo hayo ili kuandaa mazingira rafiki ya uwekezaji. Katika hatua hii Mamlaka pia huweka uhakika wa upatikanaji wa wafanyakazi wenye ujuzi na stadi mbalimbali, upatikanaji wa umeme wa uhakika, upatikajai wa Miundombinu wezeshi na kuweka mifumo ya uwekezaji na uendelezaji wa maeneo hayo; na hatua ya tatu ni usimamizi wa Maeneo ya SEZs ambapo licha ya kuwa na aina tofauti za uendelezaji wa maeneo hayo lakini bado Mamlaka ya EPZ husimamia maeneo hayo ili kuhakikisha rasilimali za maeneo hayo zinatumika kwa manufaa ya Taifa;

**Mheshimiwa Spika,** Kamati iliarifiwa kuwa katika kuhamasisha uwekezaji katika maeneo ya SEZs Mamlaka ya EPZ inatekeleza hatua mbalimbali ikiwepo kuhamasisha ushiriki wa sekta binafsi katika uendelezaji wa miundombinu wezeshi ukizingatia kuwa ufinyu wa bajeti ya mamlaka katika kuendeleza maeneo hayo; kutenga maeneo ya gharama nafuu za fidia ili kupunguza gharama za kulipa fidia za maeneo; kuhamasisha ushiriki wa Serikali za Mikoa katika kuendeleza maeneo ya SEZs; na kutekeleza mpango maalumu wa kujenga uwezo wa vijana katika stadi za kufanya kazi viwandani kwa kushirikiana na wawekezaji;

**Mheshimiwa Spika,** katika kutekeleza majukumu yake Mamlaka ya EPZ inakabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwepo upungufu wa wataalamu wa fani muhimu jambo linalokwamisha ushiriki mamlaka katika utekelezaji wa miradi kipaumbele na kimkakati katika maeneo maalumu ya uwekezaji lakini licha ya kuwa yeye ndio msimamizi mkuu wa utekelezaji wa miradi katika maeneo hayo; Ushirikiano hafifu kati ya Mamlaka ya EPZ na Taasisi/idara nyingine za Serikali katika kutekeleza baadhi ya shughuli mbalimbali za mamlaka; ukosefu wa wafanyakazi wenye taaluma ya viwandani; na ukosefu wa rasilimali fedha ukilinganisha na majukumu ya Mamlaka;

**Mheshimiwa Spika,** Mamlaka ya EPZ inatwaa maeneo mengi karibu nchi nzima na rasilimali za kuyaendeleza maeneo hayo ni chache. Kamati inaishauri Serikali kuamua kuchagua maeneo machache ya kimkakati na kuyaandaa kimiundombini. Pia iandae mkakati wa kuyaendeleza maeneo hayo kwa awamu kulingana na ufinyu wa bajeti inayopatikana;

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaishauri Serikali kuwa makini wakati wa kulipa fidia za maeneo waliyoyatwaa kwa ajili ya Uwekezaji, vilevile kuangalia kiasi cha fidia kinacholipwa katika eneo husika kiendane na ukubwa au manufaa ya Mradi utakaowekwa. Mfano kwa sasa Kurasini Logistic Centre ilifidiwa Bilioni 191 ikiwa inatizamiwa kuwekwa Business Park, lakini mradi

unaoenda kutekelezwa pale ni kuweka maghala ya chai ambapo mradi huu hautaweza rudisha fedha zilizotumika kutoa fidia;

**Mheshimiwa Spika,** katika kuhamasisha Uwekezaji kwenye maeneo ya EPZ na SEZ ni vema tukazingatia maeneo yale ambayo yamekwishalipiwa fidia, kama uwekezaji utafanyika katika maeneo hayo tutaanza kunufaika na hatimaye kurudisha gharama ya fidia iliyolipwa.

l) **Kupokea na kujadili Taarifa ya Wizara ya Viwanda na Biashara kuhusu namna Bodi ya Usimamizi wa Stakabadhi za Ghala (WRRB) wanavyoshirikiana na Soko la Bidhaa kuhakikisha mazao yanayozalisha Nchini yanapata soko.**

**Mheshimiwa Spika,** Bodi ya Usimamizi wa Stakabadhi za Ghala (WRRB) ni taasisi ya Serikali inayosimamia aina ya biashara ambapo bidhaa zinahifadhiwa ndani ya ghala lenye leseni na mmiliki wa bidhaa anapewa stakabadhi inayoonyesha umiliki mahsusi, thamani, aina, idadi na ubora wa bidhaa iliyowekwa ghalani. Jambo hili hutekelezwa kwa mujibu wa Sheria ya Stakabadhi Ghala Na.10 ya mwaka 2005 kwa lengo la kurasimisha mifumo ya masoko kwa lengo la kutafuta mazao ya kilimo, lakini pia kupunguza vipingamizi mbalimbali vinavyokinzana na uzalishaji wenye tija;

**Mheshimiwa Spika,** Jukumu kubwa la WRRB kutoa leseni kwa waendesha ghala, kutoa leseni kwa wakaguzi wa ghala na kuendesha mfumo wa kisasa na makini wa Stakabadhi ghaha. Vile vile WRRB inawajibika kukusanya, kuchambua na kutoa taarifa za mfumo wa Stakabadhi ghala kwa wadau, kushirikiana na vyombo vingine vya kitaifa na kimataifa vinavyofanya kazi kama za Bodi na kuishauri na kuiwakilisha Serikali kwenye mikutano au makongamano yanayojadili mfumo wa Stakabadhi ghala;

**Mheshimiwa Spika,** manufaa ya mfumo huu ni pamoja na kupata taarifa za soko na mauzo za kuaminika kwa wadau; wamiliki wa stakabadhi ghala kutumia stakabadhi zao kupata mikopo kutoka katika taasisi za fedha; kuongeza ushiriki wa wafanyabishara wa bidhaa za mazao katika biashara za kimataifa.

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na manufaa ya mfumo bado kuna changamoto mbalimbali zinazokwamisha utekelezaji wa majukumu ya WRRB ambazo ni pamoja na maghala mengi yaliyopo yanamilikiwa na watu binafsi hivyo huendesha shughuli hii kwa kuzingatia maslahi yao kwanza; uelewa mdogo wa jamii juu ya Mfumo wa Stakabadhi Ghala hali inayopelekea kuwakosesha fursa na faida za kuingiza mazao yao katika mfumo; na kubwa zaidi ni upungufu wa rasilimali fedha, watu na vitendea kazi jambo linalopelekea bodi kushindwa kufika kwenye maeneo mengi na kushindwa kuhudumia mazao mengi;

**Mheshimiwa Spika,** Mfumo wa Stakabadhi za Ghala unaruhusu wanunuzi wa nje kushiriki katika minada ya mauzo ya mazao, jambo linaloleta ushindani mkubwa na kuwaumiza wanunuzi wa ndani kushindwa kushindana. Kamati inaishauri Serikali kuangalia namna ya kuwasaidia wanunuzi wa ndani hususani wenye viwanda kwa kuwapatia upendeleo kununua mazao kabla ya Mfumo kufunguliwa kuuzwa kimataifa;

**Mheshimiwa Spika,** Katika kutekeleza mifumo hii Kamati inaishauri Serikali kupitia Wizara ya Fedha, TMX, Wizara ya Viwanda na Biashara (WRRB) na Wizara ya Kilimo kutoa elimu ya mfumo wa Stakabadhi Ghala na uwepo wa Soko la Bidhaa ili kuwahamasisha wakulima wetu kushirikiana katika mfumo huo. Hatua hiyo iende sambamba na kuwapa uhakika wa masoko na bei nzuri itakayowavutia wakulima wengi kuingia shambani na kuzalisha kwa wingi ambayo inaendana sambamba na malengo ya ASDP II;

**Mheshimiwa Spika,** Serikali iangalie namna ya kuandaa mfumo kama wa Stakabadhi Ghala ambao utaelekezwa kuhudumia mazao yenye changamoto ya kuharibika ndani ya muda mfupi kama zao la Muhogo na Miwa, wakulima wa mazao hayo wamekuwa wakilanguliwa na wanunuzi kwa kununua kwa bei nafuu; na

**Mheshimiwa Spika,** Uhamasishaji wa matumizi ya mfumo wa Stakabadhi Ghala uende sambamba na ujenzi wa maghala, kwani maghala yaliyopo sasa ni machache na yapo katika maeneo ambayo WRRB inayashughulikia kwa sasa.

j) **Kupokea na kujadili Taarifa ya Wizara ya Viwanda na Biashara kuhusu Utekelezaji wa Mpango wa kuboresha mfumo wa udhibiti wa biashara nchini (Blueprint for regulatory reforms to improve the business environment for Tanzania); na Maoni ya Wadau wa Sekta ya Viwanda na Biashara kuhusu Hali ya Biashara na Mazingira ya kufanyia Biashara nchini baada ya Serikali kuanza Utekelezaji wa Mpango huo.**

**Mheshimiwa Spika,** Mpango wa kuboresha mfumo wa udhibiti wa biashara nchini (Blueprint for regulatory reforms to improve the business environment for Tanzania) ni andiko maalumu lililoandaliwa kwa lengo la kuweka misingi endelevu ya kuboresha mazingira ya kufanyia biashara nchini. Andiko hili limefafanua changamoto mbalimbali zilizokuwa zikilalamikiwa kukwamisha biashara nchini pamoja na mapendekezo ya ufumbuzi wake;

**Mheshimiwa Spika,** utekelezaji wa Blueprint umekwisha anza na baadhi ya kazi zilizotekelezwa ni pamoja na kufanikisha utoaji wa Leseni za Biashara kwa Mfumo wa Kieletroniki hivyo kuokoa muda; Kufutwa kwa tozo zipatazo 54 kwenye mamlaka za udhibiti kwa mwaka 2019/2020; Kuhamisha Jukumu la Kusimamia Chakula kutoka TMDA kwenda TBS; Kuainisha maeneo ya utekelezaji kwa kila Wizara; na Maandalizi ya Sheria ya Uwezeshaji wa Biashara;

**Mheshimiwa Spika,** wakati Bunge linapitisha bajeti ya Serikali ya Mwaka wa Fedha 2019/2020, Serikali iliwaaminisha wafanyabiashara, wawekezaji na wananchi kwa ujumla kuwa inaanza kutekeleza kwa nguvu zaidi mpangokazi wa kuboresha mazingira ya biashara (Blueprint for the Regulatory Reforms to improve the Business Environment) ili mazingira ya biashara nchini yawe rafiki zaidi na yenye gharama nafuu. Tija ya utekelezaji wa mpango huo bado haijaonekana, kuna changamoto ambazo Kamati pamoja na wadau wanaona bado hazitapata ufumbuzi, changamoto hizo ni pamoja na:

**Mheshimiwa Spika,** Ugumu wa kutekeleza mfumo wa ukusanyaji kodi kwa njia ya kielekroniki (Electronic Tax Stamp – ETS), wafanyabiashara wanalalamikia gharama kubwa iliyoambatana na mfumo wa ETS kuwa zinaongeza gharama kwenye uzalishaji wa bidhaa na kupelekea kuongezeka gharama za uendeshaji wa Viwanda. Gharama inayotozwa kwa kutumia ETS ni kubwa ukilinganisha na teknolijia yenyewe na kazi inayofanya. Kamati inasisitiza Serikali kuliangalia namna ya kupunguza gharama hizo ili kuvipunguzia viwanda vyetu gharama na kuziweka bidhaa zetu za ndani katika nafasi ya kushindana katika Soko;

**Mheshimiwa Spika,** Halmashauri zetu kutambulisha tozo mpya mara kwa mara na tozo hizo zimekuwa zinaibuliwa bila kuwashirikisha au kuwapa taarifa wadau jambo ambalo limekuwa likilalamikiwa kuwa zinaongeza gharama za uzalishaji. Kamati inaitaka Serikali kupitia Mpango wa mfumo wa udhibiti wa biashara waweke vizuri suala la kodi zinazotozwa kwa wafanyabiashara (tax harmonization) ili kuweza kuboresha mazingira ya kufanyia biashara na kuepukana na kodi zinazoibuliwa ambazo hazipo kisheria;

**Mheshimiwa Spika,** rejesho la fedha za ongezeko la thamani ya bidhaa (VAT 18) na rejesho la 15% kwa Sukari ya viwandani (15% return of industrial sugar) hazirudi kwa Wafanyabiashara kama inavyotakiwa jambo ambalo ni kinyume na Sheria. Kutokurudi kwa fedha za VAT na 15 %

Sukari ya Viwandani ni changamoto ya muda mrefu takribani miaka 5 sasa jambo ambalo linapelekea kupungua kwa mitaji ya wenye viwanda na pia kuongeza gharama za uzalishaji ambapo mwisho wa siku inapelekea viwanda husika kupunguza wafanyakazi ili kufidia gharama za uzalishaji. Kamati inaishauri Serikali kutazama upya namna wanavyoendesha mfumo VAT. Kwa upande wa Sukari ya Viwandani, Kamati inatambua nia njema ya kuanzisha mfumo huu ambayo ilikuwa ni kuhakiki na kudhibiti wafanyabishara wasio waaminifu jambo ambalo kwa sasa linafanyika kupitia ETS, Kamati inashauri Serikali kuachana na suala la mfumo huu;

**Mheshimiwa Spika,** katika kutekeleza Azma ya Ujenzi wa Tanzania ya Viwanda, Serikali yetu imehamasisha uwekezaji na wawekezaji wameitikia wito wa Serikali na kwa wingi wameanzisha viwanda na kwa ambavyo vilikuwepo vimepanua uwekezaji na kuongeza uzalishaji. Changamoto katika utekelezaji wa suala hili lipo upande wa Soko ambapo bidhaa za ndani zinashindwa kushindana katika soko kutokana na uingizaji wa bidhaa za namna hiyo ambazo huuzwa bei rahisi hivyo kuua soko la bidhaa za ndani. Kamati inaishauri Serikali kutoza kodi bidhaa zinazoingia kutoka nje kwa uwiano ambao hata ikiingia nchini itaenda kuuzwa kwa bei sawa na zile zinazozalishwa nchini;

**Mheshimiwa Spika,** Malalamiko juu ya wingi wa mamlaka za udhibiti tena hazifanyi kazi kwa pamoja, mfano kuna baadhi ya kaguzi zinazofanywa na OSHA hufanywa tena na FIRE na wote hufanya kwa nyakati tofauti na kutoza tozo tofauti. Kamati inaendelea kuishauri Serikali kuunganisha au kuweka Makubaliano ya kushirikiana na pindi mmoja anapofanya ukaguzi mwingine awe tayari kutumia taarifa/ripoti ya mwenzake bila kurudi na kukagua tena;

**Mheshimiwa Spika,** Katika hatua ya kulinda soko la ndani la bidhaa zinazozalishwa nchini, Serikali iliongeza kodi ya bidhaa toka nje ya nchi ambalo ni jambo jema sana, lakini athari ya tozo hiyo imeenda hadi bidhaa ambazo hazipatikani nchini. Hivyo kuleta ugumu wa uagizaji wa bidhaa hizo na zikipatikana nchini zinakuwa na gharama kubwa. Kwa lengo la kutatua hilo, Kamati inaishauri Serikali kufanya uchambuzi wake na kubainisha bidhaa ambazo hazizalishwi nchini na kuzitolea vikwazo ili ziweze kuagizwa kwa urahisi;

**Mheshimiwa Spika,** Katika uhamasishaji wa Ujenzi wa Tanzania ya Viwanda tumefanikiwa kuweka mazingira ambayo yamewavutia wawekezaji kutoka nje na wengine wamekuja na teknolojia mpya kabisa ambalo ni jambo jema. Changamoto katika hili inakuja katika kupata vibali vya ajira au kuhuwisha (renew) vibali vya ajira ambapo kumekuwa na mlolongo na malamamiko yasiyo ya lazima ambayo yanapelekea kukatisha tamaa wawekezaji nchini. Kamati inaishauri Serikali kutia mkazo katika kusimamia suala la vibali vya ajira ili kuendelea kuvutia uwekezaji mpya na teknolojia mpya kuja kuwekeza nchini;

**Mheshimiwa Spika,** madini yatumikayo kama malighafi ya viwandani Mfano madini ya kuzalisha gypsum, saruji, chokaa, hutozwa mrabaha kama ilivyo kwa madini ya vito jambo hili linapelekea kuongeza gharama ya uzalishaji kwa kuwa mwisho wa siku bidhaa itakayozalishwa italipiwa tena kodi. Kamati inaishauri serikali kuliangalia namna ya kuondoa kodi hii katika madini hayo. n.k;

**Mheshimiwa Spika,** kutokana na changamoto hizo ambazo ni baadhi tu, inadhihirisha kuwa bado hatujafanikiwa sana kuboresha mazingira ya kufanyia biashara nchini. Kamati inaishauri Serikali kukamilisha mchakato wa kuandaa Sheria ya Uwezeshaji Biashara ambayo ndio inatazamiwa kwenda sambamba na Blueprint na kutoa nafasi ya mabadiliko pindi changamoto zinapojitokeza.

k) **Kupokea na kujadili Taarifa ya Wizara ya Viwanda na Biashara kuhusu namna Wizara ya Viwanda na Biashara kupitia Taasisi ya FCC na FTC zinavyoingia katika minada ya Mazao na kuhakikisha kunakuwa na ushindani wa haki baina ya wanunuzi na pia kuhakikisha wakulima wetu wanauza mazao yao kwa bei stahiki**

**Mheshimiwa Spika,** Tume ya Ushindani, ni chombo kilichoundwa chini ya kifungu cha 62 cha Sheria ya Ushindani, 2003, kwa madhumuni ya kuhamasisha na kulinda ushindani katika masoko, kulinda walaji dhidi ya mienendo isiyo haki na ya kupotosha katika masoko.

**Mheshimiwa Spika,** Baraza la Ushindani (FCT) limeanzishwa kwa mujibu wa Sheria ya Ushindani Namba 8 ya Mwaka 2003 (Fair Competition Act, No. 8/2003) na kupewa jukumu la kusikiliza na kuamua kesi za rufaa zinazotokana na maamuzi ya Tume ya Ushindani (Fair Competition Commission – FCC) pamoja na Mamlaka ya EWURA, TCAA, LATRA, na TCRA. Baraza la Ushindani ina hadhi ya kimahakama ambapo hushughulikia malalamiko yanayotokana na maamuzi yaliyotolewa na Tume ya Ushindani;

**Mheshimiwa Spika,** mazao ya biashara yanaratibiwa na bodi za mazao husika lakini pamoja na uwepo wa Bodi hizo, masuala ya kiushindani yanayojitokeza katika masoko hayo yanapaswa kushughulikiwa na Tume ya Ushindani. Jambo hili linatokana na ukweli kwamba kutokana na muundo wa masoko ya mazao ulivyo ushindani stahimilivu unakosekana kutokana na nguvu ya masoko kushikiliwa na wanunuzi hivyo kusababisha kutokuwa na ulinganifu sahihi wa bei anayostahili kupata mkulima;

**Mheshimiwa Spika,** Sheria ya Ushindani Na.8, 2003, kifungu cha 8, 9, 10,11 na 12 inampa mamlaka Tume ya Ushindani (FCC) kuingilia moja kwa moja katika minada au masoko na kuhakikisha kama kuna ushindani wa haki katika soko na pindi unapotokea ukiukwaji wa Sheria ya ushindani Tume huingilia kati na kutoa maamuzi ya kuleta usawa. Aidha, inapotokea washiriki wa soko kutokuridhika na maamuzi ya Tume, Sheria ya Ushindani inaelekeza kukata rufaa dhidi ya maamuzi husika katika Baraza la Ushindani (FCT) ili haki iweze kuonekana kutendeka. Kwa muktadha huu Tume na Baraza ya Ushindani kwa pamoja vinajukumu kubwa la kuhakikisha wakulima wetu wananufaika katika minada ya mazao;

**Mheshimiwa Spika,** Sheria inayotumika na Tume ya Ushindani pamoja na Baraza la Ushindani ya mwaka 2003 imepitwa na wakati na haiendeni na uhalisia wa mazingira ya sasa. Kamati inaishauri Serikali kuleta Sheria mpya Bungeni ambayo itaendana na hali halisi ya sasa ya Biashara ili kuboresha soko la bidhaa zetu ikiwa ni pamoja na mazao na kuchochea ukuaji wa uchumi kwa ujumla;

**Mheshimiwa Spika,** utekelezaji wa sheria ya Ushindani inayotumika sasa umeambatana na faini nyingi na viwango vya faini hizi havina uhalisia jambo linalozalisha kesi nyingi na migogoro baina ya Tume na wafanyabiashara walio wengi hususani katika masoko ya bidhaa (mfano mgogoro katika soko la Tumbaku na mgogoro huu unaenda kusababisha madhara katika viwanda vinavyotumia malighafi hii ambapo itaathiri ajira pia). Kamati inaishauri Serikali kurejea sheria hii na kuiweka katika uhalisia wa hali ya sasa. Vile vile, kwa kesi zilizopo Serikali kupitia FCC ikubali kukaa chini na wafanyabiashara ambao wana kesi nao na kujaribu kutafuta njia nyingine ikiwemo ya usuluhishi ili kufikia muafaka wa kesi hizo kwa manufaa ya pande zote mbili;

**Mheshimiwa Spika,** Maendeleo ya Viwanda yanategemea sana upatikanaji wa malighafi, kwa muktadha huo kuna haja ya kufungamanisha sekta ya Viwanda na Kilimo. Kwa kutambua hilo kuna haja ya kuweka jitihada za makusudi kuhakikisha wakulima wetu wanazalisha mazao ya kutosha lakini wakiwa na uhakika wa kuuza kwa bei ya ushindani. Kamati inaishauri Serikali kupitia FCC kuhakikisha wanashiriki na wakulima wetu katika hatua za awali kuhakikisha

wanafanya tafiti za minada husika na kuweka rekodi za biashara ili kuhakikisha wakati wa minada mauzo yaende kihaki bila kuwa na walanguzi wanaotaka kumiliki soko;

**Mheshimiwa Spika,** kama tunavyofahamu kupitia Bodi ya Stakabadhi Ghala (WRRB) tunaingia katika biashara huria ambapo mtu yeyote anaweza kushiriki katika minada ya manunuzi. Kamati inaishauri Serikali kujitahadhari na hili na kuziwezesha FCC na FCT kuhakikisha kunakuwa na ushindani wa haki katika minada yote kwani Makampuni makubwa yamekuwa yakifanya jitihada za kuua makampuni madogo kwa lengo la kutaka kutawala soko (monopoly)

l) **Kupokea na kujadili Wizara ya Viwanda na Biashara kuhusu namna Nchi inavyonufaika kwa kuwa washirika wa Mikataba mbalimbali ya kikanda na Kimataifa inayohusiana na Sekta ya Viwanda na Biashara**

**Mheshimiwa Spika,** nchi mbalimbali duniani zimekuwa zikishirikiana na Taasisi mbalimbali za Kimataifa, Kikanda na pia kuingia katika mikataba ya mashirikiano na nchi nyingine kwa malengo ya Kiuchumi, Kisiasa, Kiusalama na Kiutamaduni. Kwa kiwango kikubwa Jumuiya za Kiuchumi ndizo ambazo zimekuwa zikitumiwa na nchi mbambali duniani katika kuunganisha nchi husika kibiashara na kiuchumi..

**Mheshimiwa Spika**, huko duniani kuna Jumuiya mbalimbali za kiuchumi ambazo ni pamoja na EAC, SADC, ECOWAS, EU n.k. Pia kuna Taasisi kadhaa za kimataifa ambazo zilianzishwa kwa malengo mahsusi ambazo ni pamoja na Shirika la Biashara la Dunia (WTO), Shirika la Umoja wa Mataifa la Maendeleo ya Viwanda Duniani (UNIDO), Shirika la Umoja wa Mataifa la Biashara na Maendeleo UNCTAD n.k

**Mheshimiwa Spika,** ili kurahisisha mashirikiano na makubaliano baina ya nchi wanachama, nchi zimekuwa zikiingia katika mikataba katika maeneo mbalimbali kama vile ya Uchumi, Biashara, Uwekezaji, Kilimo n.k.

**Mheshimiwa Spika,** Tanzania kama zilivyo nchi nyingine duniani, imeingia katika mikataba kadhaa ya kimataifa, kikanda na baina ya nchi nyingine rafiki kwa maslahi mbalimbali kama vile ya kiuchumi, kibiashara, kiuwekezaji, kiusalama n.k. Mikataba ambayo Tanzania ni pamoja na Mkataba wa Kimataifa wa Mkataba wa kuanzisha Shirika la Biashara la Dunia – (*WTO),* Shirika la Umoja wa Mataifa la Biashara na Maendeleo – (*UNCTAD*); Mikataba ya Kikanda ambayo ni EAC na SADC; Mikataba ya baina ya nchi nan chi katika Tanzania na China, Tanzania na India na Tanzania na Marekani (AGOA);

**Mheshimiwa Spika,** Tanzania ni mwanachama wa jumuiya nyingi za kimataifa ambazo zinakuwa na mikataba ya kukuza sekta ya viwanda na Biashara duniani, lakini utekelezaji wa masharti mikataba husika umeonekana kulegalega jambo ambalo linatukosesha fursa zinazoambatana na mikataba hiyo. Kamati inaishauri Serikali kuandaa mazingira rafiki ya kutekeleza mikataba hiyo kabla ya kuisaini na kuiridhia. Hatua ya kujiandaa itatuweka katika nafasi ya kunufaika lakini pia kutuepusha na kuwanufaisha washirika kwa kubaki kuwa sehemu ya soko za bidhaa zao; na

**Mheshimiwa Spika,** Wananchi wengi hawajui kuhusu mikataba ya Kimatifa ambayo nchi ni wanachama wa mikataba hiyo. Vilevile, ufahamu kuhusu faida zinazopatikana kwenye mikataba hiyo kwa nchi na wanachi wake hususani kwa wafanyabishara na wawekezaji wa ndani ya nchi kwa maana ya wazawa. Kamati inaishauri Serikali kupitia njia mbalimbali za kutoa elimu, ijitahidi kutoa elimu ya kutosha kuhusu mikataba mbalimbali ya kibiashara inayosainiwa

na nchi ambayo inamanufaa kwa wafanyabishara na wawekezaji nchini ili kukuza sekta hizo na kufikia Uchumi wa Viwanda.

m) **Kupokea na kujadili Taarifa ya Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara hiyo kwa kipindi cha Julai – Disemba, 2019**

**Mheshimiwa Spika,** katika kipindi cha mwaka wa fedha 2019/2020 Wizara ya Viwanda na Biashara kwa Mafungu yote Mawili (Fungu **44** na **60**) iliidhinishiwa jumla ya Shilingi **100,384,738,648.00** kwa ajili ya kutekeleza majukumu yake. Kati ya fedha hizo Shilingi **48,884,738,648.00** zilitengwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida na Shilingi **51,500,000,000.00** kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Aidha, Wizara ilipanga kukusanya maduhuli ya jumla ya shilingi **6,300,000.00.**

Hadi kufikia mwezi Disemba, 2019 Wizara ilikuwa imepokea shilingi **21,716,759,173.00** kwa mafungu yote mawili, kiasi hiki kilikuwa ni fedha kwa ajili ya matumizi ya kwawaida ya Wizara pamoja na taasisi zake, kiasi hiki ni sawa na asilimia **44.42** ya kiasi kilichoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya matumizi ya kawaida.

**Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa makusanyo hadi kufikia Disemba, 2019 Wizara haijapata makusanyo yotote ya ndani jambo ambalo si sawa. Kwa mahesabu ya kawaida Wizara ilipaswa kuwa imekusanya aslimia 50 ya lengo iliyokuwa imejipangia. Kamati inaishauri Serikali kuangalia changamoto zilizokwamisha kufikia lengo ililokusudia na kuzitatua, hili liende sambamba na kuangalia kama ilijipangia makusanyo yanayoendana na uwezo wake halisi wa kukusanya.

**Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa fedha kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo, hadi kufikia tarehe 31 Desemba 2019, Wizara haikupokea fedha yoyote kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inendelea kuishauri Serikali kupeleka kiasi kilichoidhinishwa na Bunge kwa lengo la kuziwezesha wizara zetu kutekeleza majukumu yake.

## 2.5 KUPOKEA NA KUJADILI TAARIFA YA OFISI YA MAKAMU WA RAIS-MAZINGIRA NA TAASISI ZILIZO CHINI YAKE

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ya Viwanda, Biashara na Mazingira inasimamia na kushauri kuhusu utekelezaji wa Majukumu ya Ofisi ya Makamu wa Rais-Mazingira kuhusu masuala ya Usimamizi wa Mazingira. Katika kipindi cha Machi, 2019 hadi Januari, 2020 ilipokea taarifa mbalimbali za utekelezaji wa majukumu ya ofisi hii. Taarifa hizo ni kama ifuatavyo:

**a) Kupokea na kujadili Taarifa ya Ofisi ya Makamu wa Rais-Mazingira kuhusu Ofisi ya Makamu wa Rais- Mazingira kuhusu Utekelezaji wa Maazimio ya Bunge yanayohusiana na majukumu ya Wizara hii, yaliyotokana na Mapendekezo ya Kamati ya Viwanda, Biashara na Mazingira katika Taarifa yake ya Mwaka iliyowasilishwa katika Mkutano wa Bunge wa Mwezi Februari, 2019**

**Mheshimiwa Spika,** mnamo Mwezi Februari, 2019 Kamati ya Viwanda kama ilivyo kwa Kamati nyingine za Bunge iliwasilisha Bungeni ya Taarifa ya Mwaka ya Shughuli ilizotekeleza kwa kipindi cha kuanzia Machi, 2018 hadi Januari, 2019, jambo hili lilitekelezwa kwa kuzingatia matakwa ya Kanuni ya 117 (15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016. Taarifa ya hii ilitoa mapendekezo ambayo yalijadiliwa na hatimaye kupitishwa kuwa Maazimio ya Bunge.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati pia ilifuatilia utekelezaji wa Maazimio matatu (3) ya Bunge yalielekezwa kwa Ofisi ya Makamu wa kwa lengo la kuiwezesha kupata mrejesho wa maazimio yaliyotolewa na kufahamu hatua mbalimbali za utekelezaji wake na kubaini maazimio (maeneo) ambayo hayakutekelezwa kwa lengo la kuendelea kufuatilia utekelezaji wake;

**Mheshimiwa Spika,** Utekelezaji wa Azimio namba la tatu (3) la Bunge kuhusu Mfuko wa Dhamana ya Mazingira umeanza kuonyesha sura ya utekelezaji ambapo kuna baadhi ya hatua zimeanza kuonekana. Kamati inaishauri Serikali kukamilisha mchakato huo kwa lengo la kuuwezesha mfuko huu kuanza kutekeleza majukumu yake yaliyokusudiwa;

**Mheshimiwa Spika,** Sheria ya Mazingira ya Mwaka 2004 inazielekeza Halmashauri zote nchini kutenga fedha kwa ajili ya kutekeleza majukumu ya usimamizi wa Mazingira lakini fedha hizo zimekuwa hazitengwi. Kamati inaendelea kuisisitiiza Ofisi ya Makamu wa Rais- Mazingira kushirikiana na Wizara ya Tamisemi kutafuta ufumbuzi wa suala hili.

**b) Kupokea na kujadili Taarifa ya Ofisi ya Makamu wa Rais-Mazingira kuhusu Tathimini ya Athari ya Mazingira - TMA (Environmental Impact Assessment - EIA);**

**Mheshimiwa Spika,** Tathimini ya Athari ya Mazingira - TMA (Environmental Impact Assessment - EIA) ni tathimini inayofanywa kwa lengo la kuhakikisha maamuzi ya kutekeleza na utekelezaji wa mradi au shughuli fulani haina athari katika mazingira. EIA hufanyika kwa lengo la kuweka mifumo bora ya kulinda mazingira ikiwa ni pamoja na kupunguza kiwango cha taka zitakazozalishwa, kutoa kipaumbele kwa jamii kutokana na mradi unaoanzishwa, kuainisha athari zilizopo na madhara yanayoweza kujitiokeza kutokana na mradi unaoenda kutekelezwa, kutoa maamuzi sahihi kuhusu utekelezaji wa mradi, kulinda afya ya jamii na kuhakikisha usalama wa wafanyakazi;

**Mheshimiwa Spika,** thathimini ya Athari za Mazingira ni hatua muhimu sana inayotakiwa kufuatwa kabla ya mradi wowote kuanza utekelezaji wake lakini kumekuwa na malalamiko mengi ya wawekezaji kuwa EIA inawachelewesha kwa kuwa huchukua muda mrefu. Kamati inaishauri kuangalia na kutatua changamoto zinazoikwamisha NEMC kutekeleza jukumu hili kwa haraka ikiwepo kuwaongezea watumishi wataalamu ukaguzi;

**Mheshimiwa Spika,** Sheria ya Mazingira ya Mwaka 2004 inatoa wajibu kwa kila sekta kuandaa muongozo wake wa tathimini ya athari kwa Mazingira kutokana na mahitaji juu ya Sekta husika lakini jambo hili halitekelezwa na kupelekea kuleta uzito katika kutekeleza tathimini hizi. Kamati inaishauri Serikali kuzisimamia na kuziwezesha Sekta zote kuandaa miongozo hii, hatua hii itarahisisha utekelezaji wa masuala yanayohusu thathimini za athari za mazingira na kuliwezesha Baraza kutekeleza jukumu hili kwa urahisi na uharaka;

**Mheshimiwa Spika,** changamoto ya mapungufu na muingiliano wa baadhi ya Sheria, mfano mgongano wa Sheria ya Mazingira na Sheria ya Madini katika kusimamia shughuli na vibali vya uchimbaji. Kamati inaendelea kuisisitiza Serikali kufanya mapitio ya Sheria zote ambazo kwa namna moja ama nyingine inaleta ugumu katika kutekeleza Sheria ya Mazingira kwa lengo la kuyalinda mazingira yetu. Tufanye juhudi za makusudi katika kujiepusha na athari zinazoweza kujitokeza kutokana na uharibifu wa mazingira ili tuweza kuepuka madhara yanayoweza kujitokeza '**Usipoziba ufa Utajenga Ukuta**';

**Mheshimiwa Spika,** changamoto ya uelewa mdogo wa jamii juu ya masuala ya uhifadhi wa Mazingira na Sheria ya Mazingira ya Mwaka 2004 pamoja na Kanuni zake hatujafanikiwa kuitatua. Kamati inaishauri Serikali kuandaa mkakati madhubuti wa kuelimisha jamii juu ya umuhimu wa kuyahifadhi mazingira;

**Mheshimiwa Spika,** Sheria ya Mazingira ya Mwaka 2004 imeelekeza Halmashauri zote nchini kuajiri maafisa mazingira na maafisa hawa walilengwa kuongeza nguvu katika kusimamia masuala ya Mazingira. Changamoto ni kuwa maafisa hawa hawana mawasiliano ya moja kwa

moja na Wizara inayosimamia Mazingira, maafisa hawa wanaripoti kwa Wizara ya Tamisemi na hii ni kutokana na maelekeza ya Sheria yenye lakini pia maafisa hawa hawana taaluma ya mazingira. Kamati inaishauri Serikali kuhamishia maafisa mazingira au kuwataka waripoti moja kwa moja katika Wizara inayosimamia masuala ya Mazingira. Sambamba na hili ajira za maafisa mazingira zizingatie taaluma ya mazingira;

a) **Kupokea na kujadili Taarifa ya Ofisi ya Makamu wa Rais-Mazingira kuhusu Utekelezaji wa agizo la kupiga marufuku matumizi ya Mifuko ya Plastiki; Mwitikio wa jamii kuhusu katazo la kutumia Mifuko ya Plastiki; na Mipango ya Serikali katika kuhakikisha upatikanaji wa mifuko mbadala ambayo ni imara na kwa bei nafuu;**

**Mheshimiwa Spika,** matumizi ya mifuko ya plastiki yameambatana na changamoto mbalimbali za kiafya na katika mazingira. Changamoto hizo ni pamoja na kusababisha kiziba kwa mitaro ya maji ya mvua na miundombinu ya majisafi na majitaka na hatimaye kusababisha mafuriko na kuenea kwa magonjwa ikiwemo malaria na kipindupindu; kusababisha vifo vya mifugo, wanyama na viumbe wa baharini pindi wanapokula na kumeza mifuko hiyo; mifuko ya plastiki haiozi katika mazingira kwa haraka na inakadiriwa kudumu hadi miaka 500 na hivyo kuleta athari za muda mrefu kwa kuathiri mpenyezo wa maji na hewa katika ardhi;

**Mheshimiwa Spika,** kwa kutambua changamoto tajwa hapo juu, Serikali iliamua kuweka katazo la matumizi ya mifuko hiyo ambapo mnao tarehe 09 Aprili, 2019 Serikali ilitoa tamko la kupiga marufuku Uingizaji, uzalishaji, usambaziji nje ya nchi na matumizi ya mifuko ya plastiki. Katazo hili limeanza kutekelezwa rasmi tarehe 1 Juni, 2019;

**Mheshimiwa Spika,** katika kutekeleza agizo hili Serikali iliandaa kanuni za kupiga marufuku mifuko ya plastiki za mwaka 2019 lakini pia ilihamasisha na kutoa elimu kwa umma kuhusu katazo hili. Jambo la kupongeza ni kuwa jamii iliitikia wito wa Serikali na kuacha matumizi ya mifuko hiyo, pia Wafanyabiashara walibaini fursa na kuamua kuwekeza katika biashara ya mifuko mbadala. Hivyo basi, katazo hili limeambatana na faida mbili ambazo ni kuokoa mazingira yetu na athariza uchafuzi wa mifuko ya plastiki lakini pia fursa ya uwekezaji na ajira katika kutengeneza mifuko mbadala;

**Mheshimiwa Spika,** mifuko mbadala iliyopo sokoni na inayotumika kwa kiasi kikubwa haina ubora jambo linaloleta hasara kwa watumiaji ambapo imekuwa ikichanika na kumwaga bidhaa ziliyobebwa ndani. Kamati inaishauri Serikali kwa kushirikiana na Shirika la Viwango Tanzania (TBS) kuwasimamia wazalishaji wa mifuko hiyo kuhakikisha wanatumia viwango vilivyopangwa, pia kwa inayoingia kutoka nje ukaguzi ufanyike na kwa isiyokidhi viwango isiruhusiwe kuingia;

**Mheshimiwa Spika,** Bei za mifuko mbadala ni kubwa jambo linalowaumiza watumiaji. Kamati inaishauri Serikali kuwasimiamia watengenezaji kuhakikisha bei inayopangwa inakuwa na uhalisia kulingana na ukubwa na uimara wake;

**Mheshimiwa Spika,** Kanuni zetu zinazosimamia katazo la matumizi ya mifuko ya plastiki zinakataza uzalishaji na uuzaji wa nje ya nchi jambo ambalo Kamati imepata ukakasi kidogo kwa kuwa imeenda kuua viwanda vyote vilivyokuwa vinazalisha mifuko hiyo. Kamati inaona hakukuwa na haja ya kuviua viwanda hivyo, kama soko la nje lipo Serikali ingeangalia namna ya kuvisimamia na kuhakikisha bidhaa inayozalishwa haiuzwi ndani kabisa na kwa atakaekamatwa kukiuka sharti hilo kupewa adhabu kali;

**Mheshimiwa Spika,** Katazo la Mifuko ya plastiki limekuwa pigo kwa wananchi wa hali ya chini, kabla ya katazo wafanyabishara (hasa masokoni) walikuwa wanatoa mifuko bure lakini baada

ya katazo inawalazimu wateja kununua mifuko ambayo kwa kuanza bei sio rafiki lakini pia mifuko hii mingi haiwezi kutumika zaidi ya mara moja kama ilivyotarajiwa. Kamati inaishauri Serikali kuangalia namna ya kuwapatia wazalishaji vivutio au misamaha fulani ili wazalishe kwa gharama ndogo na hatimaye bei ipungue;

**Mheshimiwa Spika,** Serikali iongeze kasi ya kutoa elimu juu ya madhara ya mifuko ya plastiki kwa kuwa bado imeendelea kuingia kwa njia za panya na imeendelea kutumika kwa kuficho;

**Mheshimiwa Spika,** Wananchi waelimishwe tofauti ya vifungashio na vibebeo kwa kuwa sasa wafanyabisahara wasio waadilifu wameendelea kuwashawishi wateja wao kubeba bidhaa katika vifungashio ambapo ni kinyume na sheria.

b) **Kupokea na kujadili Taarifa ya Ofisi ya Makamu wa Rais - Mazingira kuhusu Utendaji wa Mfuko wa Mazingira;**

**Mheshimiwa Spika,** Mfuko wa Mazingira umeundwa kwa mujibu wa Kifungu cha 213 (1) cha Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya Mwaka 2004 na kupewa jukumu mahsusi la kuisaidia wizara yenye dhamana ya usimamia masuala ya mazingira kutafuta fedha kutoka maeneo mbalimbali ndani na nje ya nchi kwa ajili ya kutekeleza shughuli za usimamizi wa mazingira. Majukumu mengine ya mfuko ni pamoja na kujenga uwezo wa rasilimali watu na taasisi zinazojihususha na shughuli za uhifadhi wa mazingira; kutoa ruzuku kwa program mbalimbali za kijamii zinazohusu hifadhi za mazingira; kuwezesha kufanyika kwa tafiti zinazolenga kuboresha mahitaji ya hifadhi na utunzaji wa mazingira;

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na nia nzuri ya Serikali kuanzisha mfuko huu lakini ni takribani miaka …… sasa mfuko huu haujaanza kutekeleza majukumu yake ya kisheria na hii ni kutoka na changamoto mbalimbali ikiwepo athari za upungufu wa kisheria jambo linalopelekea kukwamisha utendaji wa mfuko kama kushindwa kusajiliwa na Msajili wa Hazina, Bodi kushindwa kutekeleza majukumu yake kwakuwa sheria haijabainisha majukumu/mamlaka yake; Sheria ya Mazingira kutoutambua Mfuko wa Mazingira kama Taasisi inayojitegemea jambo linalopelekea wadau/washiriki wa maendeleo na sekta binafsi kushindwa kuchangia katika mfuko hivyo kuukosesha mfuko mapato; Uhaba wa fedha za kuendesha shughuli za Mfuko;

**Mheshimiwa Spika,** Athari za uharibifu wa mazingira zikijumuisha na athari za mabadiliko ya Tabianchi zimeendelea kudhihirika kwa kasi sana. Kamati inaishauri Serikali kuchukua jitihada za makusudi na za haraka za kupambana na uharibifu huo. Jitihada hizo zianze kwa kutenga bajeti ya kutosha ya kushughulikia shughuli za uhifadhi na usimamizi wa mazingira nchini, na fedha zinazotengwa ifikishwe katika maeneo husika tena kwa wakati. Jitihada hizo ziende sambamba na kuuwezesha Mfuko wa Taifa wa Mazingira kuwanza kufanya kazi;

**Mheshimiwa Spika,** Mfuko wa Mazingira unaonekana kuwa ndio suluhisho la changamoto ya uhaba wa fedha za uhifadhi wa mazingira iliyopo sasa. Kamati inaishauri Serikali kuongeza kasi katika kukamilisha michakato mzima wa kuuwezesha mfuko huu kuanza kutekeleza majukumu yake ikiwa ni pamoja na kufanya marekebisho ya Sheria iliyounda mfuko na pia kutoa kibali cha kupata vyanzo vya mapata vya mfuko huu;

**Mheshimiwa Spika,** Vyanzo vya mapato ya mfuko vimekwisha ainishwa na Ofisi ya Makamu wa Rais – Mazingira na kuwasilishwa Serikalini, vyanzo vilivyowasilishwa ni vingi jambo linalopelekea mchakato wa kutafuta na kupata vibali kuwa mrefu. Kamati inaishauri Ofisi ya Makamu wa Rais-Mazingira kuchagua angalau vyanzo Kumi (10) tu na kuvitilia mkazo katika kutafuta kibali kisha kwa kila mwaka wa fedha iwe inatambulisha vyanzo vingine vipya, hatua hii itafupisha kidogo mchakato wa kupata kibali;

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaishauri Serikali kuwasilisha mabadiliko ya Sheria Mazingira kwa kifungu cha 14 na 15 kwa lengo la kuondoa muingiliano wa kimaslahi unaotokana na Sheria ya mazingira kumtambua Mkurugenzi wa Mazingira kuwa ndie Afisa masuuli wa mfuko wakati Mkurugenzi huyo ndio msauri wa Serikali kuhusu maendeleo ya mfuko. Mgongano huu ni moja ya vikwazo vya kuanza utekelezaji wa mfuko na mabadiliko ya sheria kwa vifungu tajwa yatatoa nguvu kwa mfuko na kuuwezesha kutekeleza majukumu yake na kuleta tija iliyokusudiwa.

c) **Kupokea na kujadili Taarifa ya Ofisi ya Makamu wa Rais-Mazingira kuhusu Ajenda ya Taifa ya Utafiti katika Mazingira (National Environmental Research Agenda – NERA);**

**Mheshimiwa Spika,** Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya Mwaka 2004 inalipa Baraza la Taifa la Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira jukumu la kutekeleza masuala ya utafiti kuhusu Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira nchini. Katika kutekeleza jukumu hili Baraza liliamua kuandaa Ajenda ya Taifa ya Utafiti katika Mazingira (National Environmental Research Agenda – NERA) ambapo ajenda hii inatoa muelekeo wa kitaifa wa kufanya tafiti za mazingira kwa wadau ili kuwawezesha kuandaa programu, miradi na shughuli za kitafiti kwa kuzingatia maeneo ya vipaumbele vya kitaifa katika utafiti wa Mazingira;

**Mheshimiwa Spika,** kwa sasa Baraza linatekeleza Ajenda ya Taifa ya tafiti za Mazingira ya Mwaka 2008 – 2012 ambayo ilifanyiwa mapitio na kuandaa toleo la pili la Mwaka 2017 – 2022. Toleo hili la pili limeanisha maeneo tisa ya vipaumbele ambayo ni Matumizi endelevu ya ardhi na utatuzi wa migogoro ya kugombea rasilimali za mazingira; uchimbaji madini, nishati na mazingira; hifadhi shirikishi ya rasilimali maji; uchumi mazingira; maendeleo ya bioteknolojia na mazingira; kudhibiti na kuhimili mabadiliko ya tabianchi; mifumo ikolojia ya majini na bioanuai; mifumoikolojia ya nchi kavu na bioanuai; na udhibiti wa uchafuzi wa mazingira na udhibiti taka;

**Mheshimiwa Spika,** Ajenda ya Taifa ya Utafiti katika Mazingira imeandaliwa na kuzingatia vipambele vya nchi katika kukabiliana na changamoto za masuala ya mazingira lakini utekelezaji wake unakabiliana na changamoto mbalimbali ikiwepo baadhi ya Sekta hazitoi kipaumbele kwa masuala ya mazingira hivyo ushiriki wake katika kusimamia mazingira ni hafifu; uwezo mdogo wa kifedha, miundombinu na rasilimali watu katika kutekeleza ajenda hii; na baadhi ya wadau kusita kushiriki kwenye tafiti za mazingira kwa hofu ya kudhihirika kwa matendo yao yasiyozingatia sheria;

**Mheshimiwa Spika,** matokeo ya tathimini/tafiti zinazofanywa chini ya NERA yanalenga kutoa ufumbuzi wa kudumu wa namna bora ya kukabiliana na changamoto za kimazingira hapa nchini. Kwa kuwa NERA imekwisha tambua athari za Mabadiliko ya tabianchi na kuyaweka katika maeneo ya kipaumbele, Kamati inaishauri Serikali kuliwezesha Baraza kufanya tathimini katika kipengele cha mabadiliko ya tabianchi na kuja na muongozo/muelekeo utakaotoa ufumbuzi wa namna nchi kukabiliana na changamoto hii;

**Mheshimiwa Spika,** Changamoto utoaji wa fedha za usimamizi wa mazingira zinapelekea hata umuhimu wa NERA usionekane, inatumika nguvu na rasilimali nyingi kufanya tafiti, matatizo yanabainiwa na vipaumbele vinaainishwa lakini fedha za kushughulikia changamoto zilizobainisha hazitolewi. Kamati inaishauri Serikali ili kupata tija ya kazi inayofanywa na NERA ni vema fedha zinazotengwa kwa ajili ya shuguli za usimamizi wa mazingira zikapelekwa tena kwa wakati.

d) **Kupokea na kujadili Taarifa ya Ofisi ya Makamu wa Rais-Mazingira kuhusu Mabadiliko ya Tabianchi;**

**Mheshimiwa Spika,** Tabianchi ni mwenendo wa hali ya hewa ikiwemo majira ya mwaka, wastani wa hali ya joto, utokeaji na mtawanyiko wa mawingu, mvua na theluji. Tabianchi ya kila eneo inafahamika mfano uhakika wa kuwa na mvua, joto au baridi kwa kipindi fulani cha mwaka kwa miaka iliyopita ilikuwa inafahamika vitapatikana kwa wakati upi wa mwaka;

**Mheshimiwa Spika,** kwa miaka ya hivi karibuni uhakika wa hali ya hewa haupo tena na jambo hili limesababishwa na Mabadiliko ya Tabianchi ambayo yamesababishwa na ongezeko la joto kwenye uso wa dunia, na kwa mujibu wa wanasayansi ongezeko hili limetoka na shughuli za maendeleo ya binadamu. Itifaki ya Kyoto imeripoti kuwa gesijoto zinazosababisha madhara zaidi ni zile zinazotokana na shughuli za viwandani, usafirishaji, kilimo, ufugaji, utupaji wa taka n.k;

**Mheshimiwa Spika,** tumeshuhudia athari za mabadiliko ya Tabianchi yakiendelea kudhihirika katika mazingira ambapo tumeshuhudia Ukame, Mafuriko, ongezeko la ujao wa kina cha Bahari, kuenea kwa magonjwa ya kuambukiza na kubadilika kwa mifumo ya ikolojia. Juhudi za makusudi zinatakiwa kuchukuliwa ili kudhibiti/kupunguza uzalishaji wa gesijoto na hatimaye kupunguza ongezeko la joto la uso wa dunia, juhudi hizi ziende sambamba na juhudi za kuhimili athari za mabadiliko ya tabianchi;

**Mheshimiwa Spika,** Kwa sasa shughuli za masuala ya usimamizi wa mazingira kwa kiasi kikubwa zinatekelezwa kwa kutumia fedha kutoka kwa wafadhili jambo ambazo si zuri kwani tumeshuhudia wafadhili hawa wakichagua miradi ya kufadhili na maeneo ya kutekeleza miradi hiyo hivyo kupelekea baadhi ya maeneo kutofikiwa. Kamati inaishauri Serikali kuonyesha umakini wake katika usimamizi wa mazingira kwa kutenga fedha za kutosha za kukabiliana na masuala yote ya utunzaji wa mazingira na fedha hizo zitolewe kwa wakati;

**Mheshimiwa Spika,** matunda ya utunzaji wa mazingira yana manufaa kwa Sekta mbalimbali, Kamati inaishauri Serikali kuwasimamia na kuhakikisha wanufaika wa matunda ya kuhifadhi mazingira kama sekta ya Misitu, Kilimo, maji, mifugo, uzalishaji wa umeme n.k wachangie katika juhudi za kuhifadhi mazingira.

e) **Kupokea na kujadili Taarifa ya Ofisi ya Makamu wa Rais-Mazingira kuhusu Taarifa ya Tatu ya Hali ya Mazingira nchini na Utekelezaji wa Mpango wa miaka mitano wa Maendeleo kwa Sekta ya Mazingira;**

**Mheshimiwa Spika,** Taarifa ya Hali ya Mazingira Nchini ni Taarifa inayoandaliwa kwa mujibu wa Kifungu Na. 175 (1) cha Sheria ya Mazingira ambacho kinamuelekeza Mkurugenzi wa Mazingira kuandaa na kuchapisha Taarifa ambayo itabainisha hali ya mazingira, changamoto za utekelezaji pamoja na mapendekezo ya hatua za kuchukuliwa ili kukabiliana na changamoto za uharibifu wa mazingira nchini na kuiwasilisha Bungeni;

**Mheshimiwa Spika,** Taarifa ya Tatu ya hali ya Mazingira ya Mwaka 2018 imebainisha chanagamoto kadhaa ambazo ni;-

- Asilimia 61 ya ardhi nchini ipo kwenye hatari uharibifu mkubwa unaohusisha uharibifu wa udongo na uwepo wa chumvi ardhini vinavyosababishwa na matumizi mabaya ya kemikali;
- Ukataji wa holela wa misitu unaosababishwa na shughuli za kibinadamu zisizo endelevu, takribani hekta 469,420 zinapotea kila mwaka, Tanzania imeripotiwa kuwa nchi ya tano Afrika inayoongoza kwa kukata misitu;

- Uharibifu wa mifumo ikolojia ambao unatokana na shughuli za binadamu, imeripotiwa kwa Tanzania tumepoteza asilimia 33 za mifumo ikolojia yake;

- Kuongezeka na kusambaa kwa viumbe vamizi, athari zake zimekwishaonekana katika Sekta ya kilimo kuharibu mazao mengi ikiwepo mahindi;

- Udhibiti mbovu wa taka ngumu na hivyo kusababisha kuzagaa kwa taka hizo;
- Utiririshaji wa majitaka ya viwandani umeendelea na kusababisha uchafuzi wa vyanzo vya maji; na

- Athari za mabadiliko ya Tabianchi.

**Mheshimiwa Spika,** uharibifu wa Mazingira nchini kwa kiasi kikubwa umechangia athari mbalimbali ikiwepo uharibifu wa bioanuai za misitu na viumbe wengine; kupungua kwa mazao kutokana na uharibifu wa ardhi unaoendelea; kuongezeka kwa migogoro ya ardhi inayohusisha jamii za wafugaji na wakulima; na kuongezeka kwa magonjwa kama vile kipindupindu na homa ya matumbo;

**Mheshimiwa Spika,** hali iliyoripotiwa katika taaarifa hii juu ya kasi ya ongezeko la uharibifu wa hali ya mazingira nchini inatia mashaka mfano tu ni uharibifu wa ardhi unaosababisha hali ya jangwa kuongezeka kutoka asilimia 42 mwaka 2014 mpaka asilimia 61 mwaka 2018. Kamati inaishauri Serikali kuchukua jitihada za makusudi kwa lengo la kunusuru hali hiyo. Juhudi hizo zianze kwa kutenga bajeti ya kutosha ya kushughulikia masuala ya mazingira;

**Mheshimiwa Spika,** elimu inayotolewa kuhusu utunzaji wa Mazingira haijafikia watu wengi hasa wananchi wanaoishi vijijini. Kamati inaishauri Serikali iongeze kasi ya kutoa elimu ya Mazingira hususani kwa maeneo ya Vijijini kwani huko ndipo kuna uharibifu mkubwa Mazingira sababu wananchi hao hawafahamu madhara uharibufu unaotokana na shughuli wanazozifanya. Vile vile mbinu na njia wanazozitumia kutoa elimu zizingatie aina ya shughuli za eneo husika (wafugaji, wavuvi, wakulima);

**Mheshimiwa Spika,** Hali ya ukataji miti nchini imeshamiri kwa kiasi kikubwa, hivyo kupelekea misitu iliyokuwepo kuzidi kupotea na wanaohusika kutoa vibali vya kukata miti wanaendelea kutoa vibali hivyo kwa kasi kuliko kasi ya upandaji wa miti. Kamati inaishauri Serikali kuangalia kwa ukaribu vibali vinavyotolewa kwa ajili ya ukataji miti, elimu kuhusu utengenezaji wa mkaa mbadala na gesi asilia itolewe ili kupunguza ukataji wa miti. Vile vile ufanyike uhamasishaji wa kupanda miti kwa kasi zaidi na ufuatiliaji wa utunzaji wa miti iliyopandwa ili upandaji wa miti uwe endelevu;

**Mheshimiwa Spika,** Utekelezaji wa kampeni za upandaji umelegalega na umekosa ufuatiliaji. Kamati inaishauri Serikali kabla ya kutekeleza kampeni yoyote ya upandaji miti ifanye utafiti na kubaini aina ya miti inastawi katika sehemu husika, kwani ustawi wa miti unategemea hali ya hewa ya eneo husika. Vile vile, Kamati inashauri kampeni hizi zitoe miti ya matunda kwani itawavutia sana wananchi kuitunza;

**Mheshimiwa Spika,** Vibali vya uvunaji misitu vinatolewa na TFS na tozo ya shughuli hiyo inaenda hukohuko TFS wakati marehebisho ya madhara yatokanayo na uvunaji inafanywa na Wizara yenye dhamana ya Mazingira ambao hawanufaiki na tozo za shughuli hiyo. Kamati inaishauri Serikali kuisimamia TFS na kuhakikisha zoezi la utoaji vibali linafanyika kwa kuishirikisha wizara ya Mazingira kwa lengo la kushauriana juu ya uvunaji endelevu. Vile vile, kamati inaishauri Serikali

tozo ya uvunaji misitu walau kwa asilimia chache iingie katika mfuko wenye dhamana ya mazingira ili iweze kufanya shughuli za utunzaji wa mazingira; na

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaishauri Serikali kuhamasisha wafanyabiashara wakubwa kwa wadogo kuwekeza katika uzalishaji wa mkaa mbadala ili kupunguza kasi ya ukataji wa miti kwa ajili ya kuzalisha mkaa. Vile vile, kupitia mikopo inayotolewa na Halmashauri kwa vijana, wanawake na watu wenye ulemavu, Kamati inaishauri Serikali kabla ya kuwakopesha iwapatie elimu juu ya uwepo wa fursa katika uzalishaji wa mkaa mbadala.

f) **Kupokea na kujadili Taarifa ya Ofisi ya Makamu wa Rais - Mazingira kuhusu Mwongozo wa Utekelezaji wa Sheria ya Mazingira ya Mwaka 2004 katika usimamizi wa maeneo yaliyopo ndani ya Mita 60 kutoka usawa wa vyanzo vya maji.**

**Mheshimiwa Spika,** kifungu Na. 57 (1) cha Sheria ya Mazingira ya Mwaka 2004 inaweka katazo juu ya shughuli za kibinadamu ambazo ni za kudumu katika maeneo ya vyanzo vya maji kama bahari, kingo za mito, mabwawa, miamba asilli ya ziwa ndani ya mita 60. Aidha, kifungu Na. 57 (2) cha Sheria hii kinatoa maelekezo kwa Waziri mwenye dhamana kuweka miongozo ya kuendesha shughuli za binadamu ndani ya maeneo.

**Mheshimiwa Spika,** kwa muktadha wa vifungu tajwa inadhihirisha kuna muongozo mzuri juu ya usimamizi ya maeneo haya lakini bado kumekuwa na changamoto ya uelewa mdogo wa jamii juu ya Sheria hii jambo linalopelekea ugumu katika utekelezaji wake na hatimaye kuzaa malalamiko kwa jamii kuwa kuna baadhi ya watu wanapendelewa kwa kupewa maeneo hayo. Kamati inaishauri Serikali kufanya uchambuzi wa Sheria hiyo na kuandaa vipeperushi ambavyo vipo katika lugha rahisi itakayoeleweka na jamii yote kwa ujumla;

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na kuwa na muongozo huo wa utoaji vibali vya kufanya shughuli katika maeneo ndani ya Mita 60, Kamati inaishauri Serikali kabla ya kutoa vibali hivyo ni vema kuyatembelea maeneo husika na kufanya utafiti kulingana na shughuli inayoenda kufanyika ili kubainisha kama kuna madhara yeyote ya kimazingira yanatoweza kujitokeza kutokana na shughuli hiyo;

**Mheshimiwa Spika,** Sheria ya Mita 60 ilianza kutekelezwa mwaka 2004 lakini kuna baadhi ya watu walikuwa wameshajenga/wekeza katika maeneo hayo kabla ya kipindi hicho. Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha muongozo unaandaliwa ambao utatoa jawabu (solution) endelevu juu ya utekelezaji wa Sheria hii bila kuathiri maslahi ya pande zote mbili yaani mazingira yetu na uwekezaji uliofanyika; na

**Mheshimiwa Spika,** Maeneo yanayotajwa kuwa ndani ya Mita 60 ni rasilimali ambazo zinaweza kutumika kwa ajili ya shughuli za utalii na kutuongezea mchango kiuchumi. Kamati inaishauri Serikali kuangalia uwezekano wa kuhamasisha uwekezaji wa shughuli za kiutalii katika maeneo hayo hususani maeneo ya fukwe za Bahari na Maziwa. Jambo hili liende sambamba na kuhakikisha shughuli hizo zinazingatia utunzaji wa Mazingira na matumizi endelevu ya maeneo hayo.

g) **Kupokea na kujadili Taarifa ya Ofisi ya Makamu wa Rais - Mazingira kuhusu namna Baraza la Taifa la Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) wanavyosimamia Sheria ya Mazingira katika maeneo ya Machinjio ya nyama kwa lengo la kukahakiksha Usafi na Usalama wa Bidhaa zinazotoka katika maeneo ya machinjio**

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa kifungu Na. 20 cha Sheria ya Usimamzi wa Mazingira ya Mwaka 2004 Baraza la Taifa la Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira (*NEMC*) linapewa jukumu la kuhakikisha kuwa mazingira yanatunza ili kuwa na matumivu endelevu ya rasilimali kwa ajili ya ustawi wa maisha bora ya Wananchi wa Tanzania. Katika kutekeleza hili Baraza hukagua maeneo ya machinjio pia kwa lengo la kuhakikisha usafi na usalama wa bidhaa zinazotoka katika maeneo ya machinjio;

**Mheshimiwa Spika,** hali za machinjio katika Halmashauri zetu si za kuridhisha, wamekuwa wakiendesha shughuli zao bila kuzingatia maelekezo ya kifungu Na. 115 (1 na 2) vya Sheria ya Mazingira ya Mwaka 2004 jambo ambalo linahatarisha usalama bidhaa inayotoka katika machinjio hayo lakini pia afya za walaji wa bidhaa hizo. Pia, katika ukaguzi wa machinjio hayo imebainika kuwa kuna usimamizi hafifu wa taka zitokanazo na shughuli za uchinjaji wa mifugo, utunzaji wa nyama na mazao yake kutokuwa katika maeneo safi na salama na mifumo ya maji machafu haifanyi kazi;

**Mheshimiwa Spika,** tathimini katika machinjio nchini imebaini changamoto mbalimbali ikiwepo machinjio nyingi hazina maeneo maalumu ya kusafishia nyama hususani nyama ya utumbo; hayana maji ya kutosha kwa kuzingatia idadi ya mifugo inayochinjwa hali inayotia mashaka kama nyama inayoandaliwa katika maeneo hayo inasafiswa ipasavyo; hazina maeneo ya kutunzia wanyama kabla ya kuchinjwa;

**Mheshimiwa Spika,** changamoto nyingine juu ya machinjio haya ni kuwa hayana mifumo ya majitaka hivyo kutiririsha ovyo maji hayo na kuchafua mazingira; kuna udhibiti hafifu wa taka ngumu hususani masalio ya wanyama ambayo hayahitajiki; uchakavu wa sakafu na makaro ya kuchinjia; utunzaji mbovu wa ngozi jambo linalopelekea kuoza na kutoa harufu mbaya; na hakuna taarifa na takwimu sahihi za kiasi cha mifugo inayochinjwa jambo linalokwamisha kutoa tathimini sahihi za maboresho ya machinjio hayo;

**Mheshimiwa Spika,** Tanzania kuna jumla ya machinjio 345 lakini kasi ya NEMC katika ukaguzi wa maeneo haya bado ni ndogo jambo linaloleta wasiwasi kidogo, Kamati ilipata fursa ya kutembelea Machinjio ya Mnadani – Msalato na hali iliyoikuta kule sio ya kuridhisha. Kamati inaishauri NEMC kuongeza kasi ya ukaguzi wa maeneo ya machinjio ili kuhakikisha yanafuata na kuzingatia sheria za mazingira ili kulinda Afya za walaji wa nyama nchini pamoja na wafanyakazi wa machinjio husika;

**Mheshimiwa Spika,** Baraza limekuwa likitoza faini kwa maeneo ambayo shughuli zao hazizingatii utunzaji wa mazingira kwa mujibu wa Sheria ya Mazingira. Faini hizi zimekuwa hazilipwi kwa wakati na muda mwingine hazilipwi kabisa na sababu inayotajwa ni ukubwa wa faini hizo. Kamati inalishauri Baraza kupitia upya faini hizo kwa lengo la kuziboresha kulingana na kosa husika; na

**Mheshimiwa Spika,** Serikali inatoa vibali kwa machinjio madogo au makaro ya kuchinjia (*slaughter slab*) lakini machinjio haya hayafanyiwi ukaguzi wa mara kwa mara jambo ambalo hutoa mianya kwa wamiliki kuchinja mifugo mingi zaidi ya uwezo wao na hivyo kupelekea kuathiri mazingira lakini pia usalama wa bidhaa zitokazo pale kuwa mdogo. Kamati inaishauri Serikali (NEMC na TMDA kwa kushirikiana na Serikali za Jiji au Miji) kuyatambua machinjio

madogo yote yanayopatikana katika Jiji au Miji husika kisha kuyafanyia ukaguzi wa mara kwa mara kuhakikisha wanatekeleza matakwa ya kibali chao na yanatunza mazingira.

h) **Kupokea na kujadili Taarifa ya Ofisi ya Makamu wa Rais - Mazingira kuhusu ufuatiliaji wa udhibiti wa uchafuzi wa Mazingira katika maeneo ya wachimbaji wadogo.**

**Mheshimiwa Spika,** Wachimbaji wadogo nchini wanajihusisha na uchimba madini kama Dhahabu, Almasi, vito vya aina mbalimbali ikiwemo Tanzanite, Ruby, Sapphire, Spinel, na Garnets, madini ya viwandani ikiwemo Jasi ("Gypsum"), Chokaa ("Limestone"), na Chumvi na madini ya ujenzi kama mawe, mchanga na kokoto. Inakadiriwa kuwa watanzania zaidi ya 1.5 Milioni wanajihusisha na shughuli za uchimbaji mdogo ambapo Leseni katika uchimbaji huu ni chini ya Dola za kimarekani 5 milioni.

**Mheshimiwa Spika,** shughuli za wachimbaji wa wadogo hufanyika katika eneo fulani kwa ya muda mfupi lakini inasababisha uharibifu mkubwa wa mazingira mkubwaambao hudumu kwa muda mrefu na kupelekea eneo lililowahi kufanyika shughuli hiyo kutoweza kutumiwa kwa shughuli nyingine za uzalishaji.

**Mheshimiwa Spika,** moja ya uharibifu mkubwa unaofanyika katika sehemu zinazoendesha shughuli za wachimbaji wadogo ni ukataji wa miti kwa lengo la kupata magogo ambayo hutumika katika kuzuia mashimo ya migodi yao. Kamati inaishauri Serikali kushirikiana na wachimbaji wadogo kupata teknolojia mbadala wa magogo ili kupunguza kasi ya ukataji miti. Sambamba na hilo wachimbaji wadogo wapewe eneo karibu na sehemu wanayoendesha shughuli zao la kupanda miti ili kufidia miti wanayokata na wafuatiliwe kuhakikisha wanaitunza miti hiyo;

**Mheshimiwa Spika,** Kemikali zinazotumiwa na wachimbaji wadogo wa madini zinaathari kubwa kwenye mazingira na afya za wachimbaji na wananchi wengine kwa ujumla wanaoishi karibu na maeneo hayo yenye shughuli za wachimbaji wadogo. Kamati inaishauri Serikali kudhibiti na kupunguza matumizi ya kemikali hizo hasa kemikali ya Zebaki kwani athari ya zebaki kwenye afya za binadamu na mazingira ni kubwa;

**Mheshimiwa Spika,** hakuna ushirikiano wa karibu kati ya Halmashauri, Wizara na taasisi za Serikali kwenye suala la utunzaji wa mazingira, hali hiyo inapekelea juhudi zinazoelekezwa kwenye kupunguza uharibifu wa mazingira kutofanikiwa katika kiwango stahiki. Kamati inaishauri Serikali waweke utaratibu utakaowezesha ushirikiano wa vyombo hivyo ili kuwe na usimamizi bora wa utunzaji wa mazingira wakati wananchi wakiendelea kutekeleza shughuli zao za kimaendeleo ikiwemo uchumbaji wa wadogo; na

**Mheshimiwa Spika,** Bunge lako tukufu liliridhia Mkataba wa Minamata kuhusu Zebaki (Minamata Convention on Mercury of 2013), Mkataba huu unalenga kupunguza matumizi ya kemikali ya Zebaki kwa lengo la kulinda afya ya binadamu na mazingira dhidi ya uchafuzi utokanao na Zebaki unaochangiwa na shughuli za binadamu. Zebaki inatumiwa na wachimbaji wadogo na wapo tayari kutumia mbadala wa zebaki pindi utakapopatikana. Kamati inaishauri Serikali kushirikiana na STAMICO kujitahidi kasi ya kutafuta teknolojia rahisi na rafiki kwa wachimbaji wadogo tena ya gharama nafuu, bila kupatikana kwa mbadala wa zebaki wachimbaji hawa wataendelea kuitumia na madhara yataendelea kuwepo; na

**Mheshimiwa Spika,** kuna muingiliano wa Sheria ya Mazingira na Sheria ya Madili katika kipengele cha usimamizi wa mazingira katika maeneo ya migodi, mfano Kifungu cha ufungaji mgodi ambayo kwa kiasi kikubwa kinahusiana na mazingira lakini ipo ndani ya Sheria ya Madini na utekelezaji wake hauonekani kupewa kipaumbele. Kamati inaishauri Serikali kufanya

mabadiliko ya kifungu hicho kwa lengo la kurekebisha na kuipa Sheria ya Mazingira nguvu ya kusimamia mazingira katika sekta ya madini.

i) **Utekelezaji wa Bajeti na Majukumu ya Ofisi ya Makamu wa Rais- Mazingira pamoja na Baraza la Taifa la Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira kwa kipindi cha Julai – Disemba, 2019.**

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa Fedha **2019/2020** Ofisi ya Makamu wa Rais-Mazingira pamoja na Baraza la Taifa la Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira waliidhinishiwa **22,708,713,882.00** kwa ajili ya kutekeleza majukumu yake. Kati ya fedha hizo Shilingi **18,218,915,442.00** ni kwa ajili ya matumizi ya miradi ya maendeleo na Shilingi **4,489,798,440.00** ni matumizi ya kawaida.

Hadi kufikia tarehe 31 Disemba, 2019 ambayo ni nusu ya Mwaka wa Fedha **2019/2020** ni shilingi shilingi **6,788,157766.14** ambapo shilingi **3,983,800,471.14** zilitolewa kwa ajili ya Mishahara na matumizi mengineyo na kiasi kilichobaki shilingi **2,804,357,295.00** ndio ilitolewa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

**Mheshimiwa Spika**, upatikanaji wa fedha za matumizi ya kwawaida ni wa kuridhisha lakini mwenendo wa upatikanaji wa fedha za Miradi ya Maendeleo si wa kuridhisha ambapo ni asilimia 15.4 tu ya fedha za miradi ya Maendeleo ndio zilikuwa zimepokelewa ambazo ni fedha za nje.

**Mheshimiwa Spika,** miradi ya usimamizi wa mazingira kwa kiasi kikubwa inatekelezwa na fedha za nje ambalo si jambo jema sana na athari tumekwisha anza iona ambapo kwa kipindi cha nusu mwaka ambapo kwa mahesabu ya kawaida asilimia 50 ya fedha za maendeleo ilipaswa kuwa imepokelewa na kutekeleza miradi husika lakini ni asilimia 15.4 tu ya fedha hizo ndio zilikuwa zimepokelewa. Kamati inaishauri Serikali kutenga fedha za ndani kwa ajili ya miradi ya usimamizi wa mazingira.

## 2.6 KUPOKEA, KUCHAMBUA, KUJADILI NA KUSHAURI JUU YA MIKATABA YA KIMATAIFA ILIYOPENDEKEZWA KURIDHIWA NA BUNGE AMBAYO IPO CHINI YA WIZARA INAZOSIMAMIWA NA KAMATI

**Mheshimiwa Spika,** kwa mujibu wa ya fasili ya 6(b), Kifungu cha 53 ikisomwa pamoja na fasili ya 1(b) ya Kifungu cha 7, cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, Kamati za Kudumu za Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira inatekeleza jukumu la kushughulikia Mikataba inayopendekezwa kuridhiwa na Bunge iliyopo chini ya Wizara ya Viwanda na Biashara pamoja na Ofisi ya Makamu wa Rais Mazingira;

**Mheshimiwa Spika,** naomba kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa katika kutekelezeza jukumu hilo Hoja ya Serikali kuhusu Bunge kuridhia mikataba mbalimbali iliwasilishwa kwenye Kamati na kuchambuliwa na hatimaye kuishauri Serikali juu ya namna bora ya utekelezaji wa mikataba hiyo lakini pia kulishawishi Bunge juu ya Mikataba husika. Mikataba iliyowasilishwa mbele ya Kamati na hatimaye kuwasilishwa na kuridhiwa na Bunge ni pamoja na;-

- Itifaki ya Marekebisho ya Kigali ya kupunguza uzalishaji na matumizi ya Kemikali Jamii ya Hydrofluocarbons (Hfcs) chini ya Itifaki ya Montreal inayohusu Kemikali zinazomong'onyoa Tabaka La Ozoni (Kigali Amendment on Phasing Down Hydrofluorocarbons (HFCS) to Monttreal Protocol on Ozone Depleting Substances);
- Itifaki ya Marekebisho ya Mkataba wa Marrakesh ulioanzisha Shirika la Biashara la Dunia (Protocol Amending the Marrakesh Agreement Establishing the World Trade Organization);

- Itifaki ya SADC kuhusu Usimamizi wa Mazingira na Maendeleo Endelevu (The Southern African Development Community Protocol On Environmental Management for Sustainable Development);

- Mkataba wa Marrakesh unaolenga kuwezesha upatikanaji wa kazi zilizochapishwa kwa watu wasioona, wenye uoni hafifu au ulemavu unaomfanya mtu kushindwa kusoma wa Mwaka 2013 (*The Marrekesh Treaty to Facilitate Access to Published Works for Persons who are Blind, Visually Impaired or Otherwise Print Disabled (MVT) 2013*);

- Mkataba wa Minamata kuhusu Zebaki wa Mwaka 2013 (Minamata Convention on Mercury of 2013); na

- Itifaki ya Ziada ya Nagoya – Kuala Lumpur kuhusu utaratibu wa uwajibikaji kisheria na fidia kwa madhara yanayoweza kutokea kutokana na matumizi ya Bioteknolojia ya kisasa katika kutekeleza itifaki ya Cartagena (Nagoya – Kuala Lumpur Supplementary Protocol on Lability and Redress to the Cartagena Protocol on Biosafety).

**Mheshimiwa Spika**, mikataba na itifaki hizi zikwisha wasilishwa na kuridiwa na Bunge lako Tukufu katika mkutano wa Bunge wa Kumi na Sita na Kumi na Saba. Kamati inaizisisitiza wizara husika kufanya jitihada za kuanza utekelezaji wa mikataba na itifaki husika ili tuanza kupata manufaa na faida zilizoambatana.

## 2.7 KAMATI KUSHIRIKI KATIKA WARSHA NA SEMINA

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilihudhuria Warsha, Semina na kukutana Wadau mbalimbali chini ya Sekta ya Viwanda, Biashara na Mazingira na yalilenga kuwajengea uwezo Wajumbe wa Kamati.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilijengewa uelewa kwa kupatiwa mafunzo na semina zilizosimamiwa na Mradi wa ***Legislative Support Program*** uliyo chini ya Ofisi ya Bunge. Wizara ya Viwanda na Biashara kupitia taasisi ya TBS, TIRDO, WMA, TANTRADE, BRELA na FCC. Ofisi ya Makamu wa Rais-Mazingira kupitia Baraza la taifa la Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC). Aidha, Kamati ilipata fursa kushiriki Warsa iliendesha na United Nation iliyohusu masuala ya Mazingira na Amani, Athari za Mabadiliko ya Tabianchi ikihusianishwa na Amani, warsha hii ilikuwa ni katika kuelekea siku ya Amani Dunia.

## 2.8 MAFANIKIO YA KAMATI KATIKA KIPINDI CHA MIAKA MINNE (4) YA KUANZIA JANUARI, 2016 – JANUARI, 2019

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ya Viwanda, Biashara na Mazingira imeendelea kutekeleza majukumu yake yaliyobainisha kwenye Kifungu 6(1) kikisomwa pamoja na Kifungu cha 7(1) vya nyingeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Binge Toleo la Januari, 2016. Katika kutekeleza majukumu yake kwa kipindi cha miaka minne (4) yani kuanzia januari, 2016 hadi Januari, 2020 ilishauri na kutoa mapendekezo mbalimbali.

**Mheshimiwa Spika,** maomba kuchukua nafasi hii kuipongeza na kuishukuru Serikali kwa kusikiliza na kuanza kutekeleza baadhi ya mapendekezo ya Kamati. Mapendekezo ya Kamati yaliyoanza kufanyiwa kazi ni;-

**Mheshimiwa Spika,** Kamati iliishauri Serikali kuweka utaratibu wa kukutana na wadau wa Sekta Binafsi ili kujadiliana na kushauriana namna ya kukuza Sekta za Viwanda, Biashara na Uwekezaji nchini.

Serikali imelifanyiakazi jambo hili na kuanza utaratibu wa kukutana na wadau mara nne kwa mwaka na kusikiliza changamoto zao, kuzifanyia kazi na baadae kuleta mrejesho kwa wadau kwa zilezilizofanyiawa kazi. Kwa upande wa Kamati jambo hili limetekezwa pia ambapo mara kadhaa tulikutana na wadau na wawekezaji wenye viwanda na kushauriana nao kuhusu namna bora ya uendeshaji wa sekta hii kwa lengo la kuboresha na hatimaye kuishauri Serikali;

**Mheshimiwa Spika**, Hali ya Biashara katika Bandari ya Dar es Salaam ilishuka katika mwaka wa fedha 2016/2017, Kamati ilifanikiwa kutembelea Bandari ya Dar es Salaamu na kusikiliza maoni ya wadau wa Bandari na hatimaye kushauri mambo mbalimbali, moja ya jambo lilio shauriwa ni Serikali kufuta kodi ya ongezeko la thamani kwa huduma zinazotolewa katika mizigo inayopitia bandari hiyo kwenda nchi jirani (VAT on acillary services on transit goods) kama Kongo DRC, Zambia, Malawi, Burundi, Rwanda na Uganda.

Serikali ilisikiliza ushauri wa Kamati na katika bajeti yake ya Mwaka wa Fedha 2017/2018 na iliondoa Kodi ya VAT kwenye huduma ya mizigo inayopitia Bandari ya Dar es Salaam. Hatua iliongeza idadi ya shehena za mizigo zinayopita Bandari ya Dar es Salaam;

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imekuwa ikiishauri Serikali juu ya wingi wa mamlaka za Udhibiti ambazo pia ushirikiano wake ni hafifu, Kamati ilishauri Serikali kuangalia namna ya kuunganisha mamlaka zinazofanya kazi zinazoingiliana ili kupunguza kero kwa wawekezaji wetu.

Serikali imeanza kutekeleza hili na mfano hai ni kwa majukumu ya Iliyokuwa TFDA ambayo pia yalikuwa yanatekelezwa na TBS yamehamishiwa TBS hivyo kile kilichokuwa kinalalamikiwa juu ya kukaguliwa mara mbili na kulipa kodi mbili katika bidhaa moja hakipo tena. Kamati inaendelea kuishauri Serikali kuendelea na mpango huu sababu bado zipo taasisi nyingine kama OSHA na FIRE pia kuna majukumu yanaingiliana;

**Mheshimiwa Spika**, Upungufu wa Nishati ya Umeme ambayo ni nishati muhumu katika ujenzi wa Uchumi wa Viwanda, Kamati ilishari kuwa zichukuliwe jitihada za makusudi za kupunguza au kumalilza kabisa tatizo hili.

Serikali yetu sikivu ilipokea ushauri na juhudi na mipango mbalimbali ya kuongeza Nishati ya umeme inaendelea ukiwemo mradi mkubwa wa kufua umeme wa maji wa Stiglas Guoge na miradi mingine ya gesi.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati pia imekuwa ikiishauri Serikali kupitia na kurekebisha Sheria na Kanuni mbalimbali ambazo zimeonekana kuwa kikwazo katika kuendesha biashara nchini, kwa nia ya kuongeza ufanisi wa Sekta za Viwanda, Biashara na uwekezaji.

Ushauri wa Kamati umezingatiwa ambapo Serikali imeandaa muongozo ambao unategemewa kuwa suluhisho la changamoto ya kukinzana kwa Sheria na Kanuni katika mazingira ya kufanyia biashara, muongozo huo ni Andiko maalum la Mpango wa Kuboresha Mfumo wa Udhibiti wa Biashara nchini (*Blue Print for Regulatory Reforms to Improve the Business Environment or Tanzania*). Kamati inaendelea kushauri Serikali kukamilisha maandalizi ya kutunga Sheria ya Uwezeshaji wa Biashara ambayo inategemewa kuweka misingi wa utekelezaji wa Blueprint na kusimamia maboresho ya mazingira ya biashara, jambo hili likamilike kabla ya uhai wa Bunge la Kumi na Tisa (19) kuisha kwa lengo la kuwezesha utelelezaji wenye tija wa Blueprint.

## SEHEMU YA TATU

## 3.0 MAONI NA MAPENDEKEZO

### 3.1 Sekta ya Viwanda na Biashara

**Mheshimiwa Spika**, Mheshimiwa John Pombe Magufuli, Rais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania amedhamiria kuipeleka nchi yetu katika Uchumi wa Kati kupitia Ujenzi wa Viwanda. Katika kutekeleza hili tunaendelea kushuhudia utekelezaji wa miradi mbalimbali ya kimkakati ambayo moja kwa moja inaenda kuchochea Ujenzi wa Sekta ya Viwanda **miradi hiyo ni ile inayotekelezwa na sekta mbalimbali nchini mfano mradi Julius Nyerere Hydro Power Plant (JNHPP), Standard Gauge Railway (SGR) na ununuzi wa ndege).**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaendelea kupongeza na kuunga mkono juhudi mbalimbali za Serikali ambazo zimelenga kuimarisha Sekta za Viwanda, Biashara na Uwekezaji na hatimaye kuweka mazingira mazuri ya kufanyia Biashara nchini. Takwimu za Mwaka huu zinaonyesha kuwa Tanzania tumepanda kwa nafasi tatu katika orodha ya nchi zenye mazingira mazuri ya kufanyia biashara kutoka namba 144 mpaka 141, hili linadhihirisha kuwa kuna juhudi zinafanyika;

**Mheshimiwa Spika,** pamoja na pongezi hizi Kamati inaendelea kuishauri Serikali kuyashughulikia ipasavyo masuala yafuatayo;-

#### 3.1.1 Utekelezaji wa miradi Mikubwa ya Kielelezo chini ya Sekta ya Viwanda

**Mheshimiwa Spika,** Miradi ya Liganga na Mchuchuma ni miongoni mwa miradi ya kielelezo kwa nchi yetu na utekelezaji wake unatazamiwa kuwa chachu ya ukuaji wa sekta mbalimbali nchini. Utekelezaji wa miradi hii umeonekana kuchukua muda mrefu na mpaka sasa imeripotiwa kuwa kuna majadiliano na upembuzi yakinifu ndio vinafanyika.

**Kwa kuwa,** Serikali imeitambua miradi hii kama miradi ya kielelezo kwa nchi lakini pia miradi ya kipaumbele na utekelezaji wake utachochea ukuaji wa sekta mbalimbali nchini hususani Sekta ya Nishati na Viwanda vya Chuma nchini;

**Hivyo basi,** Kamati inaishauri Serikali kuongeza nguvu katika kufanya mapitio ya utekelezaji wa miradi hii ili ipate kuanza utekelezaji wake na tuanze kunufaika kama nchi. Jambo hilimliende sambamba na kuweka miundombinu wezeshi kama barabara, umeme na maji ili kuwavutia wawekezaji;

Aidha, kwa kutambua changamoto zilizopo katika mikataba ya awali ambayo ilikwamisha utekelezaji wa miradi hii kwa muda mrefu. Kamati inaishauri Serikali kuweka umakini katika kuingia mkataba mpya wa utekelezaji wa miradi hii. Mkataba mpya ilinde na kuzingatia maslahi ya pande zote mbili yaani mbia na Serikali.

#### 3.1.2 Utekelezaji wa Mradi wa Kufufua Viwanda vilivyobinafsishwa na vilivyosimama uzalishaji kwa muda mrefu (mfano Urafiki)

**Mheshimiwa Spika,** Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa (2015/16-2020/21) pamoja na Ilani ya Chama cha Mapinduzi ambacho ndio chama tawala vinaielekeza Wizara ya Viwanda na Biashara pamoja na majukumu mengine ihakikishe kuwa viwanda vilivyobinafsishwa na havifanyi kazi vinaanza kufanyakazi na viwanda vyote nchini vinazalisha kwa kiwango cha juu kadri iwezekanavyo ikiwa ni kusudio la nchi kuingia katika uchumi wa kati kwa kupitia Viwanda;

**Kwa kuwa,** suala la kufufua viwanda vilivyobinafsishwa na vilivyosimama uzalishaji kwa muda mrefu (Urafiki, General Tyre) lilikuja baada ya kuona madhumuni ya ubinafsishaji hayakutekelezwa ambapo baadhi ya viwanda viliendeshwa kwa muda mfupi na kufungwa na vingine havikuzalisha kabisa; na

**Kwa kuwa,** eneo hili limehodhi uchumi mkubwa wa nchi ambapo ajira zimepotea, Serikali haipati mapato na tunakosa bidhaa nzuri ambazo zilikuwepo awali mfano Khanga ya Urafiki. Lakini bado zoezi la kufufua viwanda hivi linaendeshwa kwa kasi ndogo na halionyeshi matumaini ya kukamilika kurejeshwa kwa viwanda vyote hivi karibuni;

**Hivyo basi,** Kamati inaishauri Serikali kusimamia kwa karibu zoezi la kufufua viwanda vilivyobinafsishwa na vile vilivyosimamisha uzalishaji kwa muda mrefu ili kuvirudisha katika uzalishaji. Sambamba na hili upande wa Viwanda Kumi na Sita (16) ambavyo vimekwisha rejeshwa Serikalini tuangalie namna ya kuwashawishi wawekezaji wanaokuja kuwekeza katika Sekta ya viwanda baada ya kuanza uwekezaji mpya wafufue na waendeleze viwanda hivyo vya zamani;

Aidha, wahusika katika jukumu la kusimamia zoezi la kufufua viwanda hivi kwa zingatia nafasi ya kila mmoja wao wapewe muda maalumu (time frame) wa kukamilisha sehemu yake ya utekelezaji zoezi hili. Wahusika hao ni Ofisi ya Msajili wa Hazina (TR-Jukumu la Utekelezaji Mikataba), Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali (AG-Jukumu la kisheria na kikatiba kuhusu utekelezaji wa mikataba) na Wizara ya Viwanda na Biashara (msimamizi wa Sekta ya Viwanda).

### 3.1.3 Mwenendo usioridhisha wa upatikanaji wa Fedha kutoka Hazina

**Mheshimiwa Spika,** mwenendo usio mzuri wa upatikanaji wa kutoka hazina kwa Wizara ya Viwanda na Biashara, jambo linalopelekea kukwama kwa majukumu ya wizara iliyobeba muelekeo wa nchi kwa sasa wa kujenga Uchumi wa Kati kupitia Viwanda.

**Kwa kuwa** Serikali iliwasilisha mbele ya Bunge mpango wa mapato na matumizi uliojipambanua vuzuri sana lakini changamoto ipo katika kutekeleza mpango huo; na

**Kwa kuwa,** athari ya mwenendo usio mzuri wa upatikanaji fedha imeonekana katika utekelezaji wa miradi ya Maendeleo ambapo tumeshuhudia miradi hii ikichukua muda mrefu kukamilika jambo ambalo kwa upande moja linaongeza gharama ya miradi hiyo;

**Hivyo basi,** Kamati inaishauri Serikali kupanga mipango ya matumizi inayoendana na uhalisia wa makusanyo ya nchi. Sambamba na hilo Bajeti inayoidinishwa na Bunge itolewe kwa wakati ili kuwezesha utekelezaji wa majukumu yaliyokusudiwa.

### 3.1.4 VAT *refund* kwa wafanya biashara na wenye viwanda

**Mheshimiwa Spika,** Wazalishaji wengi wanakumbana na changamoto ya upungufu wa mitaji kutokana na malimbikizo makubwa ya madai ya Kodi ya Ongezeko la thamani (VAT refund) yanayolipa kwa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) kwa mujibu wa Sheria ya Fedha ya Mwaka 2014 ambayo ilianza kutumika mwaka 2015;

**Kwa kuwa,** malipo haya yanatekelezwa kisheria na kwa mujibu wa Sheria hii fedha hizo zinapaswa kurejeshwa kwa wahusika lakini mwenendo wa urejeshaji wa fedha hizi si wakuridhisha unalalamikiwa kusababisha kupungua kwa mitaji ya wafanyabiashara wanaolipa kodi hiyo jambo linalowaweka katika hali ya kulazimika kukopa ili waweze kuendelea na shughuli za uzalishaji. Madeni hayo yamekuwa makubwa na ni mzigo kwa Serikali ambapo kwa

viwanda vinne (4) tu kama vile Tanga Pharmaceutical Ltd, Allience One, Tobacco, ALAF Ltd na Mufundi Paper Mills Ltd vinadai jumla ya shilingi bilioni 55.5;

**Hivyo basi,** Kamati inaishauri Serikali kwa taarifa ambazo zimekwisha hakikiwa iangalie namna ya kurejesha fedha hizi za VAT kwa wahusika tena kwa wakati;

### 3.1.5 Ushuru wa Forodha wa 15% kwa sukari ya Viwandani (15 refundable import duty 15% on Industrial Sugar),

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inatambua nia nzuri ya Serikali kuanzisha kodi hii, lakini uchambuzi wa Kamati ulibaini kuwa hatukufanya maandalizi ya kutosha katika kusimamia utekelezaji wake na hili limedhihirika kwa kuwa ni takribani miaka minne (4) sasa tangu kuanzishwa kwake lakini mwenendo wa Serikali katika urejeshaji wa fedha hizo si wakuridhisha pamoja na kuwa baadhi ya taarifa zimekwisha hakikiwa na kuwasilishwa;

**Kwa kuwa** utekelezaji wa tozo hii umeonekana kuambatana na changamoto ambayo imepelekea kuathiri mitaji ya wafanyabiashara nchini kwa kuwa fedha hizo ni sehemu ya mtaji wa kiwanda na ilipaswa kurudishwa ili iendelee kutumika katika kuendeleza shughulu za uzalishaji; na

**Kwa kuwa** Serikali imeanzisha Ushuru wa Stampu ya Kielekroniki (*Electronic Tax Stamp – ETS*) ambayo umekwishaanza kutumika kwa baadhi ya viwanda na mfumo huu unauwezo wa kufanya kazi ya kuhakiki iliyokuwa ikikusudiwa na Sheria ya Ushuru wa Forodha wa 15% katika Sukari ya Viwandani;

**Hivyo basi,** Kamati inaishauri Serikali kuangalia namna ya kuachana na Mfumo wa Ushuru wa forodha wa 15% kwa sukari ya Viwandani na badala yake tukatumia taarifa za ETS kuhakiki matumizi ya Sukari ya Viwandani ambao ndio umeonekana kuwa wa uhakika zaidi.

Sambamba na hili Serikali iangalie namna ya kupunguza kodi ya ETS kwa kuwa kwa baadhi ya bidhaa imeonekana kuwa gharama inayolipwa kwa kutumia technolojia hiyo ni kubwa kuliko hata kodi ya bidhaa husika inayopelekwa Serikalini.

### 3.1.6 Kulinda Soko la Viwanda vya ndani

**Mheshimiwa Spika,** Serikali imenadi Azma ya Ujenzi wa Tanzania ya Viwanda na tunashukuru wawekezaji mbalimbali wa ndani na nje ya nchi wamelipokea vizuri azma hiyo na kuamua kuwekeza katika viwanda vya uzalishaji wa bidhaa mbalimbali. Kamati ilipata fursa ya kushuhudia baadhi ya viwanda ambavyo vimewekeza kwa uwezo wa kuzalisha bidhaa zinazotosheleza mahitaji ya soko la ndani na hata kuuza nje ya nchi mfano viwanda vya Chuma, marumaru, mabati, Saruji;

**Kwa kuwa,** nchi yetu ipo katika kujijenga kiuchumi wa viwanda na kwa kipindi hiki cha mpito bado hatujafanikiwa kujenga mazingira ambayo yatapunguza gharama za uzalishaji jambo linalopelekea bidhaa zetu za ndani kuwa na bei kubwa na kukumbana na changamoto ya kushindwa kushindana katika soko la ndani na bidhaa zinazotoka nje na duniani kwa ujumla;

**Hivyo basi,** Kamati inaishauri Serikali kuona namna ya kuvilinda viwanda vyetu kwa kuweka uwiano wa kodi kwa bidhaa zinazoingia ili kuhakikisha bidhaa za ndani zinaweza kushindana katika soko, hatua hii itasaidia kujiepusha kuwa soko la bidhaa za wenzetu. Suala la kulinda viwanda vya ndani limefanikiwa katika kulinda viwanda vya Sukari, kwa mfano huu inamaanisha tunaweza kuvilinda na viwanda vingine pia;

Sambamba na hili, Serikali iongeze nguvu ya kuvisimamia viwanda vya ndani kuhakikisha vinazingatia ubora unaotakiwa Sokoni. Vilevile tuongeze kasi ya kutengeneza mazingira ambayo yataenda kupunguza gharama za uzalishaji hususani kodi zinazoambatana na uzalishaji ili kuwezesha kupunguza bei za bidhaa hizo ili kuweka uwiano wa bei.

### 3.1.7 Urasimu katika kupata vibali vya ajira hasa kwa teknolojia ambayo haipatikani hapa nchini

**Mheshimiwa Spika,** katika kuhamasisha uwekezaji tumefanikiwa kuwavutia wawekezaji kuja nchini na kuwekeza na wengine wameleta teknolojia mpya ambayo haipo kabisa Tanzania, wawekezaji wengi wamekuwa wakihitaji kuhakikishiwa (*comfort*) kwa kuona wameruhusiwa kuja na watu wao ambao wanafahamu *status* za biashara zao lakini changamoto imekuwa katika kupata au kuhuwisha (*renewal)* ya vibali vya ajira hapa nchini (*work permit*);

**Kwa kuwa,** Sheria ya Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC) ndio Sheria mama ya usimamizi wa Uwekezaji nchini; na

**Kwa kuwa,** Sheria hiyo ya TIC inatoa ruhusa kwa muwekezaji kuja na watu wake watano (5) ambao anaona anawahitaji katika kuendesha shughuli/ biashara zake;

**Hivyo basi,** Kamati inaishauri Serikali katika suala la vibali vya ajira ihakikishe inasimamia matakwa ya sheria ya Uwekezaji ukizingatia kuwa muwekezaji yeyote anapotaka kuja kuwekeza nchini huwa anapitia na kutambua Sheria hii na si vinginevyo. Jambo hili litaleta uhakika (comfort) kwa wawekezaji kuhusu uwekezaji wanaoufanya;

Vilevile, suala la vibali vya ajira kwa wafanyakazi kutoka nje hasa katika zile nafasi ambazo nchi haina watu wenye ujuzi huo (experts) na uzoefu, vibali hivyo vitolewe ili kuendeleza kukuza uchumi wa nchi. Pia katika kuvutia uwekezaji tusiangalie faida za moja kwa moja zinazotokana na mradi husika, bali tuangalie na zile faida zisizo za moja kwa moja zinazopatikana kutokana na uwekezaji wa mradi husika kama vile kupata soko kwa bidhaa mbalimbali ambazo zinaweza kutumika kwenye mradi, ukusanyaji wa kodi, ajira kwa zile nafasi ambazo wataalamu wanapatikana nchini na nyingine nyingi. Hatua hii itaongeza uhakika kwa wawekezaji hivyo kupelekea kuongezeka kwa wawekezaji nchini;

### 3.1.8 Ucheleweshaji katika kutoa shehena bandarini

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inatambua nia nzuri ya Serikali ya kuwapa Shirika la Uwakala wa Meli Tanzania (*TASAC*) jukumu la kusimamia utoaji wa shehena bandarini lakini *TASAC* bado ni changa na haina uwezo wa kuhudumia wafanyabiashara wote (wa bidhaa inazozisimamia) jambo ambalo linapelekea ucheleweshaji wa kutoa mizigo bandarini na mwisho wake kuongeza gharama kwa uingizaji mzigo kwa kuanza kulipa gharama za storage na demurrage.

**Hivyo hasi,** Kamati inaishauri Serikali kwa kipindi hichi cha mpito ni vema ikaruhusu *TASAC* kusaidiwa na mawakala binafsi kushughulikia shehena bandarini mpaka pale itakapotengemaa na kuweza kuhudumia shehena zote kwa wakati.

Sambamba na hilo, Kamati inashauri wadau wote wa bandari ikiwepo TASAC TPA, TRA na wadau wengine kukaa pamoja ili kushughulikia changamoto zote zinazokwamisha upokeaji na utoaji wa mizigo bandarini kwa lengo la kuleta ufanisi.

### 3.1.9 Uwiano wa Ushuru usio sawa baina ya bidhaa za ndani na nje

**Mheshimiwa Spika,** gharama za uzalishaji kwa viwanda vya ndani bado ziko juu na kwa kiasi kikubwa zinachangiwa na kodi na tozo mbalimbali jambo ambalo linapelekea bei ya bidhaa zinazalizwa nchini kuwa juu ukilinganisha na zile zinazoingia kutoka nje. Aidha baadhi ya viwanda vya ndani vinalipa kodi ya ongezeko la thamani (VAT) katika uzalishaji wake lakini bidhaa ya aina hiyohiyo zinayoingia kutoka nje hazilipi kodi ya ongezeko la thamani (VAT) jambo linalopelekea bidhaa za ndani kushindwa kushindana, kwa mfano bidhaa za Vyandarua kutoka A to Z, bidhaa za madawa ya binadamu katika vifungashio hususani chupa;

**Kwa kuwa,** tumedhamiria kuhamasisha biashara na uwekezaji wa ndani katika kutekeleza azma ya Ujenzi wa Viwanda na kama hatutatafuta namna za kuwalinda wazalishaji wa ndani tutawatoa katika soko na hatimaye kuua viwanda vyao;

**Hivyo basi,** Kamati inaishauri Serikali kuangalia namna ya kuweka uwiano wa Kodi kati ya bidhaa zinazozalishwa nchini na zile zinazoingia kutoka nje hatua hiyo itapelekea bidhaa hizo ziweze kuuzwa kwa bei inayoendana na kuleta ushindani wa Haki.

### 3.2 Usimamizi wa Mazingira

**Mheshimiwa Spika,** Mazingira ni suala mtambuka, ili kuleta maendeleo endelevu suala la uhifadhi wa mazingira halina budi kupewa kipaumbele kwani kwa kiasi kikubwa ufanisi wa miradi yetu ya maendeleo inategemea uimara wa mazingira. Kuna haja ya Serikali yetu kuongeza umakini na kuongeza juhudi katika kusimamia masuala ya uhifazi wa mazingira.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati katika kuhakikisha inaisaidia Serikali katika masuala ya Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira inashauri mambo yafuatayo;-

### 3.2.1 Ufinyu wa Bajeti kwa ajili ya Usimamizi na Udhibiti wa Masuala ya Mazingira pamoja na mwenendo usioridhisha wa upatikanaji wa fedha hizo

**Mheshimiwa Spika,** katika taarifa hii ya Kamati tumebainisha changamoto kubwa ya uharibifu wa mazingira na jukumu kubwa lililopo ili kuhakikisha tunatatua changamoto zilizopo kwa lengo na kujinusuru na athari hizo;

**Kwa kuwa,** sisi sote ni mashuhuda wa athari za uharibifu wa mazingira ambapo hata kwenye maeneo yetu tunayotoka tumekwishaanza kuziona athari hizo lakini bajeti inayotengwa kwa ajili ya Ofisi ya Makamu wa Rais-Mazingira haitoshelezi katika kapambana na kasi ya uharibifu wa Mazingira nchini;

**Hivyo basi,** Kamati inaishauri Serikali kuangalia namna ya kuongeza bajeti ya usimamizi wa mazingira ukizingatia kuwa bila kuimarisha hali ya mazingira kutahatarisha mipango mingi ya nchi inayoendelea ikiwepo mradi mkubwa wa Stieglers Gorge;

Aidha, kwa sasa kiasi kikubwa cha bajeti ya usimamizi wa mazingira inatekelezwa na fedha za wafadhili jambo ambalo si zuri sana, tumeshuhudia kwa kipindi cha nusu mwaka yani Julai-Disemba 2019 ni asilimia **15.4** tu ya fedha zilizotengwa ndio zimepokelewa kutoka kwa wafadhili. Kamati inaishauri Serikali kuongeza Bajeti ya ndani katika usimamizi wa mazingira kwa lengo la kuleta uhakika wa utekelezaji wa usimamizi wa shughuli za Mazingira.

### 3.2.2 Kukwama kwa Mfuko wa Taifa wa Mazingira

**Mheshimiwa Spika,** Mfuko wa Taifa wa Mazingira ulianzishwa kwa lengo mahsusi la kuisaidia wizara yenye dhamana ya usimamia masuala ya mazingira kutafuta fedha kutoka maeneo mbalimbali ndani na nje ya nchi kwa ajili ya kutekeleza shughuli za usimamizi wa mazingira. Lakini mchakato wa kuanzishwa kwake unachukua muda mrefu na mpaka sasa Mfuko bado haujaanza kutekeleza majukumu yake;

**Kwa kuwa,** Mfuko huo umeanzishwa kisheria, majukumu na madhumuni yake yapo kisheria lakini sheria iliyoanzisha mfuko huo imeonekana kuwa na changamoto ambazo zinakwamisha uendeshaji wa mfuko huo; na

**Kwa kuwa,** moja ya chanzo cha mapato ni kodi ambayo kiwango chake kitaamuliwa kutoka katika tozo au ada inayotokana na shughuli za mazingira ambapo kwa sasa tozo hizo zipo nyingi na zinaingia katika mifuko mingine; na

**Kwa kuwa,** Kamati iliarifiwa juu ya hatua mbalimbali zilizopo katika kukamilisha maboresho ya Sheria ya Mfuko wa Mazingira lakini pia hatua iliyofikiwa katika kushughulikia tozo zitakazoingia katika mfuko wa mazingira pamoja na kiwango chake;

**Hivyo basi,** Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha mchakato wa maboresho ya Sheria ya Mfuko pamoja na kodi zake vikamilishwe kabla ya maandalizi ya Bajeti kuu ya Serikali kukamilika ili viingie katika mpango wa Serikali kwa Mwaka wa fedha 2020/2021 na kuanza kutekelezwa.

### 3.2.3 Uelewa mdogo wa Jamii juu ya masuala ya Uhifadhi wa Mazingira

**Mheshimiwa Spika,** tumeshuhudia shughuli mbalimbali za kibinadamu zimeendelea kuendesha bili kuzingatia Sheria ya Usimamizi wa Mazingira ya Mwaka 2004 jambo linalopelekea kutokuwepo kwa matumizi endelevu ya rasilimali zetu;

**Kwa kuwa**, hali ya ukiukwaji wa Sheria ya usimamizi wa Mazingira inaashiria inauelewa mdogo wa jamii juu Sheria yenyewe pamoja na kutofahamu umuhimu/faida ya utunzaji mazingira.

**Hivyo basi,** Kamati inaishauri Serikali kuiwezesha Ofisi ya Makamu Rais-Mazingira kwa kuiongezea rasilimali fedha na watu ili waweze kuwafikia watanzania wengi na kuwapatia elimu ya Uhifadhi wa Mazingira. Aidha, elimu inayotolewa izingatie shughuli za uzalishaji za jamii husika sababu uharibifu wa mazingira unatokana na aina husika ya shughuli za jamii mfano aina uharibifu unaotokana na kilimo ni tofauti na ule wa ufugaji na ule wa uchimbaji wa madini.

### 3.2.4 Uendeshwaji wa Biashara ya vyuma chakavu

**Mheshimiwa Spika,** katika kuendesha biashara ya vyuma chakavu kuna haja ya kuweka umakini mkubwa kwa muktadha wa kulinda mazingira yetu pamoja na viwanda vinavyotumia chuma chakavu kama malighafi katika uzalishaji wa bidhaa zake.

**Kwa kuwa,** Ofisi ya Makamu wa Rais-Mazingira kupitia Mkataba Besal inapaswa kusimamia biashara hiyo katika kuhakikisha chuma kinachosafirishwa hakina madhara kwa mazingira; na

**Kwa kuwa,** Wizara ya Viwanda na Biashara kupitia mwamvuli wa Biashara inapaswa kusimamia biashara hiyo inaenda kihalali lakini kupitia mwamvuli wa Viwanda inatakiwa kuhakikisha vyuma vinavyouzwa ni vile ambavyo havihitajiki kama malighafi kwa viwanda vya ndani;

**Hivyo basi,** Kamati inazishauri wizara zote mbili (Wizara ya Viwanda na Biashara pamoja na Ofisi ya Makamu wa Rais – Mazingira) kuhakikisha wanaimarisha ukaguzi wa mizigo ya vyuma chakavu kabla ya kupata kibali cha kusafirisha nje ya nchi ili kuhakikisha tunadhibiti masuala ya mazingira, tunadhibiti wizi wa mataruma ya reli pamoja na vifaa vya umeme lakini pia viwanda vya ndani ambavyo vinataka vyuma hivyo kama malighafi vinapatikana.

Vile vile, kuna wizi unafanyika katika maeneo ya reli, tanesco ili kupata baadhi ya vyuma hivyo, ni vyema Serikali ikatambua hilo na kuweka ulizi madhubuti katika maeneo hayo ili kujiepusha na madhara yanayoweza kutokea.

### 3.2.5 NEMC iendane na kasi ya Tanzania ya Viwanda na wapunguze urasimu katika kuwahudumia wawekezaji

**Mheshimiwa Spika,** vibali vya mazingira ni moja ya vibali muhimu vinavyohitajika katika shughuli za uwekezaji lakini mchakato wa kupata vibali hivi umegubikwa na urasimu jambo linalokatisha tamaa wawekezaji wengi.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inatambua changamoto ya upungufu wa watumishi NEMC jambo linalopelekea kazi ya tathimini ya Athari za Mazingira kufanywa na mawakala binafsi ambao kwa kiwango kikubwa NEMC inashindwa kuwasimamia mawakala hawa jambo linaloongeza urasimu uliopo sasa.

**Kwa kuwa,** kwa pamoja tumeamua kuijenga nchi yetu kufikia Nchi ya Uchumi wa kati, na pia tunatambua umuhimu wa Tathimini za Athari ya Mazingira na madhara yanayoweza kutokea kama tutapuuzia kufanya tathimini hizi;

**Hivyo basi,** Kamati inaishauri Serikali kuiwezesha NEMC kusimamia jukumu Tathimini za Athari ya Mazingira kwa weledi wa hali ya juu.

### 3.2.6 Utekelezaji wa Agizo la kupiga marufuku matumizi ya mifuko ya Plastiki

**Mheshimiwa Spika,** tumefanikiwa katika kuzuia matumizi ya mifuko ya plastiki ambayo ni hatua nzuri na yakupongeza kwa kuwa tumeweza kuyalinda mazingira yetu juu ya uchafuzi na uharibifu uliokuwa ukifanywa na mifuko hiyo. Katika kutekeleza hili tukiri kuwa hatukujiandaa vya kutosha kupata mbadala wa mifuko hii jambo linaloleta shida, jamii haina elimu juu ya mifuko inayohitajika lakini pia kuna wafanyabiashara wasiowaaminifu wanaamua kuzalisha au kuingiza mifuko isiyokidhi viwango.

**Kwa kuwa,** utekelezaji wa katazo la mifuko ya plastiki pamoja na upatikanaji wa mifuko mbadala linaendeshwa kwa kuzingatia Kanuni ambazo zimeandaliwa kwa umakini wake;

**Hivyo basi,** Kamati inaishauri Serikali kusimamia Kanuni ilizoziweka kwa manufaa ya pande zote yaani wazalishaji, wafanyabiashara na watumiaji.

Sambamba na hili itolewe elimu ya kutosha kwa jamii juu ya mifuko inayohitajikia lakini pia mamlaka zinazohusika katika kusimamia ubora na viwango vya mifuko zitekeleze majukumu yao kwa umakini sana;

**SEHEMU YA NNE**

## 4.0 HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika,** napenda kukushukuru wewe kwa uongozi wako uliotukuka na kwa ushirikiano ambao umekuwa ukiipatia Kamati wakati wa kutekeleza majukumu yake. Na pia, nakushukuru kwa kunipa fursa hii ya kuwasilisha Taarifa ya Kamati kuhusu utekelezaji wa majukumu yake kuanzia Machi 2019 hadi kufikia Januari, 2020.

**Mheshimiwa Spika,** napenda kuchukua fursa hii pia kumshukuru Naibu Spika pamoja na Wenyeviti wote Bunge kwa kuratibu na kusimamia vema shughuli za Bunge. Aidha, naomba kuchukua fursa hii kumpongeza Mhe. Mussa Azzan Zungu, Mb kwa kuaminiwa na Mheshimiwa Rais na kupewa dhamana ya kuwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira, natumai atafanya kazi kwa ukaribu na Kamati hii.
**Mheshimiwa Spika,** kwa namna ya pekee naomba kuwashukuru Wajumbe wote wa Kamati ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira, kwa kutekeleza majukumu yao kwa uadilifu wa hali ya juu. Aidha, nawashukuru na kuwapongeza kwa ushirikiano walioutoa katika kuandaa taarifa hii hadi kukamilika kwake. Naomba kuwatambua kwa majina yao kama ifuatavyo;-

| | |
|---|---|
| i. Mhe. Suleiman Ahmed Sadiq, Mb | **Mwenyekiti** |
| ii. Mhe. Kanal (Mst.) Masoud Ali Khamis, Mb | **M/Mwenyekiti** |
| iii. Mhe. Salim Hassan Turkey, Mb | Mjumbe |
| iv. Mhe. Richard Mganga Ndassa, Mb | Mjumbe |
| v. Mhe. David Cecil Mwambe, Mb | Mjumbe |
| vi. Mhe. Gimbi Dotto Masaba, Mb | Mjumbe |
| vii. Mhe. Jumanne Kibera Kishimba, Mb | Mjumbe |
| viii. Mhe. Kiteto Zawadi Koshuma, Mb | Mjumbe |
| ix. Mhe. Hawa Subira Mwaifunga, Mb | Mjumbe |
| x. Mhe. Munira Mustafa Khatibu, Mb | Mjumbe |
| xi. Mhe. Mussa Rashid Ntimizi, Mb | Mjumbe |
| xii. Mhe. Godbless Jonathan Lema, Mb | Mjumbe |
| xiii. Mhe. Omary Ahmad Badwel, Mb | Mjumbe |
| xiv. Mhe. Khamis Ali Vuai, Mb | Mjumbe |
| xv. Mhe. Zainabu Mdolwa Amiri, Mb | Mjumbe |
| xvi. Mhe. Josephine Johnson Genzabuke, Mb | Mjumbe |
| xvii. Mhe. Sylvestry F. Koka, Mb | Mjumbe |
| xviii. Mhe. Gibson Blasius Meiseyeki, Mb | Mjumbe |
| xix. Mhe. Shamsia Azizi Mtamba, Mb | Mjumbe |
| xx. Mhe. Ahmed Juma Ngwali, Mb | Mjumbe |
| xxi. Mhe. Jafar Sanya Jussa, Mb | Mjumbe |
| xxii. Mhe. Machano Othman Said, Mb | Mjumbe |
| xxiii. Mhe. Kalanga Julius Laizer, Mb | Mjumbe |
| xxiv. Mhe. Saed Ahmed Kubenea, Mb | Mjumbe |

**Mheshimiwa Spika**, naomba pia nitumie fursa hii kuwashukuru na kuwapongeza Mawaziri na Manaibu Waziri wote wa Wizara ya Viwanda na Biashara pamoja na Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingi, Makatibu Wakuu pamoja na Watendaji wote wa Wizara na Taasisi zote zilizopo chini ya Wizara hizo kwa ushirikiano waliutoa kwa Kamati kwa kipindi chote hiki.

**Vile vile,** naomba kumshukuru Katibu wa Bunge, Ndg. Stephen Kagaigai, kwa ushirikiano ambao amekuwa akiutoa kwa Kamati na kuhakikisha tunaendelea kutekeleza majukumu yetu

kiukamilifu. Pamoja na yeye, namshukuru Kaimu Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge, Ndg. Michael Chikokoto, Makatibu wa Kamati Ndg. Zainab Mkamba na Ndg. Mwajuma Ramadhan pamoja na msaidizi wa Kamati Ndg. Pauline Mavunde, kwa kuratibu vyema Shughuli za Kamati.

**Mheshimiwa Spika,** sasa naliomba Bunge lako Tukufu lipokee na kuijadili taarifa hii na hatimaye kukubali **maoni**, **ushauri** na **mapendekezo** ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira.

**Mheshimiwa Spika,** naomba kutoa hoja.

…………………………
Mhe. Kanal (Mst.) Masoud Ali Khamis, Mb
**MAKAMU MWENYEKITI**
**KAMATI YA KUDUMU YA VIWANDA,**
**BIASHARA NA MAZINGIRA**

31 Januari, 2020

**MWENYEKITI:** Ahsante. Hoja imetolewa na imeungwa mkono, nakushukuru sana Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira kwa taarifa ya Kamati. Sasa tuanze mjadala kwa muda wetu uliosalia. Nina orodha ya wachangiaji, tujitahidi sio lazima utumie dakika 10 kwa wale ambao wana dakika zao 10 wengine wana dakika tano. Nitaanza na Mheshimiwa Lucy Owenya, dakika tano.

**MHE. LUCY F. OWENYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia na kuwa mtu wa kwanza katika mjadala wa leo. Wizara ya Viwanda na Biashara katika fedha za maendeleo mwaka 2018/2019 walitakiwa watengewe shilingi bilioni 100.02 lakini zilizotolewa ni shilingi bilioni 13.63. Mwaka 2019/2020 fedha za maendeleo zilizotengwa zilikuwa ni shilingi bilioni 51.5 pungufu ya asilimia 48.7 ya zilizotengwa za mwaka 2018/2019.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kutotoa fedha za maendeleo za kutosha inachangia kutokuziwezesha taasisi ambazo ziko chini ya Wizara kama *CAMARTEC, TIRDO* na *SIDO* ili kuweza kufanya tafiti za kuweza kuendeleza vifaa vya kilimo au vifaa vya kwenye viwanda. Kwa hiyo naishauri Serikali itenge fedha za kutosha ili waweze kuendeleza shughuli za viwanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niongelee suala la viwanda vilivyoko katika Mji wa Moshi. Moshi tuna viwanda vingi sana, kulikuwa na Kiwanda cha Kibo *Match* ambacho kilikuwa kinatengeneza vibiriti, lakini kiwanda kile mpaka leo hii kimekufa na hakijaendelezwa kwa vyovyote vile. Kiwanda kile kilikuwa kinazalisha ajira zaidi ya 600 na walikuwa wanazalisha vibiriti zaidi ya 6,000, lakini kwa sasa hivi ina maana ajira zile zimepotea na vijana wanazurura mtaani wakati kiwanda kipo pale gofu, ambapo Serikali ingeweza kuvifufua na kikafanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kiwanda kingine ni kile cha ngozi kilichoko Moshi, kinatengeneza ngozi ndiyo, lakini kwa kiwango kidogo sana. sijui ni kwa jinsi gani Wizara imeenda kuangalia suala zima la mazingira kwa sababu pale wakazi wa Pasua, Mabogini, Bomambuzi wanaanthirika sana na harufu ya ngozi inayotoka katika kiwanda cha ngozi. Sasa sijui kma wameshafanya utafiti kugundua kama ile harufu inayotoka katika kiwanda kile kama inadhuru watu au la. Ningeomba Serikali ifanye utafiti iende ikaangalie suala zima la mazingira katika kile Kiwanda cha *Tanneries*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapo hapo kulikuwa na kiwanda cha magunia, mpaka leo ni gofu liko pale. hakuna chochote kinachoendelea, imekuwa ni mahali pa kuhifdhi tu vitu lakini hakuna kiwanda cha magunia pale Moshi. Sasa sijui mpaka leo hii bado tunaimba kuhusu viwanda vya magunia Moshi wakati katani zipo lakini sijui kwanini sasa viwanda vile havifufuliwi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kiwanda kingine kilichoko katika Mkoa wetu wa Kilimanjaro ni kiwanda mama cha *machine tools.* Tumekuwa tukipiga kelele kila siku. Kiwanda kile bado hakizalishi, vipuli vilivyoko pale ni teknolojia zile za zamani kwa hiyo wanashindwa kuzalisha viwanda kwa ajili ya viwanda vidogo vidogo. Sasa sijui lini sasa Serikali itafanya ule utafiti iliyosema inafanya na kutafuta mwekezaji ili watengeneze teknolojia mpya, wazalishe viwanda vidogo vidogo ili viweze kusaidiana na *SIDO* watu waweze kuzalisha na mazao yao wakiwa kule kule vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuulizia kuhusu kiwanda cha *General Tyre* Arusha. Kiwanda kile kilikuwa kinafanya kazi na kilikuwa kinazalisha matairi mazuri *East* na *Central* Africa kabisa lakini sasa mpaka leo hii ni zaidi ya miaka kumi tumekuwa tukikizungumzia kiwanda cha *General Tyre* kilikuwa kimeajiri watu wengi sana lakini bado Serikali haijaonesha ni lini sasa kiwanda kile kitaanza kwa sababu bado tuna yale mashamba yaliyoko kule Tanga ambayo yanazalisha mpira, yamekaa tu kule badala yake wamekuwa Wakenya wakienda kule wanaenda kuchukua zile *rubber* wanaenda kutengeneza *big* Nairobi na sisi ambao tungeweza kutumia ile *rubber* kwa ajili ya kwenda kutengenezea matairi yetu kule Arusha. Lakini mpaka leo hii Serikali haijasema ni lini sasa kiwanda cha *General Tyre* kitaanza kazi. Tunaomba watupe *time frame* ni lini kitaanza kazi ili vijana wetu waweze kupata ajira kwa sababu kiwanda kile kina nafasi ya kutosha, kimelala tu pale, vijana wanazurura lakini wangeweza kupata kazi katika kiwanda kile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kidogo nizungumzie kuhusu masoko. Mkoa wa Kilimanjaro tunalima sana ndizi na tunalima pia maparachichi. Lakini unakuta wakulima wanavuna maparachichi kwa wingi sana lakini yote yanaoza kwa sababu tu hawana masoko na wengine ni kwa sababu ya *packaging* na mengine unakuta…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Lucy Owenya kwa mchango wako. Dakika zako tano hizo. Mheshimiwa Julius Kalanga, atafuatiwa na Mheshimiwa George Malima Lubeleje na baadae nitawataja wengine. Mheshimiwa Kalanga.

**MHE. JULIUS K. LAIZER:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia asubuhi ya leo. Nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuendelea kutupa kibali cha kuona mwaka huu na niipongeze sana Serikali ya Chama Cha Mapinduzi kwa kuendelea kusimamia utekelezaji wa Ilani na kufanya miradi ya maendeleo ya wananchi wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nianze asubuhi hii kwa kunukuu baadhi ya maeneo ya Katiba Ibara ya 3(8), Katiba inasema; Jamhuri ya Muungano ni nchi inayofuata misingi ya demokrasia, wananchi ndiyo msingi wa mamlaka yote na Serikali itapata madaraka na mamlaka yake kutoka kwa wananchi kwa mujibu wa Katiba hii. Lengo kuu la Serikali litakuwa ni ustawi wa wananchi, Serikali itawajibika kwa wananchi na wananchi watashiriki katika shughuli za Serikali kwa mujibu wa masharti ya Katiba hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimenukuu maneno haya ili tukubaliane pasipo shaka kwamba kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Chama Cha Mapinduzi ndiyo chama kilichokabidhiwa dhamana ya kuongoza dola na Taifa hili. Tukiacha nchi yetu ikashambuliwa, ikafedheheshwa, ikanyimwa haki yake, ikadhalilishwa na watu wasioitakia mema nchi hii, siku ya siku wananchi hawatawauliza wale ambao wameishambulia nchi yetu, watatushambulia sisi ambao tumepewa dhamana ya kuilinda na kulisimamia Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo Bunge hili na hasa wanaCCM nataka niwaombe tulinde heshima ya Taifa hili kwa heshima kubwa na kwa wivu unaostahili na kumtunza n kumlinda Rais wetu ambaye ndiye kioo na ndiye msingi wa uadilifu wa Taifa letu ambaye amerudisa nchi yetu katika misingi ya haki na ya kidemokrasia na kusimamia rasilimali ya Taifa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, haiwezekani Bunge au Wabunge wa CCM wakanyamaza wakati Serikali yao inashambuliwa na watu wasioitakia mema nchi hii. Haiwezekani, lazima tuwe na wivu uliopitiliza wa kuilinda Serikali yetu na kumlinda Rais wetu pasipo shaka na bila aibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, asubuhi imezungumzwa hapa habari ya watu wanaoichafua nchi yetu lakini siku ya siku maslahi mapana ya Taifa liko katika Chama Cha Mapinduzi ambao ndiyo wamepewa dhamana na wananchi. Nataka niwaombe wale ambao tumepewa dhamana na wale ambao Rais amewapa nafasi ya kumsaidia Rais, sisi Wabunge wa Chama Cha Mapinduzi tuko nyuma yenu endeleeni kutekeleza majukumu yenu bila kusita na sisi tunawaunga mkono kwa kile ambacho mnafanya kwa ajili ya kumsaidia Rais wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili jambo ni la aibu kwa viongozi ambao wamepewa dhamana wanatumia nafasi waliyopewa katika kushambulia Taifa hili na kuinyima haki na kuidhalilisha mbele hata ya Mataifa. Sisi tuko mstari wa mbele kulinda heshima ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nitoe mchango wangu katika maeneo mawili na nianze katika kamati ya viwanda na biashara ambayo mmesikia Taarifa yake, tuliletewa Taarifa ya utekelezaji wa mradi wa Jengo la maabara mradi namba 6260, Fungu namba 60. Wakati tunaletewa mradi huu tuliambiwa jengo hili limetumia bilioni 19 kujengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati imeomba kwa miaka karibu miwili, Serikali ilete taarifa ya utekelezaji mradi huo kwa sababu inaonekana kuna ufisadi mkubwa sana lakini mpaka sasa tunavyoongea kwenye Bunge hili, Serikali haikuleta taarifa hiyo. Tunaomba Bunge lako lione namna nzuri ya kusimamia mradi huu wa *TBS* kwa sababu hata kama sisi sio wataalam wa ujenzi, lakini sehemu ya mkataba ule unakuambia umeme utawekwakwa shilingi bilioni 3.1 na kiyoyozi cha mfumo wa hewa, bilioni 3.3.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia mfumo mzima wa mradi huo, tumeomba sana mkataba huu kwenye Kamati, hatukuletewa. Tunaiomba Serikali na hasa Waziri anayeshughulikia viwanda aone namna ya kulisimamia suala hili ili haki ijulikane kama kuna ufisadi katika mradi huu, uweze kujulikana na wale walioisababishia nchi yetu hasara wachukuliwe hatua. Mradi huu kuna harufu ya rushwa na inaonekana kabisa hata katika *tendering documents.* Wale waliokuwa juu ndiyo waliopewa mkataba na wale waliokuwa chini wakanyimwa mkataba lakini ukiuliza mfumo uliotumika, hawasemi. Ninaomba muangalie jambo hili ili liweze kushughulikiwa ipasavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo langu la pili ni mradi wetu wa magadi wa Engaruka ambao wanasema inatoa tani milioni 4 kwa mwaka. Ardhi hii wananchi tumetoa karibu ekari 100,000 kwa ajili ya mradi huu lakini kwa miaka minne sasa hakuna jambo lolote linaloendelea

katika eneo la Engaruka kwenye mradi huu. Tunaomba Kamati inayohusika itusaidie Serikali ituambie ina mpango wa kuendelea na mradi huu au haina mkakati wowote wa kuendelea na mradi huu ili kama mradi huu hauendelezwi ardhi hiyo irudishwe kwa wananchi wafanye maendeleo yao na kuendeleza eneo lile kwa sababu tumezuiwa kuendeleza ile ardhi lakini mpaka sasa hakuna hatua zozote ambazo Serikali imechukua katika kuhakikisha wawekezaji katika eneo lile la magadi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri atuambie baadaye vilevile kama Serikali inahitaji kuendeleza eneo hili na hata kama haiendelezi kwa leo, ile fidia ambayo wananchi wetu walipaswa kupewa, wapewe ili ardhi ile ibaki kwenye mikono ya wananchi la sivyo wananchi wapewe nafasi ya kuiendeleza na Serikali itakapokuwa tayari kuendeleza mradi huo italipa fidia kwa wakati maendeleo yaliyokuwa yamefanyika wakati huo kuliko kuacha ardhi ya wananchi wa Monduli heka 100,000 bila kufanya maendeleo yoyote. Naomba nipate Mwenyekiti wa Kamati atusaidie katika eneo hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo langu la mwisho ni suala la miundombinu katika nchi yetu, ukiangalia Wabunge wengi humu tunalalamika uharibifu wa miundombinu iliyosababishwa na mvua, Lakini ukienda kwa wataalam hasa *TARURA* na hata *TANROADS* unaambiwa hakuna bajeti ya dharura katika kutatua matatizo haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba tunapoelekea katika bajeti na Mwenyekiti wa miundombinu atusikilize vizuri, hatuwezi tena kupitisha bajeti bila kuonekana kama kuna kipengele cha bajeti ya dharura katika utekelezaji wa miradi ya *TARURA* pamoja na *TANROADS* kwa sababu tunasema tu watu wakaribishe miundombinu lakini uhalisia hakuna fedha iliyotengwa kama dharura kwa ajili ya miundombinu pale ambapo mvua imeharibu miundombinu na siku ya siku barabara hizo na maeneo yale hayarekebishwi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba kadiri tunavyoelekea katika bajeti, hili eneo la dharura kwa ajili ya barabara zetu zitakapokuwa zimeharibiwa na mvua ziwekwe aidha katika kila Mkoa au katika ngazi ya hamashauri ili watu wa *TARURA* waweze kufanya kazi yao kwa ufanisi na waweze kusaidia pale ambapo kuna uhitaji kwa sababu nao wanaenda kuangalia tu lakini hakuna ambacho wanaweza wakafanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru lakini la mwisho kabisa ni suala hili la *blue print,* suala la *blue print* inaonekana kwamba Serikali imekubali kwamba tuwe na mfumo utakaosimamia biashara nchini lakini mifumo hii na wewe ni mwanasheria haijatungiwa sheria kwa hiyo kila mmoja anapotaka kutengeneza inaonekana kuna vikwazo vya kisheria ambavyo vinasababisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba kama Serikali itakubali katika Mwaka huu wa Fedha kabla hatujamaliza Bunge hili, tume ilete usheria hapa hata kama ni kwa dharura ili baadhi ya sheria ambazo zinakwaza biashara nchini ziondolewe na wafanyabiashara wetu waweze kufanya biashara zao katika hali ya utulivu na kwa amani kwa ajili ya usalama na utukufu wa nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuendelea kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa kwa mchango wako. Mheshimiwa Lubeleje atafuatiwa na Mheshimiwa Bhagwanji Meisuria. Mheshimiwa Lubeleje

**MHE GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia hoja hizi mbili. Kwanza kabisa nizipongeze hizi Kamati zote mbili,

niwapongeze Wenyeviti pamoja na Wajumbe kwa kazi nzuri kwa sababu hawa ndiyo wanaochambua bajeti ya wizara zinazohusika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie hasa masuala ya barabara, barabara ya kutoka Mpwapwa kwenda Kongwa ni barabara muhimu sana na nashukuru katika Bajeti ya mwaka 2019/2020 walitenga fedha kidogo kwa ajili ya kuanza kutengeneza kwa kiwango cha lami. Pamoja na kwamba ni fedha kidogo lakini nina uhakika bajeti ya Mwaka 2020/2021 Wizara ya Ujenzi watapanga fedha za kutosha kwa ajili ya kutengeneza barabara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara hii ni muhimu sana na inawezekana hata wewe Mwenyekiti umewahi kupita barabara ya kutoka Kongwa kwenda Mpwapwa. Barabara hii ndiyo inayotumika na wakandarasi Waturuki wanaotengeneza reli ya kati *SGR* sasa mitambo yote mikubwa, malori yote makubwa, yanapita katika barabara hii. Kwa hiyo, naomba sana Mwenyekiti wa Kamati pamoja na Wajumbe, wakati wa kuchangia bajeti ya 2020 naomba sana mzingatie hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili ni barabara ya kutoka Gulwe – Berege – Chitemo – Mima – Igojimoja – Isalaza – Chitope. Barabara hii iko chini ya *TARURA* na ni barabara muhimu sana, niliomba barabara hii kwa sababu *TARURA* hawana uwezo, bajeti yao ni ndogo sana, hawawezi kuifanyia matengenezo makubwa barabara hii yenye urefu wa kilometa 58. Niliomba *TANROADS* wachukue kwa sababu *TANROADS* ndiyo wenye fedha za kutosha kuweza kuitengeneza barabara hii kwa matengenezo ambayo yanatakiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, barabara hii inahitaji bilioni 1.6 ili iweze kufanyiwa matengenezo makubwa. Sasa naomba bajeti ya TAMISEMI mwaka 2020/2021 waifikirie barabara hii, waitengee bajeti ya kutosha. Lakini kutenga bajeti ya milioni 120 haitoshi kabisa! naomba zitengwe fedha za kutosha kabisa ili barabara hii kwa sababu barabara hii inahudumia wananchi wa kata 7 na ni barabara muhimu sana kwa maendeleo ya Wilaya ya Mpwapwa.

Kwa hiyo, nilikuwa naiomba sana *TARURA* watenge fedha za kutosha ili barabara hii iweze kufanyiwa matengenezo makubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuzungumza haya, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia na naunga mkono hoja mbili zote. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Lubeleje. Mheshimiwa Bhagwanji, atafuatiwa na Mheshimiwa Miraji Mtaturu.

**MHE. BHAGWANJI MAGANLAL MEISURIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, kwanza nakupongeza kwa kunipa nafasi hii ya kuzungumza. Kamati yangu ni ya Miundombinu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Spika na Mheshimiwa Naibu Spika, wanafanya kazi nzuri sana katika Bunge hili na Mheshimiwa Spika yeye ni mlezi wangu na amekuja mpaka Jimboni kwangu amekagua miradi mbalimbali. Kwa hiyo, namshukuru sana, anafanya kazi nzuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakuja kwa Waziri pamoja na Naibu Waziri wa Mundombinu, wanasimamia kazi kubwa ya Sekta ya Bandari, Uwanja wa Ndege, barabara n.k kwa hivyo nimetazama na nimeona Waziri na Naibu wake wanastahili kupongezwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nizungumze kitu cha maana kabisa. Mheshimiwa Rais, Dkt. John Joseph Magufuli amesimamia Tanzania na kufanya kazi nzuri kabisa katika awamu

yake, Mungu amuweka na uchaguzi huu yeye atarudi. Mimi namuombea kwa Mwenyezi arudi yeye pamoja na mimi. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mwenyekiti wangu wa CCM Taifa, Mheshimiwa Dkt. John Joseph Magufuli hapa Bungeni Bhagwanji Maganlal Mesuria, Baniani peke yake arudi tena. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile naangalia na nakupongeza kwa dhati kabisa Mheshimiwa Rais wangu wa Zanzibar Ally Mohamed Shein, ametekeleza wajibu wake katika awamu yake mpaka leo. Wananchi wa Zanzibar wameridhika, barabara, maji, umeme, shule pamoja na hospitali n.k aliyoyafanya sana na amekuwa kifua mbele. Mungu amuweke Mheshimiwa Ally Mohamed Shein, Rais wa Zanzibar, amefanya kazi nzuri sana na atazidi kufanya na mimi niko pamoja na yeye na yeye namuomba jina langu anirudishe tena. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, Kamati yangu ya Miundombinu, Mwenyekiti pamoja na sisi Wajumbe tunasimamia Sekta ya Miundombinu kwa hivyo Sekta hii inakuwa ina matatizo mengi, Sekta hii tumepongezwa na Sekta hii ya miundombinu tumesimamia barabara, uwanja wa ndege, *standard gauge* na tumesimamia bandari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, sisi katika Kamati yetu zikija taarifa kama hizi basi sisi tunakaa na Waziri, Katibu Mkuu wa miundombinu pamoja na wananchi na tunashirikiana kufanikisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nazungumzia Bandari, Bandari ya Dar es Salaam inafanya kazi nzuri sana lakini pana kasoro moja tu inahitajika irekebishwe, ishikwe mkono kwa sababu hizi *container* zinatoka nchi za nje na meli inakaa sana na *container* hazitoki sana katika bandari kwenda nchi zingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hivyo hata wafanyabiashara wanalalamika kwa sababu wanafanya kazi sana *TRA,* bandari na wale watu wa Shirika la Bandari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naiomba Serikali, Bandari ya Dar es Salaam isimamiwe na kwamba likija kontena, basi ianze kutoka nje haraka sana. Kwa sababu wafanyabiashara wengine wameamua kutoa mizigo yao kupeleka Mombasa kwenda nchi ya Burundi, Zambia na sehemu nyingine nasi tutakosa mapato. Kwa hiyo, naiomba Serikali isimamie bandari yetu ili kontena zote zipate kutoka kwa haraka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile namwomba Mheshimiwa Rais wetu kuhusu Bandari ya Zanzibar ambayo ina kontena nyingi pamoja na mambo mengine, ni bandari ndogo kabisa. Tunataka tushiriki Muungano wetu kupitia Bandari yetu ya Zanzibar 2020 na kuendelea mbele. Ipanuliwe na tusaidiane kwa sababu sisi ni ndugu moja na tunataka kuboresha Zanzibar na Tanzania. Kwa sasa Bandari ya Zanzibar kontena zinakuja nyingi sana na hakuna pa kuweka. Kwa hiyo, naomba Serikali ya Tanzania tufanye kazi pamoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunazungumzia uwanja wa ndege. *Terminal III* imekamilika, nashukuru sana. Bunge lililopita niliwaambia nitasafiri, kwa hiyo kweli nampongeza Mheshimiwa Rais, nilikuwa naenda India na nchi nyingine. Nilikwenda India nikafuatana na mama mtoto wangu pamoja na familia, nimeshuhudia ndege ile inafanya kazi, inajaa sana. Ndege hiyo wakati wa kurudi vile vile inajaa kwa sababu moja; ndege hii Serikali imeamua kwenda *direct.* Kwa hiyo, wananchi, watalii wa India na nchi mbalimbali wamekubali kupanda ndege yetu ya Tanzania kuja hapa. Hii itatusaidia na kutuongezea kipato. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba jambo moja lingine kuhusu uwanja wetu wa ndege wa Zanzibar. Kwa kuwa sisi ni Muungano, lazima tuboreshe kwa sababu wanakuja watalii wengi na tunapata mapato mengi. Sasa kwa sababu ni Muungano, Zanzibar na Dar es Salaam, Tanzania basi tutaongezea; na tulikwama uwanja wetu wa ndege *Terminal II,* basi tumalize haraka na tuongeze ndege nyingi kutoka Zanzibar kuja Dar es Salaam zinaunganisha kwenda India na sehemu nyingine. Naomba Serikali isaidie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, mitandao ya simu pamoja na minara yetu katika mipaka inakuwa na matatizo, wananchi wanakosa mawasiliano. Naiomba Serikali na Mheshimiwa Waziri asimamie Tanzania yetu katika sekta mbalimbali na sehemu mbalimbali hususan kwenye mitandao ya simu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara zetu tunajitahidi kufanya vizuri na tutazidi kutengeneza. Namshukuru Mheshimiwa Rais, bajeti yetu kwa upande wa miundombinu amesaidia na amesimamia na tumepata pongezi. Kamati ya Miundombinu pamoja na Mheshimiwa Waziri na Kamati yake, vile vile na Katibu Mkuu wanafanya kazi nzuri, nawapongeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu pamoja na Makamu wa Rais, wamefanya kazi nzuri sana kwa Tanzania kwa kutembelea kila mahali mpaka Zanzibar. Kwa hivyo, tunampongeza na Mungu amuweke.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naunga mkono Kamati hii pamoja na Bunge. Kwa hiyo, naiomba Serikali yangu ya CCM pamoja na Rais wangu, CCM oyee! Nami nataka nirudi tena. CCM oyee! *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Bhaghwanji, ndio wewe Baniani pekee ndani ya Bunge.

Mheshimiwa Mtaturu halafu Mheshimiwa Vedasto Manyinyi ajiandae.

**MHE. MIRAJI J. MTATURU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia hoja katika Kamati hizi mbili ambazo zimewasilisha taarifa zao, nami nipo kwenye Kamati ya Miundombinu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwanza kwa kumshukuru sana Mungu ambaye ni mwingi wa rehema kutujalia uzima na kuweza kuendelea kufanya majukumu haya kwa ajili ya Watanzania wenzetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, nitumie nafasi hii kwanza kumshukuru sana Rais wetu mpendwa, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli ambaye kwa hakika mwelekeo na dhamira yake imekuwa inarahisisha sana utendaji wa Serikali. Hii yote ni kwa sababu wananchi wa Tanzania wamekuwa na imani naye na ndiyo maana basi naye amekuwa akifanya kazi hii kama ambavyo wananchi wanatarajia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninapongeza kwa namna ambavyo tumeendelea kupata bajeti kwenye hii Wizara yetu ya Ujenzi kwa maana ya kutekeleza majukumu yaliyopo ndani ya Wizara hii. Kama alivyoeleza Mwenyekiti wetu pale asubuhi, ni kwamba tumepata fedha za kutosha kutekeleza miradi mbalimbali ambapo haya mashirika mbalimbali na taasisi yalileta taarifa zao kwenye Kamati yetu na kuona namna ambavyo Serikali iliendelea kuleta fedha. Najua bado kuna changamoto lakini ninaamini zitatatuliwa kulingana na muda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushahidi pekee ni pamoja na maeneo mbalimbali ikiwemo ununuzi wa ndege, ujenzi wa barabara za lami katika nchi yetu, mawasiliano mbalimbali, kwa maana minara inajengwa na hata juzi tumesaidi mkataba kwa ajili ya kuhakikisha kwamba tunapeleka minara kwenye vijiji vipatavyo 555 nchi nzima. Yote hiyo ni dhamira ya dhati ya Serikali kuhakikisha kwamba inaboresha mawasiliano na huduma mbalimbali zinazotokana na Wizara yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye hili nitumie nafasi hii kuendelea kumshukuru sana Mwenyekiti wetu Mheshimiwa Selemani Kakoso pamoja na Makamu wake Mheshimiwa Hawa Mchafu ambao wamekuwa wakiongoza vizuri Kamati hii. Vile vile Wajumbe kwa pamoja tumekuwa tuna ushirikiano mkubwa katika kuhakikisha kwamba tunahoji mambo ya msingi kwa ajili ya maslahi ya Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati yetu tulipata fursa ya kukutana na taasisi mbalimbali zilizopo chini ya Wizara hii ya Ujenzi, Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu Mawaziri wake walituletea wataalam hao na tumeendelea kuhojiana kwenye Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitazungumzia sekta mbili ambazo nilidhani niweze kuzitolea maelezo ndani ya Bunge lako Tukufu. Nianze na wenzetu wa Wakala wa Huduma za Meli. Kama ambavyo tunajua kwamba sisi kijiografia katika ukanda huu tumekaa vizuri sana katika biashara kwa maana ya bandari na tumekuwa tukifanya hivyo kwa miaka mingi na tumekuwa tukipata faida kubwa ya fedha tunapotoa mizigo hapa kwenda kwenye nchi mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kazi nzuri inayofanywa, changamoto moja kubwa sana ambayo tumeigundua; tumefanikiwa kukutana na wadau wa sekta hiyo ambao ni wasafirishaji mbalimbali wanaoleta mizigo kupitia bandari yetu, wamekuwa na malalamiko mbalimbali ikiwemo ucheleweshaji wa mizigo yao kutolewa kwenye bandari. Hii imesababisha baadhi ya wafanyabiashara kuhamisha mizigo yao na kushushia kwenye bandari nyingine ikiwemo Beira pamoja na pale Mombasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo hili ukilisikiliza kwenye Kamati tumeenda kwa kina sana. Kwa kweli ni jambo ambalo tusipolifanyia kazi, wafanyabiashara wataondoka wengi wataenda kushushia mizigo eneo ambalo siyo hapa kwetu. Hii itakuwa ni athari kubwa kwenye uchumi wetu; na haya ambayo tunampongeza leo Mheshimiwa Rais na Serikali yake hawawezi kufanya bila kuwa na fedha za kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la *storage* limekuwa ni tatizo kubwa lakini pia kumekuwa na urasimu mkubwa sana katika utoaji wa mizigo. Kuna manung'uniko makubwa kwa wadau. Tunaiomba Serikali ikakae na wadau iwasikilize na watoe ushauri wao namna ya kuenenda. Wao hawana tatizo na ulipaji, wana tatizo na urasimu mkubwa uliopo ndani ya mamlaka hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukifanya hivi, tutakuwa tunaitendea haki nchi yetu na kwa hakika tutakuwa tuna uwezo wa kuongeza mapato ya kutosha kwa ajili ya kuwa na uhakika wa kutekeleza miradi ya kimaendeleo ambayo tunayo katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wametueleza wenzetu pale kuhusu uchakavu wa bandari nchini. Ni ombi letu kupitia Bunge lako Serikali iende ikaboreshe miundombinu iliyopo kwenye bandari zetu. Najua juhudi zinaendelea, lakini kwa sasa wao wenyewe kama mamlaka walituambia kwamba changamoto kubwa ilikuwa ni uchakavu wa bandari zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile ushindani. Chombo hiki kinachosimamia biashara hii ni vizuri ikajua kwamba wenzetu wanafanyaje? Maana leo hii baadhi ya wengine wanaona wanakuwa na *comfort* kubwa kuwa kwenye bandari nyingine kuliko kwenye bandari yetu ya hapa Dar es Salaam. Tukifanya hivyo, tutakwenda kuongeza nguvu kubwa ya kuvutia wafanyabiashara kushushia mizigo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kwenye sekta moja ya ujenzi ambayo ni wenzetu wa *TBA*. *TBA* ni wakala, anafanya kazi nzuri. Lengo la kuanzishwa kwake ilikuwa ni kusaidia eneo la ujenzi katika majengo mbalimbali ya Serikali yaliyopo hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumegundua pamoja na juhudi wanazofanya, wenzetu wa *TBA* wana upungufu mkubwa wa rasilimali watu, hawana wafanyakazi wa kutosha katika kutekeleza miradi yao. Kwa hiyo, ombi letu wahakikishe kwamba wanaongezewa rasilimali watu ili waweze kufanya kazi yao vizuri na lile lengo la kuanzishwa kwao liwe limetimia kwa sababu wanakwenda kufanya kazi ambayo inaenda kusaidia Sekta ya Ujenzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo, ni namna ambavyo menejimenti yao, *flow* ya fedha na vitu kama hivyo nayo imekuwa ni changamoto katika usimamizi. Ombi letu ni kwamba kupitia Kamati tuliishauri na hapa ninaomba niongezee tena kwamba *TBA* wakiwezeshwa wanaweza kuwa wanafanya kazi nzuri sana na wakaingia kwenye soko la ushindani katika Sekta ya Ujenzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie tena kusema kwamba sisi wote ni Watanzania, tuendelee kwa pamoja kuwa kama Taifa moja, tofauti zetu za kimitazamo zisianze kutuingiza kwenye machafuko ambayo hayana sababu. Ninaamini kabisa wote tuna nia njema ya kuwatumikia Watanzania, lakini kila mmoja ana *views* zake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ombi langu ni hilo tu kama ambavyo leo asubuhi tumejadili baadhi ya wenzetu wanapotuchonganisha na Jumuiya za Kimataifa, nadhani inatuweka katika hali ambayo siyo salama sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maneno haya, naomba kuunga hoja mkono kwa asilimia mia moja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mtaturu. Mheshimiwa Vedasto Manyinyi.

**MHE. VEDASTUS M. MANYINYI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nami naomba nitumie nafasi hii kwanza kukushukuru kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia kwenye hotuba ya Kamati ya Miundombinu pamoja na Viwanda na Biashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi binafsi nawapongeza sana watu wa miundombinu na naipongeza sana Serikali kwa namna ilivyoweza kutoa fedha za kutosha kuhakikisha kwamba barabara na bandari zetu nyingi zinaweza kufanya kazi. Ndiyo maana kwa ushahidi ukiangalia katika bajeti iliyopita ilikuwa shilingi trilioni 4.2 lakini kwa mwaka huu tumeenda *almost 4.9.* Hongereni sana kwa hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na haya mafanikio makubwa ya Serikali lakini bado yapo mambo ya kimsingi ambayo yanahitaji kuangaliwa na hasa katika kipindi hiki. Wote tunatambua hiki ni kipindi ambacho katika nchi nzima mvua nyingi zimenyesha na kutokana na hali hiyo, barabara nyingi sasa zimeharibika kwa maana ya miundombinu. Kutokana na hali hiyo, hata zile barabara ambazo zilikuwa zimejengwa ambazo zilikuwa na hali nzuri zimeendelea kuharibika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kupata ufafanuzi kutoka kwa Mwenyekiti wa Kamati ya Miundombinu kwamba hivi wamejipangaje? Maana leo ukienda kwa mfano kule Musoma Jimboni kwangu nadhani mafuriko yameongoza kuliko mahali pengine popote pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda kwenye zile Kata kama za Nyakato, Bweri, Kitaji mpaka kwa bahati mbaya sana kumetokea maafa katika Jimbo langu kutokana na haya mafuriko, sasa ile miundombinu yote imeharibika. Napenda kufahamu Kamati ilijipangaje katika kusimamia Serikali kuhakikisha kwamba katika hiki kipindi kifupi tunarudisha ile miundombinu iliyokuwepo katika hali yake maana vinginevyo hali itakuwa mbaya zaidi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili ambalo ningependa kulielewa sambamba na hilo ni kwamba Serikali imekuwa na utaratibu mzuri wa kutenga fedha ambazo zinatengeneza hasa barabara katika kiwango cha lami. Fedha hizi zimekuwa zikipatikana aidha kutoka Serikalini na nyingine kupitia misaada kutoka maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matokeo yake kwenye zile barabara za Manispaa pamoja na Halmashauri zinazojengwa kwa kiwango cha lami, wote tunatambua kwamba Halmashauri zetu hazina uwezo wa kuendelea kuziimarisha. Sasa kutokana na hali hiyo, zile barabara za lami zinapokuwa zimeanza kuharibika maana yake zinaachiwa hata yale mashimo tunashindwa kuyaziba. Kwa hiyo, badala ya kutumia fedha kidogo kwenye kutengeneza zile barabara, matokeo yake zile barabara zinaendelea kuharibika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninayo mifano hai, siku moja kamati yako ikipata nafasi ikaja pale Musoma Mjini, kuna barabara kama ya Shabani, kama yale mashimo yangeweza kuzibwa ile barabara ingeendelea kupitika, lakini leo hii ukienda pale tunatamani tu bora ile lami yote iondolewe ibaki kuwa barabara ya vumbi kuliko ilivyokuwa barabara ya lami. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata ukienda kwenye ile barabara yetu ya Mkenda ambayo ndiyo kioo cha mjini, nayo imeanza kutoboka, Halmashauri haina uwezo wa kuziba yale mashimo. Matokeo yake baada ya miezi sita ile barabara yote itakuwa haipo na nguvu kubwa iliyotumika itakuwa imepotea bure. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vinginevyo, binafsi naishukuru Serikali kwa maana ya toka mwaka juzi 2018 tumeweza kupata fedha za kutosha. Maeneo mengi sasa pale Musoma Mjini tumejenga kwa kiwango cha lami. Ila kwa bahati mbaya sana, yale maeneo ambayo yapo usoni mwa Mji wa Musoma ndio yameendelea kuharibika. Kwa hiyo, ni imani yangu kwamba atakaposimama atapata nafasi ya kutuambia wamejipangaje kwenye fedha za kuboresha barabara zinazoharibika? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hilo, napenda kuchangia kuhusu uwanja wa ndege. Tunatambua Serikali imefanya juhudi kubwa na nzuri za kuendelea kuboresha viwanja vya ndege. Nimesikitika wakati nasoma hapa kwenye taarifa yake kwenye viwanja vya ndege ambavyo vinajengwa, Kiwanja cha Musoma hakimo, lakini kimekuwa kikisemwa na tuliona hata katika bajeti kwamba kitajengwa, lakini nimeanza kupata mashaka makubwa kwanza baada ya kuona hapa kwenye hii hotuba hakimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, nakumbuka toka mwaka jana mwanzoni uthamini ulifanyika. Kwa kawaida sisi wote tunatambua kwamba uthamini unachukua miezi sita baada ya hapo una-*expire*. Sasa madhara ambayo wale watu wa Musoma wameyapata toka uthamini ufanyike, zile nyumba zao sasa ziliwekwa X, hakuna watu, wapangaji wamekosekana wala hakuna shughuli zinazoendelea na wale watu bado hawajalipwa fidia. Halafu tunapokuja kwenye vitabu, hapaoneshi juhudi zozote za Serikali kwa ajili ya kujenga ule uwanja wa ndege

wa Musoma. Sasa hata tunapata tabu kubwa katika kusafiri, lazima tuje Mwanza ili tuweze kusafiri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda Mwenyekiti wa Kamati ya Miundombinu atakaposiamama atuambie, ule uwanja wa Musoma unajenga ama haujengwi? Kama haujengwi ni vizuri wakaenda wakafuta zile X na wakawaelimisha watu ili waweze kuendelea na maisha yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nigusie kidogo kwenye suala la bandari. Katika hili, mimi binafsi naiomba Kamati yako ipate nafasi wakati wa ziara za Kamati itembelee pale Mjini Musoma. Pale tunayo bandari ambayo nayo ilishakufa kwa sababu hakuna meli inakuja wala hakuna *activity* yoyote inayoendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, tulikua pale na mwalo wetu wa Mwigobero. Ule mwalo ndio watu wetu walikuwa wanafanya biashara ndogo ndogo, mitumbwi yote na samaki walikuwa wanagoa pale na biashara mbalimbali zilikuwa zinafanyika pale. Kilichotokea, watu wa bandari walikuja pale na wakatuambia wakati huo kwamba wanategemea watusaidie kuboresha ile bandari na wakasema wataiboresha bandari ifanane na ile Bandari ya Kirumba. Nasi tukafurahi tukaona kama ingeweza kutusaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hapo ile bandari wameichukua na hakuna kinachoendelea na wale watu wote waliokuwa wanafanya biashara pale wamefukuzwa…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa, malizia.

**MHE. VEDASTUS M. MANYINYI:** Kwa hiyo, naomba Kamati yako nayo ikiweza kupata nafasi ya kuja pale, itatusaidia kutatua hilo tatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nakushukuru sana, ahsanteni sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mathayo.

Waheshimiwa Wabunge, kwa asubuhi ya leo ndiyo tumefikia hapo. Niwataje Waheshimiwa ambao tutaanza nao jioni. Mheshimiwa Deogratius Ngalawa, Mheshimiwa Mbaraka Dau, Mheshimiwa Getere Boniphace, Mheshimiwa Kuchauka na Mheshimiwa Nsanzugwanko. Tutaendelea hivyo hivyo, wapo na wengine upande wangu wa kushoto, lakini tutafahamiana.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, naomba nisitishe shughuli za Bunge hadi saa 11.00 jioni.

*(Saa 7.00 Mchana Bunge lilisitishwa hadi saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 Jioni Bunge lilirudia)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Waheshimiwa Wabunge, nilikuwa nimewataja Waheshimiwa Wabunge tutakaoanza nao; Mheshimiwa Deogratias Ngalawa, Mheshimiwa Dau na Mheshimiwa Mwita Getere ajiandae.

**MHE. DEOGRATIAS F. NGALAWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuchangia mjadala unaoendelea wa Kamati ya Kudumu ya Miundobinu na ya Viwanda. Kwanza nipende kuipongeza Serikali kwa kazi nzuri na njema inayowafanyia Watanzania kwa sasa. Tumeona barabara zikiwa zinajengwa katika maeneo mbalimbali, tumeona minara ya simu, madaraja, bandari na vitu vingi. Hata hivyo, napenda kujikita kidogo kwenye taasisi ya *TANROADS.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *TANROADS* inafanya kazi nzuri na iliyotukuka lakini kuna baadhi ya maeneo kuna upungufu kidogo. Kuna maeneo ambayo ujenzi tayari unaendelea, lakini watu wa maeneo husika hawajalipwa fidia mpaka sasa. Mfano wa barabara ya kutoka Itoni – Njombe – Ludewa – Manda kile kipande cha Lusitu – Mawengi kimeanza kufanyiwa kazi na sasa hivi kilometa kama 12 tayari zimeshakamilika barabara ya zege, lakini watu wa maeneo ambako barabara inajengwa walio wengi bado hawajalipwa fidia kwenye maeneo yao hayo.

Kwa hiyo naiomba sasa Serikali iweze kulipa fidia kwenye barabara ambazo inazifanyia kazi, sio Ludewa tu, pia na maeneo mengine ya nchi ambako barabara zinajengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nilizungumzie kidogo Shirika la Posta; Shirika hili kweli limebeba madeni makubwa, kama ilivyozungumza Kamati, ya kulipa wale wafanyakazi waliokuwa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Mzigo ule ni mkubwa sana kwa Shirika la Posta. Tunaomba sasa Serikali iweze kuchukua huo mzigo na ikiwezekana iongezee mtaji shirika hili ili liweze kujiendesha kibiashara, ili liweze kujiendesha kwa kutumia *resources* ambazo inazitoa kuwalipa wale watu wengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekuwa tukifuatilia kwa kiasi kikubwa juu ya madeni haya ambayo Shirika la Posta linaidai Serikali kwa sababu waliopaswa kulipa zile pensheni wale watu wa Jumuiya, ni Serikali. Kwa hiyo posta inalipa kwa niaba ya Serikali, kwa hiyo matokeo yake sasa inaondoa mtaji wa uendeshaji inalipa yale madeni na Serikali imekuwa kidogo hailipi kwa wakati. Ndiyo maana unaona sasa hivi kuna madeni mengi sana Shirika la Posta inaidai Serikali. Kwa hiyo naomba na kushauri Serikali ichukue ule mzigo wa kuwalipa wale ile pensheni na pia iwaongezee mtaji ili iweze kwenda vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia niipongeze Serikali kwa maeneo ya mawasiliano. Mawasiliano ya simu kwenye maeneo mengi yamekuwa ni mazuri na tumeona, lakini upo upungufu. Imejengwa minara mingi sana, lakini kuna baadhi ya maeneo minara ile inachukua muda mrefu sana kuanza kuwashwa baada ya kuwa imejengwa. Mfano, maeneo ya kwetu kule ipo minara kadhaa ambayo tayari imeshajengwa, lakini mpaka sasa bado haijawashwa. Kwa hiyo niiombe Serikali iiwashe minara ile na tuone namna gani ya kuweza kuisadia hii *UCSAF* kuipa hela za ku-*operate* ili Watanzania walio wengi waweze kupata mawasiliano ya uhakika na yenye tija.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije kwenye Kamati ya Viwanda; kuna hili suala la Mchuchuma na Liganga, suala hili limeshakuwa ni la muda mrefu na tumesema kwamba miradi hii ni miradi kielelezo, lakini ukijaribu kufuatilia na kuiangalia hata kwenye taarifa yenyewe ya Kamati imepewa *weight* ndogo sana. Miradi kielelezo ninavyofahamu mimi ndiyo ingekuwa chachu ya kuchochea uchumi wa nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii tunaagiza chuma kutoka nje ya nchi wakati chuma Liganga kipo. Naamini tungetengeneza *concentration* kubwa kwenye eneo hilo, tungeweza kupata *impact* kubwa ya kiuchumi kwenye eneo letu. Ukijaribu kuangalia mradi wa Mchuchuma na Liganga, tafiti zinaonesha kwamba zinaajiri Watanzania wasiopungua 32,000, lakini *multiplier effect* yake inaenda mpaka kwa Watanzania 300,000. Sasa ajira za watu 300,000 ni ajira kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo kuna haja sasa pamoja na kwamba wanapitia ule mkataba lakini muda umekuwa ni mrefu sana. Yaani kuanzia tunaingia Bungeni hapa toka 2016 ule mkataba unaendelea kupitiwa, umepitiwa 2016, ukapitiwa 2017, 2018, 2019 mpaka leo 2020 bado tunazungumzia tu kupitia mkataba. Nadhani sasa ufike wakati hili suala liishe ili tujue sasa hatma ya miradi hii ya Mchuchuma na Liganga imefikia wapi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi kwa watu wa maeneo ya kusini na Tanzania kwa ujumla tunaona kabisa miradi ile ni miradi yenye tija, kwa sababu leo hii tunaagiza chuma kutoka nje wakati chuma tunacho. Miradi hii ikianza bado leo hii tunazungumzia suala la viwanda, viwanda ni umeme, viwanda ni nishati. Tunao pale umeme wa megawati 16 pale Mchuchuma, makaa yale yamekaa tu. Kwa hiyo, naomba Serikali iipe uzito unaostahili hii Miradi ya Mchuchuma na Liganga, la sivyo kila siku tutakuwa tunazungumzia Mchuchuma na Liganga na inawekwa kwenye bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu pia kuna fidia ya watu ambao wamepisha ile miradi kwenye maeneo yale ya Mchuchuma na Liganga na inawekwa kwenye bajeti kila mwaka. Mwaka huu 2019/2020 zimewekwa bilioni tano kwa watu wa Liganga pale Mundindi na imewekwa bilioni tano kwa watu wa Mchuchuma pale Nkomang'ombe, lakini hatuoni jitihada ambazo zinafanyika kuwalipa fidia watu hawa kwa sababu hizi zimeshaanza kutengwa leo ni mwaka wa tatu lakini hawajalipwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niiombe sasa Serikali iichukue yenyewe, kwa sababu mwanzo hii fidia ilisemekana kwamba italipwa na mbia, lakini sasa maadam wameingia kwenye eneo la majadiliano ya kimkataba, fidia hii ichukuliwe na Serikali yenyewe ili iweze kulipwa tuondokane na malalamiko ya wananchi ambao wamepisha hiyo miradi kwenye maeneo yale husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo kuna hii pia la reli ya kutoka Mtwara kuja Songea - Mbambabay na matawi yake ya Mchuchuma na Liganga, sijajua mpaka sasa wamefikia wapi na sijaiona kwenye ripoti. Kwenye ripoti humu sijaiona kama imezungumziwa chochote lakini nakumbuka kwenye bajeti ya mwaka jana wamesema kuna mbia amepatikana na wanaendelea na mazungumzo. Kwa hiyo naiomba Serikali ije sasa na maelezo tuone kwamba reli ya Mchuchuma imefikia wapi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nikushukuru kwa kunipa nafasi hii. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Ngalawa kwa mchango wako mzuri na ushauri mzuri. Tunaendelea na Mheshimiwa Mbaraka Dau.

**MHE. MBARAKA K. DAU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa fursa hii. Nami nianze kwa kumshukuru sana Mwenyezi Mungu aliyetujalia neema kubwa kubwa na neema ndogo ndogo, leo tumeweza kukutana hapa kujadili masuala yanayohusu nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwashukuru Wenyeviti wa Kamati zote mbili kwa taarifa nzuri kabisa ambazo zimesheheni ushauri na maazimio mazuri sana. Naamini kama tutayafanyia kazi basi tutaona nchi yetu hii ikisonga mbele zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitazungumzia Kamati zote mbili kwa pamoja. Kwanza nitaanza na Kamati ya Miundombinu; umefika wakati sasa namna ambavyo tunaendea ujenzi wa miundombinu yetu ya nchi iwe zaidi ya kimkakati na kwa nini ninasema hivyo?

Nasema hivyo kwa sababu kuna baadhi ya miundombinu ambayo ukienda kuijenga sio miundombinu ambayo inakuwa ni mzigo sana kwa Serikali bali *in the long run* miundombinu ile inakuwa na tija na yenye kuleta fedha nyingi na mapato mengi kwa Taifa na nitatolea mfano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natokea katika Kisiwa cha Mafia, kisiwa hiki kinapata wastani wa watalii kama 6,000 hivi mpaka 7,000 kwa mwaka mzima, lakini Kisiwa cha Zanzibar kwa maana ya Unguja na Pemba kwa umoja wao wanapata watalii mpaka 600,000 kwa mwaka, utaona tofauti hizo. Sasa sizungumzi kwa maana ya ku-*compete,* nazungumza kwa maana ya ku-*complement each other.* Kwa nini Mafia inakuwa na watalii wachache, ni kwa sababu miundombinu yake haiingiliki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ndiyo hicho ninachokisema kwamba kama ujenzi wa miundombinu utakwenda kimkakati zaidi kwa maana ya kufungua fursa zaidi za kiutalii kwa maeneo kama haya ya Mafia na maeneo mengine tunaamini kabisa badala ya kuwa ni mzigo kwa Serikali *in the long run* kutakuwa na mapato mengi sana kwa Serikali na vitu vyenyewe nitavielezea kwa muhtasari tu kwa sababu muda sio rafiki sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kwanza ni namna ya *accessibility* ya kuingia Mafia. Kwa sasa namna pekee salama na ya uhakika ni usafiri wa ndege ambao gharama yake ni kubwa sana, *flight* ya nusu saa inagharimu Sh.167,000. Kwa mwananchi wa kawaida ambaye uwezo wake ni mdogo, huo ni mzigo mkubwa sana. Sasa *alternative* yake ni kupita baharini ambako sasa kule baharini hali ya miundombinu sio nzuri. Vyombo vya usafiri ni vya magogo, havipo salama na kipindi kama hiki cha upepo mkali ambao upepo unaitwa upepo wa kaskazi inakuwa ni shida, inabidi wazuiwe abiria wasisafiri kwa muda wa wiki, wanakaa wanarundikana na inaleta shida kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa namna ya kipekee nimshukuru sana Mheshimiwa Rais. Mafia tumepatiwa gati pale, Gati la Nyamisati, gati la kisasa kabisa, zuri kabisa, kwamba walau sasa hata kama chombo cha usafiri cha kisasa kitakapokuja kinao uwezo sasa wa ku-*dock* mahali na kupakia na kushusha abiria pamoja na mizigo yao kwa salama kuliko ilivyokuwa kabla ya hapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukamilifu wa Gati lile la Nyamisati utakuwa hauna maana sana kama hatutakuwa na usafiri wa boti ya kisasa baina ya Nyamisati na Kilindoni Mafia. Kwa nukta hii pia niendelee kumshukuru sana Mheshimiwa Rais; kwenye bajeti ya mwaka huu tumewekewa shilingi bilioni 5.2 kwa ajili ya kujenga boti ya kisasa ambayo itakamilika ndani ya muda mfupi ujao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ukichanganya haya, ule mzigo ambao pengine wasafiri walikuwa wanaubeba mkubwa sana wa ndege na watalii wengi kwao wao kupanda boti ni sehemu kama ya *adventure* ya kwenda mahali, tunaamini sana utafungua sasa fursa nyingi zaidi kwa maana ya kwamba watalii watakuja wengi sana kwenda kutembelea Kisiwa cha Mafia baadaye na Serikali nayo itapata mapato mengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika eneo hilo hilo, miundombinu ya uwanja wa ndege; pale Mafia kuna uwanja wa ndege ambao *runway* yake ni urefu wa kilometa 1.6. Kwa urefu wa kilometa 1.6, ndege ambazo zinaweza zikatua na kuruka pale ni aina ya *Fokker* pekee.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa kuwa tunataka utalii na baadhi ya watalii wanapenda zaidi wawe na *direct flight* kutoka wanakotoka, sasa ndege kubwa kama hizi za *Boeing 737* na nyingine haziwezi kuja kutua moja kwa moja mpaka Mafia kwa sababu uwanja wa ndege una urefu wa kilometa 1.6 na unahitaji uwanja wa ndege wenye urefu wa angalau kilometa tatu na kuendelea ili kuweza ku-*accommodate* ndege kubwa zinazokuja moja kwa moja kutoka nchi za magharibi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ombi langu na ni ushauri kwa Mwenyekiti makini kabisa na ni miongoni mwa *the finest brains* za Wenyeviti wa Kamati, Mheshimiwa Kakoso; atusaidie pale Mafia sasa Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano iweze ku-*extend* ile *runway* kutoka kilometa 1.6 kwenda kilometa 3.0 ili kuweza kuruhusu ndege kubwa kutua pale na kuruka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hilo litakwenda sambamba na ujenzi wa *terminal building;* tuna ka-*terminal building* pale kadogo sana ambako hata ndege aina hizi za *caravan* ambazo zinachukua abiria 12 na 13 zikitua mbili tu mnakuwa mmesharundikana pale *passenger's lounge*. Kwa hiyo tunaomba sana upanuzi wa uwanja wa ndege huu uende sambamba na ongezeko la ujenzi wa *terminal building.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kisiwa cha Mafia kama nilivyotangulia kusema ni Kisiwa cha kitalii na utalii kwa sasa, kwa sababu kisiwa kimegawanyika katika maeneo makubwa mawili; eneo la kaskazini na eneo la kusini. Hili eneo la kusini ambapo ndipo kiwanja cha ndege kipo na shughuli za kiutawala kwa maana ya halmashauri na ofisi nyingine za Kiserikali zipo, pale miundombinu iko sawa kwa sababu watalii wakitua wanakwenda kwenye mahoteli moja kwa moja. Hata hivyo, kutoka pale Makao Makuu ya Wilaya kwenda moja kwa moja mpaka kaskazini kule kwenye *light house* ni kama kilometa 55 na ndiyo kabarabara kenyewe kamoja hakohako tu kama roho. Mheshimiwa Waziri Kwandikwa, mjukuu wangu, hebu kwanza watusaidie pale Mafia watumalizie hizi kilometa 55, sisi tena tunakuwa tumeshaagana na wao, tukiomba tutaomba mambo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo naomba kwa namna ya kipekee sana, tukimaliza ujenzi wa barabara hii ya kilometa 55, tutafungua na fursa za kiutalii upande wa kaskazini mwa Mafia ambapo nako pia kuna fukwe nzuri na kuna maeneo mengi sana ambapo mahoteli na ma-*lodge* yanaweza yakajengwa na kuweza kupata watalii wengi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuna suala la mawasiliano; namshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri, *Engineer* Nditiye, alishafika pale Mafia na akaona changamoto zetu. Sisi kule zao letu kubwa ni zao la nazi, kwa hiyo minara ya simu inapata kidogo *obstacles* kwenye kurusha *signals* zake kwa sababu kunahitaji minara mingi zaidi kutokana na uwepo wa minazi mingi. Sasa maeneo mengi ya vijiji vya Mafia yanakosa mawasiliano ya simu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana Wizara ya Mawasiliano tuangalie kwa sababu eneo linapokuwa tena la kitalii na watalii siku hizi dunia imekuwa ndogo, imekuwa kijiji, wanataka zaidi kufanya mawasiliano ya intaneti, ya simu na vitu vingine, ingependeza zaidi tukawa na mawasiliano ya uhakika zaidi. Najua hilo lipo katika mikono salama kwa sababu watu wa Mfuko ule wa Mawasiliano kwa Wote na Mheshimiwa Naibu Waziri alinihakikishia kwamba watalifanyia kazi hilo ili kuhakikisha kwamba mambo yanakwenda vizuri pale Kisiwani Mafia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa harakaharaka tu nizungumzie kidogo na Wizara…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Dau kwa mchango wako mzuri sana na ushauri, kwa hiyo muda wetu ndiyo huo, tunakushukuru sana.

**MHE. MBARAKA K. DAU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Getere.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hizi Kamati mbili na niwapongeze Wenyeviti wote wa Kamati. Nianze kwa kutazama tu jambo la mazingira na niishauri sasa Serikali yetu huko tunakokwenda sasa kuwa na Wizara maalum ya Mazingira ambapo nchi zilizoendelea sasa zina Wizara hii ya mazingira na ndiyo Wizara maarufu katika nchi zote za Ulaya na nchi zingine, kwa mfano Brazil ndiyo Wizara maarufu sana; ukienda Kenya ndiyo Wizara maarufu sana ya mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivyo kwa sababu hili tunaloliona leo ambapo tunazungumza habari ya mafuriko au habari ya kiangazi ni matokeo ya *climatic change,* ni *climatic crisis* ambazo tunaziona sasa hivi hapa na kwa bahati mbaya kitengo hiki cha mazingira hakiko kwenye viwanda, kinazungumziwa kama kitengo tu. Hata ukitazama hapa *results* zake ni kama vile watu wa ushauri, lakini huko kwenye maeneo ya nchi zote duniani hata Tanzania hapa kilitakiwa kuwa kitengo cha kuamua nini kifanyike katika nchi yetu kwa sababu nchi yetu sasa tunakokwenda suala la mazingira ni muhimu sana kuwepo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ukiangalia katika maeneo kama ya Bunda kwenye Jimbo langu barabara ya Maliwanda, Stephen Wasira yote imekatika, barabara ya Kandege Tingilima haipo, barabara ya Sarawe, Kambubu haipo, Sarawe Bukama, barabara ya Kambubu Sarawe nayo haipo, barabara ya Nyangere Unyali haipo, barabara ya Nyabuzume Kiloleli haipo, barabara ya Tingirima na Tiling'ati na Nyamso haipo, zote zimekatika; na hii yote ni kutokana na kwamba maeneo maalum ya hizo barabara, aidha watu wamelima mpaka kwenye barabara au watu wameng'oa viti yote milimani au mabonde yote yameziba kwa hiyo hakuna mahali ambapo watu wanaweza kupita kwenye maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nilikuwa nafikiri kwamba ni vizuri sasa tunakokwenda hii Wizara ya Mazingira tukaipa kipaumbele sana kwenye mambo kama haya ili yaweze kutusaidia huku tunakokwenda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie uwanja wa Musoma, uwanja wa ndege Musoma Mkoa wa Mara; Mheshimiwa Rais alifanya ziara toka wa tarehe 4, mpaka tarehe 8 Septemba, 2018 na akazungumza sana juu ya ujenzi wa uwanja wamusoma, lakini mpaka leo hatua hazijaenda vizuri na uwanja haujajengwa tunasikia tu *ten million* imetolewa uthamini yakinifu umefanyika lakini hakuna kitu kinachoendelea pale. Tunazungumza habari ya reli ya kutoka Tanga, Moshi Arusha, Musoma kila mwaka tunaiona kwenye bajeti hapa lakini mpaka leo toka Mwalimu Nyerere amekuwepo mpaka leo sisi hatujawahi gari moshi linafika kwenye Mkoa wa Mara. Kwa hiyo, nafiri kwamba ni wakati muafaka sasa wakati tunashughulika na maendeleo haya yaende kwenye Mkoa wa Mara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kusoma taarifa hapa nimeona kuna taarifa ya matrekta yaliyokuwa yananunulia na Serikali kupitia shirika letu la Suma JKT na Kampuni ya US, Russi ya Poland ambayo inaonekana asilimia 65 hela zimetolewa kwenda kununua matrekta, na matrekta 825 ndiyo yamefika kati ya 2,400 yaliyokuwa yanatakiwa kufika hapo. Sasa najiuliza katika haya matrekta yaliyokuja ni asilimia 34 *point* je, matrekta yaliyobaki hela zake zimelipwa au hazikulipwa? Na hiyo asilimia 65 ya hela zilizotoka zimekidhi vigezo matrekta yaliyokuja au

kuna mengine hayajaja, na mbaya zaidi wanasema katika shirika hilo ambalo tumefanya makubaliano nalo linaelekea kufilisika sasa najiuliza hizi hela za wakulima ambazo tunatakiwa kuleta matrekta kuwasaidia wakulima zitapotelea humo au hatua gani itachukuliwa. kwa hiyo nilikuwa nashauri Serikali katika hili uweze kifanya vitu vya haraka zaidi kwenda kuona kinachoweza kutokea katika suala hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Jimbo la Bunda kuna barabara ya inatoka Makutano Butiama, Sanzati barabara sasa ina miaka nane toka inatengenezwa na kila mwaka wanapewa muda wa kumaliza lakini wameshindwa kumaliza naomba Wizara inayohuka Wizara ya Miundombinu ichuke hatua kwenye barabara ya Makutano Sanzati ambayo inatengenezwa kwa miaka 6 sasa, kuna barabara ya kutoka Nyamswa kwenda Bunda barabara ya lami, Mheshimiwa Rais amefika pale tarehe 6 akasema Mkandarasi aanze mara moja hatujamuona mpaka leo, kuna barabara ya kutoka Sanzati kwenda Nata Mgumu, tumetangaziwa kuwa Mkandarasi yuko barabarani hajafika mpaka leo. Kwa hiyo, tunaomba Wizara inayohusika ili iweze kuchukua hatua hizo za kuweka Wakandarasi kwenye barabara ambazo zinaweka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka nizungumze hayo kwenye Jimbo langu, lakini nilishukuru Bunge kwa ujumla kwa hatua ambayo ilikuwa inazungumziwa asubuhi, kwamba katika maisha yetu ya kitanzania na katika watanzania wote mambo muhimu ya kuzingatia ni usalama wa nchi yetu na maendeleo ya nchi yetu. Kwa yoyote yule ambaye anayumbisha nchi yetu na ikiuletea giza kwenye mambo yake ya kule anakotaka yeye hatua kali zichukuliwe dhidi yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna sakata linaendelea huku Marekani la *impeachment trial,* watu wenginine wanafikiri kwamba pengine hilo linatokana na sijui Ukraine au kuzungumza jambo fulani lakini ukweli ni kwamba kwa mara ya kwanza katika Marekani uchaguzi wao 2016 uliingiliwa na Urusi, na wanajiuliza mara mbili mbili waliingiaje mpaka leo, nani aliwaruhusu kuingia lakini leo Marekani wanazungumza kuingiliwa uchaguzi wao, lakini wao toka mwaka 1948 wamekuwa wakiingia nchini zingine uchaguzi kwa mfano uchaguzi wa Italia wa mwaka 1948 wameingia na kuweka na mgombea wao, uchaguzi wa Israel, mwaka 1996 Criton amekwenda pale ameweka mtu wake kuwa Waziri wa Israel.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunaomba huko tunakokwenda nchi yetu ijue kwamba wakoloni hawatakuja hapa, lakini mipango Marais wanaowataka vibeberu wao itakuwepo. Kwa hiyo tuchukue hatua za kutosha kwenye jambo hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Getere, nimuite Mheshimiwa Kuchauka Zuberi na Mheshimiwa Mwilima ajiandae.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi niweze kuchangia hutoba hizi za Kamati mbili. Awali ya yote kama Mjumbe wa Kamati ya Miundombinu nataka nichukue nafasi hii kumpongeza Mwenyekiti wetu wa Kamati kwa kuiongoza vyema Kamati ya Miundombinu Kamati ambayo inaongoza kwa upana kwa maana ya sekta nyingi tunazozisimamia, lakini kwa usimamizi wake mahili ndiyo tumeweza kufanikiwa kuleta haya mafanikio ambayo tunayaona leo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Rais ambaye anaposema kwamba anataka kuelekea kwenye nchi ya viwanda ni kwamba alijua jambo kubwa sana ambalo anatakiwa kulifanya ni

kuuwisha miundombinu na ndiyo maana amewekeza sana kwenye upande wa miundombinu hakuna mtu ambaye hajui ni kwa namna gani nchi yetu sasa hivi kwa upande wa miundombinu hasa ya barabara, viwanja vya ndege, bandari zote hizi zimeenda kufanyiwa kazi na kazi yakiufanisi kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukizungumzia hata huko ziwa Victoria ziko meli mpya zimejengwa na zile za zamani zimekarabatiwa. Lakini hii yote ni katika kuimarisha miundombinu, kuimarisha miundombinu huko ambako kutaelekea kuimarisha uchumi wa Taifa letu. Juhudi hizi kubwa ambazo zinafanya na Mheshimiwa Rais na wananchi wote tunamuunga mkono zipo kasoro mbalimbali ambazo tunakiwa tuzichangie na tuziseme ili Serikali nao waweze kuchukue hili waweze kulifanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, liko suala limezungumzwa na Mheshimiwa Mtaturu suala la *TPA*, kwa kweli Mheshimiwa Rais amewekeza sana *TPA*, ameingiza fedha nyingi sana *TPA* kwa maana ya kuwataka kuimarisha bandari zetu ili hatimaye tuweze kuinua uchumi wetu. Vilevile aliendа mbali sana akaonda ukaletwa Muswada, Serikalini tukaletwa Muswada tukaunda hii Taasisi ya *TASAC* kwa nia hiyo hiyo ya kuimarisha au kuondoa sintofahamu iliyokuwa inapatika kule bandarini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, chombo hiki *TASAC* tumekiunda kazi zinazofanywa na *TASAC* sasahivi ni kazi ambazo zilikuwa zinafanywa na watu zaidi ya 2000 huko nyuma, wdau mbalimbali wa sehemu ya bandari. Jambo hili limeipa ugumu sana *TASAC* kiasi kwamba sasahivi tumezua tatizo jingine kubwa zaidi kwenye sekta ya bandari; tatizo la ucheleweshaji wa mizigo bandarini kama ambavyo aliyetangulia kusema ameshalisema kwamba tayari tumeanza kupoteza wateja wadau mbalimbali wameaza kuamisha mizigo yao kutoka kwenye bandari yetu lakini kikubwa zaidi siyo utendaji mbaya wala uwe sifa ya zaidi ulikuwepo wizi na vitu vingine vya ulaghai wizi mdogo mdogo. Sasa hivi wizi kule hamna wafanyakazi wa bandari, lakini tatizo kubwa linakuwa *manpower* ya *TASAC* haiwezi kumudu mzigo uliko pale bandarini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, na naishauri Serikali ukisikia watu wanasema sana ujue kuna jambo hata kwenye hali ya kawaida hapa ukienda barabara ukikuta watoto wanacheza kwenye jalala hebu chukua muda kaa uwasikilize, wasome utajifunza tu. Sasa hizi kilele zinazopigwa hizi pamoja na kwamba wale wanaopiga kelele huko nyuma walishachafuka wanamajina mbalimbali, lakini hebu tuwaangalie hebu twende ndani tuangalie kuna nini kabla hatujaingia kwenye tope zaidi, niliona niliongele hili ili serikali nao mlichukue kwenye Kamati tumelijadili sana, lakini naomba kwa usisitizotu naomba *TASAC* bandari tuangalie utendaji wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile ushauri wangu mwingine kwa upande wa Serikali suala la upembuzi yakinifu wa miundombinu mbalimbalui. Ushauri wangu suala la upembuzi yanikifu uendane na uhalisia, tunayo mikiradi mingi ya muda mrefu imeshafanyiwa upembuzi yakinifu lakini kuna miradi mengine leo inafanyiwa upembuzi yakinifu kabla ile miradi ambayo tumefanya umbembuzi yakinifu mwanzo bado haijakamilika. Kwa mfano barabara ya Nachingwea kwenda Masasi kilometa 45 imefanyiwa upembuzi yakinifu mwaka 2014, lakini barabara ile mpaka leo haijapatiwa fedha za kujenga, tangu 2014 mpaka leo 2020 tumeshafanya upembuzi yakinifu barabara ngapi kabla ya ile; mtaona kwamba bado tulikuwa tunaendelea kufanya umbembuzi yakinifu wakati barabara ambazo tayari tulishazifanyia upembezi yakinifu bado hatujazipatia fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ushauri wangu kabla hatujaanzisha miradi mingine hebu tuangalie ile miradi ambayo tayari tumeshafanyiwa upembuzi yakinifu inapatiwa fedha na hatimaye kujengwa kiwango cha lami. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye bajeti iliyopita mfano mwingine kwenye bajeti iliyopita kwenye Jimbo langu la Liwale pale kuna barabara yetu ile Nangurukuru Liwale imeshatolewa fedha za umbembuzi yakinifu, lakini matarajio wananchi wetu tukiwaambia kwamba barabara yetu tayari imeshafanyiwa upembuzi yakinifu ni mategemeo yao kwamba baada ya mwaka mmoja mwaka wa pili, barabara hiyo itaanza kujengwa kwa kiwango cha lami.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tunapowaridhisha wananchi kwamba barabara hii tumeshafanyia upembuzi yakinifu halafu tukachukua miaka 10 bado haijajengwa tunaleta sintofahamu nyingine kwa hawa wananchi ambao tunakwenda kuwasimamia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo jingine naomba niliongelee kuhusu TAZARA, Sheria ya uundwaji wa TAZARA wakati ule TAZARA inaundwa wa Zambia walikuwa wanaihitaji sana, ukiangalia hali ya jiografia kule Msumbiji na Malawi ilikuwa hakuko shwari. Kwa hiyo, TAZARA walikuwa wanahitaji sana hii reli ya TAZARA, lakini miaka hii ya karibuni naomba niiambie Serikali…

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Zuberi

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwani dakika ngapi?

**MWENYEKITI:** Muda wetu ndiyo huo.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono mia kwa mia. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, Mheshimiwa Sakaya Magdalena, Mheshimiwa wewe ni nani hapo Mheshimiwa Susani Kiwanga, basi kama hutaki napeleka kwa mwingine, haya.

**MHE. SUSAN L. KIWANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi hii nichangie kwenye hoja hizi mbili, lakini sana sana nitajikita kwenye hoja ya Kamati ya Miundombinu, Wizara ya Miundombinu kwa kuwa ni Mjumbe vilevile wa hiyo Kamati. Kwa hiyo tunafanya pamoja na Wizara pamoja na mashirika yake yote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kuzungumzia suala la TAZARA Serikali inaendelea kuwalipa watumishi mishahara, bado mazungumzo yanaendelea kufanyika kati ya nchi mbili na tuliishauri Serikali kwamba kuna haja sasa ya kukaa na kuzungumza na wenzetu wa Zambia ili tuona namna gani tunagawana tutenganishe hivi vitu Tanzania tushughulikie upande wa Tanzania na Zambia upande wa Zambia; kwa sababu kutokufanya hivyo tunaona kuna mdororo mkubwa wa TAZARA na TAZARA ni mwokozi kwa kuokoa barabara zetu na kupata mizigo mingi inayotoka katika nchi mbalimbali kwenda na kuja. Kwa hiyo nashukuru kwamba mambo haya Tanzania yameisha sasa tunawangoja ndugu zetu wa Zambia nao wafanye halafu baade mambo haya haya yatakuja kuingia kwenye Mabunge yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na Serikali kulipa watumishi mpaka leo wa TAZARA mishahara, kuna tatizo kubwa la wastaafu wa TAZARA. Kuna wale wastaafu walioenda Mahakamani na wameshinda kesi kama 270 Hazina inaendelea kuwalipa kidogo kidogo ingawaje siyo utarabu, lakini sasa sijui inategemea nani anafuatilia zaidi kwa sababu wameshashinda kesi wameambiwa walipwe lakini inaenda kidogo kidogo sana kiasi kwamba wengine wanakata tamaa na wanakufa hawajapata hiyo hela.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naiomba Serikali naishauri Serikali hebu iwalipe hawa wastaafu walioitumikia hiyo reli kwa moyo mmoja acheni kulipa kidogo kidogo, ukiachilia hawa 270 bahati nzuri kuna taarifa kwenye Kamati tuliiomba ya Hazina, na kweli wameileta inawatumishi wengine wastaafu 1,172, hao bado wanataabika wako mtaani bado kuna kizungumkuti mkubwa hawa wanaolipwa walioshinda Mahakamani inaonekana wale waliostaafishwa kwa lazima miaka 55 badala ya 60 wameshinda kesi na wanalipwa hiyo hela, lakini wale 1172 TAZARA hiyo hiyo kwa sababu hawajaenda Mahakamani wameambiwa hawana stahili ya kulipwa hilo hela na walistaafu miaka 55 wakati Sheria ilikuwa inasema kwa lazima miaka 60. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hiyo ni shida kubwa hivi kwanini hawa watu wanateseka nchi hii, kuna mlolongo mkubwa nilivyopitia ile taarifa ya Hazina kwa kweli inaenda mbele na kurudi nyuma, hebu waurumieni hawa waliofanya kazi Mainjinia, nani wataalam mbalimbali watu wa kawaida, 1,172 siyo watu wachache hao, labda deni lao limekuwa kubwa sana wanawaambia hawa hawana haki wakitaka waende Mahakamani yaani kuna taarifa kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, basi Serikali iitishe mkutano wa pamoja na hawa wananchi hao wastaafu basi wawaambie maana wanateseka wengine kutoka Mlimba wanaitwa Dar es Salam njooni msikie majibu wanaangaika wanakopa wanazani watapata yaani hali ni mbaya kwa wastaafu hawa 1,172. Hebu Serikali oneni uchungu hawa watu wanazidi kuhangaika wazidi kubwa wanazidi kuumia muwape jibu la moja kwa moja siyo la kwenye makaratasi tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongezee masuala ya *NIDA*, *NIDA* tuliwaita juzi kwenye Kamati yetu *NIDA* ingawaje utashangaa mama Kiwanga kwanini anaongelea *NIDA*, na *TCRA* ni kama uji na mgonjwa *TCRA* sisi tunasimamia kama Kamati ya Miundombinu tumewaita NIDA wanachikisema ni tofauti kabisa kwenye *ground* mimi ni Mbunge wa Mlimba NIDA mpaka tarehe ya Rais aliyotangaza tarehe 20 NIDA wako pale Ifakara tu Mlimba wamegusa Kata 5 tu Kata nyingine zote hawajakanyaga NIDA, nimemuuliza mtaalam wa *NIDA* pale Kilombero anasema tumepeleka bajeti Makau Makuu lakini hiyo bajeti haijaja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo *NIDA* wanamatatizo makubwa ya pesa wanawafungia watu simu zao wakati hawapeleki bajeti watu wakasajiliwe. Sasa nataka kauli ya Serikali wanachi ya Vijijini kama hapa Mjini watu wanapanga foleni tunawaona *NIDA* wapo watu wanaenda kusajili, je huko Vijijini hali ni mbaya *NIDA* hawapo, hela hamna mitambo haiendi kwa wananchi leo watu wanateseka na simu ni kila kitu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa tunataka majibu ya Serikali kwanini wanawafanyia hivi watu wa Vijijini hususani watu wa Jimbo la Mlimba walifika tu pale makutano Kata ya Chita kwa uchache hawajafika Ching'anda, Kalengakero, Mlimba, Kamwene, Utengule mpaka Tanganyika Masagati mpaka Uchindile NIDA mtafika lini kusajili huko hivyo vitambulisho vya watu mmeshawafungia simu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna kikwazo naomba kuishauri Serikali sharti mojawapo ili usajiliwe unatakiwa uwe na cheti za kuzaliwa au cheti cha darasa saba kule kwangu wameamia wengi kutoka katika Tanzania hii hasa kwenye Kanda ya Ziwa wapo kule Vijijini wale watu wamezaliwa huko huko Vijini kabisa hamna hospitali, wale watu hawajasoma kama unavyojua tena wafugaji wameshakuwa wakubwa hawana cheti cha kuzali wala cha darasa saba ina maana hawa watu hawatasajiliwa mpaka milele nchini nchi hii. Hebu Serikali kaeni tuwaangalie hawa watu ambao katika hizo sifa mlizoweka hawatasajiliwa milele, je, mtawahesabu ni watanzania ama ni wakimbizi hebu naomba make mfikirie namna ya kuwasaidia hawa watu katika Vijiji hasa Jimbo la Mlimba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu *TASAC* tulipitisha Sheria hapa lakini mwaka jana 2019 wameleta *amendments* za Sheria mbalimbali zile, yaani ukishasikia Sheria mbalimbali zinakuja hapa ujue hapa changalamacho kwenye Kamati haiji tena ikija hapa inapishwa haraka haraka kumbe kwenye *TASAC* pamoja na kuwa tulipitisha Sheria mama kwamba *TASAC* itashughulikia masuala ya vitu ambavyo vya usalama wa nchi matokeo yake zile Sheria tulizopitisha za nyongeza 2019 wamesema *inclusive* ina maana bidhaa zote zinazopita bandarini *TASAC* watafanya *talling* hiyo ni hatari kwa sababu wanauwa kabisa suala la ubinafsishaji halitakuwa tena na mtu anayefanya *talling* kule bandarini kuna mlundikano wa mizigo kule bandarini..

**MWENYEKITI:** Ngoja taarifa Mheshimiwa Charles

**T A A R I F A**

**MHE. CHARLES M. KITWANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, msemaji anayezungumza anasema hawa watu hawajasoma, nampa taarifa tu kwamba hawajasoma lakini uzalishaji wanaweza.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kiwanga unapokea taarifa hiyo?

**MHE. SUSAN L. KIWANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo ninaowatetea kwamba hawana cheti cha Darasa la Saba, hawana cheti cha kuzaliwa. Wamezaliwa vijijini, wamekulia machungani. Hawajui kusoma wala kuandika, kwa hiyo, hawatasajiliwa kwa sababu wamekosa sifa, hasa Wasukuma. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeenda kwenye *TASAC*…

**MBUNGE FULANI:** Hao ndiyo *tax payers* hao!

**MHE. SUSAN L. KIWANGA:** …matokeo yake kwa zile sheria tulizopitisha mwaka jana, 2019 za kuongezea ile sheria kubwa ya *TASAC,* imetokea hivi; wenye viwanda sasa, wafanyabiashara wakubwa wanahama kwa sababu wana gharama kubwa ya *storage*. Wale watu ambao wanaingiza mafuta labda, mtu anakaa bandarini mpaka miezi kadhaa hajatoa mizigo yake; watu wa madini wanaagiza vitu vya *spare* kwenye migodi, wanakaa siku kadhaa, meli zinakaa hapo; watu wanaona hiyo haiwezekani, wanaondoka…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana kwa mchango wako. *(Makofi)*

**MHE. SUSAN L. KIWANGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, bandari inakwenda kufa. Hizi ni dakika 10!

**MBUNGE FULANI:** Wewe unayeongea huwezi kujua.

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

Mheshimiwa Frank Mwakajoka dakika tano na Mheshimiwa Lema ajiandae.

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi nami niweze kutoa mchango wangu siku ya leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuko Bungeni kama Wabunge, nia na madhumuni ni kuishauri sana Serikali. Tunavyozungumza sisi upande wa Upinzani tuchukuliwe kama ni Wabunge ambao tuna haki na tunaishauri Serikali kama ambavyo Wabunge wa Chama cha Mapinduzi wanavyoweza kuishauri Serikali na kazi yetu kubwa ni kuangalia *gaps* ambazo mnashindwa kuziba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ziko kero nyingi sana za wafanyabiashara ambazo mwaka 2018/2019 Serikali ya Chama cha Mapinduzi ndani ya Bunge hili waliahidi kupunguza kero mbalimbali kwa wafanyabiashara. Huwezi kuamini, mpaka sasa hivi kwenye nchi hii bado kero za wafanyabiashara hazijatatuliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka jana 2019 wakati wa bajeti hapa ilionyesha kwamba kuna kodi karibu 54 ambazo zilitolewa. Sielewi kodi hizi ambazo zilitolewa kama kweli Serikali ilifanya utafiti na ikakutana na wafanyabiashara, kama kweli ndiyo zilikuwa kero za wafanyabiashara. Hata hivyo, bado kuna kero kubwa sana kwa wafanyabiashara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tunakaa mpakani pale, tunaona jinsi ambavyo wafanyabiashara wengi wanahamia kwenye nchi za jirani na Tanzania. Ukiangalia wafanyabiashara wengi wa Tanzania wanakimbilia Malawi, wengine wanakimbilia Zambia, lakini pia wako wafanyabiashara wakubwa sana ambao sasa hivi wanahama nchi, wanakwenda kuwekeza viwanda katika nchi nyingine na Serikali hii ya Chama cha Mapinduzi bado inaona wafanyabiashara kama ni watu ambao hawaaminiki. Hakuna nchi yoyote duniani ambayo inaweza ikapiga hatua kama itaona wafanyabiashara ni watu ambao hawaaminiki na siyo wadau wakubwa katika Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wajibu wa Serikali ni kuhakikisha kwamba wafanyabiashara mitaji yao inakua ili waweze kulipa kodi na Serikali iweze kupata fedha na kuhakikisha kwamba inatekeleza miradi mbalimbali ambayo inapendekeza katika Taifa hili. Leo Serikali hii inajinasibu kwamba inakusanya mapato mengi sana, lakini ukweli tu ni kwamba wafanyabiashara mitaji yao imeshuka na fedha ambazo zinakusanywa sasa hivi karibuni wafanyabiashara wanalalamika, wananyang'anywa tu hizo fedha, siyo kwamba wanapenda. Ndiyo maana wafanyabiashara wengi ukienda Segerea na kwenye Magereza mbalimbali wamekamatwa wamewekwa kwa kesi za *money laundering* ambazo hazina ukweli wowote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunaishauri Serikali iwajibike kuhakikisha kwamba biashara zinaboreka katika nchi hii ili kuhakikisha kwamba Watanzania wengi wanafanya biashara na mitaji inakua ili biashara Serikali iweze kukusanya mapato. Tunaamini kabisa katika mwaka unaokuja wa 2020/2021 tuna uhakika kabisa kwamba Serikali hii itashindwa kukusanya mapato ya kutosha kwa sababu wafanyabiashara wengi watakuwa wameshafilisika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka huu tulikuwa Uganda, tumeshangaa sana. Wafanyabiashara wote wa Dar es Salaam sasa hivi wanafunga bidhaa zao Kampala; wafanyabiashara wa Moshi, Arusha na Mbeya wameanza kufunga biashara zao Kampala pale badala ya Dar es Salaam. Sasa unashangaa, Jiji ambalo tulikuwa tunaamini kabisa kwamba ni soko la Afrika Mashariki, sasa hivi limeshakufa. Sasa hivi watu wanakwenda Kampala wanafanya biashara, wanafunga biashara kule, wanakwenda kufanya biashara Tanzania. Kwa hiyo, wanafunga mizigo ya madukani kwenye Mji wa Kampala. Sasa hivi Mji wetu wa Dar es Salaam umeshakufa kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunavyozungumzia biashara, tunazungumzia uchumi wa nchi. Tusipojua kwamba uchumi wa nchi ni biashara, tutakuwa tunapoteza muda. Nafikiri Waziri wa Viwanda na Biashara akae na Waziri wa Fedha wajaribu kuangalia matatizo ambayo

yako Tanzania, ambayo tunaona yanaendelea kuua biashara na yatafilisi kabisa biashara za watu na biashara zitakufa katika nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunazungumza humu na ukijaribu kusoma unaona kabisa kwamba kuna mipango mizuri sana, lakini hakuna utekelezaji mzuri ambao unatoa mwanga kwa wafanyabiashara kufanya biashara katika Taifa hili. Ndiyo maana tunawaambia kila wakati kwamba bajeti ambazo tunatengeneza, Serikali hii inatekeleza bajeti hizi kwa kuangalia uchumi wa vitu na siyo uchumi wa wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunazungumza kila wakati hamtuelewi. Ukiangalia bajeti ambazo zipo, kwa mfano bajeti ya miundombinu; ina-*cost* karibuni trilioni 4.6 lakini ukienda kuangalia kati ya hizo fedha, kwenye kilimo utaona kabisa wamewekeza shilingi bilioni 100, lakini inakwenda shilingi bilioni tatu. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mwakajoka. Mheshimiwa Lema.

**MHE. GODBLESS J. LEMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru na ninamshukuru Mwenyezi Mungu kwamba nimemaliza adhabu yangu vizuri na nimerudi nimewakuta hamjabadilika sana. Kwa hiyo, nawashukuru sana wale waliosaidia kupata adhabu ya muda mrefu, mmehuisha sana roho yangu na thamani yangu kupenda haki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili ni Bunge la mwisho. Maana yake mwaka huu Bunge hili lote tutaondoka twende kwenye uchaguzi na kwa miaka mitano ambayo tumekaa hapa ndani ya Bunge, Bunge hili kama limefanya kazi ya kusaidia nchi zaidi ya kuipamba Serikali ni kwa kiwango kidogo sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunajadili taarifa za Kamati, Viwanda na Biashara. Taifa lolote linalotaka kuimarisha biashara katika nchi yake, kitu cha kwanza ni utawala bora uonekane kwa macho na siyo tu utawala bora; leo utawala bora, utawala wa sheria, demokrasia katika Taifa hili imeonekana siyo sehemu ama siyo *part* ya mafanikio ya nchi. Juhudi kubwa sana zinafanyika za kuondoa Wapinzani katika uchaguzi unaofuata. Jambo hilo linaweza likafanikiwa, lakini halitafanikiwa na baraka za vizazi vya Taifa hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumetoka kwenye uchaguzi wa Serikali za Mitaa; ule uchaguzi hayakuibiwa matokeo, uliibiwa mchakato. Mchakato uliibiwa na CCM imeshinda kwa asilimia 100. Mnapiga makofi, mnafurahi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunakwenda kwenye Uchaguzi Mkuu Mwaka 2020; kuna *commitment* kubwa sana ya kuhakikisha kwamba hakuna Mpinzani atakayerudi. Unapoongelea biashara na viwanda, wawekezaji wanaangalia utawala bora ili kuleta biashara ambazo ni *sustainable*. Unapoongelea viwanda na biashara wawekezaji na watu wa ndani wanaangalia utawala wa sheria uliothabiti ili kuleta mitaji na kuongeza mitaji katika kujenga uchumi wa nchi. Kwa hiyo, ili ku-*improve* biashara katika Taifa hili na ku-*improve* viwanda, kitu cha kwanza cha kuimarisha ni utawala wa sheria ambao mtu yeyote hatautilia mashaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, *factors* za utawala bora katika kuamua uchumi wa nchi ni namba moja. Leo Kenya inawawekezaji wengi kuliko Tanzania. Kenya haina rasilimali nyingi kama Tanzania, lakini wawekezaji wana-*confidence* na Kenya kwa sababu hata Mahakama za

Kenya za ndani zina uhuru wa kutosha wa ku-*handle matter* za wawekezaji kuliko hata Mahakama za nje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo Kenya inapokea watalii wengi kuliko Tanzania, leo Kenya ina vitanda ziada kuliko Tanzania karibu vitanda 30,000 ni kwa sababu ya mazingira ya utawala wa kisiasa wa nchi ile. Mheshimiwa Uhuru leo na Raila wanashikana mikono pamoja kujenga Taifa lenye umoja. Leo Kenya huwezi kujua tofuati ya mpinzani na Serikali kwa sababu wameamua kujenga nchi. Hapa Mpinzani ni Mhaini. Hata akitoa maoni, yanakuja maazimio ya *AG;* yamekuja maazimio leo hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ningekuwa Serikali, suala la Mheshimiwa Zitto ningelipuuza tu, kabisa! Leo Mheshimiwa Zitto ameandika barua tarehe 22 Januari, maazimio ya *World Bank* kuhusu mtafaruku wa Sera na Serikali ya Tanzania ni mwaka juzi 2018. Barua ya tarehe 22 Janauri ya kimkakati leo mmeishikia Bango, yanatolewa maamuzi, Mwanasheria Mkuu wa Serikali anaambiwa aangalie kama kuna kosa la jinai katika maoni aliyotoa Kiongozi wa Upinzani wa Chama cha siasa. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utaratibu.

**MWENYEKITI:** Kuhusu utaratibu, kifungu gani?

**KUHUSU UTARATIBU**

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakwenda Kanuni ya 53(8) na ninaomba niiseme. "Mbunge yeyote hataruhusiwa kufufua jambo lolote ambalo Bunge lilishaamua ama katika Mkutano huo uliopo au ule uliotangulia wala kuwahisha shughuli ya Mkutano huo unaondelea isipokuwa kwa kufuata masharti ya Kanuni hizi." *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala hili analolizungumza Mheshimiwa Mbunge saa hizi akirejea kile kilichojiri asubuhi wakati kiti chako kikiwa kimekaliwa na Mheshimiwa Spika; na jambo hili lilishaamuliwa; na kwa kuwa lilishaamuliwa, kwa sasa tena siyo hoja ya kuzungumzwa Bungeni kwa mujibu wa Kanuni ya 53(8). *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nadhani jambo hili sasa liachwe liendelee kwa mujibu wa maamuzi yaliyofanywa na Bunge na kwa taratibu ambazo zinaongozwa na kanuni zetu na hizo sheria mbalimbali ambazo Kiti cha Spika wakati wa kufanya maamuzi haya leo asubuhi, kilishayafanyia maamuzi.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, niamue tu hii kama ifuatavyo: Mheshimiwa Waziri amesoma Kanuni hiyo ambayo ni sahihi, ndivyo inavyosema; lakini kufufua lazima ufufue kwa hoja mahususi. Kwa vile tuna uamuzi uliotolewa na Kiti kwa maana ya Spika kwenda kwa Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu, ni uamuzi huo. Kwa hiyo, ni sahihi kabisa kwamba hilo litachukua mkondo huo.

Sasa kwa tafsiri yangu, Mheshimiwa Lema yeye alikuwa anachangia kwa maana ya kutoa maoni yake, lakini siyo kuleta hoja ya kufufua mjadala ambao ulishafungwa.

Mheshimiwa Lema, sasa endelea tu kwa lengo ambalo siyo la kuturudisha nyuma, lakini tusaidie Utawala Bora *in the context* ya hoja hizi mbili tulizonazo mbele yetu sasa hivi.

**MHE. GODBLESS J. LEMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

Waheshimiwa Makatibu, mna tabia ya kuiba dakika tatu, nne, tano, sasa naomba muwe makini sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa…

**MHE. GODBLESS J. LEMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Mimi nachnagia Taarifa ya Kamati ya Viwanda na Biashara na hoja yangu ni moja tu, ya kwamba ili kuwepo na biashara ambazo ni *sustainable,* tunahitaji utawala bora. Sasa mimi ni Mbunge, naishauri Serikali kwamba kwa suala ambalo limetokea leo Bungeni, ambalo wala mtafaruku wake siyo Mheshimiwa Zitto, Zitto anaweza akawa amedandia, mtafaruku wake ni *confusion* ya *policy* kati ya Serikali na *World Bank.*

Sasa ndiyo nikasema, ningekuwa ni mimi, badala ya kuamuru Mheshimiwa Zitto atiwe hatiani, ningesema Mheshimiwa Zitto apuuzwe halafu Serikali mwendelee kujadili na *World Bank* mfikie *consensus.* Hiyo ndiyo ingekuwa Utawala. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa maana yake Mpinzani anapotoa maoni sasa *internationally* naye anatiwa kibano, mnatia mashaka wale watu ambao wanataka kuleta mitaji mingi hapa. Hivi vitu vinakwenda *internationally* na vikienda Kimataifa watu wanasema ile nchi Bwana, hata Mbunge akitoa maoni huwa anapewa *money laundering,* tusubiri kwanza tuone utawala upite.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo letu siyo tu kuwatoa madarakani, hata mkibaki madarakani, lakini tukiona Taifa hili linakuwa ni mahali salama pa kuishi, hiyo ni baraka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaongea biashara; leo…

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

**MWENYEKITI:** Tusikilize taarifa. Iwe ni taarifa ya kujenga.

**T A A R I F A**

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nilitaka kumpa taarifa ndugu yangu Mheshimiwa Lema kwamba maoni ya Mheshimiwa Zitto siyo maoni ambayo ameenda kwenye *tv* akatoa wala akaenda kwenye mtandao akatoa. Maoni ya Mheshimiwa Zitto ni barua rasmi aliyoandika tena kwa nembo ya Bunge. Sasa kama ni barua imeandikwa kwa nembo ya Bunge maana yake ni kwamba Bunge la Tanzania limehusika kufanya jambo hilo.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**MWENYEKITI:** Haya. Mheshimiwa unasemaje kuhusiana na hiyo?

**MHE. GODBLESS J. LEMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna wakati ilitolewa hoja kiwekwe kipimo, ile *alcoholic* nini ile, hapo. Ninafikiri kuna haja ya kukirudisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme nini? Ninachowaambia Waheshimiwa Wabunge na Serikali, leo huko mitaani sisi tunafahamu hali ya kibiashara ilivyo mbaya. Tunafahamu jinsi ambavyo watu wanaondoka, ambavyo mitaji inahama na hiyo ni kwa sababu ya mashaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *TRA* hata wakiongeza kodi kwa kiwango gani, lakini kama Taifa halina *uncertainty,* bado kodi huwa haiendi kwa yule anayefanya biashara, inakwenda kwa mlaji wa mwisho. Sasa kuna mashaka makubwa. Leo kupata *working permit* nchi ama *business permit,* mimi niko Arusha, watu wengi wameondoka kwa sababu ya *working permit.* Wamekuja Wazungu wanataka kufanya miradi wanaondoka kwa sababu ya *working permit.* Mimi najiuliza, mtu anakuja na *investment* ya labda shilingi milioni 10, una…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Mwilima dakika tano na Mheshimiwa Bonnah Kamoli, dakika tano.

**MHE. HASNA S. K. MWILIMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru nami kupata hizi dakika tano za kuchangia taarifa hizi za Kamati mbili, lakini nitajikita zaidi kwenye taarifa ya Kamati moja ya Miundombinu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natambua kwamba Serikali imefanya kazi nzuri sana ya kuboresha Bandari mfano, Mwanza, vilevile kuboresha gati kwa zile bandari ndogo ndogo kama ambavyo taarifa inavyojieleza hapa. Pia kama ambavyo taarifa inavyojieleza kumekuwa na ahadi ya Serikali ya kujenga meli mpya kwenye Maziwa Makuu mfano, Ziwa Victoria, Ziwa Nyasa na Ziwa Tanganyika. Tumeona kwenye Ziwa Victoria baadhi ya meli mpya zimeweza kuwasili, lakini pia ukarabati uliofanywa kwenye meli mbalimbali zilizopo ndani ya Ziwa Victoria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, rai yangu tu kwa Serikali, kwa kuwa ndani ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa uliowekwa wa mwaka mmoja na miaka mitano wamepanga kutengeneza meli kubwa ndani ya Ziwa Tanganyika ya kubeba abiria lakini meli pia kwa ajili ya mizigo. Tuwaombe tu Serikali waone umuhimu wa kufanya hivyo kwa sababu ndani ya Ziwa Tanganyika tumepakana na nchi jirani ya *DRC* na nchi jirani ya Zambia. Kwa kufanya hivyo tutaweza kufanya biashara ya kutoka Tanzania na kuelekea Congo *vis-a-vis* Zambia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikigusa uchukuzi naomba pia niguse suala la miundombinu kwa maana ya sekta ya barabara. Kwenye Jimbo langu Serikali ilipokea pesa kiasi cha shilingi bilioni 35 kutoka kwenye Mfuko wa Maendeleo ya Abu Dhabi kwa ajili ya kujenda barabara yenye urefu wa kilomita 51.1 kutoka Uvinza hadi Malagarasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tangu Serikali ipokee pesa hizo leo tunavyoongea ni mwaka wa tatu utekelezaji hakuna, niombe tu Serikali sasa hivi hali ya mvua ile barabara imeharibika sana, kila wakati tunapofanya *maintenance* bila kujenga barabara kwa kiwango cha lami inakuwa haitusaidii na badala yake tunapoteza pesa za Serikali. Kwa hiyo niombe Wizara ione ni namna gani itatangaza tenda ili hii barabara ya Uvinza hadi Malagarasi iweze kujengwa pamoja na kile kipande cha Chagu hadi Kazilambwa chenye zaidi ya kilomita 48. (*Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu muda ni mfupi naomba nizungumzie kidogo kuhusu *NIDA*. Natambua kwamba dhamira ya Serikali ni njema katika kusitisha wale wote ambao hawajasajili simu zao kwa alama ya vidole, lakini hii nchi ni kubwa na miundombinu yake sio rafiki. Hivi ninavyoongea katika Jimbo langu hata asilimia 20 haijafika, kwa hiyo niiombe sana Wizara niiombe Serikali wanapokuwa wanatupa taarifa Wabunge watambue kwamba hata wale Maafisa wa *NIDA* hawapo *site*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano ndani ya Wilaya ya Uvinza Maafisa wa *NIDA* hawapo, wananchi wamezimiwa simu zao, mawasiliano yao, wazazi wana watoto wao Dar es Salaam, wana watoto wao Dodoma wanatumiwa pesa kwa kutumia simu zao. Niombe tu

Serikali ije na mkakati maalum waone ni jinsi gani waweze hata kuwasajili kwa vitambulisho hivi vya wapiga kura, kwa sababu Watanzania wengi wana vile vitambulisho vya kupigia kura, lakini hivi vitambulisho vya uraia kwa masharti ambayo Serikali imeweka kwa kweli itakuwa na wakati mgumu sana, tunaweza tukamaliza mwaka bado Watanzania hawa walioandikwa humu milioni 15 wakawa bado hawajasajili simu zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, niunge mkono hoja na nishukuru sana kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Bonnah Kamoli dakika tano na Mheshimiwa Nachuma dakika zako 10.

**MHE. BONNAH L. KAMOLI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba kwanza niipongeze Serikali kwa kazi ambayo inaendelea kufanya hususan kwenye mambo ya masuala ya miundombinu, lakini nataka nichangie kwenye Sekta ya Miundombinu. Katika Jimbo la Segerea kuna wananchi ambao wanadai fidia tangu mwaka 1997, wananchi ambao walipisha *Airport Terminal Three*, hao wananchi mpaka sasa hivi hawajalipwa, kwa hiyo naiomba Serikali kwa sababu tuko sasa kwenye Bunge la mwisho ili iweze kuangalia ni jinsi gani inaweza ikatoa tamko au ikawalipa hawa wananchi kwa sababu imekuwa ni muda mrefu sana na kila siku tukisimama hapa tunaongelea kuhusu hao wananchi. Pia nimekuwa nikifuatilia bajeti zinavyotoka nione hata kama kuna bajeti wamepangiwa kwa ajili ya malipo yao sijawahi kuona bajeti yoyote katika hii miaka miwili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nataka niiulize Serikali, je, ni lini sasa itawalipa hawa wananchi kwa sababu nimekuwa hapa huu unaenda mwaka wa tano lakini nimekuwa nikichangia kila mwaka kuhusiana na hawa wananchi, lakini hawajaweza kulipwa. Naomba sana Kamati ya Miundombinu pamoja na Mawaziri wote ambao mmoja mmoja wameshawahi kufika kwenye Jimbo langu na wakafanya mikutano na wakawaahidi hawa wananchi kwamba watarudi kwa ajili ya malipo yao. Sasa umefika wakati wa kuwalipa hawa wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine ambacho nataka kuchangia ni kuhusiana na miundombinu ya barabara. Tunajua watu woe kwamba Mkoa wa Dar es Salaam kwa sasa kutokana na mvua ambayo inaendelea miundombinu ya barabara imeharibika sana na Mkoa wa Dar es Salaam pamoja na kwamba sio Makao Makuu ya Nchi lakini pia ni mji maarufu na ndio mji ambao unaingiza kipato kikubwa katika Nchi ya Tanzania. Sasa hivi kwa Mkoa wa Dar es Salaam miundombinu yake ni mibovu sana. Nataka niishauri Serikali tukisema tu kwamba tuangalie bajeti ambayo tuliipitisha 2019/2020 ambayo ndio ikatengeneze ile miundombinu, bajeti haitoshi kwa sababu tumeshaongea sana na watu wa *TARURA* wanataka kufanya kazi lakini hawana bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nina ushauri kwa Serikali, kwa kuwa Mheshimiwa Waziri wa Fedha jana alituambia kwamba, wanapanga asilimia moja ya bajeti kwa ajili ya majanga na kwa tafsiri yangu kwamba majanga sio tu lazima watu wafe, majanga ni kama haya yaliyotokea sasa hivi miundombinu ya barabara mibovu lakini pamoja na watu wamepata maafa mengi sana kuhusiana na mvua. Sasa asilimia moja ukisema nusu ya hiyo asilimia moja ni bilioni 30. Sasa kama tukipewa bilioni 15 sisemei kwa Jimbo la Segerea peke yake, lakini nasemea kwa Mkoa wa Dar es Salaam ili waweze kurekebisha hiyo miundombinu ambayo imeharibika, kwa sababu kwa kawaida, kama nilivyosema tukisema bajeti ambayo iliyopangwa 2019/2020 *TARURA* hawana pesa hizo. Sisi kama Wabunge au mimi kama Mbunge nimekuwa niliongea sana na watu wa *TARURA* kuhusiana na miundombinu ambayo imeharibika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano kwenye Jimbo langu kuna barabara kama sita hivi hazipitiki kabisa ukianza na ile barabara ya Vingunguti ambayo inatokea Vingunguti Mataa mpaka Barakuda, hiyo barabara haipitiki kabisa na watu hawataki kupitisha magari yao kwa sababu ina mashimo makubwa na watu wanaenda kujaa kwenye hii barabara ya Tabata. Sasa barabara hii ya Tabata utakuta foleni kuanzia saa moja mpaka saa nne na ndio maana inasababisha hata uchumi kushuka kwa sababu watu wanakaa muda mrefu barabarani badala ya kuwa makazini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kama Serikali itawaaachia tu *TARURA* kwamba ndio wenyewe wawe waendelee na hii kwa ajili ya kurekebisha hizi barabara naomba sana Serikali iwaongezee *TARURA* pesa na kila siku nimekuwa nikisimama hapa naomba *TARURA* waongeze bajeti kwa sababu hali ya mijini kutokana na miundombinu na barabara zetu ni chakavu na hazijafanyiwa matengenezo kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha kutokana na hiyo bajeti hiyo aliyosema kwamba kuna asilimia moja ambayo anaiweka, aweze kuwapa watu wa *TARURA* ili waweze kufanya marekebisho yaliyotokea Dar es Salaam nzima au Tanzania kote mvua inakonyesha. Kwa hiyo, naomba sana kwenye masuala ya miundombinu kwa sababu mjini sasa hivi pamekuwa hapafanyiki kitu chochote sababu ya foleni. Kwa hiyo nimwombe sana Mheshimiwa Mwenyekiti…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. BONNAH L. KAMOLI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Maftaha.

**MHE. MAFTAHA A. NACHUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nianze kwa kuwapongeza Wenyeviti wakamati zote mbili kwa mawasilisho mazuri ambayo wameyaleta leo hii. Nitachangia Kamati zote mbili kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kwanza, ni suala hili la makampuni ya simu. Makampuni ya simu yamekuwa yakiwaibia Watanzania kwa kiasi kikubwa sana, leo ukiamua kuweka bando lako kwa mfano kwenye simu kwa mfano *TIGO,* au *AIRTEL* au *VODA* ukajiunga bando la wiki moja baada ya dakika tano au 10 au 20 wakati mwingine unatumiwa meseji kwamba bando lako limekwisha, huu ni wizi mkubwa sana ambao unafanywa na makampuni ya simu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niiombe Serikali kwamba ihakikishe ya kwamba makampuni ya simu yanafuatiliwa kwa karibu sana kwa sababu yamekuwa yanatuibia Watanzania, yameachwa hovyo wafanye wanavyotaka. Ukiwauliza wanakwamba vigezo na masharti kuzingatiwa hali ya kuwa bando lako haujatumia hata siku tatu bando la wiki linaisha ndani ya masaa 24, wanakwambia ujiunge tena, wizi huu unafanywa na makamouni ya simu. Serikali kama haipo vile Tanzania tunaomba sana kwa sababu Watanzania wengi ni maskini sana, Watanzania anavyochukua Sh.500 yake akaamua kujiunga bando atumie siku halafu anatumia dakika mbili tatu anaambiwa bando lako limeisha, hakuna ufuatiliaji wowote unaofanyika na Serikali. Tunaomba Serikali ihakikishe kwamba inafanya ufuatiliaji wa karibu. *(Makofi)*

**T A A R I F A**

**MHE. JACQULINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimpe taarifa mchangiaji anayechangia sasa kwamba ni kweli kabisa anavyosema kwamba haya mashirika

ya mawasiliano yamekuwa ni tatizo kubwa kosa mfano shirika la mawasiliano la *VODACOM*. Mimi nataka nitoe ushuhuda ni jana tu usiku nimenunua kifurushi nikapiga simu nilipopiga simu nikaambiwa kwamba namba unayopiga kwa sasa haipatikani…

**MWENYEKITI:** Taarifa gani unataka kumpa.

**MHE. JACQULINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikazima hiyo simu nikalala asubuhi nachukua simu yangu…

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa…

**MHE. JACQULINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naongezea nafafanua

**MWENYEKITI:** Hapana naomba ukae chini. Mheshimiwa usijibu endelea kuchangia.

**MHE. MAFTAHA A. NACHUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja na nakubaliana kabisa na mawazo ya Mheshimiwa Ngonyani kwamba ni kweli kabisa napokea taarifa yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mashirika haya kama ikiwezekana sisi kama Wabunge ambao ni wawakilishi wa wananchi ni lazima tuweke utaratibu ikiwezekana kwa sababu kwa kuwa wizi ni dhambi katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na wizi haufai na ni kosa la jinai, ikiwezekana tuyachukulie hatua mashirika haya Waheshimiwa Wabunge ikiwezekana tuende mahakamani kuyashtaki mashirika haya ya simu kwa kuwaibia Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yangu nyingine ni suala la barabara. Sasa hivi Tanzania kwa kiasi kikubwa miundombinu inajengwa barabara nyingi zinajengwa lakini tatizo la barabara hizi zinazojengwa zinachukua muda mrefu sana kumalizika. Sasa tatizo ni nini tunaomba Serikali itueleze kwa nini barabara nyingi ambazo ni muhimu zimeanzishwa kujengwa Tanzania, lakini barabara ambayo inapaswa ikamilike kwa mwaka mmoja au kwa miezi sita au miaka miwili inachukua miaka minne mpaka miaka mitano barabara hazikamiliki. Kwa hiyo, niiombe Serikali kwamba fedha ambazo zinakusanywa kwa ajili ya barabara zipelekwe kwa wakati kwa wale wakandarasi ambao wamepewa kujenga hizi barabara ili barabara ziweze kukamilika kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano barabara ya Uchumi kule Kusini ambayo inaanzia Mtwara Mijini inafika Tandahimba, Newala mpaka Masasi muda wake umemalizika sasa hivi ni zaidi ya miaka miwili ile barabara haiajakamilika. Ukiwauliza hawa wakandarasi wanasema fedha wanachelewa kupelekewa, waki- *raise* kitu kinachoitwa *certificate* wakipeleka Wizarani kwa wahusika, wanachelewa kupata fedha zao ili waweze kuendelea na ule ujenzi. Tunaomba sana barabara hizi kwa sababu Serikali imeamua kujenga barabara, zikamilike kwa wakati, wakandarasi, wazabuni wapewe fedha zao kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilizungumza hapa ndani ya Bunge hili kwamba kuna barabara muhimu sana ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambazo Serikali ni lazima izijenge barabara hizi zikiwemo barabara zile za mipakani. Leo hii mpaka wa Kusini kuna barabara ya Ulinzi ambayo inazunguka Mkoa mzima wa Mtwara inafika Mkoa wa Lindi mpaka Mkoa wa Ruvuma, barabara ambayo ilitumika wakati ule wa kulinda wale ambao walikuwa ni wavamizi wanaotoka Msumbiji, wale Makaburu leo hii ile barabara imesahaulika sana. Tumekuwa tunazungumza ndani ya Bunge hili kwamba barabara za ulinzi ni barabara muhimu sana kwa ulinzi wa Taifa letu hili. Barabara inayotoka Mtwara kuelekea Mikoa hii ya Kusini yote hii inayozunguka Mto Ruvuma, tunataka Serikali kwa kuwa imehaidi ndani ya Bunge hili kwa muda

mrefu kwamba itakuja kujenga barabara hii, tunaomba itekelezwe hii ahadi, barabara ile ijengwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara pia ambayo inatoka Dar es Salaam kuelekea Mikoa ya Kusini ni barabara ambayo miaka ya karibuni iliweza kujengwa na Serikali lakini barabara ambayo kutokana na maroli yanayosafirisha *cement* kutoka Kiwanda cha Dangote kuja Dar es Salaam kwenye soko kuu ile barabara inaharibika sana na inachukua muda mrefu sana kurekebishwa. Barabara ya Kibiti – Lindi, ni barabara ambayo Serikali inarekebisha lakini kwa utaratibu sana, maeneo mengi imebomoka. Tunachoitaka Serikali tuliwahi kuzungumza hapa hivi sasa Serikali imejikita kujenga meli kule kwenye Maziwa Makuu kupitia ile Taasisi za Serikali *Marine Service*, tunaomba Serikali itanue wigo itengeneze meli ziweze kutumika kwenye bahari ya Hindi kwa ajili ya kusafirishia mizigo ya *cement* kutoka Mtwara kuelekea Dar es Salaam na kwingineko duniani. Tunavyoendelea kutumia barabara moja barabara ya Kibiti - Lindi barabara inaharibika sana na Serikali inatumia fedha nyingi sana kurekebisha na kuweka viraka viraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu Mwenyezi Mungu ametubariki Tanzania tuna Bahari ya Hindi na bahari yenyewe ina kina kirefu kuanzia pale Bandari ya Mtwara, Serikali neno *Marine* maana yake ni bahari lakini leo hii imejikita kujenga meli katika Maziwa Makuu kana kwamba sisi hatuna bahari hapa Tanzania. Kwa hiyo niiombe Serikali kwamba iweke mpango wa makusudi kabisa wa kununua meli mbalimbali ambazo zitasafirisha mizigo ya *cement* na mizigo mingine kutoka Ukanda ule wa Kusini kuja Dar es Salaam na kuelekea duniani mpaka huko Zanzibar.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hili Bandari ya Mtwara imekuwa inarekebishwa…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa.

Waheshimiwa Wabunge kabla hatujaanza kuwaita upande wa Serikali wachangie, nina tangazo la wageni hapa, tuna wageni wa Waheshimiwa Shaban Shekilindi na Mheshimiwa Rashid Shangazi ambao ni Walimu 28 na wanafunzi 222 kutoka Shule ya St. Mary's Mazinde Juu, Lushoto mko wapi karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge mtakumbuka hii ni miongoni mwa shule zetu zinazofanya vizuri sana katika mitihani yetu, kwa hiyo karibuni Walimu, karibuni wanafunzi endeleeni kwa kasi mfanye vizuri zaidi ya hapo karibuni sana mnaweza mkakaa. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, rangi nzuri hiyo.

**MWENYEKITI:** Kwa hiyo wachangiaji wa upande wa Serikali ambao ukimuondoa Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara ambaYe tunampa dakika 10, nitakaowataja watatu ni dakika tano tu kila mmoja. Naanza na Mheshimiwa Nditiye, atatufatiwa na Mheshimiwa Silima na Mheshimiwa Kwandikwa kwa utaratibu huo au kwa mtiririko huo. Mheshimiwa Nditiye.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ENG. ATASHASTA J. NDITIYE):** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kupata nafasi ya kuchangia kwenye hotuba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Miundombinu. Nichukue nafasi kuwapongeza sana

Kamati yetu ya miundombinu kwa taarifa yao ambayo ni nzuri sana, taarifa ambayo kwa kweli kwa ujumla ilikuwa na maelekezo mazuri sana kwa upande wetu sisi Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaongelea kwa haraka sana suala la bandari nitaongelea kidogo na *TASAC* lakini pia nitaongelea masuala ya usajili wa *line* kwa alama za vidole. Ni kweli kwamba tumeendelea kufanya maboresho ya makusudi kabisa kwenye bandari yetu ili kuongeza mzigo na kuweza kuuhudumia kama ipasavyo. Tumeendelea kufanya mchakato wa kupanua bandari kwenye gati mbalimbali lakini pia tumeagiza vifaa mbalimbali vya kufanyia kazi ya kupakua mzigo wetu ili tuweze kufanya kazi usiku na mchana pia tuweze kupakua mzigo mwingi kama inavyopaswa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba changamoto za hapa na pale zipo na sisi kama Serikali kupitia Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari tumeendelea kuwasiliana na wadau mbalimbali na tumekuwa tukifanya vikao mbalimbali kuhakikisha kwamba changamoto za hapa na pale ambazo zipo zinatatuliwa kwa pamoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongelee kidogo kuhusu suala la *TASAC;* limezungumzwa sana na Waheshimiwa Wabunge. *TASAC* ilianzishwa kwa Sheria ya Bunge Na. 14 ya mwaka 2017 na katika sheria hiyo kipengele cha 7(1)(a) kinairuhusu *TASAC* kufanya kazi ya ku-*clear* na ku-*forward* mizigo ambayo ni mahususi *exclusivity mandate*. Ni kweli kwamba sio kila mzigo unaweza ukawa *cleared* na kila mtu au kila kampuni, kuna mizigo mbalimbali ambayo kwa kweli iko kiusalama zaidi, ni lazima ichukue wajibu wake wa kulinda hiyo mzigo kuweza kuisafirisha na kuigomboa. Pia ni lazima vilevile tutengeneze mazingira ambapo meli inayokuja ni lazima tujue imeleta mzigo gani kutoka huko ilikotoka na umefikaje hapa ili tuweze kutengeneza utaratibu wa kupeleka maelezo kwa taasisi zinazohusika na bandari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia ni lazima vilevile tutengeneze mazingira ambapo meli inayokuja ni lazima tujue imeleta mzigo gani kutoka huko ilikofika na umefikaje hapa, ili tuweze kutengeneza utaratibu wa kupeleka maelezo kwa taasisi zinazohusika na bandari. Hatuna nia mbaya na wala wale ma-*shipping agency* hatujawazuwia wanaendelea kufanya kazi zao kama kawaida, hata wale ma-*clearing and forwarding* wanaendelea kufanya kazi zao kama kawaida na shughuli bandarini zinzendelea kama kawaida. *TASAC* haijaja kuuwa sekta binafsi isipokuwa imekuja kuimarisha sekta binafsi, lakini pia kulinda rasilimali za Serikali ambazo ni muhimu zilindwe na Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongelee kwa harakaharaka suala la mawasiliano. Ni kweli kwamba, kuanzia tarehe 01Mei, 2019 Serikali kupitia Mamlaka ya Mawasiliano tulikubaliana kwamba, Watanzania sasa waanze kutumia *line* zao za simu kwa kusajili kwa alama ya kidole kupitia kitambulisho cha Taifa cha *NIDA*. Na kwa kweli, mpaka sasa hivi ninapoongea na Bunge lako Tukufu *line* milioni 31 kati ya *line* milioni 43 tayari zimekwishasajiliwa kwa alama za vidole kwa kutumia vitambulisho vya *NIDA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia *line* ambazo tayari tumekwishazizima mpaka sasa hivi ni *line* 6,211,000 na tunaendelea kuzima kwa awamu. Awamu inayofuata wiki ijayo kuanzia Jumatatu ni kuzima *line* milioni 12 ambazo Watanzania walionazo bado hawajasajili kwa alama za vidole. Tunafanya hivyo kwa lengo zuri la kuhakikisha kwamba, tunawalinda watumiaji wa mawasiliano wawe salama wanapofanya mawasiliano yao au wanapofanya *transactions* mbalimbali kupitia mawasiliano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeshtushwa kidogo na maelezo yaliyotolewa na Mbunge mmojawapo wa Mtwara hapo kwamba, yeye ameibiwa kupitia Kampuni ya Simu ya *Vodacom*:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna maelezo kidogo; tunapotumia hizi simu janja za sasa hivi kuna vitu mbalimbali ambavyo vinatusaidia na vinatuletea manufaa katika kutumia hizo simu janja. Watu wanajifunza, watu wanapakuwa *document* mbalimbali, sasa unapofanya *transactions* hizo ujue kwamba, kama umeishiwa *bundle* halafu hujatoka kwenye *download* hicho kitu unapoweka *bundle* upya lazima litaendelea kuliwa. Wakati mwingine watu wanapata changamoto kutokana na hivyo, lakini watu wenye zile simu za kawaida walio wengi hatujawahi kusikia changamoto kama hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunawaomba sana Waheshimiwa Wabunge na Wananchi kwa ujumla unapotumia simu janja na unaweka *bundle* likiisha uhakikishe vile vitu ambavyo umeshaanza ku-*download* unaviondoa kwenye mfumo wa kuwa-*downloaded,* ili unapoweka *bundle* lingine lisiishe kwa haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tunashukuru sana… ahsante sana.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa *Engineer* Nditiye; tunaendelea Mheshimiwa Sima.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS, MUUNGANO NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue fursa hii kumshukuru sana Mwenyezi Mungu, lakini pia niishukuru kamati kwa kusoma taarifa yao vizuri ambayo imesheheni mambo ya msingi na kwa sehemu kubwa imetushauri sisi tunaohusika na suala la mazingira. Yako baadhi ya mambo machache ambayo naweza kuyatolea ufafanuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kamati imehitaji ili tujiimarishe zaidi katika usimamizi wa suala la mazingira. Ni kweli ziko changamoto ambazo zinajitokeza kwenye mzingira kulingana na wakati tulionao. Tumefanya maboresho ya sera yetu ya mwaka 1997, ili iweze kuendana na wakati uliopo sasa, ili iweze kutatua changamoto zinazojitokeza kwenye suala la mazingira, ikiwemo mabadiliko ya tabianchi, lakini pia, *bio* teknolojia:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kamati imegusia suala la ufinyu wa bajeti; nilitaka nilieleze tu Bunge lako kwamba, kulingana na ongezeko la mapato ya ndani sasa tunafanya mawasiliano na wenzetu wa Wizara ya Fedha, ili tuweze kuongezewa fedha, lakini jambo jingine kukwama kwa Mfuko wa Taifa wa Mazingira. Nakubaliana na kamati kwamba, huu ndio muarobaini wa matatizo ya mazingira ambayo yanajitokeza na ulikwama na sasa tunatengeneza waraka maalum kulingana na sheria yetu ya mazingira ya mwaka 2004, ili kuhakikisha kwamba, tunapeleka waraka huu kwenye mamlaka zinazohusika na kuweka ufanisi wa mfuko huu wa mazingira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini jambo lingine ni uelewa mdogo juu ya mambo ya mazingira:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara yetu imeendelea kufanya kazi hii kwa kina zaidi, kwenye vyombo vya habari, lakini pia kwenye semina, midahalo mbalimbali na tutaendelea. Tunaishukuru kamati kuendelea kutukumbusha juu ya suala la uelewa wa mazingira bado ni mdogo kwenye jamii yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo jingine ni vyuma chakavu, biashara ya vyuma chakavu ambayo sisi tunazungumzia suala la udhibiti wa taka hatarishi, tumetengeneza Kanuni ya

Mwaka 2019 ya Usimamizi wa Udhibiti wa Taka Hatarishi na kanuni hii imeanza kazi rasmi. Kwa hiyo, nilitaka niwatoe hofu wafanyabiashara wa biashara hii ya vyuma chakavu kwamba, Wizara imeweka utaratibu maalum kushirikiana na Wizara ya Fedha, lakini kushirikiana na Wizara ya Viwanda na vyombo vya ulinzi na usalama kuhakikisha tunalinda miundombinu yetu ya ndani isiweze kuharibiwa kupitia biashara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kamati imezungumzia urasimu wa kutoa vibali:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, yawezekana ni kweli, lakini jambo hili tumelichukua kama lilivyo tuende tukakae na wataalam wetu kuweka njia iliyo sahihi kuondoa urasimu uliopo. Tunatambua tumetengeneza, tumebadilisha kanuni, lakini tunatambua pia, katika suala la vibali leo tunatoa *Provision License Clearance,* tunatoa vibali vya muda mfupi ndani ya siku saba mtu anapata kibali wakati anasubiri kibali cha tathmini ya athari ya mazingira. Kile cheti cha athari ya mazingira kinachukua muda mrefu na ndio maana inawezekana wawekezaji baadhi wanaona kama vibali hivi vina urasimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tunao wataalam elekezi nao tumeboresha kanuni yao. Wataalam elekezi ambao wanatambuliwa na Baraza la Hifadhi ya Mazingira kwamba, tumeboresha kanuni yao na kanuni yao itaanza kazi rasmi mwaka huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye hoja ya Mheshimiwa Mbunge Mwita Getere,Mheshimiwa Mwita Getere amezungumza vizuri na ushauri wake tumeupokea kama Wizara kwamba, sasa ifike mahali Wizara ya Mazingira isiwe mambo mengi yanafanywa na Wizara za kisekta. Mheshimiwa Mwita Getere ametoa ushauri kwamba, sasa Wizara ijitegemee kufanya mambo hayo, ili kukabiliana na changamoto kubwa inayojitokeza. Na sisi tunakubaliana na hilo na tunalichukua kwa ajili ya kulifanyia kazi, ili tuone huko tunakokwenda tuboreshe maeneo ambayo tunaona yana changamoto, ili Wizara hii isiendelee kukabiliana na changamoto hizi na matokeo yake inaleta kutokuwa na ufanisi ndani ya Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekekelezaji wa agizo la kupiga marufuku mifuko ya *plastic*:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kamati imeeleza vizuri. Na kwa ushirikiano mkubwa wa kamati mifuko ya *plastic* leo nchini kwa sehemu kubwa sisi hatuitumii, lakini wako wafanyabiashara wababaishaji wanaopitisha mifuko hii kwa njia za panya, lakini iko mifuko ambayo haizingatii viwango na wenzetu wa *TBS* wameshatoa viwango na mifuko inahitaji kuwa na *standard.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana.

**MWENYEKITI:** Asante sana Mheshimiwa Naibu Waziri. Mheshimiwa Kwandikwa.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze kumshukuru Mwenyezi Mungu kupata nafasi ya kuchangia hoja zilizo mbele yetu, lakini nitajikita kwenye eneo moja tu la miundombinu, hususan sekta ya ujenzi. Nimshukuru sana Mwenyekiti wa kamati na kamati nzima kwa kweli, kwa muda wote ushauri wao na maelekezo yao na kwa kiasi kikubwa tuliyazingatia na kwa kweli, yametupa ufanisi maeneo mengi. Na ndio maana Mheshimiwa Mwenyekiti hapa wakati wa kuwasilisha ametoa shukrani kuona Serikali inafanya kazi kubwa na kuweza kutekeleza pia, maoni ya kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilipongeze tu Bunge kwa ujumla. Nasoma ripoti, nimezisoma ripoti tangu tulivyoanza kuzipokea katika Bunge lako, lakini utaona kuna maboresho makubwa sana. Na hata ukiiangalia ripoti ya wenzetu Kamati ya Miundombinu utaona kumekuwa na

mabiresho makubwa. Hata maoni yake ambayo tumeyapokea ni maoni ambayo yanalenga kwenda kutuboreshea shughuli zetu, lakini pia ni maoni ambayo yanatekelezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sekta ya ujenzi ni muhimu kwa sababu ni sekta wezeshi, inatoa huduma kwenye ukuaji wa viwanda, kwenye kilimo na kwenye huduma mbalimbali kwa hiyo, tumepokea maoni ya kamati. Na maeneo ambayo yalikuwa yameguswa ni upande wa *TANROADS,* upande wa barabara, ujenzi wa viwanja vya ndege, upande wa Wakala wa Majengo Tanzania, pia tumepokea maoni kwenye Chuo cha Ujenzi Morogoro na Chuo cha Mafunzo ya Teknolojia Stahiki Nguvu Kazi kule Mbeya, lakini pia upande wa wakala wa ufundi na umeme.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ufundi kabisa tumeona changamoto ambazo kamati imezitaja. Nilihakikishie Bunge lako ushauri huu mzuri sana tutaendelea kuuzingatia, ili tuone kwamba tunakwenda kufanya maboresho makubwa, lakini kwa lengo hilohilo la kuona kwamba, tunaendeleza mkakati wetu wa kuwa wezeshi, ili kuweza kuchangia kwenye ukuaji wa uchumi katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yako mambo kadhaa Waheshimiwa Wabunge pia, wakati wakichangia hoja hii wameyazungumza, lakini niwahakikishie tu Waheshimiwa Wabunge kwamba, changamoto za barabara, hususan kwenye kipindi hiki cha mvua nyingi na kamati imetushauri kwamba, tuangalie mtazamo kwamba, kipindi cha miaka hii ambapo mvua inakuwa nyingi pia, ile bajeti yetu upande wa dharura tunaweza kuiweka, lakini kimsingi ukiuangalia bajeti zetu tunavyoziunda tunakuwa tunapangilia hivyo kwamba, kuna maeneo korofi, kuna maeneo ujenzi wake ni wa muda. Tukitoa mwanya kwamba, wakati tukiwa tunazingatia kwamba, tumetenga fedha kwa ajili ya *periodic maintenance* kwa maana hiyohiyo kwamba, yako maeneo mengine ambayo kurejeshea miundombinu inategemea pia, kwamba, hali ya mvua iwe imepungua.

Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge kwa maeneo ambayo tunaona bado tuna changamoto na mvua imekuwa nyingi kwamba, tutakwenda kufanya marejesho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyokuwa nikizungumza mara nyingi kwa utaratibu wa kibajeti kama Mheshimiwa Waziri wa Fedha alivyozungumza tunafanya mawasiliano. Kwa sababu, tulikuwa na bajeti ya bilioni 8.2 kwa ajili ya dharura, lakini hadi kufikia mwezi wa kwanza mwanzoni tulikuwa tuna mahitaji ya kwenda kwenye bilioni 15, lakini hivi ninavyozungumza kumekuwa na mvua nyingi zimenyesha kwenye Mikoa ya Mara kule, lakini mvua nyingi zimenyesha pia, kule Simiyu. Tunaendelea kupokea shida mbalimbali kwenye maeneo mengi, lakini niwahakikishie tu kwa sababu, Serikali inazingatia kuona watu wanapita katika maeneo yao kwenye changamoto za barabara niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge tumejipanga kuwasiliana na wenzetu upande wa Wizara ya Fedha kwa utaratibu wa kibajeti, ili tuende kurejeshea mahitaji ya sehemu ambazo zimeharibika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nimalize tu kwa kusema kwamba, Waheshimiwa Wabunge michango yao yote waliyoisema sisi tumeichukua kwa nia hiyo ya kwenda kufanya maboresho. Na nimalizie kwa kusema naishukuru sana Kamati na tutaendelea muda wote kusikiliza maoni ya kamati kwa nia hiyohiyo ya kufanya maboresho makubwa na ninaunga mkono hoja ambazo ziko mbele yetu, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Elias Kwandikwa. Tunaendelea na Waziri wa Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Bashungwa.

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, lakini pia nikushukuru wewe Mheshimiwa Mwenyekiti kwa kunipa nafasi, ili niweze kuchangia hoja zilizoko mbele yetu. Kwanza nianze kwa kupongeza, niungane na waliokwishazungumza kupongeza Wenyeviti wa Kamati zote mbili kwa taarifa nzuri. Nawapongeza Wenyeviti hawa pamoja na Waheshimiwa Wabunge wa Kamati hizi kwa maoni na ushauri waliotupa na tunawaahidi tutaufanyia kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi hii inayoongozwa na Rais Dkt. John Pombe Magufuli na Serikali anayoiongoza pamoja na Watanzania tunafanya kazi usiku na mchana kujenga uchumi wa viwanda. Na ukiangalia takwimu tunaenda vizuri, lakini wapo wachache wanazungumza kwa ujumla na *statement* zao zinapotisha dunia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na mchango wa Mheshimiwa Lema; pamoja na mchango wake maana ameuzungumza kwa ujumla kwamba, utawala bora na sekta ya viwanda na biashara viko-*linked* na hajatumia takwimu katika kueleza hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ukiangalia nianze na takwimu ya *Rand Merchant Bank* ya Afrika Kusini kwenye ripoti ya mwaka jana mwaka 2019, Ripoti ya *Where to Invest in Africa,* Tanzania tumechukua nafasi ya saba kati ya nchi 54 Afrika ikiwa ni nchi yenye, *best nation* ya *investiment,* Tanzania tumechukua nafasi ya saba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa msisitizo nisome kipengele ambacho kinaisema hii Tanzania, kinasema hivi kwenye hii ripoti, *"in the ranking Tanzania maintains the 7th position as the most attractive country to invest in the continent with a score of 5.57 in 2018 against a score of 5.59 in 2017."* *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ukiangalia *FDI* nchini zinaongezeka, lakini ukiangalia takwimu pia za *UNCTAD FDI flows* mwaka 2018 hapa Tanzania zilikuwa ni *US Dollar* milioni 938 na mwaka jana ikapanda kwenda bilioni 1.1 sawa na ongezeko la asilimia 17.3. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Mheshimiwa Lema anavyosema kwamba, wawekezaji hawaji nchini kwa kweli, ni jambo la kupotosha. Niwaombe tu Waheshimiwa Wabunge *statement* tunazozitoa kama hazina takwimu ambazo ni *official* tunajiharibia sisi wenyewe kwa sababu, Serikali ya Awamu ya Tano inayoongozwa na Dkt. John Pombe Magufuli na Watanzania tunafanya kazi kwa bidii sana kujenga uchumi wa viwanda kwa hiyo, ni wajibu wetu sote kuhakikisha tunasemea mazuri na jitihada nzuri ambazo Serikali inazifanya, ili kuendelea kuvutia uwekezaji, lakini tunaenda vizuri Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia, ningependa kutaja takwimu chache tu zinazoonesha namna tunavyoenda kwenye sekta ya ujenzi wa uchumi wa viwanda. Mchango wa Sekta ya Viwanda kwa ajira nchini, mwaka 2015 mchango wa sekta ya viwanda ilikuwa ni 8%, lakini hivi sasa imepanda kuwa 12.5 na malengo ya Serikali ni kufika mwaka 2025 mchango wa sekta ya viwanda kwa ajira uwe ni 20%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia ukiangalia mchango wa *manufacturing sector* mwaka 2015 ilikuwa ni 5.5%, lakini hivi sasa imepanda ni 8.3%, lakini ukiangalia mchango wa ujenzi wa uchumi wa viwanda kwa ujumla wake, yaani *in aggregate terms,* mwaka 2015 mchango wa sekta ya viwanda ilikuwa ni 21.1% na hivi sasa ni 23.7% na ukiangalia mikakati ya kujenga miradi ya vielelezo hasahasa kwenye uwekezaji mkubwa ambao nchi yetu inafanya kwenye sekta ya miundombinu takwimu hizi zitaongezeka kwa sababu, miradi hii itachochea ukuaji wa uchumi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tunaenda vizuri kwenye ujenzi wa sekta ya viwanda na tuendelee kushirikiana kusemea mazuri haya, ili kuendelea kuvutia uwekezaji na kuwapa moyo wale wawekezaji ambao tayari wako hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie suala la *Development Budget.* Bajeti ya Wizara ya Viwanda na Biashara ni bajeti ya Serikali nzima, yaani trilioni 33.1 tulizopitisha kwenye mwaka huu zote zinaenda kwenye kujenga uchumi wa viwanda.

Kwa hiyo, tunakosea pale tunapoangalia ile *Development Budget* ambayo iko chini ya Wizara ya Viwanda na Biashara, yani kama sekta kwamba, ndio *Development Budget* kwa sababu, ili uweze kujenga uchumi wa viwanda sekta zote, zile sekta ambazo ni za huduma za jamii, zile sekta ambazo ni za uzalishaji, zote kwa pamoja zinaungana kujenga uchumi wa viwanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Wizara yangu pamoja na kwamba, bajeti ya maendeleo bado tunaendelea kupokea kwa mwaka wa fedha huu tunaotekeleza, lakini hata zile trilioni 4.9 ambazo ziko kwenye Wizara ya Uchukuzi, Ujenzi na Mawasiliano zile na zenyewe ni sehemu ya mchango wa sekta ya viwanda kwa hiyo, tunaenda vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo ningependa kulizungumzia ni kwenye Maoni na Mapendekezo ya Kamati wamesisitiza sana kulinda viwanda vya ndani. Serikali tunafanya jitihada kupitia kuongeza *import duties,* kutoa huduma za biashara mipakani, kudhibiti bidhaa *fake* kwenye njia za panya, lakini pia hata sisi Watanzania tuna jukumu la kuhakikisha tunalinda viwanda vya ndani na bidhaa wanazozizalisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiangalia majirani zetu wananchi wamepata elimu ya kupenda bidhaa zao za ndani na kwa kufanya hivyo, yaani ule uzalendo wa kusema kwamba, tukipenda bidhaa tunazozalisha wenyewe tutatengeneza ajira za vijana na akinamama ndugu zetu, yaani unakuta tunakuwa tumeshapunguza ule mzigo wa Serikali kufanya kila kitu kudhibiti, lakini sisi wenyewe kama raia tukihamasika tukatumia bidhaa zetu hiyo na yenyewe ni kuchochea sbhughuli za viwanda vyetu hapa nchini na kuhakikisha viwanda hivi vinazalisha, ili vizidi kutengeneza ajira hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nipende kuwaomba Waheshimiwa Wabunge tuendelee kuwaelimisha wananchi kupenda bidhaa ambazo zinazalishwa hapa nchini, lakini kwa upande wa Serikali tunaendelea kufanya jitihada kwa kufanya tafiti. Na zile bidhaa ambazo tunazalisha hapa nchini tutaendelea kuongeza kodi pale inapowezekana, ili kuendelea kulinda viwanda hivi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo ningependa kulichangia na jambo hili alizungumzia Mheshimiwa Mwakajoka kwamba kero kwa wafanyabiashara Serikali hatujafanya vizuri, ningependa nitofautiane naye kwa sababu zifuatazo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kwenye *World Bank cost of doing business* Tanzania tume-*improve* kutoka nafasi ya 144 kuja nafasi ya 141.

Kwa hiyo tume-*improve* kwa nafasi tatu. Mikakati niliyoielezea na nitakayoitaja hapa kwa mfano *blueprint,* tayari ni *document* ambayo Serikali imesha-*commit* kwa Watanzania na wawekezaji kwamba tutatekeleza *blueprint* hii ambayo imesheheni changamoto ambazo wafanyabiashara na wawekezaji wamekuwa wakiilalamikia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile Serikali imewasikiliza, tumeandaa *blueprint*, huu mwaka wa fedha tunaotekeleza kuna kero 54 zimeshafanyiwa kazi na hivi sasa kabla ya Bunge la Kumi na Moja kwisha, mkakati wa Serikali ni kuleta Muswada wa Uwezeshaji Biashara. Muswada huu ndiyo umebeba changamoto zote ambazo ziko kwenye *blueprint* ili tuweze kuhakikisha zinasimamiwa na *legal force,* yaani kwa maana tuwe tuna sheria inayosimamia utekelezaji wa *blueprint*.

Kwa hiyo, baada ya kufanya hivyo, tutazidi kuondoa keroambazo zinawakumba wafanyabiashara wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tumeendelea kuboresha taasisi ambazo ziko chini ya Wizara ya Viwanda na Biashara. Tunajua *BRELA, TBS* na *TANTRADE* ni taasisi ambazo zinatoa huduma kwa Watanzania kila siku. Kwa hiyo, mkakati wa Serikali na ninyi ni mashahidi, sasa hivi hizi taasisi tunaziboresha kwa kasi kubwa sana.

Mheshimjiwa Mwenyekiti, ukienda kwenye hizi taasisi, kipindi cha nyuma kulikuwa hakuna Idara za *customer care*, kulikuwa hakuna *hotline,* ukienda kwenye huduma za biashara mipakani kulikuwa hakuna namba za Maafisa wanaohudumia ili kama hujaridhika na huduma zao upige simu Wizarani na kumlalakimia Afisa fulani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hivi Mikakati yote tunayo kwa hiyo Waheshimiwa Wabunge tuendelee kusaidiana muendelee kutupa ushirikiano ili tutekeleze mikakati hii tuzidi kuweka mazingira mazuri ya kufanya biashara hapa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Bajeti inayokuja, tumepanga kuweka maafisa yaani *commercial attache* kwenye nchi ambazo tunafanya biashara nazo sana ili *commercial attache* hao washirikiane na *TANTRADE* kuhakikisha tunawasaidia wafanyabiashara wetu waweze kufanya biashara na mauzo ya nje ya wafanyabiashara wetu yaweze kuongezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambasamba na hilo, naomba nizungumzie mikataba iliyozungumzwa humu Bungeni kwenye maoni na ushauri wa Waheshimiwa Wabunge. Mkataba wa *Ursus* hata sisi Serikali hatujaridhika nao, tayari tumeshapendekeza kuunda *government negotiating team* kwa ajili ya kupitia mkataba huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge hili tayari tumeshalifanyia kazi, bado hii *GNT* ianze na mkataba huu utaboreshwa kwa manufaa ya nchi yetu. Pia tumeenda mbali, hata Mkataba wa *TANCOL* hatujaridhishwa nao. Tumefanya uchambuzi tumekuta Mkataba wa *TANCOL* hauna maslahi kwa nchi yetu na tayari tumeshaanza mchakato wa kuunda *GNT* ili tuweze kupitia Mkataba wa *TANCOL* kama tulivyofanya kwenye *Barrick* na kama tulivyofanya kwenye *AIRTEL.* Tutaenda na wembe huo huo kwenye Mkataba wa *TANCOL.* Pia hata *Mufindi Paper Mill* baada ya kutembelea Kiwanda kile tumegundua uhasi ambao unaukuta kwenye *TANCOL* na Mikataba mingine upo pia kwenye Kiwanda cha *Mufindi Paper Mill*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti na Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo, Serikali tutaendelea kupitia vile viwanda ambavyo vilibinafsishwa baada ya kuchambua na kujiridhisha kwamba kuna maeneo hasi, hatutasita kuchukua hatua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kwenye maoni na ushauri wa Waheshimiwa Wabunge na Taarifa za Kamati wamelalamikia urasimu katika utoaji vibali, wamelalamikia masuala ya *electronic stamps (ETS),* wamelalamikia *VAT* ambazo kwa miaka mingi zimekuwa hazilipi kwa

wafanyabiashara na wenye viwanda na vile vile wamelalamikia urasimu na mkanganyiko ambao upo ndani ya *TASAC* na kero za bandarini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge, mimi kama Waziri wa Viwanda na Biashara sekta ambayo ndiyo *driving force* ya kujenga uchumi wa viwanda, Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango tuko naye hapa, Waheshimiwa Mawaziri wa upande wa Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi wapo; baada ya kikao hiki tutakaa tuangalie namna tunavyoweza kushirikiana kama Serikali kuhakikisha tunatatua changamoto hizi ili jitihada nzuri na maoni yenu ya ushauri mliotushauri, tutakaporudi mwakani changamoto ambazo mmezitaja tuwe tumezitekeleza kwa kiasi kikubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii, lakini nawashukuru sana Mheshimiwa Mwenyekiti Suleiman Saddiq, Makamu Mwenyekiti pamoja na Waheshimiwa Wabunge wa Kamati ya Viwanda, Biashara na Mazingira kwa ushirikiano ambao mnaendelea kuipa Wizara yangu. Nawashukuru sana, tuendelee kushirikiana na maoni na ushauri ambao mmetupa tutaufanyia kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Waziri wa Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Innocent Bashungwa. Watoa hoja; nitaanza na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu Mheshimiwa Kakoso kwa ufupi tu. *(Makofi)*

**MHE. MOSHI S. KAKOSO - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kunipa fursa ya kipekee kupokea michango ya Waheshimiwa Wabunge ambao wamechangia hoja. Wabunge waliochangia wako 16. Kati ya hao, ni Mheshimiwa Julius Kalanga, Mheshimiwa George Lubeleje, Mheshimiwa Bhagwanji Meisuria, Mheshimiwa Miraji Jumanne Mtaturu, Mheshimiwa Vedastus Manyinyi, Mheshimiwa Deogratias Ngalawa, Mheshimiwa Mbaraka Dau, Mheshimiwa Boniphace Getere, Mheshimiwa Susan Kiwanga na wengineo ambao wanafika 16.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja za Wabunge waliochangia taarifa hii ni zinazohusu Sekta ya Ujenzi, Sekta ya Uchukuzi na Sekta ya Mawasiliano. Wengi wao wamejikita sana juu ya hoja ya uharibifu wa miundombinu kutokana na mvua kubwa zinazoendelea kunyesha hapa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati imezingatia hili na kufanya majadiliano katika vikao vyake na Wakala wa Barabara *(TANROADS)* katika mwaka wa fedha wa 2019/2020, fedha zilizokuwa zimetengwa kwa ajili ya matengenezo ya dharura ni shilingi bilioni 8.2, wakati gharama za kazi za dharura zimekadiriwa kuwa shilingi bilioni 15 na inaweza ikazidi karibu mara mbili ya kiasi kilichokuwa kimetengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati imeona kuwa fedha za dharura zinazotengwa ni kidogo ukilinganisha na uhitaji uliopo, hivyo kuona haja ya Serikali kufanya mapitio kwa ajili ya kuongeza fedha za dharura ili kusaidia kufanya matengenezo katika maeneo yaliyoathirika na mvua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye hili hili la barabara, Waheshimiwa Wabunge ambao wamechangia wanachanganya barabara zinazomilikiwa na *TARURA* na zile ambazo zinamilikiwa na *TANROADS*. Hili ni vyema Waheshimiwa Wabunge wakaliangalia na tutakapokuwa tumekaa kwenye vikao vya Bajeti tukajielekeza zaidi kuitengea *TARURA* uwezo mkubwa ambao wanaweza wakajenga hizo barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa barabara nchini umekasimiwa kwa *TANROADS* na *TARURA*. Wakala wa Barabara Tanzania *(TANROADS)* ina majukumu ya kupanga, kujenga, kukarabati na kutengeneza barabara kuu, barabara za mikoa za Tanzania Bara na Wakala wa Barabara za Mijini na Vijijini. Hizi barabara zinazojengwa na *TARURA* ni kwa ajili ya kuhudumia barabara za mijini na vijijini ambazo haziko chini ya *TANROADS*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge, niliona hili nilieze ili mwangalie zile barabara zinazotugusa ili tujue kwamba tunapochangia zipo barabara ambazo zinamilikiwa na *TANROADS* ambazo ziko chini yetu na zile ambazo zinamilikiwa na *TARURA* ambazo ziko Ofisi ya Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo, Kamati imekuwa ikiishauri Serikali iendelee kusisitiza kuwa inaunganisha Miji yote Mikuu na Mikoa iliyosalia kama vile Mikoa ya Katavi - Kigoma, Katavi - Tabora, Kigoma – Kagera, Njombe – Makete, Morogoro, Lindi, Mbeya, Makete – Mbeya na barabara za lami ili kufungua fursa za maendeleo katika maeneo hayo. Aidha, Serikali kukarabati baadhi ya barabara za mikoa zilizo katika hali isiyoridhisha na kutokupitika hasa wakati wa mvua na kuathiri shughuli za kiuchumi na kijamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile Serikali kuendeleza ujenzi wa barabara za lami hasa maeneo yanayochochea uchumi wa Taifa letu kama vile maeneo yenye Miradi mikubwa, vivutio vya utalii, kilimo, viwanda na madini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge, wamezungumzia sana suala la Viwanja vya Ndege hasa Kiwanja cha Ndege ya Musoma ambacho Mheshimiwa Mbunge ameiomba Kamati kwenye mwezi wa Tatu wafike kwenye eneo la Mkoa wa Mara. Katika Bajeti ya mwaka huu 2019/2020 Serikali imetenga fedha za ndani kiasi cha shilingi bilioni 3.5 kwa ajili ya Kiwanja cha Ndege cha Musoma ambacho kitakuwa katika hali ya usanifu na *TANROADS* ndiyo watakaojenga na wako katika hatua ya kukamilisha maandalizi ya *tender* kwa ajili ya ukarabati wa kiwanja hicho. Kazi za ukarabati zinatarajiwa kuanza kufanyika mwaka ujao wa fedha wa 2020/2021.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waheshimiwa Wabunge wamezungumzia suala la kuchelewa kwa mizigo na meli kukaa kwa muda mrefu bandarini. Wabunge wengi wamelizungumzia hili. Hii ni kutokana na ucheleweshaji wa mzigo unaokuja kwenye Bandari ya Dar es Salaam. Tumeshaishauri Serikali iangalie uwezekano wa kukaa na wadau ili waweze kutoa hili tatizo, kwani kutokufanya hivyo vipo viashiria vikubwa ambavyo vitakimbiza Wafanyabiashara waache kuitumia Bandari ya Dar es Salaam. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli Tanzania ni nchi iliyobarikiwa, kwani kijografia hasa katika usafiri wa usafirishaji wa majini na nchi kavu kwani tumepakana na nchi takribani tisa ambazo zinategemea kupitisha mizigo na malighafi. Kamati imeendelea kuishauri Serikali mara kwa mara; pamoja na kuwa katika mazingira mazuri ya kijografia ni muhimu sana kupunguza urasimu na vikwazo mbalimbali ambavyo vinasababisha Wafanyabiashara kuhama kutumia Bandari yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ipo changamoto ambapo na Serikali wamezizungumzia kwamba zipo changamoto kiasi ambazo ni za mawasiliano hasa maeneo ya mipakani. Ni kweli kumekuwepo na changamoto za wananchi wanaoishi maeneo ya mipakani kukosa huduma ya mawasiliano au wakati mwingine kupata huduma ya mawasiliano toka nchi jirani, jambo ambalo siyo sawa na ni hatari kwa usalama wa nchi. Hivyo, Kamati imeendelea kutoa ushauri wa kuishauri Serikali kusimamia jambo hili liweze kufanyiwa maboresho ya maeneo ya mipakani na ikiwezekana kuweka minara yenye nguvu ambayo itawezesha kupata mawasiliano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ipo michango ya Mbunge mmoja mmoja, siyo rahisi kuipitia yote, lakini kuna baadhi ya maeneo ambayo naweza nikagusa. Mheshimiwa Dau Mbaraka ametoa pongezi za ujenzi wa gati lakini ameelezea juu ya umuhimu wa kujenga boti mpya ya kisasa itakayotoa huduma kwenye eneo la bahari ya hindi kwenda eneo la Mafia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ilishaanza kulifanyia kazi. Kwa sasa inaendelea na ujenzi wa boti ambayo itatoa huduma kwenye maeneo hayo, lakini amezungumzia suala la minara penye maeneo ya Mafia. Tunavyozungumza hivi, kesho kutakuwa na uzinduzi wa minara kwenye eneo la Mafia. Hivyo, Serikali ilishasikia ombi lake na sisi kama Kamati tumekuwa tukisimamia Mfuko huu ili uweze kutoa maboresho kwenye maeneo mbalimbali. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye suala la maboresho ya Viwanja vya Ndege, Kamati imeendelea kutoa ushauri wa kuielekeza Serikali hasa kwenye Viwanja vya Ndege vya Mwanza, Mbeya, Songwe na Dodoma. Eneo hili ni muhimu sana ili kufanya maboresho ya viwanja hivi vya ndege. Viwanja hivi vinatumiwa na Watanzania walio wengi na Kiwanja cha Mwanza kinategemewa kuwa Kiwanja ambacho kitakuwa *hub* ya kutumika kwenye maeneo ya Afrika Mashariki. Hivyo, tunahitaji Kiwanja kile kifanyiwe ukarabati hasa kujenga Jengo la Abiria na kuweka wigo kwenye maeneo ambayo wananchi wanakatisha kwenye viwanja hivyo vya ndege.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchangiaji mwingine amezungumzia juu ya umuhimu wa kuboresha reli ya *TAZARA*. Reli hii ni muhimu sana katika nchi yetu na ni ya kihistoria ambayo imeelekeza wazi kwamba ilikuwa ya uhusiano kati ya nchi mbili ya Zambia na Tanzania na rafiki wa karibu, nchi ya China.

Mheshimiwa Mwenyekiti, reli hii ina changamoto, hivyo tumeishauri Serikali kuhakikisha wanakaa pamoja kati ya Serikali ya Zambia na Serikali ya Tanzania ili kupitia mapitio ya sheria ya kuweka mazingira mazuri yatakayoifanya reli hii iweze kutumika vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine kwenye suala la Reli ya TAZARA ni umuhimu wa kulipa wafanyakazi waliokuwa wanaidai Serikali. Tunaipongeza Serikali, imelipa fedha nyingi kwa wafanyakazi na wanaendelea kulipa wafanyakazi mishahara, lakini bado kuna baadhi ya Watanzania wenzetu ambao wanadai Shirika hili. Hivyo, tunaomba Serikali ipitie na kuangalia umuhimu wa kuwalipa wale wafanyakazi ili kutoa motisha kwa wale wengine waliobaki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wapo wachangiaji ambao Mheshimiwa Mwakajoka ameelezea kwa nini suala la miundombinu wanapewa fedha nyingi kwa ajili ya Bajeti? Ni ukweli usiopingika, miundombinu inapewa fedha nyingi kwa sababu Serikali ya Awamu ya Tano imetekeleza miradi mingi karibu kila mkoa, hakuna sehemu ambako hakujaonekana mradi ambao unafanyiwa kazi na Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye maeneo tu ya Mkoa wa Songwe ipo barabara inayojengwa kutoka eneo la Mloo kwenda Kilyamatundu mpaka Mkoa wa Katavi. Hiyo barabara ni muhimu sana kwa maendeleo, lakini kuna ukarabati wa barabara ya kutoka Mbeya kwenda Tunduma, hizo ni kazi zinazofanywa na Serikali sambasamba na ujenzi ule wa Songwe ambao utawanufaisha sana wananchi wa Kanda ya Nyanda za Juu Kusini kwa ajili ya kusafirisha mizigo na kutoa fursa mpya ya usafirishaji wa zao la matunda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni mengi ambayo yametekelezwa ambayo Serikali ya Awamu ya Tano imekuwa ikiyafanya. Tunawapongeza Waheshimiwa Wabunge wote walioipongeza

Kamati, Serikali kwa kazi ambayo imefanyika na juhudi ambazo zimefanywa na Serikali ya Awamu ya Tano chini ya Rais, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja ya Kamati hii na ninawashukuru sana Wabunge wote waliotoa mchango wao tunawaahidi kwamba tutaendelea kushirikiana nao kuhakikisha tunafanya maboresho. Tunawapongeza Manaibu Waziri ambao kimsingi wameungana na Kamati na kukubali yale ambayo tumeshauriana nao. Hivyo naamini tukiwa pamoja tutafanya kazi ambayo haitakuwa ngumu na itakuwa na manufaa kwa Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunawashukuruni sana, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Toa hoja Mheshimiwa.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

**MHE. JACQUELINE N. MSONGOZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Hoja imetolewa na imeungwa mkono. Sasa nitawahoji Waheshimiwa Wabunge.

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Taarifa ya Mwaka ya Utekelezaji wa Shughuli za Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu kwa Kipindi cha Februari, 2019 hadi Januari, 2020 ilipitishwa na Bunge)*

**MWENYEKITI:** Kwa hiyo, Bunge hili limepitisha rasmi maoni na mapendekezo yote ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu kwa taarifa yake ya mwaka 2019. *(Makofi)*

Tunaendelea na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira; Makamu Mwenyekiti Mheshimiwa Kanali Mstaafu Masoud.

**MHE. KANALI (MST) MASOUD ALI KHAMIS - MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA VIWANDA, BIASHARA NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuhitimisha taarifa yetu ya Kamati ya Viwanda, Biashara na Mazingira kama tulivyoiwasilisha asubuhi ya leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa yetu imechangiwa na watu takribani 15, pia na Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara pamoja na Naibu Waziri. Nawapongeza sana Waheshimiwa Wabunge kwa kutoa maoni yao na ushauri. Tunayathamini sana maoni yao na ushauri huo na ninaiomba Serikali, maoni na mapendekezo yaliyotolewa na Waheshimiwa Wabunge, yachukuliwe na kufanyiwa kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawashukuru sana Mawaziri waliochangia, Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara na Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ofisi Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira. Wizara ya hii ya Viwanda na BIashara ndio imebeba mwelekezo wa nchi kwa sasa, katika kuipeleka azima ya uchumi wa kati kupitia viwanda. Hivyo ni vyema na tuendelee kuiomba Serikali kuiwekea umuhimu na mkazo wa hali juu katika kuwapatia fedha za maendeleo ili waweze kuifikia azima hiyo tuliyoikusudia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutekeleza azima hii na kufikia mahali tulipokusudia yapo mambo ya msingi ya muhimu yanatakiwa yafanywe na kuwajibishwa na wananchi wote wa Tanzania. Moja ambao lazima niwepo katika nchi nchi lazima kuwe na ulinzi au amani na utulivu ndani ya Taifa letu. Wapo Waheshimiwa Wabunge ambao walichangia hapa na kusema kwamba hata utawala bora haupo. Siamini, lakini nasema utawala bora kama ungekuwa haupo tusingeona wimbi kubwa la wawekezaji wanaoingia nchi hivi sasa kwa ajili ya kuja kuwekeza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutekeleza azima hiyo, yapo mambo ambayo sisi kama Kamati tuliyazungumza na kuyatolea ushauri kwa Serikali. Yapo mambo tuliyafanyia kazi katika Kamati hasa katika suala la ujenzi wa jengo la *TBS*. Ujenzi wa jengo la *TBS* katika kutembelea Kamati ilishuhudia na kuingia wasiwasi na thamani kubwa ya fedha zilizotolewa kwa ajili ya ujenzi wa jengo lile. Hivyo ilishauri Wizara kuhakikisha wanafanya tathmini au kuweka Kamati Maalum itakayofuatilia na kuhakikisha waone uhalali au wafanye uhakiki wa uhakika wa kuhakikisha kwamba jengo lile lina thamani ya kiasi gani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niombe nizungumze suala la Liganga na Mchuchuma, limezungumzwa na Wabunge wengi. Sisi kama Kamati tumeliona, tumelijadili, tumelizungumza na tumelishauri sana Serikali kuhusu suala hili. Kweli suala hili ni la muda mrefu, lakini kwa sasa lazima tukubali kwamba Serikali baada ya kuona utata mkubwa katika mikataba ya jambo hili, waliona ni vyema sasa waanze kupitia tena mikataba na kufanya tathmini ya kuhakikisha tunakwenda kwenye mkataba ukao tusaidia kama Taifa. Kwa hiyo tunaiomba Serikali sasa ihakikishe mapitio haya yanafanyika haraka ili mradi huu uweze kufanya kazi na ulete tija kwa Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la matrekta ya *URSUS,* Kamati ililiona hili na ilitoa mawazo yake na ushauri kwa Serikali kwamba kwa sasa inaonekana kampuni hiyo ya Poland imeshindwa kutekeleza wajibu wake na kutekeleza mkataba kama tulivyokubaliana. Hivyo tunaomba sasa Serikali ilichukulie uzito wake na kwa sababu Serikali imeshatoa fedha nyingi katika mradi huu, ni vizuri sasa Serikali ikalifualia kwa karibu na kwa haraka ili fedha yetu hiyo iweze kuleta tija na kutuletea maendeleo mengine hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la bandari la kuchelewesha mizigo nalo lilitufikia katika Kamati yetu kwa wadau. Wadau wengi walipokuja katika Kamati walilalamikia suala la uchelewashaji wa mzigo. Ni kweli suala hili limezungumza katika Kamati ya Miundombinu, lakini sisi kama Kamati ya Viwanda na Biashara, biashara yoyote nayo inahusisha bandari. Huwezi kufanya biashara kwa ufanisi kama huna bandari yenye uhakika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo sisi katika ripoti tuliyotoa leo tuliweza kuishauri Serikali kuhakikisha kwamba wale wadau wanaofanya kazi bandarini hatuna uhakika ni nani anayechelewesha mizigo inaweza ikawa *TASAC* Inawezekana wengine, lakini ushauri wa Kamati unasema *TASAC, TRA,TPA* na wengine wadau wote wanaoshughulika na mizigo bandarini wakae pamoja watafakari na kuona kwa nini mzigo inachelewesha hapa bandari na wafikie muafaka wa kutatua tatizo hilo kwa haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kero za wafanyabiashara ni nyingi na nyingine tumetoa hapa vizuri na tumezielezea. Suala la VAT *refund,* suala la 15% ya sukari ya viwandani. Hili kwa kweli ni tatizo kubwa, sisi tunachokiomba sasa Serikali ilichukulie kwa uzito wake na kuhakikisha wanawapa faraja wafanyabiashara wetu waweze kutumia fedha zao zile kwa ajili ya maendeleo zaidi. Viwanda vingi vinapata shida ya kuendesha biashara zao kwa sababu fedha nyingi zipo

Serikalini. Tunaomba sana Serikali ilichukulie hili na kuhakikisha kwamba wafanyabiashara wetu wanapata faraja katika jambao hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kutekeleza majukumu yetu kama Wizara tunashukuru wenzetu wa *Tan Trade* kwa kweli kuna mabadiliko makubwa ya sasa hivi yanaonekana yanayaanza kutekelezwa. Sisi tunasema tunawapongeza sana *Tan Trade* kwa kuunda Kitengo cha Intelejensia ya kutafuta biashara na mazao mbalimbali na kuhakikisha tunatangaza biashara zetu ili kusudi tupate masoko katika kutekeleza azima hiyo tunayokusudia ya viwanda katika uchumi wakati. Naomba sana tunapojenga viwanda katika nchi vitu hivi viwili lazima viende sambamba. Viwanda viende na masoko pia tukijenga viwanda bila kupata masoko havitaleta tija wala havitatusaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tunaomba sana wakati wowote *Tan Trade* wahakikishe bidhaa zote zinazozalishwa ndani ya nchi zinapata masoko na zinauzwa ndani na nje ya nchi. Viko viwanda sasa hivi vimetia malalamiko makubwa sana ya bidhaa nyingi sana zinazozalisha ambazo zipo ndani ya magodauni na hazina wateja. Hivyo kiwanda kama hicho si vizuri kuwa nacho kwa sababu hakitatupa faida kubwa. Naomba sana wenzetu wa *Tan Trade* katika hili wahakikishe wanafanya kazi ya ziada ya kuhakikisha masoko ya bidhaa zetu zote zinapatikana ili waweze kuuza huko nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo lilizungumzwa hapa…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Malizia tu Mheshimiwa.

**MHE. KANALI (MST) MASOUD ALI KHAMIS - MAKAMU MWENYEKITI WA KUDUMU WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA VIWANDA, BIASHARA NA MAZINGIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo, naomba Waheshimiwa Wabunge wakubali taarifa ya Kamati na ushauri, iwe kama azimio la Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**MHE. HASNA S.K. MWILIMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Hoja imetolewa na imeungwa mkono. Kwa hiyo tudhibitishe kama tunaiamua.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira kuhusu Shughuli Zilizotekelezwa na Kamati hiyo katika Kipindi cha Mwezi Februari, 2019 hadi Januari, 2020 ilikubaliwa na Bunge)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, Bunge limekubali rasmi maoni na mapendekezo yote ya Kamati ya Kudumu ya Viwanda, Biashara na Mazingira kupitia taarifa yake ya mwaka 2019.

Waheshimiwa Wabunge, kwa leo ndio ilikuwa shughuli yetu ya taarifa hizo mbili ni muhimu sana kwa hiyo tunawashukuruni sana kwa michango yenu kwa ushauri wenu. Pia tunashukuru kwa matumaini ambayo yametolewa na michango ya Serikali wakati

wanachangia kupitia Mawaziri na Naibu Mawaziri mbalimbali. Hatuna Kamati ya ufuatiliaji wa ahadi za Serikali na taarifa hizi kwetu ni muhimu sana kama Bunge, lakini naamini kwa vile Serikali ipo Bungeni na wanayaratibu haya, kuna yale ambayo tusingependa yajirudierudie kila mwaka, hivyo, tufikie mahali maamuzi ya Serikali yapatikane.

Nina matangazo mawili hapa Waheshimiwa Wabunge; tangazo la kwanza linatoka kwa Mheshimiwa Margaret Sitta Mwenyekiti wa *TWPG,* anaomba iwatangazie Wabunge wanawake wote wa *TWPG* kuwa Jumapili tarehe 2 yaani kesho kutwa kutakuwa na mafunzo kuanzia saa nne asubuhi ukumbi wa Msekwa, wote kwa maana ya wanachama wa chama hicho mnaombwa kuhudhuria. *TWPG* unaweza ukajiunga leo tu, kesho kutwa ukahudhuria.

Tangazo la pili linatoka kwa Mheshimiwa Maulid Mtulia, Mbunge wa Kinondoni, anaomba niwatangazie Waheshimiwa Wabunge kuwa kesho Jumamosi tarehe Mosi Februari, saa 10 jioni kutakuwa na mechi ya ligi kuu kati ya *Tanzania Prisons* na *KMC* Kinondoni Boys. Wote mnakaribishwa nadhani ni uwanja wa Jamhuri, sidhani kama kuna uwanja mwingine hapa kwa sasa. Kwa hiyo mnakaribishwa wote. *(Makofi)*

Hayo ndio matangazo nimemaliza. Kwa hiyo Waheshimiwa Wabunge, baada kusema hayo, naahirisha shughuli za Bunge hadi siku ya Jumatatu tarehe 3 Februari, saa tatu asubuhi.

*(Saa 1.31 Usiku Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Jumatatu,*
*Tarehe 3 Februari, 2020 Saa Tatu Asubuhi)*